Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 15 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Bodi ya Korosho Tanzania kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Septemba, 2004 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Cashewnut Board of Tanzania for the Year ended 30th September, 2004.*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Chai Tanzania kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2004 *(The Annual Report and Accounts of the Tea Board of Tanzania for the Year ended 30th June, 2004).*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:**

Maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni yake kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 264

**Ujenzi wa Kituo cha Afya – Mima na Tarafa ya Mpwapwa.**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Tarafa ya Mpwapwa Wilayani Mpwapwa hugemea zaidi kupata huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa kutokana na kukosekana kwa Kituo cha Afya, katika Tarafa hiyo na kwa kuwa, Serikali iliahidi kujenga Kituo cha Afya katika Kijiji cha Mima:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Tarafa ya Mpwapwa?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa iwapo Kituo cha Afya kitajengwa katika Kijiji cha Mima, kitasaidia sana kuwapatia huduma za afya wananchi wa Kata za Berege, Mima, Mlunduzi, Chipogoro na Mtera?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kulingana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, Wilaya ya Mpwapwa ina wakazi 264,365 (Wanaume 127,838 na Wanawake 136,527) kwa wastani wa ongezeko la watu la asilimia 2.1 kwa mwaka. Aidha, Wilaya ina Tarafa tatu za Mpwapwa, Kibakwe na Rudi na ina Vituo vya Afya 2 vya Rudi na Kibakwe. Kutokana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002 Tarafa ya Mpwapwa ina wakazi 135,397 kwa wastani wa ongezeko la watu la asilimia 2.1 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Tarafa hiyo kwamba haina Kituo cha Afya. Hata hivyo, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa George Lubeleje Mbunge, kwa juhudi ambazo amekuwa akizifanya yeye pamoja na Halmashauri katika kuondoa tatizo hili. Tayari Halmashauri imekwishakutoa kusudio la kupandisha hadhi zahanati ya Mima na Mbori zilizoko katika Tarafa ya Mpwapwa kuwa Vituo vya Afya. Aidha, katika kutekeleza kusudio hili Halmashauri pia imeendelea kutafuta wafadhili mbalimbali

kusaidia kutekeleza Mradi huu ikiwa ni pamoja na kuandaa andiko la Mradi na kuandaa Mpango na Mkakati wa Wilaya katika kipindi cha mwaka 2003 – 2007 ulioainisha upanuzi wa Zahanati za Mima na Mbori kuwa Vituo vya Afya kwa awamu. Awamu ya kwanza ya upanuzi wa zahanati ya Mima unatarajia kuanza kutekelezwa kwa wakati wowote fedha zikapokuwa zimepatikana. Upanuzi wa Kituo hiki unakadiriwa kugharimu kiasi cha Tshs 304,075,925/=

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana kimsingi na Mheshimiwa Lubeleje Mbunge wa Mpwapwa kuwa iwapo Kituo cha Afya kitajengwa katika Kijiji cha Mima, kitasaidia sana kuwapatia huduma za Afya wananchi katika Kata alizozitaja. Aidha, Zahanati ya Mima, ikipandishwa hadhi na kuwa Kituo cha Afya kitapokea wagonjwa kutoka Zahanati ya Chitemo, Seluka, Chinyanghuku, Chipogoro, Mtera, Kisima, Wiyenzele, Mlunduzi na Iwondo. Hii itasaidia kupunguza adha ya wananchi kutembea muda mrefu au kukosa huduma zinazohitaji utaalam zaidi na msongamano usio na lazima katika Hospitali ya Wilaya.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, majibu ambayo yanawapa matumaini wananchi wa maeneo hayo.

(a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na mipango mizuri ya Halmashauri ya Wilaya, pamoja na Serikali. Je, atakubaliana nami kwamba kujengwa vituo vya Afya katika maeneo aliyoyataja zahanati za Mbori na Mima kutasaidia sana kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali yetu ya Wilaya ya Mpwapwa?

(b) Mheshimiwa Spika, napenda niishukuru sana Serikali kwa kutoa kibali cha kufungua zahanati ya Inzomvu, Chitemo pamoja na Kiboriana. Je, Serikali itakuwa tayari kupeleka wataalam/waganga kwa sababu tungepata kibali cha kupata madawa kila mwezi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza kama nilivyosema tunakubaliana naye kabisa kwamba vituo hivyo vitasaidia sana katika kujaribu kupunguza kero na naomba niongeze tu kwamba kwa sababu kiwango cha fedha kinachohitajika ni kikubwa namwomba Mheshimiwa George Lubeleje ajaribu kuishinikiza Halmashauri yake waanza kuingiza mipango hii katika Bajeti ya kawaida ya Serikali kupitia mkoani na kama hapana budi tutasaidia Mkoa kuweza angalau kuanza kidogo kidogo kutenga fedha kuharakisha zoezi hili badala ya kungoja wahisani kwa upana wake.

Lakini kuhusu swali la pili tatizo la wataalam tulivyokuwa tunalieleza mara nyingi ni kubwa kwa maana ya kwamba wataalam hawa nao wana mipangilio yao ya namna ya kufanya kazi hizi.

Lakini naomba niseme tu maadamu Serikali imeshakubali sasa kutoa wataalam hawa moja kwa moja bila kupitia utaratibu ule ambao tulikuwa tunautumia kutangaza

basi naomba tusaidiane tu na Mheshimiwa George Lubeleje, kuomba sana wataalam hawa waweze kupatikana kwenda moja kwa moja kwenye vituo hivyo ili kupunguza tatizo hili. (*Makofi*)

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu mazuri ya ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba zahanati za Mima na Mbori katika Wilaya ya Mpwapwa zitapandishwa daraja kuwa vituo vya afya. Je, hatua hiyo itafikiwa mwisho lini kwa sababu katika Tarafa yangu ya Mbwela kulikuwa na kituo cha afya tangu mwaka 1993 au 1994 mpaka leo kinataka kupandishwa daraja hakijafikia hatua ya kituo cha afya, tatizo hilo Naibu Waziri analijua vizuri zaidi. Je, anafikiri hizi zahanati kuwa vituo vya afya kamili itakuwa lini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nilipomuona amesimama nikajua litakwenda Mbwela tu. Sasa kituo cha afya cha Mbwela ni kweli tumekihangaikia sana na Profesa amejitahidi sana kujaribu kusukuma jambo hili liweze kukamilishwa mapema. Lakini kumekuwa na matatizo ambayo mimi naweza nikasema zaidi yake mkoani kwake kwa kipindi kirefu sana licha ya juhudi zote nilizofanya pamoja na yeye pamoja na Ofisi kwa ujumla. Kwa hiyo, naomba labda nijaribu kumhakikishia kwa mara nyingine tena kwamba ngoja tushirikiane hata kama ni hatua za mwishoni kikubwa ni kwamba kituo cha afya kipatikane tutaona nini cha kuweza kufanya katika hatua za mwisho. (*Makofi*)

Na. 265

**Barabara za Usa – Oldonyosambu na Tengeru – Mererani.**

**MHE. LEKULE M. LAIZER (K.n.y. MHE. TALALA BANA MBISE)** aliuliza:-

Je, ni lini Barabara ya Usa – Ngarenanyuki – Oldonyosambu na ile ya Tengeru – Mererani zitajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, barabara za *Usa River* – Engarenanyuki – Oldonyosambu ambayo ni km 57 na ile ya Tengeru hadi Mererani Km 32 ni barabara za Mkoa zinazohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Arusha. Barabara ya *Usa River* hadi Ngarenanyuki inayokwenda mpaka Oldonyosambu inapitia sehemu zenye umuhimu wa kilimo katika kilometa 7 za mwanzo kuanzia *Usa River* ambapo pamoja na mazao mengine wanalima kahawa kwa wingi. Baada ya kilometa 7 barabara hii inapitia ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Arusha kwa umbali wa kilometa 16 ambayo ni eneo muhimu kiutalii hadi Kijiji cha Ngarenanyuki. Kuanzia Ngarenanyuki hadi Oldonyosambu (km.34) barabara inapitia eneo muhimu la kilimo na mifugo tena.

Kutokana na umuhimu wa barabara hii, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara imekuwa ikifanyia matengenezo maalumu na yale ya kawaida kutegemea na Bajeti ya Serikali. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2004/2005 fedha kiasi cha shilingi milioni 120 zilitengwa na kutumika kugharamia ukarabati wa kilometa 12 za barabara hiyo hadi kiwango cha changarawe. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 36 zilitumika kugharamia matengenezo katika sehemu korofi (*Sport Improvement*).

Katika mwaka huu wa fedha 2005/2006 barabara hiyo itafanyiwa ukarabati kupitia Mfuko wa Kahawa (*STABEX*) kwa gharama ya *Euro* 216,000. Aidha, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili kuweka lami kilometa 2 kuanzia *Usa River* na shilingi milioni 50 zimetengwa ili kukamilisha ukarabati sehemu ya Engarenanyuki na Oldonyosambu kwa kiwango cha changarawe.

Barabara ya Tengeru – Mererani inaunganisha Jiji la Arusha na Mashamba ya maua pamoja na machimbo ya *TANZANITE* yaliyopo Mererani.

Serikali kila mara imekuwa ikitenga fedha za matengenezo ya barabara hiyo ili ipitike wakati wote. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 jumla ya shilingi milioni 42 zilitumika katika kugharamia matengenezo maalum yenye ukorofi wa kilometa 2 na matengenezo ya kawaida ya kilometa 20.

Katika mwaka huu wa fedha 2005/2006 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 90 kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ufupi sana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufunyu wa bajeti kwa sasa Serikali haiwezi kuzijenga barabara hizo kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, kama nilivyoeleza kwenye utangulizi, Serikali itajenga kilometa 2 za kutoka *Usa river* kuelekea Hifadhi ya Taifa ya Arusha kwa kiwango cha lami katika mwaka huu wa fedha 2005/2006 na sehemu zilizobaki zitaendelea kufanyiwa matengenezo kwa kiwango cha changarawe ili zipitike wakati wote.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya Engarenanyuki, Ngabobo, Oldonyosambu ni barabara inayounganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Kilimanjaro na inaunganisha Jimbo la Longido, Jimbo la Arumeru Mashariki, Jimbo la Arumeru Magharibi na Jimbo la Siha na inatumiwa na watu wengi sana. (*Makofi*)

(a) Je, isingefaa barabara hii Serikali ihudumie kuiweka lami au kama ni changarawe basi iwekwe haraka sana kwa sababu barabara hii haipitiki kwa sasa? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa barabara ya Tengeru – Mererani ni barabara inayotumiwa na wafanyabiashara wengi na sana sana Serikali inapita kila wakati kwa ajili ya usalama wa Mererani. Je, isingefaa iwekwe lami kuliko kuweka changarawe kila mwaka na kufanya gharama iwe kubwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba barabara hii ya *Usa River* – Engarenanyuki hadi Tengeru inaunganisha Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, lakini ukweli bado uko pale pale kwamba na kwamba inaunganisha Mikoa, kigezo kizuri lakini ukweli kwa fedha kwa kutokuweko ni ukweli ambao unaofanya barabara hii isitengenezwe kwa kiwango cha lami na ndiyo maana mwaka huu tunatengeneza Km 2 tu mpaka kwenye hifadhi ya wanyama pale, baada ya hapo tutaendelea kutengeneza kwa kiwango cha changarawe mpaka fedha zitakapopatikana. Tunajua kabisa umuhimu wa barabara hii.

Hali kadhalika barabara ya Tengeru - Mererani inapitika na watu wengi sana na sisi Serikali pamoja na wananchi wanataka kutumia sana barabara hiyo kwa lami. Lakini wananchi wakubali ukweli kwamba Serikali haiwezi kutengeneza kila barabara kwa kiwango cha lami kwa sababu haina fedha za kutosha. (*Makofi*)

Na. 266

**Barabara Kuu Iendayo Mutukula**

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE** aliuliza:-

Kwa kuwa, limejitokeza tatizo la ajali za mara kwa mara kwenye eneo la Rwamishenye Sokoni katika barabara kuu iendayo Mutukula na watu wengi wamekuwa wakigongwa na magari yapitayo kwa kasi kwenye eneo hilo:-

(a) Je, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, inachukua hatua gani za haraka kurekebisha kasoro hizo ili kuwanusuru watu wanaoitumia barabara hiyo licha ya hali hiyo kutolewa taarifa kwenye mamlaka zinazohusika kama *TANROADS*?

(b) Kwa kuwa, moja ya hatua tulizoomba zichukuliwe ni pamoja na kuweka matuta hasa ikizingatiwa idadi kubwa ya raia wakaao eneo hilo. Je, ni kitu gani kinachozuia kutekelezwa kwa pendekezo hilo, au ni hatua gani nyingine zichukuliwe ili utekelezaji ufanyike?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** ajilibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mutukula - Bukoba – Muhutwe yenye urefu wa kilometa 112 ni sehemu ya mtandao wa Barabara Kuu iliyopo kwenye Kanda Kuu ya

Usafirishaji ya Ziwa (*Lake Circuit*) inayounganisha Mkoa wa Kagera na nchi jirani ya Uganda pamoja na Mikoa ya Mwanza na Shinyanga.

Mradi wa barabara ya Mutukula – Muhutwe imegharimu shilingi 15.15 bilioni. Vile vile mradi umehusisha ujenzi wa barabara yenye upana wa mita 6.5 kwa ajili ya matumizi ya magari na mabega ya upana wa mita 1.5 kila upande, vituo vya basi, madaraja, makalvati ya chuma, mifereji ya zega na ya kawaida kwa ajili ya maji ya mvua, alama za barabarani kwa ajili ya kuelekeza watumiaji wa barabara, njia za mchepuko kwenda barabara nyingine na majumbani mwa wananchi (*accesses and junctions*) na mchepuko wa barabara ya lami yenye urefu wa mita 500 inayounganisha bandari ya *Kemondo Bay*. Ujenzi wa barabara hii katika kiwango hiki umezingatia usanifu uliokamilika mwaka 1996 na makubaliano ya kiwango cha ujenzi kati ya *ADB* na Serikali kwenye mkataba wa mkopo wa kugharamia mradi uliosainiwa mwaka 1997.Baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe kumekuwepo na ongezeko la shughuli za biashara kandokando mwa barabara, hususani sehemu za Rwamishenya, Bukoba Mjini. Shughuli hizi zimevuta watu wengi na hivyo kuongeza watumiaji wa barabara kuzidi makisio ya awali. Kutokana na hali hii umeonekana umuhimu wa kuboresha sehemu hizo kwa kujenga njia za watembea kwa miguu. Hivyo Wizara kupitia katika Bajeti ya mwaka 2005/2006 imepanga kurekebisha sehemu hizo ili kukidhi mahitahi ya usalama kwa watumiaji wa barabara katika sehemu hizo.

(b) Uboreshaji wa sehemu hizi unaoelezwa kwenye kifungu (a) hapo juu unakusudiwa kuweka alama zinazostahili kwa kuzingatia usalama wa watumiaji bila kukiuka sheria na kanuni za ujenzi wa barabara kuu nchini. Aidha, tunamshauri Mheshimiwa Mbunge kuhamasisha wananchi na watumiaji wa brabara kwa ujumla sheria zilizopo kuhusu utumiaji wa barabara kwa usalama ili kuepusha ajali kwa watu na mali zao na uharibifu wa vifaa/alama za barabarani.

(c) Kwa hatua zilizoelezwa hapo juu Wizara haioni sababu kwa hivi sasa kujenga matuta ambayo mara nyingi husababisha kuharibika kwa barabara hiyo mapema

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba mimi ninayezungumza ni Mbunge wa Bukoba Mjini, ambaye nafuatilia kwa umakini matatizo yanayotokea na hivi sasa ninavyozungumza watu watatu wamepata ajali mahali pale siku tatu zilizopitwa. Sasa kufuatana na majibu yake kwamba nihamasishe wananchi kujua namna ya matumizi ya barabara na anasema Serikali inataka kuboresha sehemu za watembea kwa miguu. (*Makofi*)

(a) Je, katika hali halisi pale ni soko na watu wanatoka upande mmoja kwenda mwingine. Sasa je, Waziri haoni bado kuna haja ya kuweka matuta ili kuweza kunusuru watu wanaotoka upande mmoja kwenda mwingine?

(b) Ni kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri, anataka kuniambia nini kuhusu barabara inayotoka Dar es Salaam kuja Dodoma ambako ukipita sehemu ya Mbande, sehemu ya Kibaigwa, sehemu ya Chalinze ina matuta, matuta hayo ni hali kwa barabara hiyo, lakini kwa Bukoba kwenda Mtukula siyo halali? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Wilfred Lwakatare Mbunge wa Bukoba Mjini, ambaye anafuatilia kwa makini kabisa masuala ya barabara hii. Katika jibu langu la awali nilieleza kwamba barabara ilifanyiwa usanifu mwaka 1996 mkataba ukaingiwa kujenga barabara hii mwaka 1997 *design* ile ya 1996 ilikuwa inaonyesha hakuna watu pale wanaofanya biashara kwa kiwango kile. Sasa baada ya ujenzi wa barabara hii kiwango cha watu kimeonzeka na sasa hivi tunachokifanya tumefanya *design* mpya ili kuweza kutoa njia za miguu huku na huku na kuweka alama ya kuvuka ambayo siyo lazima uweke tuta. Tutaweka alama za barabara kuonyesha kwamba hapo pana watu wanavuka kwa miguu. Juu ya Barabara ya Dar es Salaam hadi Dodoma kwamba ina matuta. Bado narudia unapofanya *design* ya barabara ndiyo maamuzi yanakuwa wakati huo na hili utaweza kuona hata barabara mpya ya Chalinze tumefanya maamuzi ya kuweka matuta wakati barabara inajengwa. Sasa hivi tukiweka matuta kwenye barabara hizi lazima tuharibu barabara kutokana na utengenezaji wake wa awali. Kwa hiyo, haya matuta anayoyaona yametengenezwa wakati barabara inatengenezwa.

Na. 267

**Barabara ya Galula – Namkukwe**

**MHE. PAUL E. NTWINA** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la barabara ya Galula – Namkukwe ni ufumbuzi wa maendeleo ya uchumi kwa wananchi waishio kwenye eneo hilo na kwa kuwa Serikali imekuwa ikipiga chenga kutatua tatizo la msingi juu ya barabara hiyo inayopata katika Vijiji vya Galula, Ilembo, Magamba, Iyovyo, Malangali, Mheza, Isanzu na Namkukwe licha ya ahadi nyingi zinazotolewa na Serikali ili kuondoa tatizo hilo;

(a) Je, ni lini tatizo hilo litaondolewa?

(b) Je, kwa nini barabara hiyo isiwekwe kwenye mikakati ya Wizara ili kumaliza malalamiko ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Barabara ya Galula – Namkukwe yenye urefu wa kilomita 46 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Ofisi ya Meneja wa Mkoa, wakala wa barabara Mkoa wa Mbeya. Barabara hiyo ni ya udongo na haina umbo la barabara iliyo wazi wala mpito (*alignment*) unaoeleweka. Hali hii imetokana na sehemu kubwa ya barabara hiyo kupita kwenye Bonde la Ziwa Rukwa ambalo wakati wa masika hujaa maji na kuharibu barabara. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali baada ya kuliona tatizo linaloikabili barabara hii, imeanza kutatua tatizo la msingi ambalo ni kuainisha mchepusho (*alignment*) muafaka wa barabara hiyo kutoka Galula hadi Namkukwe. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 Serikali ilitenga Shilingi milioni 30 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa barabara hiyo. Mhandisi Mshauri *inter-consult* wa Dar es Salaam alipewa kazi hiyo ambayo imekamilika tarehe 30/06/2005 na sasa Serikali inapitia mapendekezo ya Mhandisi Mshauri huyo.Sambamba na kazi hiyo ya upembezi yakinifu, Serikali ilitenga Shilingi milioni 50 katika mwaka wa fedha 2004/2005 kwa ajili ya matengenezo ya dharura ya sehemu korofi ili kuifanya barabara iendelee kupitika. Aidha Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo matengenezo ya sehemu korofi barabara iliyopo sasa ili kuhakikisha inapitika, wakati inatafuta fedha za kutosha kuijenga kwa kiwango cha changarawe kulingana na mapendekezo ya usanifu wa barabara hiyo uliofanywa na Mhandisi Mshauri. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Songwe kuwa, barabara ya Galula hadi Namkukwe ipo katika mikakati ya Wizara na ndiyo maana imefanyiwa upembuzi yakinifu ili kujua mahitaji halisi ya ukarabati kwa kiwango cha changarawe ambayo ni hatua muhimu ili kufanikisha ujenzi wa barabara ya kudumu itakayomaliza kabisa kero ya barabara hiyo.Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Paul Ntwina siyo tu kwa kuuliza maswali mengi ambalo sasa ni la nne juu ya barabara hii, bali pia kwa kuifuatilia Wizarani mara kwa mara. (*Makofi*)

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali kama ifuatavyo: Kwa kuwa juzi nilikuwa nafuatilia yale matengenezo ya ghafla na nikakutana na Wazee wa Magamba akiwepo Mwene, Ilanga na Mwenyekiti, Mzee Sasuni wamefurahisha sana na kazi hii ya Chama cha Mapinduzi kwa kuanza kutengeneza ile barabara na kwa kuwa barabara inakwenda kwa mwenzangu kule Jimbo la Mbozi;

(a) Je, kwa kuwa upembezi yakinifu umeishia pale Namkukwe unaweza ukaendelea kule kwa wenzangu ili tukafungua upande ule mpaka tukafika sehemu za Sumbawanga? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa yeye Naibu Waziri amesema kuwa mwanzo ilipita karibu na ziwa sasa imepelekwa juu kidogo ambapo kunapitika na upembuzi yakinifu umefanyika sasa kuna kata ambayo imetengwa kata ya Totowe, Je, zile km kama 10 Serikali inaweza baadaye ikashusha barabara kuelekea kwenye kata ile? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii imefanyiwa *alignment* kwa sehemu ile ya tuta, kwingine kule hakuna haja ya kufanya *alignment* ila ni kuendeleza barabara hiyo kwa matengenezo bora zaidi ambacho ni kitu kinachowezekana kufuatana na uwezekano wa kupata pesa za kutosha tu.

Mheshimiwa Spika, juu ya Kata iliyotengwa, Mheshimiwa Spika, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge angojee kwanza kukubaliwa kwa ushauri huu wa Mtaalam na Wizara na sasa hivi mtaalam anawakilisha hii na Wizara haijasema kama tumekabali ama sivyo na tutakapokuwa tumekubali basi tutachukua ushauri wake, ili tuone Kata ile iliyotengwa tutaisaidiaje. *(Makofi)*

Na. 268

**Ranchi ya Kongwa**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2002/2003 Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo alitoa ahadi ya kuifanya ranchi ya Kongwa ibakie kuwa mali ya Serikali na kuendelezwa kama eneo lisilokuwa na magonjwa na kwa kuwa ilitolewa pia ahadi kwa wananchi wanaozunguka ranchi hiyo kufaidika kwa kuwezeshwa kuwa na ufugaji bora:-

(a) Je, tangu ahadi hiyo ilipotolewa hapa Bungeni hadi leo wananchi jirani na ranchi hiyo wamewezeshwa vipi kuwa wafugaji bora?

(b) Je, ni lini ranchi hiyo itaanzisha Kitengo cha ujirani mwema kitakachoshughulikia mahusiano mema?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa Serikali iliamua kufanya Ranchi ya Kongwa kuwa sehemu isiyo na magonjwa *(disease free zone)* pamoja na kuwa kitovu cha mfano cha ufugaji bora.

Tangu ahadi hiyo itolewe hadi sasa wananchi wa vijiji vya Chamae, Nalimbo, Sejeli, Msingisa, Mtanana, Laikala na Chigwindwili ambavyo vinaizunguka Ranchi ya Kongwa wameshirikiana vizuri na Ranchi hiyo na wameweza kunufaika kama ifuatavyo:-

(i) Wafugaji wa vijiji hivyo jirani ya Ranchi na wafugaji wengine wa Mkoa wa Dodma wameuziwa madume 81 na mitamba 730 ya ng'ombe aina ya boran ambayo ni

mbegu bora ya ng'ombe wa nyama. Wafugaji hao kwa sasa wanafuga mifugo bora kuliko ilivyokuwa hapo awali.

(ii) Ranchi ya Kongwa imetoa huduma za ugani hususan ushauri wa kinga na tiba uundaji wa vikundi vya wafugaji na ufugaji wa kibiashara kwa vijiji vyote nilivyovitaja. Hata hivyo kwa vile vikundi hivi bado ni vidogo na havijawa na nguvu, nashauri wafugaji hawa waimarishe umoja wao ili waweze kupata huduma za mifugo kwa urahisi.Hili linawezekana, kama walivyofanya wenzao wanaoizunguka Ranchi ya Mzeri huko Handeni na Korogwe, ambapo wafugaji wadogo wameanzisha umoja wao. Umoja huo umewawezesha kupata huduma muhimu za utaalamu, madawa, mifugo na madume bora kutoka kwenye Ranchi ya Mzeri.

(iii) Ranchi ya Kongwa imetoa huduma za kijamii kwa wananchi wa vijiji hivyo kwa kuwaruhusu wananchi hao kutumia zahanati, shule ya msingi, duka na huduma ya majisafi, huduma ambazo zote zikko ndani ya ranchi na hivyo kuimarisha ujijrani mwema.

(b) Mheshimiwa Spika, Ranchi ya Kongwa ina uhusiano mzuri na vijiji jirani na uhusiano huo umeendelea kuimarika siku hadi siku. Katika kuimarisha ujirani huo, uongozi wa Wilaya ya Kongwa uliteua Kamati ya mseto mwaka 2004 inayojumuisha wenyeviti wa Serikali za vijiji, watendaji wa vijiji na maofisa watendaji wa kata zinazozunguka Ranchi ya Kongwa na watumishi watatu waandamizi wa Ranchi.

Kamati hii ambayo kwa sasa Mwenyekiti wake ni Afisa Mtendaji wa Kata ya Mtanana imepewa majukumu ya kuratibu na kutathmini mipango ya kimaendeleo kwenye vijiji vinavyozunguka maeneo ya ranchi, kutatua migogoro inayoweza kutokea kati ya ranchi na vijiji, kuelimisha wananchi kuhusu shughuli za ranchi na umuhimu wake kwa jamii inayoiizunguka.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imekwisha kukutana mara nne (4) tangu iteuliwe. Katika kipindi hicho Kamati imeweza kubainisha mipaka kati ya ranchi ya vijiji vinavyoizunguka.

Imesuluhisha matatizo ya uvamizi, imeelimisha wananchi kuhusu madhara na uharibifu wa mazingira yanayoweza kutokana na kuchoma moto ovyona hata kukata miti na imesaidia kuelimisha wananchi kuhusu umuhimuwa kutumia dawa za kuogeshea ili kuzuia magonjwa yanayoenezwa na kupe. Mpaka sasa vijiji vya Sejeli, Makawa, Matongolo na Matui vimenunua dawa za kuogesha mifugo yao kwa bei nafuu au kwa mkopo kutoka Ranchi ya Kongwa.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza. Lakini nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Pamoja na ushirikiano mwema uliyopo alioueleza Mheshimiwa Naibu Waziri na mimi ninaushuhudia kama ni kweli upo, hapo nyuma ilikuwa inaruhusiwa baadhi ya wananchi wa vijiji vya Chamai, Chingwingwili, Mtanana, Ndalibo, Msingisa na Ikala kulima pembezoni pembezoni mwa Ranchi hii ilikuwa

inasaidia kuondoa misitu na kuweza mazingira mazuri zaidi kwa ajili ya wafugaji. Wananchi wana ombi hilo kwamba muwaruhusu waendeleze na zoezi hilo Serikali inasemaje? La kwanza.La pili, Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri ameelezea kwamba wako wafugaji wanaofuga vizuri kwa kutumia vikundi vya ushirika huko Mzeri, Handeni na maeneo mengine. Je, Wizara itakubali kuwachukua viongozi wa vikundi vya wafugaji wa Kongwa wanaozunguka Ranchi ya Kongwa kwenda katika maeneo hayo ili waende kujifunza kutoka kwa wenzao ili waweze kuboresha ufugaji wao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, uzoefu umetuonyesha kwamba tunaporuhusu lile ambalo Mheshimiwa Mbunge analiomba watu waingie kidogo kwenye Ranchi, wengi wanapenda kuhalalisha, lakini inakuwa ni tabu sana kuja kuwatoa. Na pili, migogoro iliyokuwepo huko nyuma ni pamoja na ile tuliyokuwa tunawaruhusu kulima pembezoni. Kwa hiyo, mifugo ambayo ni mali ya Ranchi wanapoingia huwa wenyewe hawajui hizi ni nyasi zilizolimwa na binadamu au zimeota asili. Kwa hiyo, tatizo mojawapo lilikuwa ni hilo kwamba wanakwenda kulisha kwenye mazao. Kwa hiyo, kuzuia hilo na nadhani katika jitihada ambazo zimefanyika kwa kupitia hiyo Kamati walizuia hilo kwa misingi hiyo na mpaka sasa hivi wananchi wanaishi kwa amani na hawana migogoro yoyote. Hilo swali la pili, la kuwapeleka Mizeri kuangalia nina hakika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kuna Idara ya Mifugo.

Sasa ni vizuri tuwaombe kupitia Bunge lako Tukufu ili watenge mafungu ya kuhamasisha wananchi waende kwenye sehemu ambazo wanaweza kujifunza. Nina hakika Waheshimiwa Madiwani wanasafiri karibu nchi nzima kutoka Halmashauri mbalimbali kwenda kujifunza katika mafunzo ya namna hiyo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Ndugai aende awahamasishe ili waweze kufanya hilo nina hakika kwamba kwa kushirikiana na Ranchi wanaweza kutekeleza hilo na kufaidisha wananchi wanaozunguka. *(M akofi)*

Na. 269

**Mahitaji ya Maji - Himo Mjini**

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI** aliuliza:-

Kwa kuwa mji wa Himo kwenye Jimbo la Vunjo Mkoani Kilimanjaro unakua kwa haraka sana hasa baada ya kupewa hadhi kuwa *Himo Township Authority* hapo tarehe 1 Julai, 2003 na kwa kuwa mji huo hauna maji ya kutosha licha ya jitihada za kujenga tanki kubwa jipya kwa ajili ya maji ya bomba toka kwenye chemchem za Marangu Arisi na Marangu Kinukamori zenye maji mengi na mianguko mikali:-

(a) Je, Serikali ina mpango wowote wa kufikisha maji hayo kwenye mji wa Himo kabla ya awamu ya nne ya uongozi (2005 – 2015)?

(b) Kwa kuwa mtegemea cha nduguye hufa maskini na nchi kutegemea misaada ya nchi za nje hulemaa na kudumaa kimaendeleo. Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa

kwa ajili ya kuhakikisha kuwa maji yanafikishwa mjini Himo ili kupunguza adha kubwa inayoukabili mji huo, watu wake pamoja na wanyama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Meja Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mji wa Himo unapata huduma ya maji toka katika chemchem za Kero na Lyasongoro ambazo zipo Marangu. Hata hivyo maji hayo hayatoshelezi mahitaji ya wananchi kutokana na ukuaji haraka wa mji wa Himo.

Mpango wa Serikali uliokuwepo wa kuboresha huduma ya maji katika mji wa Himo kabla ya awamu ya nne ya uongozi (2005 – 2015) ulianza mwaka 2001/2002 kwa kuainisha vyanzo zaidi vya maji kwa ajili ya mji wa Himo. Vyanzo zaidi vilivyoainishwa ni chemchem za Tsiro na Shokoni pamoja na maji chini ya ardhi kwa kuchimba visima virefu. Hadi sasa ujenzi wa chemchem ya Tsiro umekamilika na tayari maji yamevutwa na yamewafikia wananchi wa Himo. Ujenzi wa chemchem ya Shokoni nao utaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, hatua zingine ambazo Serikali imechukua ni kuchimba kisima kirefu katika eneo la Himo-Njia Panda. Kwa hivi sasa kazi ya kufunga pampu kwenye kisima inaendelea na huduma ya maji itaanza kupatikana kabla ya awamu ya nne ya uongozi.

Hatua hizi zitaongeza upatikanaji wa maji katika mji wa Himo, kutoka mita za ujazo 2718 kwa siku hadi kufikia mita za ujazo 2890 kwa siku. Mahitaji ya mji wa Himo ni mita za ujazo 3000 kwa siku.

(b) Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba utekelezaji wa miradi yetu unategemea misaada pekee. Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya hutenga fedha katika Bajeti zake kwa ajili ya miradi mbalimbali na wananchi huchangia kulingana na uwezo wao. Pale inaponekana mahitaji ya mradi ni makubwa kuliko uwezo wa Serikali ama wananchi, Serikali huomba msaada kwa wafadhili mbalimbali. Utaratibu huu umetuwezesha kukamilisha miradi mingi na hivyo kuleta maendeleo nchini. Napenda kuitumia nafasi hii kuwashukuru marafiki na wafadhili wote wanaounga mkono juhudi hizi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini imekuwa ikitenga fedha kiasi cha shilingi milioni 10,000,000/= kila mwaka kati ya mwaka 2002/2003 na 2004/2005 kwa ajili ya uchimbaji wa kisima kirefu katika mji wa Himo. Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 30,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika mji wa Himo.

Na. 270

**Magofu ya Kaole**

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza:-

Kwa kuwa magofu ya Kaole huko Bagamoyo yanaonekana kutotunzwa ipasavyo kama mataifa mengine yanavyofanya kama nchi ya China katika Mkoa wa *Xian – Teracota Warrior* na kadhalika ambako mabaki hayo yamejengewa ili kuyalinda yasiharibike na kwa kuwa magofu hayo ni kivutio kikubwa cha watalii na kwa historia ya Tanzania:-

(a) Je, Serikali hadi sasa inatoa fedha kiasi gani ili kuyahifadhi magofu hayo kwa ajili ya vizazi vijavyo?

(b) Je, Serikali imewasiliana na mashirika ya kimataifa kama *UNESCO's World Heritage* na *The World Monuments Fund – New York* ili mabaki hayo yajengewe na yasiendelee kuharibika na kuomba utaalam zaidi?

(c) Je, kuna mipango gani mahususi ya kulinda na kujenga upya majengo ya zamani ya Bagamoyo kwa manufaa ya vizazi vijavyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Leonard N. Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye vipengele (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kwa kutambua na kuthamini rasilimali za urithi wa utamaduni ambazo Taifa letu limejaliwa kuzirithi. Kaole na Mji Mkongwe wa Bagamoyo ni baadhi tu ya rasilimali muhimu ambazo zinahifadhi utajiri mkubwa wa kihistoria pamoja na kuwa kivutio muhimu cha utalii wa urithi wa utamaduni.

Magofu ya Kaole yanahifadhi masalia ya makazi na makaburi ambayo yana umuhimu kihistoria na yenye asili ya ustaarabu wa Kiswahili yanayofahamika kuwepo tangu karne ya tisa (9) hadi leo hii. Mji Mkongwe wa Bagamoyo unahifadhi majengo kwa ajili ya makazi ambayo mengi yao bado yanatumiwa. Aidha, makazi haya yanakadiriwa kujengwa mnamo mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa (19). Kwa sababu ya umuhimu wa kihistoria ya mji wa Bagamoyo na pia kuhusishwa kwake na biashara dhalili ya utumwa. Mji huo umewekwa katika orodha ya awali ya urithi wa dunia kupitia Sherika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa *UNESCO.* Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Sweden ina mpango wa kuuorodhesha mji mkongwe wa Bagamoyo pamoja na Njia Kuu ya Kati ya biashaa ya utumwa na vipusa katika orodha ya urithi wa dunia.

Mheshimia Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maeneo kama magofu ya Kaole na mji mkongwe wa Bagamoyo ni mengi hapa nchini, hivyou si rahisi kuyaboresha yote kwa wakati mmoja.

Hata hivyo Wizara yangu inafanya jitihada za kuboresha maeneo ya kihistoria nchini kwa awamu na kwa fedha ambazo hutokana na vyanzo vyetu hapa nchini pamoja na kushirikisha wahisani mbalimbali. Katika kipindi cha fedha 2001/2002, 2002/2003 na 2003/2004 Wizara ilitenga kiasi cha shilingi 24,750,551/= kwa ajili ya kuboresha kituo na hali ya wafanyakazi katika kituo hicho.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na ushauri wa kuasiliana na Mashirika ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja kwa lengo la kuimarisha na kuboresha kituoi cha magofu ya Kaole. Hata hivyo, kwa kuwa waombaji wa misaada hiyo ni wengi, ni vigumu wote kupata misaada wanayoiomba. Mwaka 1999/2000, Serikali ya Sweden kupitia shirika lake la misaada la *SIDA* ilitoa msada wa fedha kwa ajili ya kuboresha makumbusho ya Kaole pamoja na maeneo yaliyo katika kituo cha magofu ya Kaole.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumthibitishia Mheshimiwa Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kuwa kituo cha magofu ya Kaole kimeboreka na kitaendelea kuboreshwa. Yeyote aliyewahi kutembelea Kaole miaka ya nyuma atakubaliana nami kuwa Kaole ya juzi si Kaole ya leo. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, ukarabati wa majengo ya kihistoria unahitaji utaalamu na fedha nyingi. Wizara yangu imewasiliana na inaendelea kuwasiliana na Wahisani katika azma yake ya kuyakarabati na kuyaboresha majengo ya zamani katika mji Mkongwe wa Bagamoyo. Mwaka 2001/2002, Serikali iliingia mkataba na Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la misaada la *SIDA* ili kuyaimarisha baadhi ya majengo wakati yakisubiri ukarabati mkubwa. Chini ya mkataba huo majengo saba yameimarishwa. Katika kipindi cha fedha cha 2004/2005, Serikali imeingia tena mkataba na Serikali ya Sweden. Katika mkataba huo Serikali ya Uswisi, itatoa ushauri na utaalamu pamoja na fedha kwa ajili ya kukarabati baadhi ya majengo ya kihistoria nchini yakiwemo baadhi ya yale ya Mji Mkongwe wa Bagamoyo.

Na. 271

**Uvuvi katika Ziwa Nyasa**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika maelezo yake imetamka wazi kuwa Ziwa Nyasa halina samaki kwa sababu maji yake hayana chakula cha kutosha kwa ajili ya samaki hivyo wavuvi huvua samaki na dagaa kidogo sana zinazowasaidia wao wenyewe kwa chakula na wala si kwa biashara:-

Je, katika hali ya namna hiyo ambayo ni ya uzalishaji duni, kuna sababu gani kwa Serikali kuendelea kuwalipisha wavuvi hao leseni za mitumbwi na nyavu?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, naomba kutoa maelezo ya awali yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nikijibu maswali ya Bunge Na.2596 na Na.2695 yaliyoulizwa na Mheshimiwa Dr. Luoga, nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa utafiti uliofanyika Ziwa Nyasa ulibaini kuwa Ziwa Nyasa halina samaki wengi ukilinganishwa na maziwa mengine kama Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Hii ni kutokana na sababu za kisayansi kwamba sehemu kubwa ya ziwa hili iko kwenye kina kirefu kinachozidi mita 250 ambako hewa safi ya oksijeni ni kidogo.Baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, rasilimali ya samaki katika Ziwa Nyasa ni ndogo ikilinganishwa na maziwa Victoria na Tanganyika. Matokeo ya utafiti uliofanywa kwa pamoja na nchi zinazomiliki Ziwa hilo yanaonyesha kuwa Ziwa Nyasa lina wastani wa tani za samaki 168,400 ambapo tani 33,300 zinaweza kuvuliwa kwa mwaka bila kuathiri rasilimali hiyo. Kati ya samaki hao kuna samaki wa mapambo *(ornamental fish)* wachache ambao huvuliwa na kuuzwa nje ya nchi. Takwimu pia zinaonyesha kuwa Ziwa Nyasa lina wastani wa wavuvi wasiopungua 6,000 kwa mwaka na vyombo vya uvuvi vipatavyo 2,000 na zaidi kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hilo Serikal imeweka utaratibu wa kukata leseni za vyombo na za uvuvi kama njia mojawapo ya kusimamia rasilimali ya samaki kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu.Pamoja na lengo la kuwa na uvuvi endelevu, mapato yanayotokana na uvuvi yanatumika katika kuendeleza shughuli za Halmashauri za Wilaya zinazolizunguka ziwa hilo. *(Makofi)*

Na. 272

**Ugonjwa wa Malaria kwa Watoto na Wajawazito**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa ili kupambana na ugonjwa sugu wa malaria na vifo kwa akina mama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano vinavyosababishwa na malaria sugu, Serikali imeamua kuwa na mpango kabambe wa kuuza vyandarua kwa makundi hayo kwa bei nafuu katika zahanati, vituo vya afya, na maduka:-

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika kusambaza vyandarua hivyo ili kuhakikisha kuwa vinawafikia walengwa na katika maeneo ambayo hakuna maduka makubwa yanayouza bidhaa hizo au vituo vya afya viko mbali, walengwa wananufaika vipi na huduma/mradi huo?

(b) Je, ni wanawake na watoto wangapi ambao wameshanufaika kutokana na mradi huo?

(c) Je, ni kwa kiwango gani taarifa za mradi huo zimewafikia walengwa hasa wale waliopo katika maeneo ambayo redio, magazeti na vyombo vingine vya habari havifikishi habari huko?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali imebuni utaratibu wa kuuza vyandarua vyenye viuatilifu kwa bei nafuu kwa makundi maalum ya walengwa yaani akina mama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Mpango huu hujulikana kama Hati Punguzo.Utaratibu unaotumika ni kuweka nyaraka za Hati Punguzo kwenye kliniki ambapo akina mama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano hupatiwa wanapohudhuria kliniki. Hati hizi zenye thamani ya sh.2,750/= hupelekwa kwa muzaji wa vyandarua na baada ya mhusika kuongeza fedha kidogo kufikia bei halisi ya chandarua hupewa chandarua. Kwa maeneo mengine mpango huu umechangia mama na mtoto sh.2,750/= kwa kila chandarua anachonunua.

(b) Mheshimiwa Spika, kati ya wanawake 428,155 waliolengwa kunufaika na mpango huu katika mikoa kumi iliyoanza utekelezaji, wanawake wajawazito 204,000 wamenunua vyandarua vyenye viuatilifu kwa kutumia Hati Punguzo.Vyandarua vya ziada vyenye viuatilifu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano vimeanza kutolewa mwezi Mei, 2005.

(c) Taarifa za mpango zimetolewa kwa njia mbalimbali zikiwemo radio, magazeti na televisheni. Hata hivyo kwa sehemu ambazo vyombo vya habari havikuweza kufika, sasa kama ngoma, maigizo na nyimbo zimetumika kufikisha ujumbe na taarifa za mpango wa Hati Punguzo.Aidha, elimu hii imetolewa kwa walengwa na watumishi wa Afya pale akina mama na watoto wanapohudhuria kliniki na vile vile mabango yaliyowekwa katika vituo vyote vya kutolea huduma. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, swali langu la kwanza ninaomba kufahamu kwa kuwa ni mikoa 10 tu

mpaka sasa ambayo imeingia mradi huo.  Je, Serikali haioni kwamba kutokueneza mradi huo katika mikoa yote katika nchi yetu ya Tanzania ni kuwakosea haki wanawake wengine ambao wako katika maeneo yakiwemo katika mradi huo?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa katika maeneo mengi ya nchi yetu na hasa katika Wilaya ya Songea zahanati ama huduma za afya zimekuwa zikitolewa na mashirika ya kidini.  kwa mfano, kule Isinga ambako ni mbali sana ni eneo la kijijini kabisa na maeneo mengine ya Wilaya hiyo.  Je, Serikal iko tayari sasa kushirikiana bega kwa bega na mashirika haya ya dini ili kuhakikisha maradi huu na vyandarua hivyo vinawafikia hawa akina mama na watoto kwenye maeneo hayo vijijini.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, mpango wowote hauwezi ukaanza nchi nzima kwa wakati mmoja.  Kutakuwa na matatizo ya utekelezaji , ndiyo maana kulikuwa na pilot project ya mpango huu katika wilaya mbili baada ya hapo kuonekana una manufaa ndiyo ukaanza kusambazwa katika mikoa hiyo 10 tunayozungumzia.  Bila shaka mpango huu utaendelea ktika mikoa iliyobaki hivi karibuni.

Pili, kuhusu kushirikiana na mashirika ya dini, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mpango huu hautabagua kituo chochote kinachotoa huduma hizi kwa sababu lengo ni kuwafikia akina mama wajawazito na watoto wote walio chini ya miaka mitano.  Kwa hiyo, mpango huu utashirikisha watoa huduma wa aina zote.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.  Kwa kuwa wananchi na hasa makundi haya maalum wanashukuru sana Serikali kwa kuweza kupewa ruzuku hiyo ili waweze kupata vyandarua na hivyo kupambana na malaria.  Lakini ni ukweli kwamba wale ambao wanaugua malaria na kufa ni wale akina mama au watoto wanaokaa na familia maskini kabisa na hivyo wanashindwa kupata hizo fedha za kulipia kwa kazi ambazo Serikali inaweza kutoa ruzuku.  Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ni vizuri basi ili kupambana na huu ugonjwa wa malaria ikaweza kutoa msaada ka Halmashauri zetu ili ziweze kutoa vyandarua bure kwa hawa akinamama ambao wako chini katika umaskini. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya wananchi wanashindwa kulipia hata hicho kidogo kilichobaki.  Nitoe mfano tu ni kwamba 2,750 vyandarua vingi kati ya vile vinavyouzwa vina gharama ya Shilingi 3,000. Kwa hiyo, mhusika anahaitajika kutoa 250 tu.  Jambo hili limefanywa kwa makusudi kabisa ili kuweza kuwapa njia wale ambao wananunua waweze kuwa na uchungu na chandarua husika.  Tatizo la kutoa vitu bure huenda likatumika vibaya.

Yapo baadhi ya maeneo ambayo vyandarua hivi vimetumika kwa kazi nyingine kwa mfano kuvulia na kadhalika.  Kwa hiyo, Sh.250/= au zaidi imewekwa makusudi ili kumfanya yule anayenunua aweze na kutumia kwa mahitaji ambayo yanatakiwa. *(Makofi)*

Na. 273

## *Bed Grant* kwa Hospitali ya *ST. Gasper*

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA** aliuliza:-

Je, tangu Januari, 2004 hadi Octoba, 2004, Serikali imekuwa ikitoa shilingi ngapi kila mwezi kama ruzuku ya *bed grant* kwa hospitali ya *ST. Gasper* na kwa vitanda vingapi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya *St. Gasper Itigi* inayomilikiwa na Kanisa Katoliki, Jimbo la Singida, inaendeshwa na Mapadre Katoliki wa Shirika la Damu Takatifu ya Yesu (*Precious Blood Fathers).*

Hospitali hii inatambuliwa na Wizara ya Afya kama Hospitali ya Shirika la Kujitolea (*Voluntary Agency Hospital*) na inatoa huduma bila faida. Kwa misingi hii Wizara yangu hutoa ruzuku ya vitanda (*Bed Grant*) na ruzuku ya mishahara kwa wafanyakazi wenye vyeti (*Staff Grant*) vinavyotambuliwa na Serikali. Hospitali hii ina vitanda 100 vinavyotambuliwa na Serilai na kila kitanda hulipiwa sh.30,000/= kwa mwaka. Katika kipindi cha Januari hadi Octoba, 2004 hospitali ya Mtakatifu Gasper ilipata ruzuku kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ruzuku ya mishahara shilingi 113,027,490/=. Ruzuku ya vitanda shilingi 3,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, ruzuku hii hutolewa ili kuzipunguzia mzigo wa uendeshaji hospitali hizi na kuziwezesha kutoa huduma kwa wananchi kwa bei nafuu.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa hii hospitali toka mwezi Novemba mwaka 2003 wakati walipokuwa wakifungua idara ya watoto yenye vitanda 156, kulitolewa taarifa na kulikuwa na mwakilishi wa Wizara ya Afya kwamba vitanda vya zamani vilikuwa 200 na vile vipya katika ile idara mpya ya watoto ni 156, kwa hiyo jumla ni 356.

Je, Serikali itakuwa tayari kurekebisha utoaji wa ruzuku ili ilingane na vitanda 356 na vile vile walipe yale mapunjo ambayo hawakuyatoa kwa mwaka uliopita?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA**: Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia vitanda ambavyo Serikali utoa ruzuku ni vitanda ambavyo tuna makubaliano kati ya Wizara ya

Afya na Hospitali husika. Si jumla ya idadi ya vitanda kwa hiyo hospitali zinapoongeza vitanda wanawajibu wa kuomba kibali Wizarani ili hatimaye tuelewane, maana wanaweza wakaongeza vitanda 150 lakini uwezo wa Serikali ukawa kulipia vitanda 50 tu. Kwa hiyo, ni vema uongozi wa hospitali hii wafike Wizara ya Afya ili kufanyike makubaliano ya idadi gani ya vitanda ambavyo Serikali itatoa ruzuku.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha sasa kuna matangazo, Kamati mbili zimepagiwa kufanya vikao vyake leo, ya kwanza ni Kamati ya Maliasili na Mazingira Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti anawaomba wajumbe wa Kamati wakutane saa tano asubuhi hii chumba Na. 432. Kamati ya pili ya Maendeleo ya Jamii Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane kuanzia saa tano asubuhi hii chumba Na. 231, hivyo ni vikao vya Kamati.

Kesho hakuna Semina iliyopangwa badala yake Mheshimiwa Joel Bendera anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kutakuwa ile mbio maalum kwa Waheshimiwa Wabunge zile. Mbio maalum kwa Wabunge *The VIP Five Kilometres less* ambayo itaanzia *Jamhuri Stadium,* Waheshimiwa Wabunge saa 12 kujiandaa na mbio hizo za kila mwaka ambazo huwa tunafanya kipindi hiki cha mkutano wa Bajeti. Mwisho wa matangazo Katibu endeleo na *Order Paper*.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006
### - Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO**: Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo na Ardhi inayohusu Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokea, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Sekta ya Ardhi na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kwa ushauri, maoni na maagizo ambayo yameisaidia Wizara yangu katika kuandaa mipango na bajeti kwa miaka mitatu iliyopita. Nalihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu ilitekeleza kikamilifu ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo. Naishukuru Kamati hiyo kwa kupitia na kuidhinisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa uchaguzi mkuu ambapo Watanzania watapata fursa ya kumchagua Rais mpya atakayeongoza nchi yetu kwa miaka mitano ijayo. Napenda kuchukua fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mhe. Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa umahiri wake aliouonyesha katika kuongoza na kusimamia mabadiliko ya kiuchumi na kijamii nchini katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu ambacho kinakaribia kumalizika.

Kutokana na jitihada hizo, Jumuiya ya Kimataifa, wakiwemo wafadhili na wawekezaji, wamekuwa na imani na nchi yetu na sasa wanatoa ushirikiano mkubwa katika Sekta za Maji na Mifugo ambazo Wizara yangu inazisimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza mwenzetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa na CCM, kwa kura nyingi, kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM. Pia nampongeza Mheshimiwa Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa kiti cha Urais, vile vile namponge Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar kwa kuteuliwa tena na CCM kuwa mgombea wa Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM. Nawataki wote ushindi wa kishindo cha Sunami katika uchaguzi mkuu ujao. Chaguo hilo ambalo limetokana na umakini wa mchakato uliowekwa na Chama cha Mapinduzi, limedhihirisha ukomavu wa demokrasia ndani ya Chama, na ni mfano unaostahili kuigwa na vyama vingine vya siasa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka huu, pia utawachagua Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu. Napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa busara na hekima zako zilizowezesha kuongoza na kusimamia kwa utulivu shughuli zetu za Bunge. Nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti kwa uongozi wao mzuri kwa kipindi chote.

Aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya kusukuma na kusimamia maendeleo ya wananchi. Pamoja na pongezi hizi, nawatakia mafanikio mema katika uchaguzi ujao, Inshaallah, tutakutana tena katika Bunge lijalo!

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu; Mheshimiwa Margreth James Bwana, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Theodos James Kasapila, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki; Mheshimiwa Frank Michael Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki; Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo; na Abu Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu, ndugu na wananchi wa majimbo waliyokuwa wanayawakilisha Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amin.

Naomba pia nitumie fursa hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali na mikasa mbalimbali katika kipindi cha mwaka 2004/2005, akiwemo Mhe. Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini; Mhe. Isaack Cheyo, Mbunge wa Jimbo la Bariadi Magharibi na Mheshimiwa Makongoro Nyerere, Mbunge wa Kuteuliwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mhe. Frederick Tluway Sumaye, Mbunge wa Hanang', kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa malengo na mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2005/2006. Nawapongeza pia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mhe. Dr. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni; na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mbunge wa Rombo, kwa hotuba zao zilizoainisha kwa makini mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Serikali katika mwaka 2005/2006. Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Brigedia Jenerali (Mstaafu) Hassan Ngwilizi (Mb); na Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo; kwa hotuba zao ambazo zimeanisha maeneo tunayoshirikiana katika kutoa huduma kwa wananchi. Pia, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha Hotuba zao ambazo zimetoa taswira za kisera na kiutendaji katika kufikia malengo yaliyoainishwa katika Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kutoa shukrani kwa wananchi wote, wakiongozwa na wawakilishi wao Waheshimiwa Wabunge na Madiwani, kwa michango yao ya hali na mali, katika kusimamia na kutekeleza programu za maji na mifugo. Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao katika kuboresha hali ya maisha yao.

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ya mawazo na ushauri wanaoutoa ndani na nje ya Bunge lako Tukufu kwa nia ya kuboresha utoaji huduma za maji na kuendeleza Sekta ya Mifugo hapa nchini. Aidha, napenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la uchaguzi la Monduli kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninaposhindwa kuwa nao kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa yanayonikabili.

Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu (1995 – 2005) Serikali ya Awamu ya Tatu ilidhamiria kupunguza umaskini kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na katika Mkakati wa Taifa wa Kuondoa Umaskini. Kwa kutambua umuhimu wa Sekta za Maji na Mifugo katika kuinua hali ya maisha ya wananchi na katika kuinua Pato la Taifa, Serikali iliendelea kuweka kipaumbele katika sekta hizo. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka kumi ya Serikali ya Awamu ya Tatu kwa Sekta za Maji na Mifugo ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji, Uboreshaji wa Huduma ya Maji Vijijini, Sera ya Maji ya mwaka 1991 ilianzisha utaratibu wa ushirikishwaji wa wananchi katika miradi ya maji. Sera mpya ya maji ya mwaka 2002 imesisitiza umuhimu wa wananchi kumiliki na kuiendesha miradi yao kwa kutumia vyombo huru vya watumiaji maji vijijini.

Serikali iliendelea kuhamasisha uundaji na uimarishaji wa vyombo hivyo vilivyoundwa kisheria kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma ya maji vijijini na katika miji mikuu ya wilaya na miji midogo. Utekelezaji wa sera hiyo umeleta mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na ongezeko la mwamko wa wananchi kumiliki na kugharamia uendeshaji wa miradi ya maji vijijini, ambapo hadi sasa:

(a) Kamati za maji 9,283 zimeundwa vijijini;

(b) mifuko ya maji 8,099 imeanzishwa ikiwa na jumla ya shilingi bilioni 1.07;

(c) jumuiya za watumiaji maji 77, makampuni ya maji 23, vyombo vya udhamini 3 na vikundi vya watumiaji maji 1,932 vimeundwa; na

(d) Miji 92 ya wilaya imetangazwa kuwa na mamlaka za maji na kati ya hizo, 62 zimeunda bodi za maji.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma ya maji vijijini hadi sasa, umefikia asilimia 53.56 ya wananchi waishio vijijini ikilinganishwa na asilimia 42 mwaka 1995. Kiwango hiki cha upatikanaji wa maji kimetokana na juhudi za Serikali ya Awamu ya Tatu kwa kushirikiana na Wananchi, Halmashauri za Wilaya na Wadau mbalimbali wa Sekta ya Maji katika kutekeleza programu na miradi mbalimbali ya maji kulingana na Sera iliyopo. Utafutaji wa maeneo ya kuchimba visima virefu na vifupi vya maji uliongezeka kwa mwaka kutoka wastani wa maeneo 131 mwaka 1995 hadi kufikia 1,033 mwaka 2004/2005. Katika kipindi hicho, jumla ya maeneo 4,963 yalipatikana kwa ajili ya kuchimba visima virefu na vifupi.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuimarisha na kuendeleza shughuli za uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa, mwaka 1997 Serikali ilianzisha Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa. Uwezo wa kuchimba visima kwa mwaka umepanda na kufikia visima 450 mwaka 2005 ikilinganishwa na visima 50 mwaka 1998. Katika kipindi hicho, jumla ya visima virefu 4,007 vilichimbwa vikiwa na uwezo wa kutoa maji mita za ujazo milioni 176 kwa mwaka na kujenga mabwawa madogo 14 ya maji vijijini na kukarabati mabwawa 78.

Katika juhudi za kueneza teknologia ya uvunaji wa maji ya mvua, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo na kuhamasisha utumiaji wa teknolojia rahisi ya uvunaji wa maji ya mvua. Idadi ya matangi ya kuvuna maji ya mvua vijijini iliongezeka kutoka 2,875 mwaka 1995 hadi 5,325 mwaka 2004. Uboreshaji wa Huduma za Maji Mijini, katika jitihada za kuinua ubora wa huduma ya maji mijini, mwaka 1994 Serikali ilianzisha Idara za Maji Mijini. Mwaka 1997 marekebisho ya Sheria ya Usambazaji Maji Mijini Na. 8 ya mwaka 1981 yalifanywa ili kuunda Bodi za Maji Mijini. Huduma za maji mijini zilianza kutolewa na Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini chini ya Bodi za Maji katika Makao Makuu ya Mikoa 18, ambapo hadi sasa, huduma hiyo inatolewa katika mamlaka 19 baada ya kuanzisha Mamlaka ya Mji wa Babati, makao makuu ya Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na haya yafuatayo;

(a) Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa mijini kutoka asilimia 68 mwaka 1995 hadi 74 kwa sasa;

(b) Uzalishaji wa majisafi kwa mamlaka zote 19 uliongezeka kutoka lita bilioni 71 mwaka 1995 hadi lita bilioni 110 mwaka 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 38;

(c) Ukusanyaji wa mapato umeongezeka kutoka shilingi bilioni 0.4 mwaka 1995 na kufikia shilingi bilioni 17.9 mwaka 2004/2005 (Kiambatanisho Na. 1); na

(d) Kati ya mamlaka 19 za maji, mamlaka 8 zinajitegemea kimapato na kulipia gharama za uendeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma ya uondoaji wa majitaka, Serikali iliendelea kukarabati na kupanua mifumo ya majitaka kwenye miji ya Dar es salaam, Morogoro, Tanga, Moshi, Arusha, Mwanza, Tabora, Dodoma, Mbeya na Iringa. Huduma katika miji hiyo imeongezeka kutoka asilimia 2 mwaka 1995 hadi kufikia asilimia 17 mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kuziimarisha Mamlaka za Maji Mijini ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma za majisafi na uondoaji majitaka na hivyo kuziwezesha kujitegemea. Tangu mwaka 1995 hadi sasa, Serikali imekarabati na kupanua miundombinu ya majisafi katika miji mikuu 19 ya Tabora, Arusha, Moshi, Tanga, Morogoro, Singida, Shinyanga, Musoma, Bukoba, Kigoma, Iringa, Sumbawanga, Mtwara, Songea, Dodoma, Mbeya, Lindi, Mwanza na Babati.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria Kwenda Miji ya Kahama na Shinyanga, katika kutimiza azma ya muda mrefu ya kutumia maji ya Ziwa Victoria kutatua uhaba wa maji katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Singida, Tabora na Dodoma, mwaka 2003 Serikali ya CCM ilianza ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama na Shinyanga. Mradi huo ambao utagharimu takribani shilingi bilioni 176 utakapokamilika utawanufaisha wananchi milioni moja pamoja na mifugo yao katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, Menejimenti ya Rasilimali za Maji kulingana na Sheria ya maji Na. 42 ya mwaka 1974, na marekebisho Na. 10 ya mwaka 1981, katika kipindi cha 1995 hadi mwaka 2005 Serikali iliendelea kuimarisha mfumo wa kusimamia rasilimali ya maji kimabonde, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na haya yafuatayo; Hadi kufikia mwaka 2005, ofisi za mabonde zilikuwa zimefunguliwa katika mabonde yote 9 ya maji nchini ikilinganishwa na ofisi 2 tu zilizokuwepo mwaka 1995.

Mheshimwa Spika, nchi yetu inachangia na nchi nyingine rasilimali ya maji ambayo yapo kwenye mabonde ya maji ya kimataifa yakiwemo maziwa ya Victoria, Nyasa, Tanganyika, Natron, Jipe na Ziwa Chala. Pia, rasilimali za maji katika mito ya Kagera, Ruvuma, Songwe na mto Umba. Katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005, Serikali iliendelea kushirikiana na nchi tunazochangia matumizi ya maji kupitia

majadiliano ili kuweka utaratibu shirikishi na endelevu wa kusimamia matumizi na kutunza rasilimali ya maji katika mabonde husika.

Aidha, nchi yetu ilishiriki kuandaa itifaki za ushirikiano wa matumizi ya maji na nchi za *SADC,* Nile Basin Initiative na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Ziwa Victoria. Miongoni mengine ni pamoja na kutayarisha Sera ya Maji ya Jumuiya ya *SADC* na kukamilisha maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Bonde Shiriki la Mto Songwe ambapo miradi 12 imebuniwa.

Mheshimwa Spika, kumekuwepo na ongezeko la ufanisi katika kufuatilia na kuratibu ubora wa maji kwa lengo la kulinda afya za wananchi. Katika mwaka 1995 sampuli za maji zilizopimwa ubora kwa mwaka ni 750 wakati mwaka 2004 sampuli za maji zilizopimwa ubora zimeongezeka na kufikia 2,707. Aidha, maabara za maji za Ubungo, Mwanza, Mbeya na Tanga zilishindanishwa na maabara nyingine ulimwenguni, ambapo maabara zetu nchini zilionyesha majibu yanayokubalika kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo katika Sekta ya Maji, kuanzia mwaka 1995 hadi 2004/2005, Serikali iliendelea kukiimarisha Chuo cha Maji cha Rwegalulila. Katika kipindi hicho, jumla ya wanafunzi 272 wa fani ya ufundi sanifu na 635 wa ufundi stadi walihitimu. Aidha, hadi Juni 2005, chuo kilikuwa na wanafunzi 451 sawa na asilimia 84 ya uwezo wake, ikilinganishwa na wanafunzi 300 sawa na asilimia 55 ya uwezo wake mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo, Uzalishaji wa Mifugo na Mazao ya Mifugo Serikali ya Awamu ya Tatu iliendelea kuimarisha huduma za mifugo, ikiwa ni pamoja na udhibiti wa magonjwa ya mifugo, utafiti, ugani, usambazaji wa maji na uboreshaji wa malisho pamoja na kuuisha Sheria mbalimbali zikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo; Sheria ya usimamizi wa utoaji wa huduma za mifugo Na. 16 ya mwaka 2003 ambayo inaunda baraza kuu la huduma ya mifugo ambalo linasimamia utoaji huduma za mifugo. Sheria ya Magonjwa ya Na. 17 ya mwaka 2003 ambayo inasimamia uzuiaji wa kuenea kwa magonjwa ya mifugo nchini. Sheria ya maziwa Na. 8 ya mwaka 2004 ambayo inaunda bodi ya maziwa inayosimamia na yenye uendelezaji wa maziwa nchini. Kutokana na juhudi hizo, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005, idadi ya mifugo iliongezeka kama ifuatavyo:

(a) Ng'ombe kutoka milioni 15.6 hadi milioni 18.5;
(b) Mbuzi kutoka milioni 9.2 hadi milioni 13.1;
(c) Nguruwe kutoka milioni 0.43 hadi milioni 1.2; na
(d) Kuku wa asili kutoka milioni 27 hadi milioni 30.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuzalisha na kusambaza ng'ombe na mbuzi bora wa maziwa kwa wafugaji nchini, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kusambaza ng'ombe na mbuzi kwa wafugaji wadogo. Hii ni pamoja na utaratibu uliobuniwa wa "Kopa ng'ombe lipa ng'ombe" na "Kopa mbuzi lipa mbuzi". Kutokana na utaratibu huo, ng'ombe bora wa maziwa waliongezeka kutoka 212,334 mwaka 1995 hadi ng'ombe 434,760 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 100.

Mbuzi wa maziwa nao waliongezeka kutoka 13,500 mwaka 1995 na kufikia 75,761 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 460.

Mheshimiwa Spika, asilimia 97 ya ng'ombe tulionao nchini ni wa asili wenye ukosaafu mdogo ambao huzalisha chini ya wastani wa lita 500 za maziwa kwa mwaka ikilinganishwa na lita kati ya 2,500 na 3,000 kwa ng'ombe chotara. Serikali imeendelea kukiimarisha kituo cha madume cha *Usa River (NAIC)* cha kuzalisha mbegu bora kwa ajili ya kuongeza ukosaafu wa ng'ombe wa asili. Kituo hicho kwa sasa kina madume 22 yenye uwezo wa kuzalisha mbegu dozi 230,000 kwa mwaka ikilinganishwa na dozi 190,000 mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi za Serikali ya Awamu ya Tatu katika kuinua ubora wa mifugo, kukabiliana na magonjwa ya mifugo na kuongeza tija, kumekuwepo na ongezeko la kuridhisha la uzalishaji wa mazao ya mifugo kama ifuatavyo:

(a) Uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita milioni 555 hadi bilioni 1.38 sawa na ongezeko la asilimia 149;

(b) Uzalishaji wa nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku uliongezeka kutoka tani 244,000 hadi 378,509 sawa na ongezeko la asilimia 55;

(c) Uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka milioni 380 hadi bilioni 1.8 sawa na ongezeko la asilimia 374; na

(d) Uzalishaji wa ngozi za ng'ombe uliongezeka kutoka vipande milioni 1.323 hadi milioni 1.6 sawa na ongezeko la asilimia 21.

Mheshimiwa Spika, usindikaji wa mazao ya mifugo ni njia ya kuiwezesha Sekta ya Mifugo kuchangia zaidi katika Pato la Taifa na kuongeza faida kwa wafugaji kwa kuwa mazao yao yanapata soko la uhakika ndani na nje. Wizara yangu, inaratibu na kuhamasisha usindikaji wa maziwa kwa lengo la kuongeza thamani na muda wa matumizi ya zao hilo. Kwa sasa kuna viwanda 22 ambavyo vina uwezo wa kusindika lita 510,000 za maziwa kwa siku tofauti na ilivyokuwa kabla ya mwaka 1995 ambapo kulikuwa na viwanda 7 vyenye uwezo wa kusindika maziwa lita 310,000.

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kuongeza usindikaji wa zao la maziwa. Hatua hizo ni pamoja na:

(a) Kuondoa kodi kwa vifungashio vyote vya maziwa;
(b) Kuweka kodi ya asilimia 20 ya maziwa kutoka nje (*suspended duty);*
(c) Kuweka kodi ya *VAT* ya asilimia 20 ya maziwa kutoka nje;
(d) Kuweka kodi ya asilimia 15 ya maziwa yanayoingizwa nchini (*import duty);*
(e) Kuanzisha wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa;

(f) Kuanzisha sheria mpya ya maziwa ya mwaka 2004 inayounda Bodi ya Maziwa inayosimamia uendelezaji wa Sekta ndogo ya maziwa nchini; na
(g) Kuanzisha programmu ya unywaji maziwa mashuleni.

Mheshimiwa Spika, katika kupanua soko la ndani la unywaji wa maziwa na utumiaji wa mazao yatokanayo na maziwa, kuanzia mwaka 1999 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ilianzisha maadhimisho ya "Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa" mwezi Juni kila mwaka. Maadhimisho hayo yanalenga kuinua kiwango cha unywaji wa maziwa kwa mtu kwa mwaka kufikia viwango vya kimataifa. Nchi yetu ina uwezo wa kuzalisha nyama ya kutosheleza soko la ndani na ziada kuuzwa nje. Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika viwanda vya kusindika nyama. Hali hiyo imeongeza idadi ya viwanda vya nyama kutoka 1 mwaka 1995 hadi kufikia 6 mwaka 2004. Serikali ilikamilisha ujenzi wa machinjio ya kisasa katika Manispaa ya Dodoma kwa madhumuni ya kuzalisha nyama safi kwa ajili ya matumizi ya wakazi wa Manispaa hiyo na vitongoji vyake pamoja na Manispaa ya Morogoro na Jiji la Dar es Salaam.

Serikali pia, ilikamilisha ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ukataji Nyama Dodoma na kukibidhi kwa Mamlaka ya Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) kwa uendeshaji. Chuo hiki kitatoa mafunzo kwa wataalam 74 kila mwaka katika ngazi ya ufundi sadifu wa kuchinja na kutengeneza mazao mbalimbali yatokanayo na nyama.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, ulaji wa mazao ya mifugo kwa mtu kwa mwaka uliongezeka kama ifuatavyo:-

(a) Unywaji wa maziwa umeongezeka kutoka wastani wa lita 20 hadi lita 39 kwa mtu kwa mwaka, sawa na asilimia 95;
(b) Ulaji wa nyama umeongezeka toka kilo 5 hadi kilo 11 kwa mtu kwa mwaka, sawa na asilimia 120; na
(c) Ulaji wa mayai umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 270 kutoka wastani wa mayai 14 hadi mayai 53 kwa mtu kwa mwaka.

Ongezeko la ulaji wa mazao ya mifugo ni ishara muhimu katika ukuaji wa uchumi wa Taifa na ongezeko la kipato cha wananchi. Lengo ni kufikia unywaji wa maziwa wa lita 50, ulaji wa nyama kilo 14 na mayai 75 kwa mtu kwa mwaka ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Masoko ya Mifugo, katika jitihada za kuboresha soko la mifugo, kuanzia mwaka 1995 hadi sasa, Serikali iliendelea kukarabati na kujenga miundombinu ya masoko ya mifugo ambapo ilijenga na kukarabati vituo vidogo 90 vya kupumzikia mifugo, vituo 15 vya kukagulia mifugo, minada 56, sehemu za kupakilia na kupakulia mifugo 10 na kukarabati mabehewa ya kusafirishia ng'ombe 60.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imewekeana mikataba mbalimbali ya kibiashara na inayo nafasi kubwa ya kufanya biashara ya mifugo na mazao yake na nchi nyingine za Afrika kupitia Mpango wa *NEPAD;* Marekani kupitia Mpango wa *AGOA;* Jumuiya ya

Afrika Mashariki; na Jumuiya ya nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika (*SADC*). Kutokana na fursa hizo, kuanzia mwaka 2002 nchi yetu imeanza kuuza mifugo hai nje ambapo ng'ombe 4,796 na mbuzi 1,996 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.39 waliuzwa nchini Comoro. Aidha, minada 7 ya mipakani imejengwa kwa lengo la kuimarisha biashara ya mifugo na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, Mbegu Bora za Malisho na Huduma za Maji kwa Mifugo,ili kuendeleza ufugaji bora nchini, ni muhimu kuhakikisha kwamba mbegu bora za malisho zinapatikana karibu na wafugaji. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, uzalishaji wa mbegu bora za malisho uliongezeka kutoka tani 1.25 hadi tani 14.5 ikiwa ni ongezeko la zaidi ya mara kumi. Aidha, uzalishaji wa hei nchini uliongezeka kutoka marobota 20,000 mwaka 1995 hadi kufikia marobota 120,000 mwaka 2004/2005 ikiwa ni ongezeko la asilimia 500.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1997, Serikali ilianza tena kuchangia uchimbaji na ukarabati wa malambo kwa ajili ya kuipatia mifugo huduma za maji. Hadi sasa, uchimbaji wa malambo 236 kati ya 316 yaliyochangiwa na Serikali umekamilika katika Wilaya 63 za mikoa 18.

Mheshimiwa Spika, Uwezeshaji Wananchi na Huduma za Ugani, kuanzia mwaka 1995 Serikali ilikuwa na mkakati wa kubinafsisha mashamba yake makubwa ya mifugo ili kutoa nafasi kwa wananchi kuyamiliki na kuyaendesha kwa ufanisi zaidi. Mkakati huo uliboreshwa ili kugawa Ranchi za Taifa kwenye maeneo ya hekta 4,000 na yale yaliyokuwa ya *DAFCO* kwenye maeneo ya hekta 50 kwa ajili ya kumilikisha wananchi wafuge kibiashara. Hadi sasa, Serikali imekamilisha upimaji na ugawaji wa mashamba ya *NARCO* ya Mkata, Dakawa, Mzeri, Usangu na Kalambo kwa wawekezaji 48. Ranchi za Kitengule, Misenyi, na Kikulula *Complex* zilizopo Mkoani Kagera na Uvinza Kigoma zimepimwa katika ranchi ndogo 73 na kutangazwa katika vyombo vya habari ili kupata wananchi watakaokuwa tayari kuwekeza. Taratibu za kuwamilikisha wawekezaji hao zinaendelea. Katika kipindi hicho, jumla ya wafugaji 44,450 walipatiwa huduma za ugani kwa kutumia mbinu mbalimbali za mafunzo ya ufugaji bora ikiwemo kuanzisha mashamba darasa ya mifugo 160. Aidha, Serikali ilitoa mafunzo juu ya uandaaji mipango shirikishi ya shughuli za ugani kwa wataalam 1,707 wa ngazi za Wilaya, Kata na Vijiji. Ziara za mafunzo zilitolewa kwa wataalam 1,090 wa ugani.

Mheshimiwa Spika, Sheria za Mifugo, ili kuendesha kikamilifu shughuli za Sekta ya Mifugo sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinatumika. Kutokana na mabadiliko ya Sera za Kitaifa na Kimataifa, Serikali imefanyia mapitio sheria mbalimbali za Sekta ya Mifugo ili ziendane na mabadiliko ya sera hizo. Sheria zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu ni pamoja na:-

(a) Sheria ya Usimamizi wa Watoaji Huduma za Mifugo Na. 16 ya mwaka 2003, ambayo inaunda Baraza Kuu la Huduma ya Mifugo ambalo linasimamia utoaji huduma za mifugo;

(b) Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya mwaka 2003, ambayo inasimamia uzuiaji wa kuenea kwa magonjwa ya mifugo nchini; na

(c) Sheria ya Maziwa Na. 8 ya mwaka 2004, ambayo inaunda Bodi ya Maziwa inayosimamia uendelezaji wa maziwa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kudhibiti Magonjwa ya Mifugo, Serikali inandaa na kutekeleza mipango ya kudhibiti magonjwa ya mifugo ya milipuko na yenye kuleta madhara makubwa kwa wafugaji na Taifa kwa ujumla. Magonjwa hayo ni pamoja na Sotoka, Homa ya Mapafu, Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Mdondo, Homa ya Nguruwe na Kichaa cha Mbwa. Magonjwa mengine ambayo madhara yake siyo makubwa na ambayo yanatibiwa au kukingwa kwa urahisi hushughulikiwa kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa Sotoka uliojitokeza nchini mwaka 1981 na kudhibitiwa lakini ulijitokeza tena mwaka 1997. Kampeni za chanjo ziliendelea kuanzia wakati huo ambapo hadi kufikia mwaka 1998 nchi yetu ilitangaza kutokomezwa kwa ugonjwa huo. Kuanzia kipindi hicho, nchi yetu imekuwa ikifuatilia mwenendo wa ugonjwa huo kulingana na maelekezo ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (*OIE*). Tanzania imetambuliwa rasmi kuwa imetokomeza ugonjwa huo mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 Serikali ilitangaza kuwa ugonjwa wa Homa ya Mapafu ni janga la kitaifa baada ya kuenea karibu mikoa yote nchini. Tokea kipindi hicho, Serikali ilinunua na kusambaza chanjo dozi milioni 20.24 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 ambapo jumla ya ng’ombe milioni 16.3 walichanjwa. Udhibiti wa ugonjwa huo umeonyesha mafanikio hasa katika wilaya za Mbozi, Ileje, Kyela na Rungwe ambazo hazijaripoti matukio ya ugonjwa huo kwa miaka mitatu mfululizo. Aidha, idadi ya matukio ya ugonjwa huo imepungua kutoka matukio 3,904 mwaka 2001/2002 hadi matukio 70 mwaka 2004/2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupe wanaeneza magonjwa mbalimbali ya mifugo ikiwemo ugonjwa wa Ndigana Kali ambao husababisha asilimia 43.7 ya vifo vya mifugo vitokanavyo na magonjwa ya kupe.

Aidha, Ndigana Baridi husababisha vifo kwa asilimia 16.6, Maji Moyo asilimia 6.5 na Kukojoa Damu asilimia 5.2. Hasara zinazotokana na magonjwa ya kupe zinakisiwa kufikia Dola za Marekani milioni 64.7 kwa mwaka. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

(a) Kujenga majosho mapya 118 na kukarabati 969 na kuyakabidhi vikundi vya wafugaji na kati ya hayo, Sekta binafsi ilikarabati majosho 47;

(b) Kupungua kwa vifo vya ng’ombe kutokana na ugonjwa wa Ndigana kutoka asilimia 40 hadi 10 kwa ng’ombe waliochanjwa**;**

(c) Kutengeneza ramani mpya za mtawanyiko wa kupe na magonjwa yaenezwayo na kupe ili kutoa kipaumbele kwa maeneo yaliyoathirika zaidi; na

(d) Kuchunguza usugu wa kupe kwa madawa ya kuogeshea ili kutoa ushauri kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, asilimia 40 ya nyanda za malisho zina tatizo la mbung'o hivyo kuzuia ufugaji katika maeneo hayo. Kuanzia mwaka 1995, Serikali iliandaa mpango wa kudhibiti ueneaji wa mbung'o kwa kutumia teknolojia ya kuhasi madume ya mbung'o yanayozalishwa nchini.

Mafanikio yaliyopatika ni kutokomeza mbung'o katika kisiwa cha Zanzibar ambapo kwa kutumia uzoefu huo, juhudi za kutokomeza mbung'o zimeendelezwa katika maeneo ya Karagwe, Bukoba, Pangani, Handeni, Serengeti, Kigoma Vijijini, Kibondo, Kasulu na Kisiwa cha Mafia.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Utoaji Huduma za Afya ya Mifugo, Serikali inasimamia utoaji wa huduma za afya ya mifugo kwa lengo la kuhakiki viwango na ubora wa utoaji wa huduma za mifugo, ikizingatiwa kuwa huduma hizo sasa zinatolewa na sekta binafsi.

Kati ya mwaka 1995 na 2005, Serikali imesajili madaktari wa mifugo 161 na kufanya idadi ya madaktari wa mifugo waliosajiliwa kuongezeka kutoka 334 mwaka 1995 hadi 517, sawa na ongezeko la asilimia 58.8. Kati ya hao, madaktari 225 wameajiriwa na Serikalini na taasisi za umma na waliobakia 292 wapo katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Utafiti wa Mifugo, Serikali imeendelea kufanya utafiti na uzalishaji wa ng'ombe aina ya Mpwapwa ambao wamethibitika kuwa na sifa ya kuhimili magonjwa na wana uwezo wa kutoa maziwa na nyama kwa wingi. Lengo ni kuongeza idadi ya mifugo hiyo katika kituo cha utafiti cha Mpwapwa ili ifikie majike zaidi ya 1,000 ili kuweza kuzalisha mitamba ya ziada kwa ajili ya kuwauzia wafugaji. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 1995, ng'ombe hao wameongezeka kutoka 290 na kufikia 890 mwaka 2004. Serikali imeendelea kutengeneza na kusambaza chanjo ya ugonjwa wa mdondo kwa majaribio kwa lengo la kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo. Hadi sasa, jumla ya chanjo dozi milioni 16 zimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji. Udhibiti wa ugonjwa huo umefanikiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya chanjo hiyo inayostahimili joto. Tathmini katika maeneo ambayo chanjo hiyo imetumika, imeonyesha kupungua kwa vifo vya kuku kutokana na ugonjwa huo kutoka asilimia 90 hadi asilimia 5.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo katika Sekta ya Mifugo, Serikali inaendesha vyuo 5 vya mafunzo ya mifugo vya Morogoro, Mpwapwa, Tengeru, Buhuri na Madaba kwa lengo la kupata wataalamu wenye ujuzi na mbinu za kuhudumia wafugaji kwa ufanisi zaidi. Pia, vyuo hivyo hutoa mafunzo kwa wafugaji kwa lengo la kuwapa mbinu za

ufugaji bora. Kuanzia mwaka 1996 vyuo vya mafunzo ya mifugo hatua kwa hatua vilianza tena kutoa mafunzo kwa ufanisi zaidi na hadi kufikia mwaka 2004/2005 vyuo hivyo vilikuwa na jumla ya wanafunzi 770 sawa na asilimia 90 ya uwezo wa vyuo hivyo tofauti na mwaka 1996 vilipokuwa na jumla ya wanafunzi 32 tu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2004/2005, vyuo vya mifugo viliendela kutoa mafunzo mbalimbali ya muda mfupi kwa wafugaji kuhusu mbinu za ufugaji bora na utunzaji wa mazingira. Wafugaji waliopatiwa mafunzo vyuoni waliongezeka kutoka 515 mwaka 1995 hadi 1,434 mwaka 2004/2005. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, jumla ya wafugaji 10,952 walipatiwa mafunzo katika vyuo vya mifugo.

Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2000, ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 ililenga kuboresha Sekta za Maji na Mifugo ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Lengo ni kuzifanya Sekta hizo zichangie zaidi katika vita dhidi ya umaskini kulingana na dhamira ya Serikali ya CCM ya Awamu ya Tatu. Mikakati, malengo na programu za kuendeleza Sekta za Maji na Mifugo katika kipindi cha miaka 5 kuanzia Novemba 2000 hadi Juni 2005 zilizingatia kikamilifu Mwongozo wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imetekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2000, kama inavyoainishwa kwenye muhtasari ufuatao:

(i) Mheshimiwa Spika, sasa kuhuasu sekta ya Maji:

(a) Kuboresha mtandao wa kufuatilia mwenendo wa maji juu na chini ya ardhi kwa kukarabati vituo 179 na kuchunguza maeneo ya kuchimba visima ambapo maeneo 3,082 yalipatikana;

(b) Kujenga skimu mpya za maji 99 na kukarabati 293;

(c) Kuchimba visima virefu vya maji 1,389 na kukarabati 1,045;

(d) Kuchimba visima vifupi vya maji 3,932 na kukarabati 9,014;

(e) Kuhamasisha uundaji wa Kamati za Maji Vijijini ambapo kamati 2,639 zilianzishwa na Mifuko ya Maji 7,254 imefunguliwa ikiwa na shilingi bilioni 1.3;

(f) Kujenga mabwawa madogo 14 na kukarabati mabwawa 78;Kujenga matangi 815 ya uvunaji maji ya mvua;

(g) kuongeza uzalishaji wa majisafi mijini kwa lita bilioni 13.2 na hivyo kuongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 63.1 mwaka 2000 hadi asilimia 74 mwaka 2005;

(h) Kuongeza ukusanyaji wa mapato kwenye Mamlaka za Maji Mijini kwa shilingi bilioni 11.6;

(i) Kuziwezesha Mamlaka 8 kati ya 19 kupanda na kufikia daraja A ambazo sasa zinajitegemea kifedha;

(j) Kuanza ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama na Shinyanga;

(k) Kuanza ukarabati mkubwa wa miundombinu ya majisafi na uondoaji majitaka Jijini Dar es Salaam na miji ya Kibaha na Bagamoyo;kuongeza usajili wa wanafunzi kutoka 272 mwaka 2000 hadi 319 katika Chuo cha Maji Rwegarulila, sawa na asilimia 57 ya uwezo wake.

(ii) Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu sekta ya Mifugo:

(a) kuongeza idadi ya ng'ombe kutoka milioni 16.7 mwaka 2000 hadi milioni 18.5 mwaka 2005; mbuzi kutoka milioni 11.8 hadi milioni 13.1; kondoo kutoka milioni 3.5 hadi milioni 3.6; nguruwe kutoka milioni 0.6 hadi milioni 1.2; na kuku wa asili kutoka milioni 27 hadi milioni 30;

(b) Kuongeza uzalishaji wa nyama kutoka tani 323,000 mwaka 2000 na kufikia tani 378,509 mwaka 2004;

(c) Kuongeza uzalishaji wa mayai kutoka milioni 600 mwaka 2000 hadi bilioni 1.8 mwaka 2004;

(d) Kuongeza uzalishaji wa maziwa kutoka lita bilioni 0.8 hadi bilioni 1.2 mwaka 2004;

(e) Kuongeza uzalishaji wa ngozi ya ng'ombe kutoka vipande milioni 1.3 hadi milioni 1.6;

(f) kuongeza ng'ombe bora wa maziwa kutoka 363,504 mwaka 2000 hadi 434,760 mwaka 2004 na mbuzi wa maziwa kutoka 72,448 mwaka 2000 hadi 75,761 mwaka 2004;

(g) Kumilikisha wawekezaji 48 mashamba 5 ya NARCO na kupima mashamba 4 katika ranchi ndogo 73;

(h) Kuhuisha Sheria ya Maziwa; Sheria ya Magonjwa ya Mifugo na Sheria ya Huduma za Mifugo;

(i) Kujenga machinjio ya kisasa na Chuo cha Ukataji Nyama katika Manispaa ya Dodoma;

(j) Kujenga na kukarabati malambo 280;

(k) Kutokomeza ugonjwa wa sotoka;

(l) Kununua nakusambaza chanjo milioni 20.2 ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu;

(m) Kujenga majosho 38 na kukarabati 714;

(n) Kuchanja ng'ombe 190,000 dhidi ya ugonjwa wa Ndigana Kali;

(o) Kupunguza maambukizi ya Ugonjwa wa Nagana kutoka 14,406 hadi 4,520;

(p) Kuchanja kuku milioni 5.4 katika vijiji 255 dhidi ya ugonjwa wa mdondo;

(q) Kuchanja mbwa 173,000 dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa;

(r) Kusajili madaktari wa mifugo 102 na vituo vya afya ya mifugo 47;

(s) Kutafiti na kuongeza ng'ombe 463 aina ya Mpwapwa toka 370 waliokuwepo mwaka 2000 na kufikia 833;

(t) Kutengeneza na kusambaza kwa majaribio dozi 256,000 za chanjo ya Kimeta na 245,000 za Chambavu; na

(u) kuongeza usajili wa wanafunzi kutoka 206 mwaka 2000 hadi 722 mwaka 2005 sawa na asilimia 84 ya uwezo wa vyuo vya mifugo.

(iii) Mheshimiwa Spika, sasa ni maeneo ya jumla:

(a) Kutoa mafunzo kwa watumishi 960;

(b) Kupandisha vyeo kwa mserereko watumishi 1,500 wa Wizara na 2,318 wa Halmashauri za Wilaya na Miji; na

(c) Kusimamia masuala ya Jinsia, UKIMWI na Rushwa.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Milenia na Utekelezaji wa Mkukuta, kama nilivyoeleza hapo awali, Dira ya Taifa ya mwaka 2025 inatekelezwa kwa mikakati ya muda mfupi na muda wa kati. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali imeridhia Malengo ya Kimataifa ya Millenia *(MDGs)* ambayo kwa Sekta ya M aji ni pamoja na kupunguza kwa asilimia 50 idadi ya watu wasiokuwa na huduma ya majisafi na salama na wasiokuwa na huduma ya usafi wa mazingira ifikapo mwaka 2015.

Aidha, kwa upande wa Sekta ya Mifugo, lengo ni kuchangia kupunguza kwa asilimia 50 ya wananchi wasiokuwa na chakula cha kutosha na wenye kipato cha chini ya dola moja kwa siku ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Malengo ya Milenia, Serikali imeandaa Mkakati wa Kuinua Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) kama mkakati wake wa muda mfupi. Katika mkakati huo, Sekta ya Maji imepewa jukumu la kuwapatia wananchi majisafi na salama karibu na makazi yao.

Upatikanaji wa majisafi utawawezesha wananchi kutumia muda wao katika kazi nyingine za kuinua kipato chao na kupunguza maambukizi ya magonjwa yatokanayo na maji yasiyo salama. Aidha, upatikanaji wa maji kwa wingi na kwa ubora unaotakiwa ni kigezo muhimu katika kuendeleza ukuaji wa sekta nyingine zikiwemo nishati, kilimo, maliasili, viwanda na utunzaji wa mazingira. Sekta ya Mifugo nayo imepewa majukumu ya kuinua kipato cha mfugaji pamoja na kuhakikisha usalama wa chakula, kutoa ajira na kuliingizia Taifa fedha za kigeni. Utekelezaji wa majukumu hayo kutaongeza mchango wa Sekta ya Mifugo katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, malengo ya MKUKUTA kwa Sekta ya Maji ni kuongeza idadi ya wananchi wanaopata majisafi na salama kutoka asilimia 53.5 ya sasa hadi 65 ya wananchi waishio vijijini na kutoka asilimia 74 ya sasa hadi 90 ya wananchi waishio mijini ifikapo mwaka 2010. Kwa upande wa Sekta ya Mifugo, lengo la MKUKUTA ni kuongeza ukuaji wa sekta hiyo kutoka asilimia 2.7 ya sasa hadi asilimia 9 kwa mwaka ifikapo mwaka 2010 ili kuweza kupunguza umaskini kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2004/2005 na Malengo ya Mwaka 2005/2006 kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu, utekelezaji wa MKUKUTA unaanza mwaka huu wa fedha. Naomba sasa kutoa maelezo ya utekelezaji wa mwaka 2004/2005 na mpango wa mwaka 2005/2006 kwa Sekta za Maji na Mifugo ambao umezingatia malengo ya MKUKUTA, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji, Hali Halisi ya Sekta ya Maji, nchi yetu imebahatika kuwa na rasilimali za maji za kutosha. Kiasi cha maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu na kinachopatikana kwa sasa ni kilomita za ujazo 89 sawa na mita za ujazo 2,700 kwa mtu kwa mwaka. Vyanzo vikubwa vya rasilimali hiyo ni maziwa yenye eneo la jumla ya kilomita za mraba 60,000 na vingine ni mito, maeneo oevu, chemchemi, mabwawa na maji chini ya ardhi. Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 60 ya eneo la nchi yetu ni kame kutokana na kupata mvua chini ya milimita 800 kwa mwaka hivyo kusababisha upungufu wa rasilimali ya maji nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa mvua, kwa kipindi cha miaka 4 mfululizo kuanzia 2000 hadi 2004, vyanzo vingi vya maji vimekuwa vikipungua. Mathalan, kina cha chini cha maji katika Bwawa la Mtera katika mwaka 2000 kilifikia mita 690.7 na mwaka 2004 kilishuka zaidi na kufikia mita 688.4. Upungufu wa maji

kwenye mabwawa ya Mtera, Kihansi, Nyumba ya Mungu na Pangani umeendelea kuathiri uzalishaji umeme.

Mheshimiwa Spika, kulingana na takwimu zilizopo inakadiriwa kwamba karibu watu bilioni 1.1 duniani kote hawana huduma ya majisafi na salama, na kati ya hao watu milioni 300 wako katika Bara la Afrika. Pia, inakadiriwa kwamba watu wapatao bilioni 2.4 duniani hawana huduma ya uondoaji majitaka na usafi wa mazingira na kati ya hao watu milioni 540 wapo Barani Afrika. Kutokana na hali hiyo, inakadiriwa kwamba asilimia 50 ya watu katika nchi masikini duniani wanaugua magonjwa yanayosababishwa na huduma duni za majisafi na uondoaji wa majitaka.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama imefikia asilimia 53.56 ya wananchi waishio vijijini (Kiambatanisho 3), na asilimia 74 ya wakazi waishio mijini. Aidha, upatikanaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka mijini umeendelea kuwa asilimia 17 ya wakazi wote. Hata hivyo, bado tuna safari ndefu, lakini naamini kuwa sera na mwelekeo tulionao ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maji, Wizara yangu ina jukumu la kuhakikisha kuwa Sera ya Maji inasambazwa na inaeleweka vizuri na wadau ili kufanikisha utekelezaji wake. Mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Sera ya Maji ya 2002 ni pamoja na:-

(a) Ushiriki wa wananchi katika kupanga, kutekeleza, kuendesha na kugharamia huduma ya maji;

(b) Maamuzi na utekelezaji utafanyika katika ngazi ya chini zaidi iwezekanavyo;

(c) Ushiriki wa sekta binafsi katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maji;

(d) Kuainisha majukumu ya Serikali, Halmashauri za Wilaya, sekta binafsi, wananchi, na wadau wengine;

(e) Wananchi waonyeshe nia ya kuhitaji huduma ya maji, watamiliki miradi yao na watashirikishwa katika ngazi zote za utekelezaji wa miradi; na

(f) Kutoa kipaumbele katika kutunza mazingira na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, mbinu zinazotumika katika kusambaza sera hiyo ni pamoja na warsha, makongamano, semina, mikutano ya hadhara, vipindi vya redio, luninga, kuchapisha na kusambaza vipeperushi na makala magazetini. Aidha, Wizara yangu imekuwa ikitumia tovuti ya Serikali na katika mwaka 2004/2005 imeanzisha tovuti yake *(www.maji-mifugo.go.tz),* ambayo inatumika kama njia muhimu ya mawasiliano kati ya Wizara na Wadau katika kueneza Sera na taarifa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wiki ya Maji,siku ya Maji Duniani huadhimishwa tarehe 22 Machi kila mwaka kulingana na Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Na. A/RES/47/193 la mwaka 1992. Nchi yetu huitumia siku hiyo kama kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Maji ambayo huanza tarehe 16 hadi tarehe 22 Machi. Maadhimisho hayo yanafanyika katika ngazi zote kuanzia kijiji hadi Taifa na yanalenga kutoa nafasi kwa wadau wa Sekta ya Maji kupata ufafanuzi kuhusu Sera ya Maji na tathmini ya utoaji wa huduma hiyo. Maudhui ya Wiki ya Maji kwa mwaka 2005 yalikuwa "Maji kwa Uhai". Maadhimisho hayo kitaifa yalifunguliwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Mheshimiwa Alhaj Ali Hassan Mwinyi.

Katika maadhimisho hayo, yalifanyika maonyesho yanayohusu utoaji wa huduma ya maji. Pia, warsha na semina ziliendeshwa katika wilaya zote za Mkoa wa Mtwara. Mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho hayo alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ambaye alizindua mradi wa maji wa mkoa wa Mtwara na Lindi unaotekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali yetu na Japan.

Mheshimiwa Spika, Kongamano la Mwaka la Wataalam wa Maji, njia nyingine ya kuhakikisha kwamba Sera ya Maji inaeleweka na kuhamasisha utekelezaji wake ni kwa kubadilishana uzoefu na kujifunza mambo mapya yanayojitokeza katika Sekta ya Maji. Kila mwaka Wizara yangu hufanya kongamano la wataalam wa maji nchini. Katika mwaka 2004/2005 Kongamano hilo lilifanyika mjini Tabora kuanzia tarehe 19 hadi 22 Januari 2005 ambapo wataalam wa maji nchini walipata fursa ya kujadili masuala mbalimbali yanayohusu mabadiliko ya usimamizi na uendeshaji katika Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Mwaka wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini, Wizara yangu iliandaa na kuendesha mkutano wa mwaka wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini kama njia mojawapo ya kueneza Sera pamoja na kutathmini utendaji kazi wa Mamlaka hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za maji mijini. Katika mwaka 2004/2005, mkutano huo, ambao huwakutanisha watendaji wakuu wote wa Mamlaka za Maji Mijini, ulifanyika kati ya tarehe 26 – 28/5/2005 katika Manispaa ya Tanga. Msukumo wa mkutano huo ulikuwa kuandaa mipango ya Mamlaka kuelekea katika kujitegemea kikamilifu na kuanza kwa matumizi ya Sheria ya *EWURA* ambayo itasimamia utoaji wa huduma za maji.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Maji, Wizara yangu imekamilisha uandaaji wa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Maji utakaotumika katika utekelezaji wa Sera ya Maji. Mkakati huo unaainisha majukumu mbalimbali ya wadau ikiwa ni pamoja na muundo wa kisekta, mabadiliko ya sheria na uwekezaji unaohitajika ili kufikia malengo ya muda wa kati na mrefu.

Aidha, Mpango wa Kutekeleza Mkakati huo unakamilishwa na utaainisha Programu ya Uendelezaji na Usimamizi wa Rasilimali za Maji; na Programu ya Uendelezaji wa Huduma za Maji Mijini na Vijijini. Katika kutekeleza Sera ya Maji, Wizara kwa sasa inazipitia upya sheria zinazohusu matumizi na utunzaji wa rasilimali za maji pamoja na utoaji wa huduma za maji ili ziendane na mabadiliko ya sera na

kuoanisha na sheria za sekta nyingine zikiwemo ya Afya, Kilimo, Mazingira, Maliasili na Nishati kwa lengo la kuondoa migongano.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya Rasilimali za Maji, Wizara yangu inalo jukumu la msingi la kuchunguza na kutathmini wingi na ubora wa maji juu na chini ya ardhi ili kubaini na kufuatilia mwenendo wa vyanzo vya maji kwa ajili ya maendeleo ya sekta mbalimbali. Takwimu na taarifa zinazopatikana huwezesha Serikali kuchukua hatua za tahadhari ili kuepukana na madhara ya kiafya, uharibifu wa mazingira, mafuriko, ukame, upungufu wa chakula na maji ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inasimamia mtandao wa vituo vya kufuatilia mwenendo wa maji kwenye mito, maziwa na mabwawa; hali ya hewa; kiasi cha mvua; na mwenendo wa raslimali za maji chini ya ardhi. Mtandao huo una jumla ya vituo 216 vya kufuatilia mwenendo wa maji kwenye mito, maziwa na mabwawa, 65 vya hali ya hewa, 93 vya kupima kiasi cha mvua na 40 vya kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu na taarifa za mwenendo wa rasilimali za maji nchini zinaonyesha kuwa kuna kiwango kikubwa cha maji juu ya ardhi kwa ajili ya umwagiliaji katika Ziwa Victoria, Tanganyika, Rukwa, Nyasa na katika maeneo ya mito mikubwa ya Rufiji, Ruvu, Wami, Malagarasi, Songwe, Kagera na Ruvuma. Aidha, taarifa hizo zinaonyesha kuwa kuna uwezo mkubwa wa kuzalisha umeme katika mito hiyo.

Katika mwaka 2004/2005, vituo 7 vya kufuatilia mwenendo wa maji kwenye mito vilifanyiwa ukarabati katika mabonde ya Wami/Ruvu (4), Pangani (1), Rufiji (1) na Ziwa Nyasa (1). Vilevile, vituo 20 vya hali ya hewa vinavyojiendesha vyenyewe vilifanyiwa matengenezo na kati ya hivyo, 12 vipo katika Bonde la Rufiji na 8 Pangani.

Aidha, upatikanaji wa maji chini ya ardhi unatofautiana katika maeneo mbalimbali kutegemeana na tofauti za kijiolojia. Kutokana na baadhi ya maeneo ya nchi yetu kuwa kame, vyanzo vya maji chini ya ardhi ambavyo hutoa maji kwa kuchimba visima ndivyo njia ya uhakika ya kuwapatia wananchi maji ili kukidhi matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kuimarisha mtandao wa vituo vya kukusanya takwimu na taarifa mbalimbali za rasilimali za maji kote nchini. Jumla ya shilingi milioni 487.5 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa vituo 38 vya kufuatilia mwenendo wa maji kwenye mito, maziwa na mabwawa, 25 vya kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi na 13 vya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo muhimu itafanyika katika mabonde sita ya Mto Ruvuma, Ziwa Nyasa, Rukwa, Tanganyika, Victoria na Bonde la Kati. Aidha, vituo 35 vya kukufuatilia mwenendo wa maji juu ya ardhi na hali ya hewa vitakarabatiwa katika Bonde la Mto Wami/Ruvu kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilikamilisha ufunguaji wa ofisi za mabonde yote tisa na kuanzisha Bodi za Mabonde hayo zenye wawakilishi kutoka Halmashauri za Wilaya na makundi ya watumiaji maji. Bodi hizo zimepewa uwezo kisheria wa kukusanya mapato yatokanayo na matumizi ya maji. Aidha, Bodi hizo zilikusanya jumla ya shilingi milioni 440.5 kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanzisha mfumo huo wa usimamizi wa rasilimali za maji kimabonde, bado kuna matatizo ya upungufu wa wataalam, vitendea kazi na kutoeleweka vizuri na baadhi ya wadau na hivyo kuathiri ufanisi wa usimamizi wa rasilimali za maji nchini. Mwaka 2004/2005 Wizara yangu iliendelea kuziimarisha ofisi za mabonde kwa kuzipatia vitendea kazi, wataalam na kukarabati ofisi ili kuzipa uwezo wa kusimamia kikamilifu matumizi bora ya rasilimali za maji katika mabonde husika.

Katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kuziimarisha ofisi za mabonde matatu ya Mto Ruvuma, Ziwa Nyasa na Tanganyika kwa kufanya ukarabati wa ofisi katika miji ya Mtwara, Tukuyu na Kigoma na kuzipatia vitendea kazi na wataalam.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa asilimia 43.4 ya rasilimali za maji katika nchi yetu ni maji-shiriki. Nchi hizo nazo zinakabiliwa na maendeleo duni na matatizo ya uharibifu wa mazingira hali inayosababisha kila nchi kubuni mikakati ya kuinua maisha ya wananchi wake. Hii ni changamoto kwetu katika usimamizi na uendelezaji wa raslimali hizo.

Katika mwaka 2004/2005 Wizara yangu iliendelea na majadiliano na nchi zilizopo kwenye bonde la Mto Nile kuhusu uanzishaji wa mfumo wa ushirikiano unaozingatia uwiano mzuri wa matumizi endelevu ya rasilimali za maji shiriki. Aidha, mwezi Novemba 2004 Bunge lako Tukufu liliridhia Itifaki ya Maendeleo Endelevu ya Bonde la Ziwa Victoria kwa ajili ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Itifaki hiyo ni mwongozo wa matumizi bora ya rasilimali katika Bonde hilo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Tanzania, kwa kushirikiana na Kenya na Uganda, iliendelea kutekeleza Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria. Mradi huo hivi sasa uko katika hatua za mwisho za utekelezaji ambapo taarifa juu ya hali ya ubora wa maji ya Ziwa hilo itatolewa. Waheshimiwa Wabunge wa Kamati za Bunge za nchi za Kenya, Tanzania na Uganda, zinazosimamia Mazingira na Maliasili, walipata fursa ya kukagua mradi huo. Wabunge hao wameisifu sana Tanzania kwa kuwa na kiwango cha kazi kinachofanywa na wataalam wetu katika kutekeleza Mradi wa Hifadhi Mazingira Ziwa Victoria.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea na utayarishaji wa taarifa ya utekelezaji wa mradi na kuendelea na utayarishaji wa mradi kwa ajili ya awamu ya pili chini ya uratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Itifaki ya *SADC* iliyoridhiwa na Bunge lako Tukufu Mwezi Agosti 2003 juu ya Maji-Shiriki, vitaundwa vyombo vya ushirikiano

vitakavyosimamia rasilimali za maji shiriki. Mwaka 2004/2005 Wizara yangu iliendelea kutekeleza Mkakati wa miaka mitano wa kuweka mazingira mazuri ya kutumia rasilimali za maji katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

Aidha, Serikali za Tanzania na Msumbiji zimeanza taratibu za kuunda Kamisheni ya Bonde la maji shiriki la Mto Ruvuma kutumia msaada wa dola za Marekani 200,000 kutoka Serikali ya Switzerland. Pia, Wizara imeshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mpango wa kuendeleza Bonde la Mto Zambezi kwa kuandaa taratibu za kuridhia Mkataba wa kuanzishwa kwa Kamisheni ya Bonde hilo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 Wizara yangu iliendelea kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya vyanzo vya maji nchini. Jumla ya vyanzo vya maji 1,050 katika mabonde ya Mto Rufiji, Pangani, Wami/Ruvu na Mabonde ya Maziwa ya Victoria, Nyasa, Rukwa na Bonde la Kati vilikaguliwa kwa lengo la kuhakiki ubora wa maji. Aidha, viwanda 59 na migodi mikubwa 8 ilikaguliwa na ushauri wa kitaalamu wa kurekebisha mifumo ya majitaka ulitolewa ili kuimarisha udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji. Pia, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, wananchi walihamasishwa juu ya hifadhi ya vyanzo na matumizi bora ya maji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kuwaelimisha watumiaji wa maji kuwa na hati za kutumia maji ili kudhibiti, kusimamia matumizi bora ya maji na kuboresha ukusanyaji wa mapato. Mwaka 2004/2005, jumla ya hati mpya 170 za haki ya kutumia maji zilitolewa. Aidha, katika kuhakikisha majitaka yanayorudishwa kwenye vyanzo vya maji ni salama, taratibu za kisheria za utoaji wa hati za utupaji wa majitaka zipo katika hatua ya mwisho ya kukamilishwa. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kudhibiti uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kukagua viwanda 89 na migodi 10. Aidha, hati mpya 440 za haki ya kutumia maji zitatolewa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha unakuwepo ufanisi wa kutosha katika maabara za maji nchini ikilinganishwa na maabara nyingine ulimwenguni, maabara za Ubungo, Mwanza, Mbeya na Tanga zilishiriki kwenye mpango wa ushindani chini ya mradi unaopima uwezo na ufanisi wa upimaji maji *(Inter Laboratory Comparison).* Matokeo yalionesha kwamba upimaji wa sampuli kwenye maabara yetu ya maji unatoa majibu yanayokubalika kimataifa. Katika mwaka 2004/2005, maabara 15 zilizopo nchini zilipatiwa madawa na vifaa ili kuzipa uwezo wa kuhakiki hali ya ubora wa maji kwenye vyanzo mbalimbali. Jumla ya sampuli za maji 2,707 zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi wa kemikali na vijijidudu. Matokeo ya uchunguzi huo yalionyesha kwamba asilimia 90 ya sampuli zilizopimwa zilionekana kuwa safi na salama kwa matumizi ya binadamu. Wizara pia, ilifanya ukaguzi wa madawa ya kusafisha maji ili kujua kama yanakidhi viwango vinavyokubalika na kugundua kuwa yana ubora unaokubalika.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea na ufuatiliaji wa ubora wa maji katika vyanzo na kuziimarisha maabara za maji kwa kuzipatia wataalam, madawa, vifaa na usafiri.

Mheshimwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kutafuta vyanzo vipya vya maji chini ya ardhi hususan katika maeneo kame kwa lengo la kuchimba visima vya maji. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu iliendelea kutafuta vyanzo vipya vya maji katika maeneo mbalimbali.

Kati ya maeneo 1,033 yaliyopimwa, jumla ya maeneo 597 yalionekana kuwa yanafaa kwa ajili ya kuchimba visima vya maji katika mikoa ya Arusha (44), Dar es Salaam (338), Dodoma (17), Kilimanjaro (25), Kigoma (33), Lindi (4), Manyara (24), Mtwara (18), Mwanza (7), Pwani (48), Morogoro (10), Rukwa (27), Shinyanga (43), Singida (25), Tabora (2) na Tanga (20). Kati ya hayo, maeneo 275 yalichunguzwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kufanya uchunguzi katika maeneo mbalimbali nchini ili kubaini maeneo yanayofaa kuchimba visima virefu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara yangu iliendelea kusimamia kwa karibu uchimbaji wa visima vya maji nchini ili kuhakikisha kwamba taratibu za kitaalam zinafuatwa. Jumla ya visima 571 vilivyochimbwa vilisajiliwa. Kati ya visima hivyo, 434 vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na 137 vilichimbwa na makampuni binafsi. Pia, vibali vya kufanya utafiti na kuchimba visima vya maji kwa kampuni nne vilitolewa baada ya kuhakiki na kuridhika kuwa zina sifa zinazokubalika.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ni muhimu katika utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini nchini. Hadi sasa, asilimia 53.56 ya wananchi waishio vijijini wanapata huduma hiyo karibu na makazi yao.

Katika mwaka 2004/2005 Wizara yangu iliendelea kuandaa miradi ya usambazaji maji katika maeneo ambayo hayana huduma ya kuridhisha. Uchunguzi na usanifu wa awali wa miradi ya maji ulifanyika kwenye miji ya Geita na Tarime. Aidha, usanifu wa kina wa mradi wa Mbwinji utakaohudumia maeneo ya Masasi na Nachingwea umeanza na utakamilika mwezi Septemba 2005. Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, ilifanya uchunguzi na ilikamilisha usanifu wa kina wa miradi ya maji kwenye vijiji 33 katika Mkoa wa Lindi na vijiji 31 katika Mkoa wa Mtwara. Pia, upembuzi yakinifu wa miradi ya maji vijijini umeanza katika wilaya zote katika mikoa ya Mwanza na Mara.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan imegharamia uchunguzi wa awali ili kubainisha vyanzo vya maji katika vijiji 49 vya mkoa wa Pwani na mitaa 42 ya mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi vijijini imekamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 122.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itafanya usanifu wa miradi ya maji kwa ajili ya miji ya Muleba, Urambo, kijiji cha Nyakagomba (Geita) na awamu ya pili ya

mradi wa Chalinze ambapo mkataba wa maelewano umefikiwa na *BADEA* kuhusu utekelezaji wa awamu hiyo. Aidha, upembuzi yakinifu utaendelea katika mikoa ya Mwanza na Mara.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Ukarabati wa Miradi ya Maji Vijijini, Wizara yangu iligharamia ukarabati wa miradi 34 ya maji ya Libango, Tukuyu mjini, Magugu, Kayenze, Nassa, Rombo vijijini, Sikonge, Kitomanga, I*windi Group,* Majengo/Eslalei na Chato. Miradi mingine ni Nyang'hanga/Kabila, Elerai/Longido, Nzega Vijijini, Njombe, Mpanda, Kwanyage, Kamachumu, Mwisanga, Tunduma, Chunya vijijini, Mafia vijijini, Makete, *HTM*, Makondeko, Tarime mjini, Korogwe mjini, Misasi, Kilulu, Mto wa Mbu, Mugango/Kiabakari , Gabimori, Hedaru na Lotima.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu imetenga shilingi bilioni 2.477 kwa ajili ya kukarabati miradi 65 ya maji katika maeneo ya Kayenze (Ilemela), Nassa, Sikonge, Kitomanga (Lindi), *Iwindi Group* (Mbeya Vijijini), Chato (Biharamulo), Tunduma, Makete, Nyang'hanga/Kabila, Singa-Kibosho, Elerai/Longido, Same, Dindimo, Majengo/Eslalei, Njombe vijijini, Usangi, Galula/Mbuyuni/Mbagala, Rondo, Kwanyange, Nzega Vijijini, Korogwe vijijini na Kamachumu. Maeneo mengine ni Chunya vijijini, Njombe mjini, Mwisanga/Ntomoko, Kilosa, Manyoni, Maswa, Mwanga, Magu, Kongwa, Ngudu, Sengerema, Igunga, Chamwino, Nderemo-Handeni, Kwenjugo *(HTM),* Namanyere, Tukuyu, Magubike, Litumbakuhama/Kingirikiti - Mbinga, Sumve/Mantare na Lesingita.

Aidha, Wizara yangu itakarabati miradi ya maji ya Gonja Maore, Kilulu, Kiponzelo, Iramba Vijijini, Gabimori, Hedaru, Makonde, Nanyamba, Lushoto, Mafinga, Wakichi Kibena Njombe, Muleba, Kayanga, Ubembe/Kwamhosi - Muheza, Nganyeni, Makoro, Useri, Kwasondo, Munga, Nduruma, Nkoarua na Moshono.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Halmashauri ya wilaya Moshi Vijijini, itaanza kukarabati na kupanua miradi 30 ya maji katika awamu ya kwanza ya utekelezaji. Mradi huo unategemewa kuchukua muda wa miaka 4 na utakapokamilika utawanufaisha wananchi 65,400.

Mheshimiwa Spika, Upanuzi wa Miradi ya Maji Vijijini, Wizara yangu, imeendelea kuimarisha na kuboresha huduma ya maji vijijini kwa kupanua na kujenga miradi mipya ya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilijenga na kupanua miradi ya maji ya Chiuwe (Lindi Vijijini), Chalinze, Malya (Kwimba), Nachingwea, Igombe (Ilemela), Nyakagomba (Geita), Kilwa Masoko na Ilula (Kilolo). Miradi mingine ni Tukuyu, Ngara, Kitomanga (Lindi Vijijini), Nanyamba, Mwanga, Newala, Masasi, Nachingwea, Liwale, Kilwa, Kilosa, Same na uchimbaji wa visima 3 katika wilaya ya Ilemela.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kueneza teknologia ya uvunaji wa maji ya mvua, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo na kuhamasisha utumiaji wa teknolojia

rahisi ya uvunaji wa maji ya mvua. Katika mwaka 2004/2005, Wizara ilitoa mafunzo ya ujenzi wa matangi kwa ajili ya mafundi 24 wa vijiji vya Wilaya za Chunya na Magu.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea na upanuzi wa miradi ya maji ya Tarime, Maswa, Mbarali, Chiuwe, Chalinze, Pangani, Ilula, Igombe, Mbwinji Masasi/Nachingwea, Malya, Kilwa Masoko, Geita, Nachingwea. Mradi mwingine ni wa uhamasishaji wa ujenzi wa matangi ya mfano ya kuvuna maji ya mvua katika maeneo ya Urambo na Uyui. Jumla ya shilingi milioni 523 zimetengwa.

Pia, Wizara imetenga shilingi milioni 675 kuchimba visima virefu 30 katika maeneo ya Tunduru (3), Nzega (3), Ruangwa (1), Gairo (6), Kisarawe (3), Igula-Njombe (2), Iringa Vijijini (2), Lukale-Karagwe (1), Nyakayanja (1), Usangi-Butu (Mwanga) (2), na Ilemela (6). Aidha, Wizara itaendelea na ujenzi wa bwawa la Mugumu na mabwawa madogo 3 kwenye maeneo yenye ukame.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya na Serikali ya Ujerumani, ilikamilisha upanuzi wa mradi wa maji wa Wilaya ya Hai awamu ya tatu ambao unahudumia watu wapatao 39,000 katika vijiji vya Magadini, Lawate-Fuka, Masama na Rundugai kwa gharama ya shilingi bilioni 6.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaanza utekelezaji wa awamu ya nne ya mradi wa maji Hai utakaohudumia vijiji vya Lyamungo na Mailisita utakaowanufaisha watu wapatao 15,000. Jumla ya shilingi milioni 104.8 zimetengwa kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi, iliendelea kutekeleza programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini inayohusisha wilaya zote za mkoa wa Shinyanga. Katika mwaka 2004/2005, utekelezaji wa programu hiyo uliendelea kwa kuchimba visima virefu na vifupi; ukarabati na ujenzi wa miradi ya bomba; na uchimbaji wa mabwawa ambapo jumla ya shilingi bilioni 2.184 zimetumika.

Katika mwaka 2005/2006, utekelezaji wa programu hiyo utaendelea kwa kuchimba visima virefu na vifupi 142 na uchimbaji wa mabwawa madogo 8. Pia, miradi ya maji mipya 9 ya bomba itajengwa vijijini na upanuzi wa miradi ya maji utafanyika katika miji 5 ya Bariadi, Bukombe, Maswa, Meatu na Kahama. Aidha, matangi 55 ya kuvunia maji ya mvua yatajengwa maeneo mbalimbali pamoja na kujenga miradi 2 itakayotumia nguvu ya upepo. Jumla ya shilingi bilioni 2.071 zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa iliendelea kutekeleza kazi mbalimbali kwenye miji tisa iliyo chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira katika miji midogo ya Utete, Ikwiriri, Kibiti, Turiani, Mvomero, Kilosa, Gairo, Kibaigwa na Mpwapwa. Uchunguzi wa awali wa vyanzo vya maji katika miji yote tisa umekamilika.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea na uchimbaji wa visima vya majaribio na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa mifumo ya usambazaji maji katika miji hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 Wizara yangu, ilianza maandalizi ya ujenzi wa miradi ya maji itakayogharamiwa kwa mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*). Halmashauri ya Wilaya ya Monduli iko katika hatua za kuingia mikataba na Washauri na Wakandarasi watakaosimamia na kujenga miradi katika vijiji 18 na miji 2 ya Monduli na Namanga. Aidha, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, ilianza utekelezaji wa Mradi wa Maji katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ambapo vifaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na mitambo ya kuchimbia visima na magari vilinunuliwa na kupokelewa. Mradi huo utawanufaisha wakazi 201,967 katika vijiji 64. Katika mwaka 2005/2006, ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 13 vya mkoa wa Lindi na vijiji 21 vya mkoa wa Mtwara utaanza.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Kitaifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini,Wizara yangu imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa kutumia fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Miradi ya maji katika vijiji 29 vyenye wakazi wapatao 134,000 ilikamilika katika wilaya tatu za Rufiji, Kilosa na Mpwapwa. Ujenzi wa miradi mingine katika wilaya hizo unaohusisha vijiji 15 utakamilika Desemba, 2005. Aidha, mikataba ya ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 94 vya wilaya nyingine 11 za mradi imesainiwa mwezi Juni 2005 na ujenzi unategemewa kuanza mwezi Julai 2005. Wilaya 11 zitakazohusika ni: Morogoro Vijijini, Mvomero, Handeni, Kilindi, Kiteto, Kondoa, Manyoni, Singida vijijini, Iramba, Igunga na Kongwa. Aidha, usanifu wa miradi ya maji katika miji midogo 4 ya Igunga, Kiomboi, Kondoa na Kongwa uko katika hatua za kukamilika na ujenzi wa miradi hiyo utaanza mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu imekamilisha maandalizi ya kupanua mradi huo kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Maji na kuzingatia uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini inayogharamiwa na wahisani wengine. Upanuzi wa mradi huo, utabadilisha mfumo wa utekelezaji wake ili uwe Programu ya Kitaifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ambayo itashirikisha wafadhili mbalimbali na kutekelezwa katika wilaya zote nchini. Programu hiyo inayolenga utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira nchini kote tayari imekuwa ikijadiliwa na wadau na wafadhili mbalimbali. Lengo ni kupeleka fedha za utekelezaji moja kwa moja kwa Halmashauri za Wilaya kwa kuzingatia vigezo vitakavyokubaliwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuanzishwa kwa Programmu ya Kitaifa ya Maji Vijijini, wafadhili mbalimbali wamekubali kushiriki katika utekelezaji wake. Wafadhili hao ni pamoja na Benki ya Dunia; Benki ya Maendeleo ya Afrika; Umoja wa Nchi za Ulaya; na Serikali ya Uholanzi; Ujerumani; Japan; na Ufaransa. Majadiliano yanaendelea na wafadhili hao kwa lengo la kupata fedha za utekelezaji ifikapo Julai 2006. Kwa sasa miradi midogo midogo imeainishwa katika wilaya zote nchini kwa lengo la kuitekeleza mapema ili kuondoa kero ya maji kwa wananchi. Baadhi ya miradi hiyo imetekelezwa

katika wilaya 38 ambazo ziliainishwa kwa ajili ya upanuzi katika mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa, Wakala umechimba visima virefu 480 vyenye uwezo wa kutoa maji mita za ujazo milioni 17.6 kwa mwaka. Aidha, imeendelea na ujenzi wa bwawa la Mugumu ambapo jumla ya shilingi milioni 380 zilitumika kujenga utoro wa maji na msingi wa tuta ambapo asilimia 75 ya kazi imekamilika. Vilevile, mabwawa madogo 6 yenye uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo 80,000 kwa ajili ya mifugo na kilimo yalichimbwa katika Wilaya za Bagamoyo na Kibaha.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara imetenga shilingi milioni 300 kuendelea na ujenzi wa bwawa la Mugumu. Pia imetenga shilingi milioni 228 kwa ajili ya kukarabati mitambo chakavu ya kuchimba visima na ujenzi wa mabwawa na shilingi milioni 450 kununulia mitambo mipya ili kuimarisha utoaji huduma za Wakala.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma ya Maji Vijijini katika jitihada za kuboresha huduma za maji vijijini, Serikali imeanzisha utaratibu mpya wa kupeleka fedha za Sekta ya Maji moja kwa moja kwenye Halmashauri za Wilaya kwa kutumia kigezo cha idadi ya watu ambao bado hawajapata huduma za maji. Utaratibu huu utaanza kutumika mwaka 2005/2006 ambapo jumla ya shilingi bilioni 9.3 zimetengwa. Nachukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa wabunge na wananchi kwa ujumla kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumika kwa lengo lililokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Wizara yangu ilikuwa inasimamia na kuendesha Kitaifa miradi 6 ya maji ya Maswa, Wanging'ombe, Mugango/Kiabakari/Butiama, Chalinze, Makonde na *Handeni Trunk Main (HTM).* Katika jitihada za kuboresha usimamizi na uendeshaji wa miradi hiyo, mwaka 2004/2005 Wizara ilikabidhi miradi hiyo kwa Halmashauri za Wilaya husika ambazo zina jukumu la kusimamia Bodi za Maji zilizoundwa kwa ajili ya kuendesha miradi hiyo.

Katika mwaka 2005/2006, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 377.4 ambazo zitapelekwa moja kwa moja katika Halmashauri za Wilaya husika kwa ajili ya uendeshaji wa miradi hiyo na kuijengea uwezo wa kujitegemea. Fedha hizo ni nyongeza ya fedha ambazo wilaya hizo zitapata kulingana na vigezo vilivyokubaliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Huduma ya Majisafi na Uondoaji Majitaka Mijini, upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa mijini umefikia asilimia 74. Uzalishaji wa majisafi kwa mamlaka zote 19 ulifikia lita bilioni 110 na ukusanyaji wa maduhuli ulifikia shilingi bilioni 17.9. Huduma ya uondoaji wa majitaka, imeendelea kuwa asilimia 17 ya wakazi waishio mijini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* na *OPEC* zinagharamia upanuzi na ukarabati wa mfumo wa majisafi na ujenzi wa mfumo wa majitaka mjini Singida kwa gharama ya shilingi bilioni 12.43. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 5.5 zinatoka BADEA, bilioni 5.0 kutoka

*OPEC* na bilioni 1.93 kutoka Serikali yetu. Kazi ya upembuzi yakinifu ya mradi huo ilianza mwezi Septemba 2004 na itakamilika mwezi Oktoba 2005 ambapo ujenzi wa mradi utaanza. Pia, *BADEA* ilitoa shilingi milioni 280 ambazo zimetumika kukamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa majitaka ambao umekamilika mwezi Juni 2005. Katika mwaka 2005/2006, shilingi bilioni 2.4 zimetengwa kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa mfumo wa majisafi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa, kupitia Shirika lake la Maendeleo *(AFD),* ilikamilisha upembuzi yakinifu wa miradi ya majisafi na majitaka katika miji ya Bukoba, Musoma na Misungwi kwa gharama ya shilingi milioni 226.1.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara itaanza majadiliano na Serikali ya Ufaransa kupitia AFD ili kupata fedha za ujenzi wa miradi hiyo ambayo itagharimu *Euro* milioni 5.0.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ikishirikiana na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU)* na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)* iliendelea na mpango wa kuimarisha huduma za majisafi na uondoaji wa majitaka katika Jiji la Mwanza; na Manispaa za Mbeya na Iringa. Mwaka 2004/2005 kazi za usanifu na utayarishaji wa zabuni za miradi ya majisafi na majitaka zilitekelezwa katika Jiji la Mwanza na Manispaa ya Mbeya. Usanifu wa Mradi, awamu ya pili katika miji ya Mwanza, Iringa na Mbeya umeanza kwa kutafuta Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hiyo.

Katika mwaka 2005/2006, jumla ya shilingi milioni 40 zimetengwa kwa ajili ya usanifu na utayarishaji wa zabuni ya mradi wa majisafi katika Manispaa ya Iringa.

Mheshimiwa Spika, Ukarabati wa Miradi ya Majisafi na Majitaka Mijini Wizara yangu inalo jukumu la kuziimarisha Mamlaka za Maji Mijini ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma za majisafi na uondoaji majitaka na hivyo kuziwezesha kujitegemea. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilikarabati mifumo ya majisafi kwenye miji ya Kigoma, Mbeya, Mtwara, Musoma, Sumbawanga, Songea na Lindi kwa gharama ya shilingi milioni 115. Aidha, shilingi milioni 40 zilitumika katika kukarabati mifumo ya majitaka kwenye miji ya Dodoma na Iringa.

Katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu itakarabati miradi ya majisafi kwenye miji ya Sumbawanga, Songea, Shinyanga na Lindi kwa gharama ya shilingi milioni 360. Pia, mifumo ya majitaka katika miji ya Dodoma na Morogoro itakarabatiwa kwa gharama ya shilingi milioni 53.

Mheshimiwa spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la fedha la *KfW,* imekamilisha awamu ya kwanza ya ukarabati wa mradi wa majisafi katika mji wa Songea kwa gharama ya shilingi bilioni 6.38. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani itatekeleza awamu ya pili ya mradi huo inayohusu ujenzi wa mfumo wa majitaka kwa gharama ya shilingi bilioni 9.6.

Mheshimiwa Spika, Upanuzi wa Miradi ya Majisafi na Majitaka Mijini, katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu iliendelea kuboresha huduma za majisafi katika Jiji la Mwanza, Manispaa za Dodoma, Morogoro, Shinyanga na Tabora na Miji ya Bukoba, Singida na Babati kwa gharama ya shilingi milioni 90. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itatumia shilingi milioni 189 kwa ajili ya kupanua mifumo ya majisafi kwa miji ya Iringa, Babati na Singida.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa mradi wa majisafi na uondoaji wa majitaka katika Jiji la Mwanza na Manispaa ya Mbeya, mwaka 2005/2006 kazi ya ujenzi wa mradi huo itaanza katika Jiji la Mwanza. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na upanuzi wa kituo cha kusukuma maji; mtambo wa kusafisha maji na mtandao wa kusambaza majisafi; ujenzi wa matangi ya maji; na upanuzi wa mfumo wa uondoaji wa majitaka. Jumla ya shilingi milioni 40 zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo. Aidha, katika Manispaa ya Mbeya upanuzi wa mifumo ya majisafi na majitaka utafanyika na dira 10,000 zitafungwa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kutoa Maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Shinyanga na Kahama, mwaka 2004 Wizara yangu ilianza ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama na Shinyanga. Mradi huo utakapokamilika utaleta manufaa yafuatayo:

(a) Upatikanaji wa majisafi, salama na ya kutosha kwa wananchi zaidi ya milioni moja pamoja na mifugo yao katika vijiji 54 vilivyopo mikoa ya Mwanza na Shinyanga;

(b) Kupungua kwa magonjwa ya kuambukiza yatokanayo na matumizi ya maji yasio salama, na hivyo wananchi watakuwa na afya nzuri za kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kijamii ili kuwawezesha kuchangia katika kupunguza umasikini;

(c) Kuvutia wawekezaji katika nyanja za viwanda, migodi na biashara; na

(d) Kutoa ajira kwa wananchi wakati wa ujenzi na uendeshaji wake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukubwa wa mradi huo, Wizara yangu ilibuni mbinu za kufupisha muda wa utekelezaji, ambapo kazi zote zilipangwa katika kandarasi nne. Mkataba wa kutekeleza kandarasi Na.1 yenye gharama ya shilingi bilioni 27.52 ilisainiwa mwezi Februari 2004. Kandarasi hii ambayo itakamilika mwezi Septemba 2005, inahusu kazi zifuatazo:-

(a) Ujenzi wa chanzo cha maji ziwani na ulazaji wa mabomba makubwa ya kipenyo cha milimita 900 na urefu wa kilomita 3.3 hadi chujio la kusafishia maji; asilimia 75 ya kazi hii kwa sasa imekamilika;

(b) Ujenzi wa chujio la kusafishia maji wenye uwezo wa kusafisha lita milioni 80 kwa siku; asilimia 65 ya kazi hii hadi sasa imekamilika;

(c) Ulazaji wa mabomba ya kipenyo cha milimita 900 na urefu wa kilomita 6.3 kutoka kijiji cha Ihelele hadi mlima Mabale kwenye tangi kubwa la kuhifadhia maji; asilimia 65 ya kazi hii kwa sasa imekamilika;

(d) Ujenzi wa tangi kubwa la kuhifadhia maji lenye uwezo wa lita milioni 35 katika mlima Mabale; asilimia 10 ya kazi hii kwa sasa imekamilika; na

(e) Kazi za ufungaji wa pampu za kusukuma maji yasiyosafishwa na yaliyosafishwa bado hazijaanza.

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari 2005 Wizara ilisaini Mkataba wa kutekeleza Kandarasi Na.2 ya gharama ya shilingi bilioni 47.69. Kandarasi hii inahusu ulazaji wa mabomba ya kipenyo cha milimita 1,200 na urefu wa kilomita 27.7 kutoka mlima Mabale hadi kijiji cha Mawile; ulazaji wa mabomba ya kipenyo cha milimita 300 na urefu wa kilomita 22 kutoka kijiji cha Mawile hadi Tarafa ya Mwamashimba; na ulazaji wa mabomba ya kipenyo cha milimita 1,100 kutoka kijiji cha Mawile hadi Solwa na urefu wa kilomita 18.3. Kazi za kandarasi hiyo zimepangwa kukamilika mwezi Februari 2006. Kazi za upelekaji wa mitambo ya kufanyia kazi na ujenzi wa kambi ya mkandarasi zimekamilika. Kazi za upimaji wa njia ya bomba na upelekaji mabomba ya chuma katika eneo la mradi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni 2005 Wizara yangu ilisaini mkataba wa kutekeleza kandarasi namba 3 na 4. Kandarasi hizo zitatekeleza kazi za ulazaji wa mabomba ya kipenyo cha milimita 750 na urefu wa kilomita 62.1 kutoka Solwa hadi mji wa Kahama; usambazaji wa maji katika mji huo; ulazaji wa mabomba ya kipenyo cha milimita 700 lenye urefu wa kilomita 64.4 kutoka Solwa hadi Manispaa ya Shinyanga; na upanuzi na ukarabati wa mfumo wa usambazaji wa majisafi katika Manispaa ya Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, Uendeshaji wa Huduma ya Maji Mijini, katika jitihada za kuhakikisha huduma za maji mijini zinatolewa kwa ufanisi na kwa gharama nafuu, mwaka 2004/2005, Wizara ilitathmini upotevu wa maji na kuchunguza gharama halisi za matumizi ya umeme katika utoaji wa huduma za maji kwenye miji ya Bukoba na Babati.

Tathmini hiyo ilibaini kuwa sababu za upotevu wa maji zinatokana na uchakavu wa mitambo na mitandao ya usambazaji, matumizi holela ya maji hasa kwa wateja wanaolipa kiwango kimoja (*flat rate)* pamoja na hujuma zinazofanywa na wateja wanaotumia dira. Mamlaka zimeshauriwa zichukue hatua za kurekebisha dosari hizo ikiwa ni pamoja na kufunga dira kwa wateja wake wote, kuelimisha umma juu ya umuhimu wa dira na kudhibiti matumizi ya umeme.

Katika mwaka 2005/2006, tathmini ya upotevu wa maji kwa miji ya Musoma, Kigoma, Morogoro, Lindi, Mtwara na Tabora itafanyika.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Majisafi na Majitaka Jijini Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma za maji kwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo uliendelea katika mwaka 2004/2005 chini ya usimamizi wa *DAWASA*. Kazi za kukarabati mitambo ya kuzalisha maji kutoka vyanzo vya Ruvu Juu na Ruvu Chini pamoja na mabomba makuu yanayosafirisha maji kutoka mitambo hiyo zilikamilishwa kwa gharama ya shilingi bilioni 5.8. Pia, mradi huo ulihusisha ununuzi wa dira za maji 103,986 kwa gharama ya shilingi bilioni 5.4. Dira 10,000 zilifungwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Aidha, ukarabati wa mabomba makubwa na madogo ya kusambaza majisafi Jijini na bomba kuu linalomwaga majitaka baharini pamoja na mabomba ya kukusanya majitaka unaendelea kutekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 57.95.

Mheshimiwa Spika, maji katika mto Ruvu ambao ni chanzo kikuu cha maji kwa ajili ya Jiji na miji ya Kibaha na Bagamoyo yameendelea kupungua kutokana na ukame, uharibifu wa mazingira na ongezeko la matumizi. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilianza kutafuta vyanzo vipya ambapo awamu ya kwanza ilikamilika na awamu ya pili itakamilika Juni 2006. Utekelezaji wa kazi hizo kwa awamu zote mbili utagharimu shilingi bilioni 1.5.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea na ukarabati wa mabwawa ya majitaka na vituo vya kusukuma majitaka kwa gharama ya shilingi bilioni 8.57. Pia, itaanza upanuzi wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira hususan vijiji vya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi bilioni 3.0.

Mheshimiwa Spika, tarehe 19 Februari, 2003 *DAWASA* iliingia mkataba wa ukodishaji wa miundombinu kati yake na kampuni binafsi ya *City Water Services* baada ya uamuzi wa Serikali kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka mijini. Lengo la Serikali lilikuwa ni kuongeza ufanisi katika utoaji huduma, kuingiza teknolojia mpya na kuongeza mtaji wa uwekezaji katika miundombinu. Tangu kampuni hiyo ilipoanza kazi tarehe 1 Agosti, 2003, yamejitokeza matatizo mbalimbali ambayo yameathiri utendaji kazi na masharti ya mkataba wa ukodishaji kama ifuatavyo:-

i. Kupungua kwa ukusanyaji wa mapato kutoka wastani wa shilingi bilioni 1.2 zilizokuwa zinapatikana kabla ya mkataba hadi wastani wa bilioni 0.8 kwa mwezi tangu Kampuni ya *City Water Services* kuanza kazi hiyo;

*ii.* *City Water Services* kushindwa kulipa malimbikizo ya ada ya ukodishaji kwa DAWASA yaliyofikia shilingi bilioni 3.6;

*iii.* *City Water Services* kushindwa kuweka fedha kiasi cha Shilingi milioni 900 katika mfuko wa kuunganisha maji kwa wateja wenye kipato kidogo;

*iv. City Water Services* kushindwa kuwekeza mtaji uliokuwa umekubaliwa kimkataba wa dola za kimarekani milioni 4.4. Katika kipindi cha miaka miwili;

*v. City Water Services* kutowasilisha taarifa za utekelezaji zinazoonyesha mwenendo wa uendeshaji na utendaji wao kifedha jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya mkataba; hivyo kuifanya Serikali kutojua kinachofanyika;

*vi. City Water Services* kushindwa kufikia malengo yaliyokubaliwa katika mkataba. Kwa mfano walitakiwa kufunga dira za maji 16,500 hususan kwa wateja wake kwenye maeneo ya biashara, katika kipindi cha mwaka wa kwanza wa mkataba badala yake walifunga dira 8,751 kwa wateja wa kawaida;

vii. Mkataba uliwataka *City Water Services* kuunganisha wateja wapya 1,000 katika kipindi cha mwaka mmoja na badala yake waliunganisha wateja wapya 400 tu;

viii. Pamoja na kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji maji katika mitambo ya Ruvu kwa asilimia 15, utoaji wa huduma ya maji katika baadhi ya maeneo ulipungua. Kwa mfano, maeneo ambayo yalikuwa yanapata maji mara mbili kwa wiki yakawa yanapata mara moja kwa mwezi au kukosa kabisa;

Mheshimiwa Spika, licha ya kasoro nilizotaja hapo juu, *City Water Services* walitaka yafanyike mabadiliko yafuatayo:

(i) Kuongeza bei ya maji kwa wateja wa kibiashara kwa asilimia 12.2 na asilimia 10 kwa wateja wa matumizi ya nyumbani;

*(ii) City Water Services* kutolipa asilimia 100 ya ada ya ukodishaji;

*(iii) City Water Services* kutolipa asilimia 100 ya gharama za umeme;

(iv) Serikali kufuta deni lote la *City Water Services* kwa *DAWASA* na;

(v) Serikali kuipatia *City Water Services* shilingi bilioni 4.1 kugharamia kupunguza wafanyakazi waliowakubali kimkataba.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali haikukubali kufanya mabadiliko hayo kwa sababu kufanya hivyo kungekuwa sawa na Serikali yenyewe kugharamia majukumu yote yaliyoainishwa kwenye mkataba. Kutokana na hali hiyo na kwa lengo la kuhakikisha huduma za maji zinaendelea kutolewa, Serikali ilisitisha mkataba wa *DAWASA* na *City Water Services*. Utaratibu wa kuendesha shughuli zilizokuwa zinafanywa na *City Water Services* uliandaliwa ambapo Kampuni ya *DAWASCO* iliundwa na kupewa jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo katika Sekta ya Maji, mwaka 2004/2005 Chuo cha Maji cha Rwegarulila kiliendelea kutoa mafunzo yanayolenga kutosheleza mahitaji maalum ya Halmashauri za Wilaya na taasisi nyingine. Jumla ya wanafunzi 54 walihitimu katika fani ya ufundi sanifu na 265 katika fani ya ufundi stadi. Aidha, chuo kilikamilisha mapitio ya mtaala wa mafunzo ili uendane na Sera ya Maji na kukidhi mahitaji ya ujuzi katika soko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, chuo kitaendelea kutoa mafunzo katika fani za ufundi sanifu na stadi. Chuo kitaanza kutumia mtaala mpya wa mafunzo ambao utakuwa unatoa stashahada ya taaluma za maji katika fani za uhandisi wa maji; utafiti wa maji chini na juu ya ardhi na uchimbaji wa visima; na teknolojia ya maabara za maji. Wizara imetenga shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuimarisha chuo hicho kwa kukarabati majengo ili kiweze kupokea wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo, Sera ya Mifugo, mwaka jana nililieleza Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itaifanyia mapitio Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997 ili kuwa na Sera ya Mifugo. Nafurahi kueleza kuwa mapitio hayo yamekamilika na taratibu za kuipitisha Rasimu ya Sera ya Mifugo ya Taifa (2005) zinaendelea. Sera hiyo imezingatia mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025;

(b) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA);

(c) Mkakati wa Maendeleo Vijijini;

(d) Masuala ya Utandawazi yanayotokana na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia;

(e) Mwelekeo na Dira ya Maendeleo ya Sekta ya Mifugo hadi mwaka 2025;

(f) Malengo ya Kimataifa ya *Millenia (MDGs);* na

(g) Sera za Sekta mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Mifugo ya Taifa itapitishwa rasmi na Serikali hivi karibuni. Wizara yangu itatumia mbinu mbalimbali katika kueneza Sera hiyo kwa wafugaji na wadau wengine ili ieleweke vizuri kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wake. Mbinu zitakazotumika kueneza sera ni pamoja na warsha, makongamano, semina, mikutano ya hadhara, vipindi vya redio/luninga na kuchapisha na kusambaza vipeperushi na makala zitatolewa magazetini.

Mheshimiwa Spika, Maonesho ya Nanenane, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula; Wizara ya Ushirika na Masoko; na Mikoa huandaa na kushiriki kwenye Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima na Wafugaji nchini ambayo

huadhimishwa kitaifa tarehe 8 Agosti kila mwaka. Lengo la maadhimisho hayo ni kutathmini mafanikio na matatizo ya Sekta ya Mifugo na pia kutoa nafasi kwa wadau wa Sekta hiyo kupata ufafanuzi kuhusu Sera na utoaji wa huduma za mifugo nchini. Aidha, wafugaji na wadau wa sekta hupata fursa ya kujifunza mbinu bora za uzalishaji, usindikaji, na hifadhi ya mazao yatokanayo na mifugo.

Katika mwaka 2004, kitaifa maonesho hayo yalifanyika mkoani Mbeya na yalifunguliwa na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha. Aidha, kilele chake kilihitimishwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa ni "Zalisha Kibiashara na Hifadhi Chakula cha Kutosheleza Mahitaji ya Kaya". Nachukua fursa hii kuwashukuru Makamu wa Rais na Waziri Kiongozi kwa kukubali mwaliko na kushiriki katika maadhimisho hayo. Pia, nawapongeza wafugaji na wananchi wote walioshiriki katika kufanikisha maonesho hayo. Maonesho ya Nane Nane ya mwaka 2005 yatafanyika kitaifa Mjini Mbeya kwa mara ya tatu mfululizo.

Mheshimiwa Spika, Makongamano ya Wataalam wa Mifugo, makongamano ya vyama vya kitaalam vya Madaktari wa Mifugo (Tanzania *Veterinary Association –TVA*) na Maafisa wa Mifugo (*Tanzania Society of Animal Production -TSAP)* yameendelea kufanyika kwa madhumuni ya kubadilishana uzoefu na kujifunza mambo mapya yanayojitokeza katika maendeleo ya Sekta ya Mifugo nchini ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya sera na utoaji wa huduma. Kongamano la Wataalam wa Mifugo lilifanyika mjini Moshi mwezi Oktoba, 2004 na kaulimbiu ilikuwa "Mbinu Bora za Uzalishaji Mifugo katika Kuboresha Maisha ya Mfugaji".

Aidha, Kongamano la Madaktari wa Mifugo lilifanyika mjini Arusha mwezi Desemba, 2004 na kaulimbiu ilikuwa "Changamoto za Uendelezaji wa Mifugo katika Uchumi wa Utandawazi". Maazimio mbalimbali yalitolewa na makongamano hayo na Wizara yangu inaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ushauri ya Wataalam wa Mifugo, mara baada ya kuundwa kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, mwaka 2001 niliunda Kamati ya Wataalam wa Sekta ya Mifugo (*Think Tank*).

Kamati hiyo inajumuisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Mifugo wakiwemo wataalam wa fani mbalimbali; wafugaji; wasindikaji; na wahadhiri kutoka vyuo vikuu nchini. Lengo la kuunda kamati hiyo ni kuishauri Wizara namna ya kuendeleza Sekta ya Mifugo ili ichangie kikamilifu katika kupunguza umaskini kwa wafugaji na kuongeza mchango wa sekta katika Pato la Taifa. Kamati hiyo imetoa mchango mkubwa wa ushauri katika kuendeleza Sekta ya Mifugo ikiwa ni pamoja na kuchambua matatizo yanayoikabili sekta na ufumbuzi wake na kushiriki katika kuandaa Sera ya Taifa ya Mifugo. Napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati hiyo kwa mchango wake na naiomba iendelee kutoa ushauri wake kila inapobidi.

Mheshimiwa Spika, Siku ya Chakula Duniani,Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula pamoja na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani, iliandaa na kushiriki maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani ambayo yalifanyika kitaifa katika kijiji cha Malinzaga, wilaya ya Iringa Vijijini. Maadhimisho hayo hufanyika duniani kote tarehe 16 Oktoba kila mwaka kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuzalisha chakula cha kutosha na kuwa na lishe bora. Kaulimbiu ilikuwa "Tumia Bioanuai kwa Uhakika wa Chakula".

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani katika kuandaa maadhimisho hayo.

Mheshimiwa Spika, Sheria za Mifugo, Wizara imefanyia mapitio sheria mbalimbali za Sekta ya Mifugo ili ziendane na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2004/2005, imepitishwa Sheria ya Maziwa Na. 8, ambayo inaunda Bodi ya Maziwa inayosimamia uendelezaji wa Sekta ndogo ya maziwa nchini. Aidha, Sheria ya Nyama ipo kwenye hatua za mwisho za kutungwa na sheria nyingine 5 zipo katika hatua mbalimbali za mapitio nazo ni: Sheria ya Ngozi Na. 30 ya mwaka 1965; Sheria ya Kulinda Wanyama *Cap. 153* ya mwaka 1926; Sheria ya Kudhibiti Ndorobo *Cap. 100* ya mwaka 1943; Sheria ya Kuzuia Uzururaji wa Wanyama *Cap. 154* ya mwaka 1930; na Sheria ya Mbolea na Vyakula vya Mifugo *Cap. 467* ya mwaka 1962.

Katika kuhakikisha kuwa sheria zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu zinatumika, katika mwaka 2004/2005 Wizara yangu ilitayarisha kanuni 10 chini ya Sheria ya Usimamizi wa Utoaji Huduma za Mifugo Na. 16 ya mwaka 2003. Mwaka 2005/2006 Wizara itaendelea kutayarisha kanuni zaidi zinazohusu sheria zilizopitishwa na kukamilisha sheria zilizobakia.

Mheshimiwa Spika, Maadhimisho ya Miaka 100 ya Utoaji Huduma za Mifugo Nchini,napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mwezi Juni 2005 nchi yetu iliadhimisha miaka 100 ya utoaji wa huduma za mifugo nchini na kuanzishwa kwa kituo cha kwanza cha mifugo cha Mpwapwa mwaka 1905.

Katika maadhimisho hayo wadau wa Sekta ya Mifugo walishiriki katika kongamano la kitaifa na semina mbalimbali za wafugaji ambapo walipata fursa ya kutathmini mafanikio na matatizo yaliyojitokeza katika kipindi hicho. Kilele cha maadhimisho hayo kilikuwa tarehe 11 Juni na mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein ambapo pamoja na mambo mengine nchi yetu ilikabidhiwa rasmi cheti cha kutambuliwa na Shirika la Kimataifa la Afya ya Wanyama kwa Kutokomeza Ugonjwa wa Sotoka nchini. Aidha, changamoto ilitolewa kwa wataalam na wafugaji kuangamiza kupe nchini ambao kwa sasa ndio chanzo kikubwa cha vifo vya mifugo. Nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kukubali kushiriki katika maadhimisho hayo ya kihistoria. Vilevile, nawashukuru viongozi na wananchi wa Mkoa wa Dodoma kwa kufanikisha maadhimisho hayo.

Mheshimiwa Spika, Uzalishaji wa Mifugo na Mazao ya Mifugo, katika mwaka 2004/2005, uzalishaji wa maziwa ulifikia lita bilioni 1.3 ikilinganishwa na lita bilioni 1.18 mwaka 2003/2004. Jumla ya mitamba 7,169 ilisambazwa kwa wafugaji wadogo nchini. Kati ya hiyo, mitamba 1,165 ilitoka mashamba 6 ya Wizara na kampuni ya *NARCO* na mitamba 5,450 ilitoka mashirika yasiyo ya kiserikali (Kiambatanisho Na. 7). Aidha, jumla ya mbuzi 1,522 walisambazwa kwa wafugaji. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali itaendelea kusambaza mitamba na mbuzi bora wa maziwa kwa wafugaji wadogo.

. Mheshimiwa Spika, asilimia 97 ya ng'ombe tulionao nchini ni wa asili wenye ukosaafu mdogo ambao huzalisha chini ya wastani wa lita 500 za maziwa kwa mwaka ikilinganishwa na lita kati ya 2,500 na 3,000 kwa ng'ombe chotara. Serikali imeendelea kukiimarisha kituo cha madume cha *Usa River (NAIC)* cha kuzalisha mbegu bora kwa ajili ya kuongeza ukosaafu wa ng'ombe wa asili.

Katika mwaka 2004/2005, jumla ya ng'ombe 41,440 walihamilishwa ikilinganishwa na ng'ombe 39,894 kwa mwaka 2003/2004. Ongezeko la matumizi ya uhamilishaji linatokana na kupanuka kwa matumizi ya mbegu bora katika mashamba binafsi, mashamba ya kuzalisha mitamba na wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa nchini. Pia, Wizara ilianzisha vituo viwili vya uhamilishaji vya Kanda ya Kusini (Mbeya) na Kanda ya Ziwa (Mwanza) ili kuongeza kasi ya uhamilishaji kwa lengo la kuboresha mifugo katika kanda hizo

Katika mwaka 2005/2006, ng'ombe 50,000 wanatarajiwa kuhamilishwa. Wizara pia, itaendelea kuongeza vituo vya kanda vya uhamilishaji katika kanda nyingine mbili za Kati (Dodoma), na Mashariki (Dar es salaam) na kuimarisha vituo vipya vya Mbeya na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, usindikaji wa mazao ya mifugo ni njia ya kuiwezesha Sekta ya Mifugo kuchangia zaidi katika Pato la Taifa na kuongeza faida kwa wafugaji kwa kuwa mazao yao yanapata soko la uhakika ndani na nje. Wizara yangu, inaratibu na kuhamasisha usindikaji wa maziwa kwa lengo la kuongeza thamani na muda wa matumizi ya zao hilo.

Kwa sasa kuna viwanda 22 ambavyo vina uwezo wa kusindika lita 510,000 za maziwa kwa siku. Hata hivyo, kutokana na matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na gharama kubwa za usindikaji na ukusanyaji wa maziwa, viwanda hivyo vinasindika lita 150,000 kwa siku sawa na asilimia 30 tu ya uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, katika kupanua soko la ndani la unywaji wa maziwa na utumiaji wa mazao yatokanayo na maziwa, mwaka 2004/2005 Wizara yangu iliendelea kuadhimisha "Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa" ambayo kitaifa ilifanyika Mkoani Tanga ambapo ujumbe ulikuwa "Kunywa Maziwa kwa Afya Yako". Hadi sasa, mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Pwani na Dar es salaam ina programu za kuwapatia wanafunzi maziwa kwa baadhi ya shule za msingi. Nachukua fursa hii kuipongeza mikoa

ya Pwani na Dar es Salaam kwa kuitikia wito wangu na naiomba mikoa mingine iige mfano huo.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta ndogo ya maziwa na kulinda viwanda vya ndani ili kuongeza kiwango cha usindikaji wa maziwa yanayozalishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, uzalishaji wa nyama uliongezeka kufikia tani 378,509 kutoka tani 348,800 kwa mwaka 2003/2004, ambayo ni sawa na asilimia 2. Kati ya kiasi hicho kilichozalishwa, mchanganuo ni kama ifuatavyo: tani za nyama ya ng’ombe 204,520; mbuzi na kondoo 78,093; nguruwe 27,000; na kuku tani 68,896.

Aidha, katika mwaka 2004/2005 jumla ya vifaranga milioni 21.2 vya kuku wa kisasa vilizalishwa nchini ikilinganishwa na vifaranga milioni 18.4 mwaka 2003/2004. Pia, uzalishaji wa mayai uliongezeka hadi kufikia bilioni 1.8 kutoka mayai 910,000 mwaka 2003/2004. Ongezeko hili lilitokana na matumizi ya chanjo ya Ugonjwa wa Mdondo. Mayai ya kutotolea vifaranga milioni 7.5 yaliagizwa toka nje na hivyo uzalishaji wa vifaranga kuwa milioni 29.9. Katika mwaka 2005/2006 matarajio ni kuzalisha vifaranga milioni 36 na mayai bilioni 2.1.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka uliopita, Wizara yangu ilikamilisha ujenzi wa machinjio ya kisasa katika Manispaa ya Dodoma, nia ya Serikali ni kuihusisha sekta binafsi katika kuendesha machinjio hayo. Hivyo, maandalizi yanaendelea ya kumpata mwekezaji wa kuendesha machinjio hayo kwa utaratibu wa kuuza asilimia 51 ya hisa kwa mwekezaji na asilimia 49 zitabakia Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, ngozi ziliendelea kuwa zao la mifugo linalouzwa kwa wingi nje na kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Ngozi za ng’ombe vipande milioni 1.6, za mbuzi vipande milioni 1.5 na za kondoo vipande 750,160 zilinunuliwa kutoka kwa wafugaji na kuwaingizia jumla ya shilingi bilioni 5.5. Kati ya hizo, ngozi zilizouzwa nje baada ya kukaguliwa ni vipande milioni 1.4 za ng’ombe, milioni 1.2 za mbuzi na 597,155 za kondoo zenye jumla ya shilingi bilioni 4.025. Ili kudhibiti biashara ya ngozi nchini, makampuni 18 yenye sifa zinazotakiwa yalipewa leseni za kununua na kuuza ngozi nje.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kuboresha zao la ngozi kupitia uboreshaji wa huduma za uchinjaji kwa kuwapatia mafunzo wachunaji, wawambaji na wachambuzi wa madaraja ya ngozi.

Mheshimiwa Spika, Masoko ya Mifugo, katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilijenga vituo vidogo vya mifugo 10 katika mikoa ya Mwanza, Manyara na Shinyanga na pia imekamilisha ujenzi wa kituo kikubwa cha mifugo cha Kindai mkoani Singida. Aidha, minada 7 ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi katika mikoa ya Iringa (3), Lindi (1), Mtwara (1), Morogoro (1) na Mbeya (1).

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea na ukarabati wa miundombinu katika maeneo ya Mbuyuni (Mbeya), Kimande (Iringa), Lumecha (Ruvuma), Malolo (Morogoro) na Kasesya (Rukwa). Aidha, ujenzi na ukarabati wa mnada wa mpakani wa Buhigwe mkoani Kigoma utafanyika na minada ya upili ya Meserani (Arusha) na Mhunze (Shinyanga) itawekewa uzio. Vilevile, vituo 11 vya kupakilia mifugo vitajengwa katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Ruvuma, Morogoro, Mtwara, Rukwa, Pwani, Kigoma, Arusha, Shinyanga na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Nyanda za Malisho, uendelezaji wa nyanda za malisho ni pamoja na kutambua, kutathmini uwezo wake, kutenga maeneo na kuyawekea miundombinu muhimu. Wizara yangu iliendelea kuzihamasisha Halmashauri za Wilaya kutenga maeneo ya mifugo na kuhakikisha wafugaji wanamilikishwa na kuyaendeleza ili kuwa na mipango ya ufugaji wa kisasa na endelevu.

Ili kuharakisha utengaji wa maeneo ya ufugaji, Wizara yangu iliwezesha utoaji wa mafunzo ya kutumia njia za kisasa za upimaji wa maeneo kwa wataalamu 24 kutoka Halmashauri za Wilaya 15 nchini ili wasaidie wafugaji kutoka Halmashauri hizo kutenga maeneo ya ufugaji. Aidha, wafugaji 34 na wataalamu 4 waliwezeshwa kupata mafunzo ya uanzishaji na uendeshaji wa ranchi kibiashara. Katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu itatoa mafunzo kwa wafugaji 70 kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa ranchi kibiashara.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza ufugaji bora nchini, ni muhimu kuhakikisha kwamba mbegu bora za malisho zinapatikana karibu na wafugaji. Katika mwaka 2004/2005, mashamba ya kuzalisha mbegu bora za malisho ya Vikuge (Pwani) na Langwira (Mbeya), yaliendelea kuimarishwa ili kuzalisha mbegu bora za nyasi na za jamii ya mikunde. Jumla ya tani 9.5 za mbegu bora za malisho na marobota 65,000 ya hei yalizalishwa katika mashamba hayo. Vilevile, uzalishaji wa mbegu na hei ulifanywa na sekta binafsi pamoja na taasisi mbalimbali za Serikali ambapo mbegu tani 5 na marobota 55,000 ya hei yalizalishwa.

Katika mwaka 2005/2006 lengo ni kuzalisha tani 10.5 za mbegu bora za malisho na marobota 70,000 ya hei katika mashamba ya Serikali. Aidha, sekta binafsi inategemewa kuzalisha tani 6.5 za mbegu bora za malisho na marobota 60,000 ya hei.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilichangia jumla ya shilingi milioni 105 kwa ajili ya uchimbaji na ukarabati wa malambo 22 katika mikoa ya Tanga (3), Mwanza (3), Arusha (1), Mara (2), Dodoma (3), Kilimanjaro (1), Kagera (1), Lindi (1) Mbeya (1) Morogoro (5) na Iringa (1). Pia, Wizara iliongeza kiwango cha uchangiaji kutoka shilingi milioni 3 hadi kufikia milioni 5 kwa lambo kwa lengo la kuongeza kasi na ubora wa uchimbaji na ukarabati wa malambo.

Nachukua fursa hii tena kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wasaidie juhudi za kuhamasisha Halmashauri za Wilaya na wananchi ili wachangie kikamilifu gharama za

uchimbaji na ukarabati wa malambo katika maeneo yao ili kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo yao.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara imetenga shilingi milioni 745 kwa ajili ya kuchangia uchimbaji na ukarabati wa malambo 120 katika Halmashauri za Wilaya 50 zenye ukame nchini.

Mheshimiwa Spika, Uzalishaji wa Vyakula vya Mifugo, vyakula vya mifugo vyenye virutubisho ni muhimu katika kuongeza uzalishaji na tija ya mifugo. Uzalishaji wa vyakula hivyo uliendelea kufanywa na Sekta binafsi. Katika mwaka 2004/2005, jumla ya tani 529,300 za vyakula vya mifugo zilizalishwa ikilinganishwa na mahitaji ya tani 650,000 kwa mwaka. Katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ili sekta binafsi iongeze uwekezaji katika uzalishaji wa vyakula hivyo katika viwango vinavyokubalika.

Mheshimiwa Spika, Uwezeshaji Wananchi Kufuga Kibiashara,uamuzi wa Serikali wa kugawa mashamba ya mifugo uliendelea kutekelezwa ambapo wawekezaji wamepatiwa maeneo kwenye mashamba yaliyogawanywa. Mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilikamilisha kupima na kugawa mashamba ya *NARCO* ya Mkata, Dakawa, Mzeri, Usangu na Kalambo kwa wawekezaji 48.

Ranchi za Kitengule, Misenyi, na *Kikulula Complex* zilizopo Mkoani Kagera na Uvinza Kigoma zilipimwa katika ranchi ndogo 73 na kutangazwa katika vyombo vya habari ili kupata wananchi watakaokuwa tayari kuwekeza. Kazi inayoendelea kwa sasa ni uchambuzi wa maombi hayo ili kuwapata waliokidhi vigezo vya kugawiwa mashamba hayo. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa wananchi wengi wamejitokeza kuwekeza katika mashamba hayo kwa lengo la kufuga kibiashara ambayo ni ishara nzuri kwa maendeleo ya Sekta ya Mifugo nchini. *(Makofi)*

Katika mwaka 2005/2006, Wizara itakamilisha ugawaji wa ranchi za Misenyi na Uvinza na upimaji wa ranchi ya West Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko iliendelea na juhudi za kuwahamasisha wafugaji na wadau wengine wa Sekta ya Mifugo kuunda vikundi na mitandao ili kuwa na nguvu ya pamoja katika kutatua matatizo yao ya ufugaji na kutafuta masoko. Vikundi ambavyo vimeanzishwa vimeendelea kuimarishwa na vingine kuunda mitandao katika ngazi mbalimbali. Mpaka sasa, kuna mitandao 15 mkoani Tanga na 24 Kagera ya wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa. Mikoa ya Iringa, Mbeya na Rukwa ina vikundi 365 vya wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa, vikundi 40 vya kuweka na kukopa na 93 vya uendeshaji wa majosho. Uundaji wa vikundi na mitandao utasaidia kusimamia shughuli zilizokuwa zinaendeshwa na wafadhili. Katika mwaka 2005/2006 uhamasishaji wa uundaji vikundi zaidi utaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Ugani, katika mwaka 2004/2005 huduma za ushauri ziliendelea kutolewa kwa wafugaji ili kuwawezesha kuongeza ubora wa mifugo

na mazao yatokanayo na mifugo hivyo kuongeza tija na mapato. Katika kutimiza azma hiyo, nakala za vijitabu vya ufugaji bora wa kuku, nguruwe na ng'ombe wa nyama zilisambazwa. Aidha, kitabu cha ufugaji bora wa kuku wa asili kilitayarishwa na kitasambazwa kwa wafugaji. Vilevile, mafunzo kwa wafugaji kwa njia ya vipindi vya redio na luninga yalitolewa ambapo jumla ya vipindi 52 vya redio vilirushwa hewani. Aidha, aina 10 za vipeperushi kuhusu ufugaji bora vilitayarishwa na zaidi ya nakala 10,000 zilisambazwa kwa wadau. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itaendelea kutoa huduma za ugani kwa wafugaji ili kufuga kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Huduma za Afya ya Mifugo, Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo, Serikali inaandaa na kutekeleza mipango ya uzuiaji wa magonjwa ya mifugo ya milipuko na yenye kuleta madhara kwa wafugaji na Taifa kwa ujumla. Magonjwa hayo ni pamoja na Sotoka, Homa ya Mapafu, Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Mdondo, Homa ya Nguruwe na Kichaa cha Mbwa. Magonjwa mengine ambayo madhara yake siyo makubwa na ambayo yanatibiwa au kukingwa kwa urahisi hushughulikiwa kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilinunua dawa za chanjo ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu *(CBPP)* dozi milioni 4 zilizogharimu shilingi milioni 400 (Kiambatanisho Na. 9). Aidha, Tanzania imepatiwa na *FAO* chanjo ya *CBPP* dozi milioni 2, majokofu 13, pikipiki 5 na vifaa mabalimbali vya maabara vyenye thamani ya shilingi milioni 600. Kazi ya uchanjaji iliendelea kutekelezwa chini ya mpango ambao ugonjwa unadhibitiwa eneo kwa eneo kwa kuanza na maeneo yaliyopata ugonjwa mwisho kuelekea maeneo ugonjwa ulipoanzia *(roll back vaccination plan)*. Kufikia mwezi Desemba 2005 ng'ombe milioni 5.1 watakuwa wamechanjwa.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara imetenga shilingi milioni 440 kwa ajili ya kununua dozi milioni 4 za chanjo ili kuendelea kudhibiti ugonjwa huo. Lengo ni kuwa na ukanda usio na maambukizo Kusini na Kusini Magharibi mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 ugonjwa wa Miguu na Midomo ulitokea katika Wilaya 68 na idadi ya mifugo iliyoambukizwa ni 56,610. Ili kupambana na ugonjwa huo, Halmashauri za Wilaya na wafugaji walishauriwa kuchanja ng'ombe dhidi ya ugonjwa huo, kuweka na kusimamia karantini wakati wa milipuko na kutoa taarifa za kila wiki kuhusu mwenendo wa ugonjwa huo.

Aidha, mradi wa pamoja wa kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo na Homa ya Mapafu uliwasilishwa na kupitishwa na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*. Hivi sasa, Mradi wa muda mfupi wa kudhibiti magonjwa hayo unaofadhiliwa na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa unatekelezwa katika nchi za Malawi, Tanzania, Zambia na Zimbabwe kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 2.6.*(Makofi)*

Katika mwaka 2005/2006 juhudi za pamoja zitaendelea ili kupata fedha za kutekeleza mradi wa kudhibiti Homa ya Mapafu na ugonjwa wa Miguu na Midomo.

Aidha, Wizara itakamilisha ujenzi wa maabara ya Ugonjwa wa Miguu na Midomo iliyoko Temeke na kununua vifaa vya maabara kwa gharama ya shilingi milioni 66.5.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Nguruwe ulitokea katika mikoa ya Kigoma, Kagera na Mwanza. Katika matukio hayo, kati ya nguruwe 138,775 waliokuwa hatarini, 2,976 walikufa.

Uchunguzi uliofanywa na Wizara ulibainisha kuwa aina ya virusi vya ugonjwa huo vinafanana na virusi vilivyopo nchini Burundi na Uganda. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika ilielekeza juhudi katika kudhibiti usafirishaji holela wa nguruwe; kuchinja nguruwe wote katika makundi yaliyoathirika; kusafisha mabanda kwa kutumia viuadudu; na kutoa elimu. Mwaka 2005/2006 Wizara kwa kushirikiana na Wilaya itaendelea kudhibiti ugonjwa huo usiendelee kuathiri ufugaji wa nguruwe.

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa Mdondo husababisha kuku wengi kufa kwa muda mfupi na hivyo kupunguza jitihada za wafugaji vijijini kuondokana na umaskini. Mwaka 2004/2005 Wizara ilitengeneza na kusambaza kwa wafugaji jumla ya dozi milioni 7.3. Mahitaji ya chanjo hiyo yanaongezeka kutokana na wafugaji wa kuku wa asili kuona matokeo mazuri ya chanjo hiyo.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kuweka mikakati na mipango ya kudhibiti ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya usambazaji wa chanjo ili iwafikie wananchi wengi zaidi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kudhibiti ueneaji wa magonjwa yaenezwayo na kupe nchini. Katika mwaka 2004/2005 Serikali kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs),* ilitoa shilingi milioni 549 kwa ajili ya kukarabati majosho 140. Aidha, Sekta binafsi kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ilikarabati jumla ya majosho 47 na hivyo kufanya jumla ya majosho yaliyokarabatiwa kufikia 187. Pia, jumla ya ng’ombe 12,494 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa Ndigana Kali.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Sekta binafsi na Wananchi itaendelea kujenga na kukarabati majosho na kuhamasisha wafugaji juu ya uchanjaji wa mifugo dhidi ya Ndigana Kali na kuchangia gharama za kuendesha majosho. Aidha, Serikali itatoa ruzuku kwa madawa ya kuogeshea mifugo ambapo shilingi milioni 500 zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 jumla ya ng’ombe 63,630 walipatwa na ugonjwa wa nagana. Aidha, taarifa za Wizara ya Afya zinaonyesha kuwa watu 146 walipatwa na maambukizi mapya ya ugonjwa wa malale ambapo watu 9 walikufa katika wilaya za Kasulu, Kigoma Vijijini na Kibondo mkoani Kigoma; Urambo mkoani Tabora na Mpanda mkoani Rukwa. Jumla ya viwambo 2,695 viliwekwa katika wilaya hizo.

Mbinu shirikishi zilitumika kuhamasisha wananchi kudhibiti mbung'o kwa kutumia mitego na vitambaa vyenye sumu katika vijiji vya Wilaya za Mpanda mkoani Rukwa na Urambo mkoani Tabora. Jumla ya wananchi 398 walipatiwa mafunzo ya kutengeneza viwambo (*targets*) na uwekaji wa mitego ya kuua mbung'o katika mikoa ya Rukwa na Tabora. Pia, mafunzo yalitolewa kwa maafisa ndorobo kutoka wilaya 29 zenye tatizo la mbung'o kuhusu mbinu shirikishi za kuzuia mbung'o na kudhibiti ugonjwa wa nagana katika wilaya zao. Vilevile, uchunguzi wa ueneaji wa mbung'o na utayarishaji wa ramani umefanywa katika wilaya zote za mikoa ya Shinyanga na Mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 udhibiti wa mbung'o utaendelea katika wilaya zenye tatizo la ugonjwa wa nagana na malale. Mafunzo ya wataalam juu ya teknolojia mpya za kudhibiti mbung'o yataendelezwa ili kuongeza ufanisi. Aidha, mashamba darasa 10 yaliyoanzishwa wakati wa mradi wa *FITCA* yataimarishwa. Uchunguzi wa maeneo mengine yenye mbung'o na uchoraji wa ramani mpya katika mikoa mingine yenye mbung'o utafanyika.

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa ni moja ya magonjwa yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama na hivyo kupewa kipaumbele na Wizara katika kuudhibiti. Mwaka 2004/2005 dozi 100,000 zilinunuliwa na kusambazwa katika wilaya 68 zilizokuwa na matukio mengi ya ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa. Pia, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya iliandaa mkakati wa kudhibiti ugonjwa huo nchini. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itanunua dozi 100,000 za chanjo hiyo ili kuendelea kupambana na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 ugonjwa wa Kimeta ulitokea katika mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma na Dar es Salaam. Katika juhudi za kuudhibiti ugonjwa huo, jumla ya ng'ombe 24,840, mbuzi na kondoo 8,203 na nguruwe 93 walichanjwa. Katika mwaka 2005/2006 Wizara itashirikiana na Halmashauri za Wilaya kuhakikisha uchanjaji unafanyika kikamilifu ili kuudhibiti ugonjwa huo ambao pia unaambukiza binadamu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kutoa kipaumbele katika kudhibiti ugonjwa wa Kutupa Mimba ambao pia huambukiza binadamu. Mwaka 2004/2005 jumla ya ng'ombe 5,130 walifanyiwa uchunguzi wa ugonjwa wa Kutupa Mimba katika Kanda ya Ziwa (4,867) na kanda ya Nyanda za Juu Kusini (263). Kati ya hao, ng'ombe 732 sawa na asilimia 7 walionekana kuwa na vijidudu vya ugonjwa huo na hivyo kushauriwa wachinjwe, ili kupunguza hatari ya kuenea kwa ugonjwa huo. Aidha, maandalizi ya kutengeneza chanjo ya ugonjwa huo (S.19) yalianza ambapo jumla ya vichupa 12 vya vimelea *(master seed),* vilinunuliwa kutoka Kenya kwa ajili ya kuanza kutengeneza chanjo hiyo.

Katika mwaka 2005/2006, ng'ombe 10,000 watafanyiwa uchunguzi wa ugonjwa wa kutupa mimba katika kanda za Kati na Ziwa na kuanza kuzalisha chanjo ya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kuwa huru kutokana na magonjwa mapya ya mifugo yanayoisumbua dunia kwa sasa. Magonjwa hayo mapya ni pamoja na

Kichaa cha Ng'ombe *(Bovine Spongiform Encephalopathy - BSE)* na Mafua Makali ya Ndege *(Highly Pathogenic Avian Influenza - HPAI)*. Ugonjwa huu wa Mafua Makali ya Ndege ambao pia huambukiza binadamu ulitokea kwa mara ya kwanza Mashariki ya mbali na hivi karibuni umeonekana katika kundi la mbuni huko Afrika Kusini.

Jitihada zilizofanyika kuzuia magonjwa hayo yasiingie nchini ni pamoja na kupiga marufuku uingizaji wa ndege, ng'ombe na mazao yao kutoka nchi zilizoathirika; kuimarisha ukaguzi wa mifugo na bidhaa zitokanazo na mifugo mipakani; na kuelimisha wananchi kuhusu athari za magonjwa hayo.

Mheshimiwa Spika, Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo,Wizara yangu iliendelea kuimarisha ufuatiliaji wa mienendo ya magonjwa ya mifugo ikiwa ni pamoja na kujenga mfumo wa kutoa taarifa na kuimarisha Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo vya Kanda *(VICs)* na Maabara Kuu ya *ADRI Temeke.* Pia, Maabara Kuu ilichunguza jumla ya ndege 5,439 dhidi ya ugonjwa wa mdondo kabla ya kusafirishwa kuuzwa nchi za nje.

Katika mwaka 2004/2005 Wizara iliimarisha Kitengo cha Kufuatilia Mienendo ya Magonjwa ya Mifugo kwa kukipa uwezo wa kuchambua takwimu kwa kutumia programu ya mawasiliano ya ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za magonjwa ya mifugo. Kutokana na juhudi hizo, takwimu zilizowasilishwa kutoka wilayani zimeongezeka toka wilaya 61 mwaka 2003/2004 hadi kufikia wilaya 85 mwaka 2004/2005 na Wizara ilipokea wastani wa taarifa 896 kwa kila mwezi ikilinganishwa na 789 mwaka 2003/2004. Aidha, majengo na maabara ya vituo vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo vya Mpwapwa, Arusha, Tabora na Mtwara yalikarabatiwa na kupatiwa madawa ya maabara na vifaa vya ofisi.

Katika mwaka 2005/2006, ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za magonjwa ya mifugo utaendelea kuimarishwa katika ngazi zote. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha vituo vya uchunguzi wa magonjwa ili viweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Mifugo, Ubora wa Mazao na Pembejeo, ukaguzi wa mifugo na mazao yake unalenga kuepusha uingizaji na usambaaji wa magonjwa nchini. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilijenga kituo cha ukaguzi wa mifugo cha mpakani cha Kasesya wilayani Sumbawanga na kuimarisha kituo cha Kibaha eneo la Mizani. Aidha, pikipiki 34 na baiskeli 300 zimetolewa kwa maafisa mifugo na wakaguzi katika wilaya za mipakani. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaimarisha vituo vya ukaguzi vya Kasumulu, Isongole, Mutukula/Kyaka, Manyovu, Mabamba, Pangani na Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za Afya na Viwanda na Biashara; pamoja na Halmashauri za Wilaya, inasimamia udhibiti wa usalama na ubora wa mazao yatokanayo na mifugo, vyakula na madawa ya mifugo.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilikagua machinjio na mabanda ya ngozi katika mikoa ya kanda za Mashariki na Kaskazini ili kuhakiki hali ya machinjio na

mabanda hayo kama yanakidhi viwango vinavyokubalika. Ukaguzi huo ulibainisha kuwa machinjio nyingi zilizopo katika makao makuu za wilaya na mikoa hiyo zipo katika hali mbaya kimajengo, usafi na zinakosa vitendea kazi muhimu. Kufuatia ukaguzi huo, Wizara yangu ilitoa ushauri kwa Halmashauri za wilaya, Miji na Manispaa husika kutoa kipaumbele katika kukarabati, kujenga, kusimamia na kuendesha machinjio hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea na ukaguzi wa machinjio na mabanda ya ngozi katika kanda za Magharibi na Ziwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 udhibiti wa ubora wa pembejeo za mifugo ulihusisha uchunguzi wa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa viwandani pamoja na malisho katika kanda mbili za Ziwa na Magharibi. Pia, uwezo wa kuchunguza ubora wa pembejeo za mifugo katika Maabara Kuu ya ADRI-Temeke uliongezwa kwa kukamilisha uwekaji wa mashine mpya ya kupimia vyakula vya mifugo yenye uwezo wa kupima sampuli 10 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, uchunguzi wa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa viwandani pamoja na malisho utafanyika katika kanda za Kati, Kaskazini, Kusini na Nyanda za Juu Kusini. Vilevile, udhibiti wa ubora wa dawa za tiba na kinga ya magonjwa ya mifugo, vyakula vya mifugo na mbegu za uzalishaji utaimarishwa ili kulinda afya ya mifugo na walaji. Wizara yangu itanunua vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuimarisha maabara za kanda *(VICs),* ili kusogeza huduma za udhibiti wa ubora wa mazao ya mifugo na pembejeo karibu na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 uhamasishaji wa jamii juu ya kudhibiti ubora na usalama wa vyakula vitokanavyo na mifugo ulifanyika kwa njia ya vipeperushi na mikutano ya wadau. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kuimarisha udhibiti wa ubora na usalama wa vyakula vinavyotokana na mifugo. Aidha, wadau mbalimbali na jamii kwa ujumla watahamasishwa kuzingatia ubora katika uzalishaji wa vyakula hivyo ili kukidhi viwango vilivyowekwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Utoaji Huduma za Afya ya Mifugo,Wizara yangu ina jukumu la kusimamia utoaji wa huduma za afya ya mifugo kwa lengo la kuhakiki viwango na ubora wa utoaji wa huduma za mifugo, ikizingatiwa kuwa huduma hizo sasa zinatolewa na sekta binafsi. Mwezi Oktoba, 2004 Wizara yangu ilizindua Baraza la Tiba ya Wanyama lenye jukumu la kusajili, kudhibiti na kusimamia utendaji wa madaktari, wataalam wasaidizi, na vituo vya kutolea huduma za tiba ya wanyama. Ili kusogeza huduma za Baraza karibu na wananchi, mwaka 2004/2005, Baraza lilikasimu baadhi ya majukumu yake kwa wasajili wasaidizi 68 walioteuliwa katika ngazi ya wilaya.

Pia, Baraza lilifanya ukaguzi wa vituo vya kutolea huduma za mifugo katika wilaya za mkoa wa Ruvuma ili kuhakiki hali ya huduma na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Baraza liliandikisha wataalam wenye stashahada 64 na kuorodheshwa wenye astashahada 67 kwa lengo la kusimamia utoaji wa huduma za afya za mifugo katika ngazi zote. Aidha, jumla ya vituo 11

vilisajiliwa na kufanya jumla ya vituo vya kutolea huduma nchini vilivyosajiliwa kufikia 100. Katika mwaka 2005/2006, Baraza litaendelea kuhamasisha utoaji wa huduma na usajili kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba huduma nyingi za afya ya mifugo kwa sasa zinatolewa na sekta binafsi ambayo ina asilimia 60 ya Madaktari wa Mifugo nchini, mwaka 2004/2005 Wizara ilitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa madaktari 10 wa Sekta Binafsi na kufanya idadi ya waliopata mafunzo hayo kufikia 30. Aidha, Halmashauri za Wilaya 16 zilihamasishwa juu ya ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutoa huduma za tiba ya mifugo na uzuiaji wa kupe na magonjwa yaenezwayo na kupe.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kuhamasisha Halmashauri za Wilaya juu ya ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutoa huduma za afya ya mifugo. Pia, Wizara itahamasisha wataalam kuunda na kuimarisha umoja ili waweze kutetea maslahi yao. Aidha, Wizara itaendelea kutoa miongozo inayohusu taaluma na kuimarisha mawasiliano na watoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utafiti na Mafunzo katika Sekta ya Mifugo, Wizara inalo jukumu la kufanya utafiti wa mifugo kwa lengo la kuzalisha na kusambaza teknolojia zinazoongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo; kutambua; na kudhibiti magonjwa ya mifugo. Wizara iliendelea na utafiti wa mifugo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine; Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa; Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (*International Livestock Research Institute*); na Chuo Kikuu cha Sayansi cha Austria.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea na uzalishaji wa ng’ombe aina ya Mpwapwa ambao wamethibitika kuwa na sifa ya kuhimili magonjwa na wana uwezo wa kutoa maziwa na nyama kwa wingi. Katika mwaka 2004/2005, madume 90 yaliuzwa kwenye vikundi vya wafugaji vya Chipogoro - Mpwapwa (4); Longido (32); Ngorongoro (32); Manyoni (16) na Kiteto (6) kwa lengo la kuboresha ng’ombe wa asili. Jumla ya ndama 414 wamezalishwa kutokana na madume hayo.

Mheshimiwa Spika, mbuzi chotara (*Blended goat),* wameongezeka katika vituo vya Mpwapwa (225), Kongwa (281) na West Kilimanjaro (135) na wanaendelea kufanyiwa utafiti. Hivi sasa, madume aina ya Boer yaliyopatikana kupitia *Heifer Project International* (*HPI*), yanatumika kuboresha na kuondoa tatizo la kuzaliana kwa koo moja.

Katika mwaka 2005/2006, jumla ya ndama 315 aina ya Mpwapwa wanatarajiwa kuzalishwa na madume zaidi yataendelea kuuzwa kwa vikundi vya wafugaji. Aidha, uzalishaji wa mbuzi chotara utaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, utafiti na uzalishaji wa mbegu za malisho umeendelea katika Taasisi ya Mpwapwa. Katika mwaka 2004/2005, mbegu bora ya nyasi kilo 2,418 na mikunde kilo 235 zilizalishwa. Aidha, Kituo cha Utafiti wa Mifugo Tanga kiliendelea na utafiti wa michanganyiko bora ya lishe ya ng’ombe wa maziwa na matokeo yake yalionyesha kuwa lishe hiyo iliweza kuongeza uzalishaji wa maziwa kutoka lita 6.0 na

kufikia 7.5 kwa siku sawa na ongezeko la asilimia 16.4 ya uzalishaji. Pia, majaribio ya ulishaji wa majani ya mihogo yaliyosindikwa yaliongeza uzalishaji wa maziwa kwa wastani wa lita 2 kwa siku. Matokeo ya utafiti huo hutumiwa na Wizara yangu na wadau wengine kuelimisha wafugaji ili kuboresha uzalishaji wa maziwa. Katika mwaka 2005/2006 utafiti kuhusu michanganyiko bora ya lishe utaendelezwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utafiti shirikishi wenye lengo la kutambua, kuendeleza na kuhifadhi koo mbalimbali za mifugo ya asili uliendelea kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa *(FAO)*. Ng'ombe wa asili aina ya *Singida White, Iringa Red,* Tarime, Ankole (Kigoma na Kagera) na Mkalama (Kondoa) walitambuliwa kwa lengo la kudumisha na kuhifadhi koo hizo. Ng'ombe wa aina hizo wana sifa ya kustahimili mazingira magumu ya malisho, maji na magonjwa ikilinganishwa na ile ya kutoka nje.

Pia, aina mbili za mbuzi wenye sifa ya kuzaa mapacha wameainishwa kutoka Ujiji Kigoma na Newala Mkoani Mtwara. Katika mwaka 2005/2006 utambuzi na uhifadhi wa koo zingine utaendelea kufanywa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua ubora wa ng'ombe wa asili, Chuo Kikuu cha Sayansi cha Austria kimekubali kuzisaidia nchi za Tanzania, Uganda, Burundi na Rwanda kufanya tathmini ya kina ya ng'ombe aina ya Ankole na hatimaye kuwaendeleza na kuwadumisha. Pamoja na sifa zingine, ng'ombe aina ya Ankole wana rehemu *(Cholesterol)* kidogo ambayo haileti madhara kwa walaji ukilinganisha na aina nyingine za ng'ombe.

Katika mwaka 2005/2006, utafiti kuhusu ng'ombe aina ya Ankole utaendelea kufanyika katika mikoa ya Kigoma na Kagera.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 utafiti wa kujua aina ya mbung'o waliopo kisiwani Mafia ulifanyika ambapo imeonyesha kuna aina moja tu ya mbung'o aina ya *Glossina brevipalpis*.

Pia, utafiti wa aina hiyo ulifanyika katika mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Manyara ambapo mbung'o aina ya *Glossina swynnertoni* walionekana. Kupatikana kwa mbung'o aina moja katika eneo husika itarahisisha uangamizaji wake kwa kutumia madume ya aina hiyo yaliyohasiwa na ambayo yatazalishwa hapa nchini.

Vilevile, uzalishaji wa madume ya mbung'o yaliyohasiwa uliendelea kwa lengo la kuwasambaza nchini na katika nchi za Ethiopia na Afrika ya Kusini. Katika mwaka 2005/2006, kazi ya kufuatilia matukio ya usambaaji na aina ya mbung'o itaendelea.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendesha vyuo 5 vya mafunzo ya mifugo vya Morogoro, Mpwapwa, Tengeru, Buhuri na Madaba. Katika mwaka 2004/2005 jumla ya wataalam 395 wamehitimu mafunzo yao katika ngazi ya stashahada na astashahada kutoka vyuo vya Mifugo vya Tengeru, Morogoro na Mpwapwa. Aidha, katika kukabiliana na upungufu wa wataalam wa maabara za mifugo, maandalizi ya kuanzishwa

kozi ya stashahada ya mafundi sanifu wa maabara ya mifugo yalianza katika chuo cha *LITI Temeke.* Pia, mafunzo mbalimbali ya muda mfupi yalitolewa kwa wafugaji 1,434 kuhusu mbinu za ufugaji bora na utunzaji wa mazingira.

Katika mwaka 2005/2006, lengo ni kuwa na idadi ya wanafunzi 800 katika vyuo vya mifugo nchini ili kutumia kikamilifu uwezo uliopo. Kati ya wanafunzi hao, 241 watagharamiwa na Serikali na 559 watajigharamia. Aidha, mafunzo ya stashahada katika teknolojia ya maabara ya mifugo yataanza rasmi. Pia, jumla ya wafugaji 1,560 watapatiwa mafunzo ya ufugaji bora.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara yangu iliendelea kuboresha mazingira ya vyuo kwa kukarabati majengo, miundombinu na kuvipatia wataalam na vifaa kwa gharama ya shilingi milioni 105. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu imetenga shilingi milioni 310 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya vyuo kwa kuendelea na ukarabati na kuvipatia vifaa.

Mheshimiwa Spika, kazi za kuboresha mitaala, kuchapisha vitabu vya kiada na ziada na kuhuisha mihutasari ya mafunzo ni muhimu ili kukidhi mahitaji ya wadau na kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Mwaka 2004/2005 kitabu cha uzalishaji wa mifugo na uhamilishaji kiliandaliwa na kuchapishwa. Aidha, ili kudhibiti ubora wa mafunzo vyuoni, Wizara yangu ilifanya ukaguzi wa taaluma na kuendesha mitihani ya pamoja kati ya vyuo vyenye kozi zinazofanana.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara itaandaa kitabu cha kiada cha mazao ya mifugo; kuandika moduli za kozi za ufugaji bora wa nguruwe, mbuzi wa maziwa, kuku wa mayai na nyama kwa ajili ya kozi za muda mfupi. Ili kuboresha taaluma, vyuo vyote vitakaguliwa na pia maandalizi ya awali ya kuweka mihutasari ya kozi za astashahada na stashahada katika moduli ili kozi zinazotolewa na vyuo hivyo ziweze kuandikishwa na kutambuliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*).

Mheshimiwa Spika, Masuala ya Jumla ya Sekta za Maji Na Mifugo, Maendeleo ya Watumishi, Wizara yangu ina jumla ya watumishi 3,110 ikilinganishwa na mahitaji yake ambayo ni watumishi 3,446. Kati ya hao waliopo sasa, watumishi 1,610 ni wa Sekta ya Maji na 1,500 ni wa Sekta ya Mifugo. Katika mwaka 2004/2005, jumla ya watumishi 1,353 walipandishwa vyeo, watumishi 83 walibadilishwa vyeo, watumishi 150 walithibitishwa kazini, 29 waliajiriwa na watumishi 200 walipata mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu imepewa ikama ya kuajiri watumishi 336. Aidha, watumishi wenye sifa watapandishwa vyeo kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma. Watumishi 500 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje. Pia, Wizara itaendelea na zoezi la kuwathibitisha kazini watumishi wanaomaliza muda wao wa majaribio kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Usimamizi na Uratibu, Wizara yangu inashirikiana na TAMISEMI, Halmashauri za Wilaya, Taasisi ya Takwimu ya Taifa na Wizara nyingine katika kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza takwimu na taarifa kwa

watumiaji kulingana na mahitaji. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, Wizara yangu inashiriki kutoa takwimu mbalimbali zinazohusu kupunguza umaskini kwa ajili ya usambazaji kupitia tovuti ya kitaifa inayohusu taarifa za kiuchumi na kijamii. Takwimu hizo zinatumika kutathimini maendeleo ya Sekta za Maji na Mifugo katika suala zima la kupambana na umasikini. Aidha, kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la *WaterAid*, Wizara yangu, ilianzisha tovuti ambayo inatumika katika kueneza Sera na taarifa mbalimbali za Sekta za Maji na Mifugo kwa wadau. Tovuti hiyo inapatikana kwa anwani *www.maji-mifugo.go.tz*.

Katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa takwimu na taarifa mbalimbali zinazohusu sekta za Maji na Mifugo.

Mheshimiwa Spika, Jinsia, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuainisha masuala ya jinsia katika kutekeleza malengo ya MKUKUTA na Sera za Maji na Mifugo. Katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu imetekeleza masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha Dawati la Jinsia kwa kuteua Mratibu wa jinsia wa Wizara; kuandaa mkakati wa jinsia wa Sekta za Maji na Mifugo; kuunda kamati ya kuratibu masuala ya jinsia na kutoa mafunzo na uhamasishaji kwa viongozi na watumishi.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara husika pamoja na wadau wengine itatekeleza Mkakati wa Jinsia pamoja na mpango wa kuongeza ushiriki wa wanawake katika maamuzi kulingana na mwongozo wa Tume ya Utumishi wa Umma kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kujenga uwezo wa dawati la jinsia;

(b) Kutoa mafunzo ya kijinsia kwa viongozi na wafanyakazi;

(c) Kuelimisha na kuwahamasisha watumishi wanawake kujua haki zao na sheria mbalimbali za nchi;

(d) Kuweka vigezo vyenye mtazamo wa kijinsia vitakavyohakikisha kuwepo kwa usawa na haki za kijinsia kweye Idara zote ili kutoa mwongozo katika uandaaji wa sera, bajeti na ajira; na

(e) Kuimarisha ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu pamoja na taarifa zenye kuainisha masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Spika, UKIMWI, mojawapo ya malengo ya mkakati wa Wizara wa kudhibiti UKIMWI ni kuhamasisha watumishi kuhusu mbinu za kujikinga na kutoa huduma kwa watumishi walioathirika na wanaoishi na virusi. Kulingana na mkakati huo, Wizara itatoa msaada wa hali na mali kwa watumishi watakaojitokeza. Kutokana na Kanuni na Haki za Binadamu, mwathirika wa UKIMWI anapaswa kujitangaza au kutoa taarifa kwa mwajiri wake kwa ridhaa yake bila kushinikizwa. Katika kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti UKIMWI, mwaka 2005/2006, yafuatayo yatatekelezwa:-

Kuendesha semina za uhamasishaji wa watumishi kuhusu namna ya kukwepa maambukizi mapya ya UKIMWI;

Kununua na kusambaza kondomu kama kinga dhidi ya UKIMWI;

Kusambaza vipeperushi, mabango pamoja na vitabu vyenye ujumbe wa UKIMWI; na

Kuendelea kushirikiana na Tume ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI kuona kuwa ni namna gani waathirika wanaweza kupunguziwa makali ya ugonjwa na kuboresha afya zao.

Mheshimiwa Spika, Rushwa, katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu iliendelea kuziba mianya ya rushwa katika Sekta za Maji na Mifugo pamoja na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia Rushwa. Katika kutekeleza mkakati huo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Kitengo cha Utawala Bora pamoja na Taasisi ya Kuzuia Rushwa, imetoa mafunzo kwa Watumishi kwa njia ya Semina kwa lengo la kuwaelimisha madhara ya kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kuziba mianya ya rushwa na kuboresha huduma kwa wateja ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia Rushwa na mpango uliowekwa kutekelezwa kisekta. Aidha, Wizara itaimarisha kitengo cha Sheria cha Wizara ambacho kitakuwa mhimili wa kutoa na kufafanua mambo mbalimbali ya kisheria na pia itaendelea kusimamia kikamilifu Sheria Na.4 ya mwaka 2004, ambayo kwa kiasi kikubwa inapunguza mianya ya rushwa katika manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Shukrani, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2004/2005 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa nchi wahisani, mashirika ya misaada, taasisi zisizokuwa za kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za kifedha. Napenda kuzishukuru Serikali za nchi ya Ujerumani, Japan, Ufaransa, Jamhuri ya Watu wa China, Uholanzi, Denmark, Uswisi, Ireland, Ubelgiji na Uingereza. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa taasisi za fedha za kimataifa, yaani Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA),* Mfuko wa Kuendeleza Mazao ya Kilimo na Mifugo *(CFC),*

Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB),* Umoja wa Nchi zinazouza Mafuta Duniani *(OPEC),* Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU),* Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNDP, UNICEF, FAO, UNIDO, IFAD, Global Environmental Facility (GEF),* Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki na Taasisi ya Raslimali ya Wanyama ya Umoja wa Afrika *(AU/IBAR)* kwa misaada na michango yao ya utaalamu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu. (*Makofi*)

Aidha, nayashukuru Mashirika ya kidini ya World Islamic League, Shirika la *Al Munadhanat Al Dawa Al Islamia,* Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT),

Kanisa la Kilutheri la Ujerumani na Kanisa Katoliki Tanzania *(TEC),* pamoja na Taasisi nyingine za hiari za *WaterAid, Vet Aid* na *OXFAM* za Uingereza, *Austro-Project, Heifer Project International (HPI), World Vision, FarmAfrica,* Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili *(IUCN), World Wildlife Fund (WWF),* na wale wote ambao kwa njia moja au nyingine wanaendelea kuisaidia Wizara yangu katika kutoa huduma kwa wananchi. Naomba, kwa dhati kabisa, kupitia kwako nitumie fursa hii kuwashukuru wote na niwaombe waendelee kushirikiana na Wizara yangu kwa mwaka ujao wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Mbunge wa Mwanza Vijijini kwa msaada na ushauri wake wa karibu. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Ndugu Vincent Mrisho na Naibu Katibu Mkuu Dr. Charles Nyamrunda, Wakuu wa Idara, Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara yangu pamoja na watumishi wote kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Sekta za Maji na Mifugo. Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2005/2006, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 148,087,271,500/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2005/2006. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi 24,870,271,500/= ambapo shilingi 6,018,671,500/= ni Mishahara ya Watumishi *(PE),* na shilingi 18,851,600,000/= ni fedha za Matumizi Mengine *(OC).* Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 123,217,000,000/=, ambapo kati ya hizo shilingi 70,207,000,000/= ni fedha za ndani na shilingi 53,010,000,000/= ni fedha za nje. Kwa mara ya kwanza tumeongeza fedha za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Waliomba kuchangia hoja hii wanafika 16 lakini hawataweza kupata nafasi wote, kwa hiyo naomba niwataje ambao kwa muda uliopangwa wataweza kupata nafasi ya kuchangia kwa mdomo ili wajiandae kufanya hivyo na wengine wachangie kwa maandishi. Waliochangia mara moja ni watatu wote watapata nafasi nao ni Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Esha Stima na Mheshimiwa Herbert Mntangi. Waliochangia mara mbili watakaopata nafasi ya Mheshimiwa Michael Lekule, Mheshimiwa Faustine Kabuzi, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Abdillahi Namkulala. Sasa

namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi aweze kutoa maoni ya Kamati yake. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka uliopita na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi ambao ndio waliochambua Bajeti hii nao ni :-

1. Mheshimiwa Eliachim Simpassa, Mb. - Mwenyekiti;
2. Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mb. - M/Mwenyekiti;
3. Mheshimiwa Dr. Suleiman J. Omar, Mb. - Mjumbe;
4. Mheshimiwa Joel Bendera, Mb. - Mjumbe;
5. Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mb. - Mjumbe;
6. Mheshimiwa Abdillah Namkulala, Mb. - Mjumbe;
7. Mheshimiwa Edward Nziriye Ndeka, Mb. - Mjumbe;
8. Mheshimiwa Robert Mashalla, Mb - Mjumbe;
9. Mheshimiwa John Singo, Mb. - Mjumbe;
10. Mheshimiwa Masoud Salim, Mb. - Mjumbe;
11. Mheshimiwa Ali Salim, Mb. - Mjumbe;
12. Mheshimiwa Phillip Magani, Mb. - Mjumbe;
13. Mheshimiwa Anatory Choya, Mb. - Mjumbe;
14. Mheshimiwa Charles Kagonji, Mb. - Mjumbe;
15. Mheshimiwa Kidawa Saleh, Mb. - Mjumbe;
16. Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mb. - Mjumbe;
17. Mheshimiwa Salama Islam, Mb. - Mjumbe;
18. Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mb. - Mjumbe;
19. Mheshimiwa Said Nkumba, Mb. - Mjumbe;
20. Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mb. - Mjumbe;
21. Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mb. - Mjumbe; na
22. Mheshimiwa Paul Makolo, Mb. - Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji Wa Ushauri Wa Kamati Kwa Mwaka 2004/2005, katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati yangu ilitoa ushauri na maagizo takriban 16 katika maeneo kadhaa, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika imeshauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio na Matatizo Katika Utekelezaji wa Bajeti 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio, Kamati yangu ilifahamishwa mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa mwaka wa fedha uliopita. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na:-

(i) Rasimu ya mwisho ya Sera ya Mifugo ya Taifa (2005), imekamilika na kuwasilishwa Serikalini mwezi Aprili.

(ii) Sheria mbili muhimu, zinazohusu Magonjwa ya Mifugo na Huduma za mifugo *(Animal Diseases Act, 2003 na Veterinary Act, 2003)* zilizopitishwa na Bunge na Mheshimiwa Rais ameridhia zianze kutumika. Aidha, Baraza la Madaktari wa Mifugo *(Veterinary Council of Tanzania)* limeundwa mwezi Oktoba 2004 kulingana na Sheria ya Huduma za Mifugo *(Veterinary Act).*

(iii) Sheria mpya ya Maziwa ya mwaka 2004 *(The Dairy Industry Act 2004)* iliyopitishwa na Bunge mwezi Aprili 2004 imekwishaanza kutumika. Pia, Bodi ya Maziwa imeanzishwa rasmi.

(iv) Dozi 100,000 za chanjo dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa zimenunuliwa na kusambazwa katika Wilaya 68 zilizokuwa na matukio mengi ya ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa.

(v) Mamlaka za usimamizi wa rasilimali za Maji katika mabonde yote tisa ya maji nchini zimeanza kazi baada ya kukamilika taratibu za uanzishwaji wa mamlaka (Bodi) za mabonde mawili ya mwisho (Ziwa Tanganyika na Bonde la Mto Ruvuma na Lukuledi).

(vi) Tanzania kwa kushirikiana na Msumbiji imeanza maandalizi ya kuunda chombo cha pamoja cha kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji katika Bonde Shirikishi la Mto Ruvuma.

(vii) Serikali imechunguza jumla ya maeneo 311 yanayofaa kuchimba visima vya maji sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Matatizo, pamoja na mafanikio hayo Kamati pia ilifahamishwa matatizo yanayoikabili Wizara ambayo baadhi yake ni kama ifuatavyo:-

(i) Juhudi za Wizara za kupeleka majukumu ya utekelezaji kwenye Halmashauri za Wilaya hazijaonyesha mafanikio ya kutosha. Hali hii inasababishwa na kutokuwa na wataalamu wa kutosha katika ngazi za Wilaya na pia uelewa mdogo katika ngazi ya Wilaya kuhusu umuhimu wa kuwa na Wataalamu wenye kiwango cha elimu kinachotakiwa.

(ii) Katika Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2004/2005 kiasi cha fedha za nje kilichokasimiwa hakikutolewa chote kutokana na baadhi ya wahisani kushindwa kutoa fedha zote kama walivyoahidi.

(iii) Tija ndogo katika uzalishaji wa mifugo hasa kwa wafugaji wa Sekta ya Asili *(Traditional Sector),* umefanya sekta hii kushindwa kuchangia kikamilifu katika pato la Taifa.

(iv) Tatizo la kuenea kwa magonjwa mbalimbali ya Mifugo na hasa ya milipuko yanaathiri kwa kiasi kikubwa tija na maendeleo ya Sekta ya Mifugo nchini.

(v) Sekta za Maji na mifugo hazivutii wawekezaji binafsi kutokana na gharama kubwa za uwekezaji. Kwa upande wa Sekta ya Maji mwelekeo zaidi ni kutoa huduma badala ya faida, wakati kwa upande wa Sekta ya Mifugo viwango vya uwekezaji ni vikubwa na inachukua muda mrefu kuanza kuzalisha kwa faida.

(vi) Uhaba wa viwanda vya kusindika mazao yatokanayo na mifugo, masoko ya uhakika na kukosekana kwa miundombinu ya kuwezesha kuuza bidhaa za mifugo katika soko la Kimataifa.

(vii) Wafugaji wengi hawana uwezo wa kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha kutokana na masharti magumu yanayowekwa na vyombo husika.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati, Sekta ya Maji. Kwa upande wa mfuko wa maji, Kamati inashauri Sheria mbili zinazohusu Sekta ya Maji yaani *Water Resources Act Water Supply and Sanitation Act* zirekebishwe kuwa pamoja ili kutowachanganya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri fedha za miradi ya maendeleo zipelekwe moja kwa moja vijijini bila kuwepo kwa masharti kama ya kuchangia asilimia 50 kama ilivyo katika mipango ya MMEM na MMES na hili Mheshimiwa Waziri amelitaja sasa hivi hapa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upungufu wa Wataalam wa maji, jambo linalosababisha miradi mingi kukwama. Pia kuna miradi ambayo bado haijaendelezwa pamoja na kuwa fedha zilikwishatengwa. Kamati inaishauri Wizara itafute njia ya kuweza kuongeza Watalaam wa maji. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kubuni mbinu za ufuatiliaji wa miradi iliyokwisha tengewa fedha ili kubaini tatizo ni nini hasa na hatimaye ufumbuzi upatikane.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebarikiwa kuwa na Vyanzo vingi vya maji, je kuna mpango gani ili kuhakikisha kwamba vyanzo hivyo vinatumika ipasavyo ili kukidhi haja ya mahitaji ya maji? Kwa mfano, Maji ya Mto Pangani hadi sasa hayatumiki kwa kunywa. Kamati inashauri Mito hii itumike vizuri ili tatizo la maji safi nchini litoweke kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuwa bei za maji zinapangwa kiholela na kwamba ankara zinazotolewa ni kubwa kuliko matumizi halisi. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za maji itafute

mbinu za kudhibiti tatizo hilo na hasa kwa Watendaji wa mamlaka wenye mtindo wa kubambikizia wateja ankara zisizo halali.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati ilipata Taarifa kuhusu matatizo yaliyojitokeza kati ya Serikali na Kampuni ya *City Water.* Kamati ilizipokea na kuunga mkono hatua zilizochukuliwa na Serikali. Lakini ikashauri kwamba, hatua zozote zitakazo chukuliwa katika mabadiliko haya, hazina budi kuangalia maslahi ya Wafanyakazi waliopo, pamoja na kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo husika wanapata huduma ya maji bila kuathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo, hali ya majosho bado si nzuri. Kamati inaishauri Wizara iwe na mkakati maalum kushughulikia majosho katika Wilaya zote ili kuokoa maisha ya mifugo. Aidha jitihada zisiwekwe katika majosho yaliyopo tu bali utafutwe uwezekano wa kujenga majosho mapya. Hata hivyo, Kamati inapongeza sana Serikali kwa hatua ambazo Wizara inaendelea kuzichukua kuhusu tatizo hili hali ya majosho bado si nzuri. Kamati inaishauri Wizara iwe na mkakati maalum kushughulikia majosho katika Wilaya zote ili kuokoa maisha ya mifugo.

Aidha, jitihada zisiwekwe katika majosho yaliyopo tu bali utafutwe uwezekano wa kujenga majosho mapya. Hata hivyo, Kamati inapongeza hatua ambazo Wizara inaendelea kuzichukua kuhusu tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado haijafanikiwa sana katika kusaidia Wafugaji hasa katika suala la kuwatafutia masoko na kuwapatia ushauri wa kitaalamu. Kamati inaishauri Serikali iwasaidie wafugaji katika nyanja hizo. Aidha, kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali, Wizara iboreshe minada ya mifugo na kupiga marufuku minada isiyotambuliwa rasmi na Serikali ili kuepusha ukwepaji wa ushuru na uenezaji wa magonjwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Wizara kukabiliana na magonjwa kama kupe/ndorobo na minyoo, bado Halmashauri haziwajibiki ipasavyo katika suala hili. Kamati inaishauri kuwepo na mahusiano baina ya Wizara na Halmashauri ili usimamizi uweze kufanyika na hivyo kuleta ufanisi. Wizara ipaswa kuwa na kauli dhidi ya utendaji na utekelezaji wa miradi yake kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kichaa cha mbwa bado ni tishio. Kamati inashauri Wizara iangalie ni vipi itashirikiana na TAMISEMI kuona uwezekano wa dawa za ugonjwa zinavyoweza kupatikana kwa wingi. Kwani Wanyama hawa wanaambukiza wanyama wengine kama mbweha, mbwamwitu n.k. hivyo kuhatarisha usalama wa watu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na uhaba mkubwa nchini katika suala zima la uwekezaji wa viwanda vya usindikaji wa mazao ya mifugo. Kamati inashauri Wizara iwahamasishe wananchi na hata wageni wenye uwezo ili wawekeze katika aina hii ya viwanda. Si vema kwa Serikali kujitoa kabisa bali iangalie ni jinsi gani itawasaidia

wawekezaji hao kwa kuweka miundombinu na masuala mbalimbali yanayoweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, huduma za ugani imekuwa ni tatizo kubwa. Bwana Shamba anafanya kazi za Bwana Mifugo na kinyume chake. Kamati inashauri Wataalam warudi kwenye fani zao hata kama itachukua muda mrefu kufikia lengo lakini mafanikio yataonekana. Huu utaratibu wa kuchanganya wataalam wa mifugo na kilimo unasababisha kudorora kwa ufanisi. Hivyo Serikali inashauriwa kutenganisha fani hizo Kiofisi na Kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa afya ya mifugo ni zaidi ya dhana ya kuondoa magonjwa. Bali inahusisha pia malisho ya mifugo, hivyo suala la malisho litiliwe mkazo. Kamati inashauri kuwepo na zahanati za mifugo ili kuweza kuhudumia vema mifugo hiyo na ziwepo kila Wilaya. Suala la madawa ya mifugo liangaliwe upya hususan upatikanaji wa dawa hizi kwa wafugaji kwa njia nyepesi.

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa Kiwele (Mastitis) umekuwa ukiathiri sana mifugo na hatimaye uzalishaji. Athari yake ina kwenda mbali. Kamati inashauri wafugaji wapatiwe elimu ya kukabiliana na ugonjwa huu na elimu hii iwe endelevu kwani ugonjwa huu hudhuru hadi binadamu.

Mheshimiwa Spika, Hitishimo, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mb, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Antony Diallo, Mb, na wataalam wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Dr. Vincent Mrisho, kwa jinsi walivyoweza kufafanua hoja mbalimbali zilizotolewa na Wajumbe wa Kamati wakati wa kuchambua Bajeti hii.

Aidha, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati hii kwa michango yao na ushirikiano walionipatia mimi na Makamu wangu Mheshimiwa Alhaji Shaweji Abdallah katika kufanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Ofisi yako hasa Katibu wa Bunge Ndugu Damian Foka na wasaidizi wake Makatibu wa Kamati hii Bi. Nenelwa Mwihambi na Ndugu Abdallah Hancha kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kutoka kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii yaweza kuwa nafasi yangu ya mwisho kwa kipindi hiki, kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kusikilizwa na Wabunge wote, naomba kutumia fursa hii kwa kutakiana kheri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa Uchaguzi unaokuja mbele yetu. Nikiwa Mwenyekiti wa Kamati hii, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na Mwenyekiti wa Bunge, nimekuwa nikipata ushirikiano mkubwa kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Kwa wale wanaopanga kutetea nafasi zao nawatakia mafanikio, *aim high your failure will be a success.* Ukisema mimi nataka nipate asilimia 80 ukipata 70 hukufikisha 80 lakini umefaulu. Lakini ukisema nataka you aim low you success will be a failure, mimi hata nikipata C utapata D kweli umefaulu lakini umeanguka. Kwa hiyo kwa wale walioamua kuwa hiki ni kipindi chao cha mwisho naomba nao niwatakie kila la kheri katika maisha yao na shughuli za kujenga Taifa letu. Kwa wale ambao wanastaafu Ubunge nawaomba kama Wazalendo wenzetu, wawe tayari kutumikia Taifa hili pale watakapohitajika kufanya hivyo. Mungu atubariki na Mungu atusaidie sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtovu wa nidhamu na shukrani kama siwezi kuwashukuru wale wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi ambao wamenipa nafasi hii kwa vipindi viwili mfulululizo na wameniahidi kwamba watanipa nafasi hiyo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku zote mimi nasoma maandishi ya mwandishi mmoja Mfalme Daudi katika kitabu aya ya 27 anasema hivi "bwana ni nuru yangu na wokovu wangu nimwogope nani? Bwana ni ngome ya uzima wangu nimhofu nani? Watenda mabaya waliponikaribia watesi wangu na adui zangu walijikwaa wakaanguka. Jeshi lijapojipanga kupigana nami moyo wangu hautaogopa, vita vijapo nitokea hata hapo nitatumaini ushindi". Mungu atubariki wote na Mungu atusaidie wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe kwa pekee kwa jinsi ulivyonisadia sana katika kunishauri kwa muda wote na kunipa nafasi ya kuketi kwenye kiti chako. Nakushukuru sana na Naibu wako na ninawashukuru sana Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, kuwa Kamati yangu inaunga mkono hoja ya Bajeti ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Kwa heshima kubwa naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kukubali kupitisha kiasi cha fedha kinachoombwa katika Fungu 49 ambacho ni Sh.148,087,271,500/= zikiwa ni 24,870,271,500/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na 123,217,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambapo fedha za ndani ni Sh.70,207,000,000/= na fedha za nje ni 53,010,000,000/= .

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati yangu napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO**: Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye nguvu na mwenye hekima, ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini na yeye ndiye aliye juu, mkuu, mwenye uwezo wa kuweka Serikali za wanadamu na Mabunge ya Mataifa kwa kutupa uhai na afya njema tukaweza kukutana hii leo ndani ya jengo hili kutekeleza wajibu wetu.

Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya

Mifugo, kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43 (5) (b) (c) toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, pia naungana na wenzangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Utaani kutoa rambirambi zetu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliotangulia mbele ya haki. Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi Amina. Aidha, napenda kuwashukuru wale wote ambao waliungana nami na kunifariji kutokana na msiba wa kufiwa na mjomba wangu Sheikh Salim bin Ali Salim na ndugu yangu Asha Abbas Jecha, waliofariki hivi karibuni, nasema ahsante sana. Mwenyezi Mungu awape marehemu hao makazi mema peponi Amina.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza wale wote ambao wameteuliwa kutoka katika Kambi ya Upinzani kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wagombea wenza. Kadhalika nimpongeze Maalim Seif Sharrif Hamad Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi *CUF* kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar. Pia ninawatakia wagombea wote walioteuliwa na vyama vyao na ambao watateuliwa waendeshe kampeni zao katika muda muafaka kushindana kwa nguvu za hoja kwa namna ya kistaarabu, kiungwana bila kutumia hila wala ghilba na kwa kuzingatia kudumisha amani, utulivu na upendo uliopo miongoni mwa Watanzania ili hatimaye tuendeshe uchaguzi ulio huru na wa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji, maji ni muhimu mno kwa maisha ya viumbe, mfumo wa maisha ya viumbe haukamiliki pasipokuwepo maji. Mwenyezi Mungu amekuwa anaruzuku waja wake neema hii kuendeleza mfumo wa maisha. Ushahidi wa maneno haya ni pale Mwenyezi Mungu alipotuambia katika *Quran* Tukufu sura ya 16 aya ya 10 na ninanukuu: “Yeye ndiye anayekuteremshieni maji kutoka mawinguni, kwa hayo mnapata kinywaji na kwa hayo inaota mimea ambayo humo mnalisha wanyama,” mwisho wa kunukuu. Aidha, kitabu cha nabii Yeremiah aya ya 6 mstari wa 24 kinatuambia na ninanukuu: “Wala hawasemi mioyoni mwao. Basi na mche Bwana Mungu wetu aletaye mvua, mvua ya mwaka na mvua ya vuli; kwa wakati wake na kutuwekea juma za mavuno zilizoamriwa,” mwisho wa kunukuu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, maji ni kiungo muhimu sana kinachochangia kwa kiasi kikubwa kuondoa umaskini, kutokana na kutoa nishati ya umeme, kuwa na usalama wa chakula, maendeleo ya viwanda, madini na kustawisha mazingira na kwa maana hiyo kuendeleza uhai wa viumbe. Kwa hiyo ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba wakati wote majisafi na salama yanapatikana kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, napenda nikubali na nikiri kwamba Serikali imekuwa inajitahidi sana kuondoa matatizo ya upatikanaji wa majisafi na salama, mradi wa maji wa Chalinze na ule wa Ziwa Victoria na mingineyo miongoni mwa ushahidi wa hayo. Lakini pia tukiri kwamba huduma za kuwapatia maji safi wananchi waishio vijijini haijapiga hatua kubwa sana. Tegemeo lao la upatikanaji maji kwa watu wengi walio vijijini ni madimbwi, visima vifupi, mito, mabwawa na malambo. Vyanzo hivi vya maji mara nyingi havikidhi mahitaji yao ya kila siku hasa nyakati za kiangazi.

Aidha, nyakati za mvua vyanzo hivi huchafuka kwa taka na matope na hivyo kuhatarisha afya za watumiaji. Pamoja na ukweli kwamba Tanzania ni nchi ambayo imejaliwa na raslimali ya maji kwa wingi mno na yanapatikana kirahisi kutoka katika vyanzo vyake. Takribani asilimia sita ya eneo la nchi yetu ni maji, lakini bado mwanamke wa Kitanzania kwa wastani hupoteza masaa manne akitafuta maji. *(Makofi)*

Mahitaji ya maji huongezeka sambamba na ongezeko la watu, shughuli za uzalishaji viwandani, kilimo na kadhalika. Hivyo basi usimamizi madhubuti wa raslimali hii ni muhimu sana kuondoa umaskini, kuboresha afya za jamii, kuhakikisha usalama wa chakula maendeleo ya kiuchumi na uendelevu wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Wizara, kasi ya usambazaji wa maji vijijini bado ni ndogo kiasi kwamba imekuwa ni kero kwa wananchi wengi. Inakadiriwa kuwa asilimia 46 ya wananchi waishio vijijini hawapati huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa visima vifupi bado haijawa suluhisho la kudumu la tatizo la maji, ni dhahiri kwamba hakuna mwekezaji atakayewekeza kiwanda kijijini ikiwa tatizo la maji halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Kukosekana kwa viwanda vijijini kuna athiri sana kukua kwa uchumi na upatikanaji wa ajira na hatimaye kuongezeka kwa umaskini. *(Makofi)*

Huduma ya maji safi na salama mijini nayo imekubwa na matatizo kadhaa, pamoja na kwamba inakisiwa kuwa asilinia 73 ya wakazi wa mjini wanapata huduma hiyo. Kwa ujumla tatizo la upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama linatokana na sababu kuu nne, nazo ni:-

1. Kasi ya ongezeko la watu.

2. Uharibifu wa vyanzo vya maji.

3. Uchafuzi wa mazingira.

4. Uchakavu wa miundombinu ya kusambazia maji.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kuifanyia ukarabati miradi ya maji vijijini zimekuwa ni kwa awamu kutokana na ufinyu wa Bajeti kutotosheleza mahitaji makubwa ya kazi hiyo. Mingi ya miradi hiyo imechakaa kwa kuwa imejengwa zamani, pia kukosa matengenezo ya mara kwa mara na kutowashirikisha kikamilifu wananchi wenyewe katika uendeshaji wa miradi hiyo. *(Makofi)*

Aidha, matatizo mengine ni pamoja na kukosekana kwa mikakati madhubuti ya uratibu juu ya mpango wa kuvuna maji na kuhifadhi maji ya mvua kwa matumizi ya binadamu. Pamoja na kubinafsisha baadhi ya mamlaka za maji mpango huu mpaka sasa haujafanikiwa kuondoa kero za upatikanaji wa maji. Maji hayafikii walengwa wengi kama ilivyotarajiwa na hata hayo wanayoyapata ni kwa baadhi ya nyakati na wakati mwingine huwa si safi. Wananchi bado wanalazimika kuingia gharama ya kuchemsha

maji hayo au kutia dawa za kuulia wadudu. Maji ya visima yanayotumiwa na wananchi wengi siyo safi na salama kwani visima vingi ni vifupi na vimechimbwa kwenye maeneo yenye msongamano mkubwa wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwepo na miundombinu chakavu ya mji taka au kutokuwepo kabisa kwa miundombinu hiyo maji mengi ya visima huchanganyika na vinyesi hasa wakati wa mvua kutokana na hali hii kipindupindu kimekuwa ni ugonjwa wa kudumu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kupanua wigo wa uwekezaji katika ujenzi na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka mijini. Lakini ni vyema ikatoa kipaumbele kwa mashirika na makampuni ya Kitanzania ili kuepuka uwekezaji korofi kutoka nje ya nchi ambao hatimaye wanaweza kututia mkenge kama ilivyofanya Kampuni ya *City Water. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua kukatisha mkataba na Kampuni ya *City Water,* kutokana na utendaji wake mbovu wa majukumu yake ya kuwapatia majisafi wananchi wa Dar es Salaam na baadhi ya sehemu za mkoa wa Pwani. Ni vyema tukalichukulia kuwa hili ni funzo kwetu na sasa tuwe makini zaidi katika kutafuta wawekezaji walio bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama wananchi watatupa ridhaa ya kuongoza nchi hii katika hatua za kuondoa kero za upatikanaji wa maji safi na salam na uondoaji wa maji taka katika miji yetu tunatarajia kufanya yafuatayo;

Kazi ya usambazaji wa maji tutaiweka chini ya Mashirika ya Umma ambayo yanaweza kuingia ubia na Makampuni yenye uzoefu wa kujenga miundombinu ya mji na kusimamia usambazaji. Mashirika hayo yataundwa kila kanda ili kupata wawekezaji wa uhakika na wenye uwezo, Mashirika hayo ya Umma yataingia mikataba na Serikali itakayowawajibisha kusambaza maji Mijini na Vijijini katika uwiano ulio sawa.

Aidha, mikataba hii itakuwa wazi na kwamba Serikali haitavumilia ukiukwaji wa namna yoyote ya masharti ya mikataba itakayowekwa.

Makampuni yanayoshughulika na uchimbaji wa visima na yale yanayotengeneza maji ya chupa nchini yatakuwa na haki ya kuendelea na kazi zao bila kuathiriwa na mikataba baina ya serikali na makampuni hayo ya uzalishaji na usambazaji wa maji ya bomba.

Mabonde ya asili yenye uwezo wa kutumika kama mabwawa ya kuhifadhia maji yatatayarishwa ili mito ielekezwe kwenye mabonde hayo au mabwawa badala ya maji kupotea baharini.

Tutahakikisha maji kutoka katika Maziwa yanatumika ipasavyo kwa kuyaelekeza nchi kavu kwa njia ya mifereji na kusambazwa katika mabonde na mabwawa ya maeneo kame. Kadhalika maji ya mvua ambayo hugeuka kuwa mafuriko na kuleta maafa

yanaweza kubadilishwa mwelekeo kwa kujenga mikondo na mifereji itakayoelekea kwenye mabonde au mabwawa.

Wananchi watapewa jukumu la kuyamiliki na kuyatunza maji katika utaratibu watakaojipangia wenyewe. Miradi mikubwa ya maji vijijini itakabidhiwa kwa wananchi ili waweze kuisimamia, kuiendesha na kuiendeleza kwa kutumia vyombo vinavyotambulika kisheria na vitavyoundwa na wananchi kwa ridhaa yao wenyewe.

Aidha, Wananchi watatunga sheria ndogo za utumiaji na utunzaji wa maji yao na vyanzo vyake. Wataalam watahusika pale tu itakapohitajika ufundi na ushauri.

Kwa kuzingatia umuhimu wa maji kwa maisha ya binadamu na vyote vinavyomzunguka tutaipa kipaumbele na kuiongezea bajeti Sekta ya Maji iwe si chini ya asilimia 10 ya bajeti yote ya mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuimarisha taaluma ya maji. Serikali ina wajibu mkubwa wa kuwaandaa vijana wetu kuwapa taaluma ya maji ili kuwawezesha kuchukua nafasi za ajira kwenye mashirika na makampuni yanayozalisha na kusambaza maji.

Aidha Serikali inashauriwa kukiimarisha zaidi Chuo cha Maji cha Rwegarulila na kuanza kuchukua hatua za kukipandisha hadhi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Sambamba na hatua hiyo taaluma iwe inatolewa shuleni juu ya uvunaji, utumiaji na utunzaji wa maji. Wanafunzi wataweza kujifunza mapema na kupata mwamko wa kuona umuhimu wa kutumza mazingira na vyanzo vya maji hatua itakayopelekea kuimarika upatikanaji wa maji ya kutosha nchini.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo. Sekta ya Mifugo kwa mujibu wa Takwimu zilizopo inachangia asilimia 6.1 ya pato la Taifa, aidha kiasi cha asilimia 40 ya kaya za wakulima ni wafugaji na kwa hivyo ni chanzo cha upatikanaji wa ajira nchini. Ni dhahiri kwamba sekta hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa.

Inakisiwa Tanzania kuna jumla ya ng'ombe milioni 17.7, Mbuzi milioni 12.5, Kondoo milioni 3.5, Nguruwe 880,000 na kuku milioni 47. Huu ni utajiri mkubwa wa nchi kwani licha ya kuchangia pato la Taifa, huwapatia wananchi ajira, mbolea, chakula bora na hivyo kuboresha afya zao.

Mheshimiwa Spika, la kushangaza pamoja na wingi wa mifugo tuliyo nayo mwamko wa ulaji wa mazao ya mifugo ni mdogo mno na hasa ukizingatia viwango vinavyopendekezwa Kimataifa. Kwani kwa wastani Mtanzania kwa mwaka hula kilo 12 za nyama, mayai 54 na maziwa lita 39.

Viwango vinavyopendekezwa kwa mwaka *FAO* kwa mwaka kwa afya ya mwanadamu ni kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300. Tunaweza kuona ni kiasi gani sisi Watanzania tulivyo nyuma katika matumizi ya raslimali zetu za mifugo, hii ni kasoro kubwa na hatuna budi tubadili mifumo yetu ya chakula kwa manufaa ya afya zetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa sekta ya mifugo kwa mwaka, katika nchi zilizo chini ya Jangwa la Sahara ni wastani wa asilimia 2.2. Hiki ni kiwango kidogo sana ukilinganisha na mahitaji yanayotokana na ongezeko la watu la asilimia 2.8 kwa mwaka. Nchi hizi zina wajibu wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo ili kukidhi mahitaji ya wanadamu.

Hapa nchini kwetu hatua kadhaa zinachukuliwa ili kuleta maendeleo ya mifugo, mkazo zaidi umewekwa kuongeza uzalishaji, utafiti, kudhibiti maradhi ya mifugo na kukuza soko la mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio yanaonekana na hii ni kutokana na juhudi na mashirikiano baina ya wataalam na watendaji wa Wizara hii. Program mbalimbali zimeandaliwa kwa lengo la kuinua kipato cha mfugaji na kujiondolea umaskini. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

1. Kuongeza uzalishaji wa maziwa na kuboresha ng'ombe wa asili.

2. Kuongeza ubora wa malisho.

3. Kuzalisha mitambo bora ya maziwa na kuwapatia wafugaji.

4. Kuendeleza vyanzo vya maji, kujenga mabwawa na kuchimba malambo kwa ajili ya upatikanaji wa maji.

5. Kukuza taaluma ya mifugo kwa watendaji na wafugaji.

6. Kudhibiti maradhi ya mifugo.

7. Upatikanaji wa vifaranga bora wa mayai na nyama.

Mheshimiwa Spika, Takwimu zinaonyesha kwamba vifaranga milioni 29.9 vimezalishwa mwaka huu unaomalizika na uzalishaji mayai umeongezeka kufikia milioni 1800 ukilinganisha milioni 910 mwaka uliopita.

Maziwa yameongezeka kutoka lita bilioni 1.18 mwaka 2003/2004 hadi kufika lita bilioni 1.38 mwaka 2004/2005.

Uzalishaji wa nyama nao umeongezeka kutoka tani 348,000 mwaka uliopita hadi kufikia 378,509 mwaka 2004/2005.

Maendeleo haya ni ya kupongezwa na ni vyema basi nikachukua nafasi hii kuwapongeza Viongozi na Watendaji wote wa Wizara hii kwa juhudi kubwa wanazochukua katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na maendeleo yanayopatikana wafugaji bado wanakabiliwa na matatizo kadhaa ambayo kwa namna moja au nyingine yanawakwaza katika kuleta maendeleo ya ufugaji hapa nchini. Matatizo hayo ni pamoja na :-

1. Madawa ya mifugo yamekuwa hayapatikani kwa wakati na hasa vijijini na na mara nyingi yanakuwa ghali sana, matokeo yake ni kuenea kwa magonjwa mbalimbali na hasa ya milipuko.

2. Hakuna utaratibu ulioandaliwa ama unaoeleweka wa kuwapatia mikopo wafugaji, aidha wafugaji wengi hawana uwezo wa kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha kutokana na masharti magumu yanayowekwa. Kadhalika kwa bahati mbaya sekta hii haivutii wawekezaji binafsi kutokana na gharama kubwa za uwekezaji.

3. Upatikanaji wa maji ni tatizo hasa katika sehemu kame za nchi. Aidha mabwawa na malambo ni machache na mengi ni ya kina kifupi.

4. Kilio cha wafugaji cha kutaka paundwe Bodi ya kuendeleza Ufugaji Nchini bado hakijasikilizwa.

Mwisho, tafiti nyingi zinazofanywa hazilengi katika kutatua matatizo halisi ya wafugaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa chanzo cha haya yote ni kutokana na :-

1. Serikali kutosimamia kwa makini sheria ndogo zilizowekwa ili kudhibiti kuenea kwa maradhi ya mifugo nchini. Uhaba wa viwanda vya kusindika mazao yatokanayo na mifugo, masoko ya uhakika na kukosekana miundombinu ya kuwezesha kuuza bidhaa za mifugo humu nchini na soko la Kimataifa. *(Makofi)*

Lakini kubwa zaidi ni ufinyu wa bajeti. Fedha zinazotengwa kwa matumizi ya Wizara hii hazitoshelezi kulingana na umuhimu wa maendeleo ya Sekta yenyewe ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu itakapoingia madarakani Novemba mwaka huu inakusudia kufanya yafuatayo:-

Bajeti kwa ajili ya miradi na shughuli za Sekta ya Mifugo itaongezwa kukidhi mahitaji yake. Vivutio mbalimbali vitawekwa ili kuvutia wawekezaji kuwekeza katika sekta hii ya mifugo.

Maeneo maalumu ya ufugaji yatatengwa ili kupunguza tatizo la wafugaji kuhamahama kunakosababisha uharibifu wa mazingira, migogoro kati ya wafugaji na wakulima na kuenea kwa magonjwa ya mifugo.

Tutaanzisha Bodi ya Mifugo nchini. Hii itapewa jukumu la kuendeleza mifugo ikiwa ni pamoja na kuanzisha taasisi za fedha zitakazowawezesha wafugaji kupata mikopo yenye masharti nafuu. *(Makofi)*

Sheria zilizotungwa na zitakazotungwa zitasimamiwa ipasavyo na kwa umakini katika utekelezaji wake ili pamoja na mambo mengine kudhibiti kuenea kwa maradhi ya mifugo.Viwango vya elimu kwa watendaji vitaendelezwa ili kuongeza tija kwa kuboresha uelewa na uwezo wao. Huduma za ugani, upatikanaji wa madawa na pembejeo nyingine utaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Napenda nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Edward Baraka Lowassa Ngoyai Mbunge ambaye ni Waziri wa Maji na Mifugo, Mheshimiwa Anthony Mwandu Diallo Mbunge na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza wajibu wao na kusukuma Mbele maendeleo ya Taifa hili. Ninaami bila ya mshikamano ulio madhubuti maendeleo haya yasingeweza kupatikana, ninaomba wazidishe juhudi na ari ya kazi ili kuongeza ufanisi na tija katika kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru kwa namna ya pekee wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo na Ardhi na hasa Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Alhaji Shaweji bin Abdallah Makamu Mwenyekiti kwa kunipa ushirikiano wa hali ya juu katika muda wote. Walikuwa wananithamini kama mwenzao kadhalika wamekuwa wanauthamini sana mchango wangu ninaotoa katika Kamati. Nawatakia kila la kheri wateuliwe tena na vyama vyao kugombea nafasi ya Ubunge katika uchaguzi mkuu ujao. Kadhalika niwashukuru Ndugu Nenelwa Mihambi na Hancha Abdallah Makatibu wa Kamati hii kwa kazi yao nzuri waliyokuwa wanaifanya ya kuratibu shughuli za Kamati. Ama pia niwashukuru Wabunge wenzangu wote kwa maelewano na mashirikiano mazuri tuliyokuwa nayo kwa kipindi chote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Viongozi wote wa Kambi ya Upinzani, Wanakambi wenzangu pamoja na watendaji wote katika ofisi yetu kwa jinsi ambavyo tumekuwa tunashirikiana. Kusema kweli wameifanya kazi yangu kama Mbunge na kama Msemaji Mkuu wa Wizara hii kuwa nyepesi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa takribani Wabunge wote tuliomo humu ndani tumeingia kupitia vyama vya siasa basi ni vyema nikachukua fursa hii adhimu kuwashukuru kwa dhati kabisa viongozi na wanachama wa chama changu cha Wananchi *CUF* kwa kuniteua kuwa mgombea wa nafasi hii ya Ubunge katika uchaguzi uliopita. Aidha, nawashukuru wananchi wa jimbo langu la Utaani kwa kunichagua kwa kura nyingi sana kuniwezesha kuwa Mbunge wao na kuwatumikia katika kipindi chote cha Ubunge wangu. Nasema ahsanteni sana kwa uamuzi wenu na kwa ushirikiano mkubwa mlionipa.Ni vyema sasa nikachukua nafasi hii adhimu kumshukuru mke wangu, watoto wangu pamoja na familia yangu yote kwa kunivumilia na kuniunga mkono wakati wote hasa ninapokuwa mbali nao nikitekeleza wajibu wangu. Mwenyezi Mungu atawalipa thawabu nyingi juu ya subira yao. *(Makofi)*

Mwisho kabisa siyo kwa umuhimu napenda nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeviti wote kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mnaifanya kuliongoza Bunge hili Tukufu. Kadhalika nimshukuru Katibu wa Bunge na Watendaji wote kwa kuweza kubeba majukumu yao vizuri na kuweza kutulea vizuri sisi Wabunge kwa kipindi chote ambacho tumekuwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba naomba kuwasilisha na bila shaka naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa tunaanza mjadala wa jumla Waheshimiwa Wabunge, namwita Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Esha Stima sasa jiandae.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo ili niweze kuchangia katika hotuba iliyo mbele yetu, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.Kwanza kabisa naomba nitamke wazi kwamba naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ningelipenda vilevile nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Rais Mkapa na Wizara hii kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Edward Lowasa Waziri pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Anthony Diallo na Katibu Mkuu wake na Watendaji Wakuu wake akina Njau pamoja na wenzake. Napenda niwashukuru sana kwa ushirikiano ambao walinipa hasa katika Jimbo letu na Mji wetu wa Shinyanga.

Tulikuwa na matatizo makubwa sana ya maji katika Mji wetu wa Shinyanga lakini ushirikiano wa Serikali ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa mwenyewe pamoja na Wizara hii wamenipa ushirikiano wa hali ya juu sana. Nawashukuru sana na ninaamini kabisa kwamba kwa kuwa nitagombea tena ninaamini kabisa wamenipa visemeo vya uhakika katika kujinadi kwa hiyo nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mji wetu wa Shinyanga ulikuwa na matatizo makubwa sana ya maji lakini leo matatizo pamoja na kwamba hayajatatuliwa kikamilifu kwa asilimia mia moja angalau wamejitahidi kutatua matatizo haya ni asilimia ninaweza nikasema mapungufu ya maji sasa hivi labda ni asilimia 40 kwa hiyo nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, binadamu kama tulivyo kwamba baada ya kutatua tatizo wakati mwingine yanajitokeza matatizo mengine ambayo yanazaliwa baada ya maendeleo na matatizo kama haya ni kwamba mtakumbuka kwamba mafuta yamepanda bei na umeme umepanda bei kwa mfano katika Mkoa wetu waShinyanga zamani mafuta ya *diesel* tulikuwa tunanunua shilingi mia tano (500) leo ni shilingi 1200. Kutokana na matatizo hayo vilevile Wizara baadaye imesema kwamba sisi watu wa mjini lazima tujitegemee na katika kujitegemea zamani Wizara ilikuwa inatulipia umeme katika upatikanaji wa maji mjini halafu ilikuwa inatulipia watumishi na gharama nyingine.

Lakini kwa leo Wizara imetuagiza kwamba lazima tujitegemee na kwa kufanya namna hiyo baadaye katika mkutano uliofanyika kule Tanga walijaribu kutushauri kwamba tuone namna gani tunaweza tukatoa hizi huduma na kwa bahati mbaya baada ya

kuona kwamba kwa kuwa Serikali haitulipii umeme na kwa kuwa Serikali hailipii tena Watumishi utakuta kwamba bili za maji zimekuwa kidogo juu kidogo na kwa sababu hiyo watu kidogo wameanza kulalamika.

Mheshimiwa Spika, nawaomba wananchi wa Shinyanga wazidi kuvumilia kwa sababu upatikanaji wa huduma hii kwa sasa hivi siyo wa bure. Huko nyuma watu walikuwa hawalipii maji, maji yalikuwa yanatolewa bure na mimi wakati naomba kura niliwaambia kabisa kwamba kidole changu hiki na vidole vyenu hivyo tutavunja huyo chawa na chawa huyo ni kero ambazo zilizokuwa zinatukabili za maji katika Mji wetu wa Shinyanga. Ninaamini kabisa kwamba kidole changu kimesukuma Serikali na wafadhili mbalimbali na niliwaomba kwamba vidole vyao visaidie katika kulipa bili za maji ili watupe uwezo wa kuweza kutatua tatizo hili pamoja na kwamba mradi wa maji wa *Lake Victoria* maji haya hayajafika Shinyanga lakini kama nilivyosema tatizo la maji katika Mji wetu limetatuliwa kwa kiwango kikubwa sana.

Wenzetu wapinzani juzi walikuwepo kule watu wa CHADEMA walikuwa wanasema kwamba eti kupanda kwa maji ni tatizo, lakini huduma hii ni lazima ilipiwe. Unajua zamani kulikuwa na agenda mbalimbali lakini sasa agenda hizi tumezitatua na sasa wanaanza kuongelea kwamba bei ya maji inakuwa kubwa watu wasilipe sasa ninasikia kwamba kama kwa mfano watu wasilipe bili ya maji halafu umeme ukikatwa na madhara tutakayoyapata sidhani kama yatakuwa ni makubwa sana. Ninaamini kabisa kwamba upinzani wakati mwingine wanakuwa na maneno ambayo kwa kweli ukiyatazama yana nia ya kuvuruga maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wakati mimi naomba ubunge mwaka 1995 Kaka yangu Bob Makani tuliyekuwa tunagombea naye aliniambia kwamba mimi sijui kusema. Ni kweli nikamwambia mimi sijui kusema lakini bahati nzuri nilikuwa nakwenda na Biblia mahali aliposema kwamba mimi sijui kusema. Niliwasomea Biblia kwamba Musa alipotumwa na Mwenyezi Mungu kwenda kuwakomboa Waisrael alisema kabisa kwamba yeye ana kigugumizi. Lakini kazi ya kuwakomboa Waisrael aliifanya, mimi niliwaambia kwamba nichagueni mimi ni Musa wenu wa Shinyanga. Pamoja na kigugumizi changu lakini neno langu moja ni rungu kwa hiyo ninapenda niwaeleze kabisa kwamba waendelee kuniamini na waendelee kuniunga mkoni kama nilivyosema kwamba kidole changu hiki na vidole vyao hivyo tutamvunja huyo chawa, lakini kwa ushirikiano.

Kwa hiyo, napenda niliseme hili na ninaamini kabisa kwamba watu wa Shinyanga msipotoshwe kwa maneno ya watu ambao kwa kweli sasa hivi ninaamini kabisa hawana agenda. *(Makofi)*

Kwa sababu mradi wa *Lake Victoria Contract* zote, *contract* ya kwanza bahati nzuri nilikwenda kule wiki mbili zilizopita kazi inafanyika vizuri sana na Mheshimiwa Waziri amesema ni kazi imefanyika asilimia 75. *Contract* ya pili ya kuleta maji kutoka *Iherere mpaka* Solwa na yenyewe sasa hivi inafanyika kwa nguvu zote. Halafu *contract* ile ya tatu na ya nne, tarehe 21 nimeambiwa na Waziri kwamba anakwenda kuzindua na kukabidhi pale *Old Shinyaga* tarehe 21/7/2005, kwa hiyo wananchi wa Shinyanga lazima

muamini kabisa kwamba Serikali yenu ya Chama Cha Mapinduzi ndiyo mkombozi wenu. *(Makofi)*

Naamini kwamba mimi ni mtu wa CCM, ni mtoto wa nyumbani, siyo! Ukija nyumbani ukamtuma mtu kwamba akuletee maji kutoka ndani ya nyumba kwao akasema hayamo maji, ukamtuma wa jirani atayapata? Mimi mtoto wa nyunbani bwana. Mimi mtoto wa CCM niamini mimi na ninaamini kabisa, watu wanapokosa agenda wanajaribu kutafuta vitu vya kupotosha watu na vitu hivi wakiwapotosha watawafanya watu tukose manufaa.

Mheshimiwa Spika, wakati mimi wananichagua kuwa Mbunge najua kulikuwa na agenda nyingi sana, *agenda* mojawapo ilikuwa ni maji, maji yanakuja na matatizo ya maji yamepungua. *Agenda* nyingine ilikuwa ni barabara ya lami. Barabara ya lami Wananchi wa Shinyanga mnaiona inajengwa.

Agenda ya tatu ilikuwa ni matatizo ya elimu kazi hizi mnaziona zinafanyika lakini nashangaa watu wengine wanasema kwamba ni mipango ya Serikali si kweli, sisi Wabunge ndiyo tunaisimamia Serikali, sisi Wabunge ndiyo tunahakikisha kwamba Serikali inaweka mipango mizuri ya kutatua matatizo na kero za wananchi.

Sasa watu wengine wanasema kwamba hiyo ni mipango ya Serikali kwani zamani ilikuwa wapi Serikali na Wabunge zamani si walikuwepo? Wakati wananichagua waliniambia kwamba walinipa hizi agenda na nimezimamia kwa ukaribu, nimefuatilia Ofisi ya Rais na nimefuatilia kwa Wizara mbalimbali zinazohusika. Baadaye watu wanasema kwamba haya ni mambo ya Serikali, si kweli wananchi ni lazima muamini kabisa kwamba mkichagua mtu lazima mhakikishe.

Mheshimiwa Spika, siku moja niliwaambia wananchi wa Jimbo langu kwamba Majimbo wanayochagua Mbunge mara moja wakati mwingine hayapati maendeleo kwa sababu wakati mwingine Serikali hai - *voluntee information,* siyo? Kwa hiyo mimi kwa mfano sasa hivi Mawaziri hawawezi kunidanganya kama ni ng'ombe wa kulima siyo wa kupiga tambo tena ni wa kufungwa joki na kwenda kazini, siyo? Kwa hiyo mimi nawaambia kabisa kwamba wanapopemda kubadilisha kila wakati walete mtu mpya wakati mwingine ninaamini kabisa kwamba kazi hii nimeifanya kwa kushirikiana na Wizara mbalimbali na ndiyo maana napenda nimshukuru Mheshimiwa Rais Mkapa na Wizara zake mbalimbali kwa kutupa ushirikiano Wabunge tuliopo hapa sasa.

Katika Majimbo yetu sasa hivi kazi zimeonekana kama ukienda Bukoba utakuta barabara inajengwa, miradi mbalimbali ipo. Ukienda kusini kule utakuta kazi zinafanyika, ukienda Arusha utakuta kazi zinafanyika lakini watu wengine ambao agenda sasa naona kama wamechemsha wamepungukiwa agenda wanaanza kuleta agenda nyingine za uchochezi ambazo kwa kweli zitatuletea matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lingine napenda niongelee kuhusu tatizo la Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga. Nalisema hili kwa masikitiko makubwa sana, nimefuatilia kwa ngazi za hali ya juu sana fuatilia kwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu mwenyewe alipokuja

Shinyanga mwaka 2000 alinithibitishia kabisa kwamba ubinafsishaji wa kiwanda hiki utafanyika kabisa kwa sababu tunaamini kiwanda hiki kilianza kujengwa mwaka 1976 na kwa bahati mbaya hakuna chochote mle ndani hata mitambo haimo, sijui ilikwenda wapi lakini kwa bahati nzuri Waziri Mkuu aliagiza kabisa kwamba kiwanda hiki wapewe wananchi wafanyabiashara wa Shinyanga na wapo wengi wamejitokeza kwamba kiwanda hiki tungelipewa sisi wananchi wa Shinyanga halafu baadaye tungeliweza tukatafuta Mwekezaji tukashirikiana naye wafanyabiashara wa Shinyanga ili tuhakikishe kabisa kwamba mifugo yetu inakuwa na soko la uhakika.

Tumekuwa tukiongea mambo mengi hapa kila wakati kwamba Serikali inakuwa na mtindo wa kwa mfano wanatafuta wawekezaji katika kuwekeza katika suala la madini ambao wanayatafuta chini kwa gharama kubwa sana. Kwa bahati nzuri mifugo ni moja ya rasilimali ambayo ipo haina gharama huwezi ukatumia sidhani kama hata dola bilioni moja kama wanavyofanya kwenye machimbo. Hivi Serikali inapata kigugumizi gani? Kama hawawezi kukibinafsisha.

Nimehangaika Wizara ya Ubinafsishaji, nimekwenda mara nyingi Waziri nimemwuliza lakini mara nyingi wanasema kwamba sasa hawajawa na msimamo leo ni miaka 10 na ukichukulia kuanzia mwaka 1976 mpaka leo ni miaka karibu 28, sasa hivi kuna tatizo gani?

Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri wakati ana wind - up ajaribu kunieleza kuna tatizo gani la hiki kiwanda? Ninaamini kabisa kwamba kiwanda hiki kingelikamilika kingeliwasaidia sana wafugaji wa Shinyanga katika kuwa na soko la uhakika la mifugo yao na hii katika suala la MKUKUTA hii ilikuwa ni *number one* katika kuwakomboa wafugaji na wananchi katika masuala ya umaskini.

Sasa kuna kigugumizi gani ambacho kinafanya hiki kiwanda kama bahati nzuri walipatikana wawekezaji na wakalipa na hela lakini hela zile zikarudishwa, sasa mimi nikashangaa. Nimekuwa nikifuatilia sipati jibu.

Mheshimiwa Edward Lowasa rafiki yangu *Sobai* nilikuwa nakuomba leo basi unipe jibu nijue kwa sababu kwa kweli *agenda* mojawapo ambayo kwa kweli sikutekeleza ni hii ya kiwanda ambacho kwa kweli nilikuwa nasema kwamba hiki kiwanda kingelifanya kazi Mji wetu wa Shinyanga vijana wangelipata ajira ya uhakika. Wafugaji pia wangelipata soko la uhakika, kwa hiyo Ndugu yangu naomba nipate jibu leo ili kusudi nione hasa ni tatizo gani kwa sababu Mkoa wa Shinyaga, Mwanza na Tabora mifugo iko zaidi ya milioni 10 nafikiri.

Mkoa wa Shinyanga peke yake una mifugo zaidi ya milioni 4. Ninaamini kabisa kwamba hata kama kiwanda kile una *crop up* ng'ombe kama laki 5 hivi sidhani kama ungeliweza ukawamaliza hata milioni 1 kwa sababu wanazaana.

Mheshimiwa Spika, ningelipenda nihitimishe hoja yangu kwa kumwomba sana Mheshimiwa Ndugu yangu Edward Lowasa kwa umahiri wake ametatua matatizo ya

maji katika Mji wetu wa Shinyanga. Sasa hivi kuna mradi mkubwa unafanyika, hivi limemshindaje hili la Kiwanda cha Nyama? Eeh! *Brother* naomba unisaidie. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ESHA E. STIMA:** Mheshimiwa Spika, mimi nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia namba mbili baada ya Kaka yangu Mheshimiwa Derefa kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mimi kama inavyofahamika ni Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Shinyanga. Najumulisha matatizo ya Wilaya nane (8) kwa hiyo nitakachochangia hapa ni kuhusu matatizo ya maji ya Mkoa mzima ambayo wananchi na wapiga kura wangu wameniomba nilizungumzie katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri, Kaka Edward Lowasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hoja ni nzuri na yenye mwelekeo mimi nichukue nafasi pia kumpongeza yeye Mwenyewe, Naibu Waziri,Katibu Mkuu na Watumishi wote wa ngazi zote nchini kwa kazi nzuri wanayoifanya na pia nisimsahau Afisa Mifugo wa Kata ya Chamaguhu ambako mimi mwenyewe ninaishi.

Ni kijana anayefanya kazi vizuri, anatibu na ni mwepesi unapomwita ukiwa na matatizo ya ng'ombe wanaumwa anajitokeza, basi na huyu wamfikirie amuulize tu Mkurugenzi wa Manispaa huyu kijana ni nani basi wamwendeleze wampe hata ngazi ya uongozi wake kwa sababu anafanya kazi nzuri.

Mimi nilichokipata kutoka kwa wapiga kura wetu na kitu ambacho wananchi hawakipendi au wanaomba Mheshimiwa Waziri akitatue ni ule mtindo wa kulipishwa gharama za maji kwa ujumla.

Kila mteja ana mita yake inazunguka kwa kadri anavyotumia maji, lakini Bodi ya Maji ya Mkoa wetu wa Shinyanga, imefanya utaratibu ambao kidogo kwa Wananchi wameona ni kero kwamba, mtu anayetumia maji kuanzia ujazo 0 - 20 kima cha kulipa ni shilingi 8,000/=, umetumia kiasi hicho au hujatumia kiasi hicho lazima ulipe. Hiyo ndiyo kero ambayo Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, kwa kadri nilivyopita na kupata taarifa, ndiyo wanaona kero.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anahitimisha hoja yake katika Bunge hili Tukufu, basi utoe ufafanuzi ili Wananchi hao waweze kuridhika na fedha zao wanazotoa ili isiwe kero kwa hiyo bodi. Kwa sababu gharama zilizopanda kwa ajili ya utekelezaji wa masuala ya maji katika Mkoa wetu zinafahamika. Lakini kwa nini sasa,mtu akitumia lita tano alipe gharama ya lita 20 wakati hakuzitumia. Hapo ndipo inapokuwa kero na watu wanasema kwamba, wasilipe maji kwa sababu wanaongezewa mzigo. Wanaomba kila mteja abebe mzigo wake mwenyewe na asitokee jirani wa kubeba mzigo mtu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hata mimi katika familia yangu, situmii maji yenye gharama ya zaidi ya shilingi 6,000/=, kwa sababu nina kisima cha maji, ng'ombe, kuku na mifugo mingine wanakunywa maji ya kisima siyo yale ya bomba. Sasa tukifanya hiyo hesabu ya jumla, wapo wanaoumia na wapo wale wanaoshangilia kwamba, kuna watu wanaotusaidia kubeba mizigo ya kichwani na kwenye mabega kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Spika, tumeiona Serikali hapa na sisi tumeshuhudia jinsi ilivyothamini elimu kwa kufuta ada za shule za msingi na kupunguza ada za shule za sekondari, kwa nini Serikali imefikiria hivyo? Kwa sababu hizo ndizo huduma za jamii, haiwezekani kuwaacha watoto wasiendelee na shule. Hali kadhalika na suala la maji nalo lingefikiriwa kwa utaratibu huo. Kwa sababu bila maji, tutaongeza gharama kwa upande wa Wizara ya Afya, milipuko ya magonjwa itazuka kwa wanyama na kwa binadamu. Sasa tusipopunguza gharama ya maji, maana yake watu waendelee kwenda kuchukua maji kwenye madimbwi ambayo siyo salama. Kwa hiyo, tunaweza tukaona ni vizuri kwa upande wa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kupandisha gharama za maji kwa Bodi ya Maji za Mikoa yetu, lakini itaku ni tatizo kwa Wizara ya Afya, mahospitalini watajaa watu wanaotumia maji machafu, kila siku watu wataugua na watahitaji dawa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa umahiri wake na uwezo wake mkubwa wa kazi, safari hii ajaribu kuwasilisha hoja hii kwenye Baraza la Mawaziri mtakapokaa, kuona umuhimu wa kupunguza kabisa gharama ya maji kwa matumizi ya nyumbani. Yale maji ya kwenye Taasisi, wale wanaotumia maji kwenye viwanda, wale wanaotumia maji kwa ajili ya biashara, sina kauli nao kwa sababu wao wanapata kitu kutokana na yale maji. Lakini kwa matumizi ya nyumbani, nitashukuru kama mtalifikiria hilo, pamoja na watendaji wako na Bodi yetu ya Maji ya Mkoa wa Shinyanga, wakae waone ubinadamu ukoje katika suala la aina hii. Kila mtu abebe mzigo wake mwenyewe, ndiyo kauli ambayo Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, wanamwomba Mheshimiwa Waziri, aifikirie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia namwomba Mheshimiwa Waziri kama kutakuwa na uwezekano, akae na Bodi ya Maji ya Mkoa wa Shinyanga, waone jinsi watakavyopunguza hii gharama ya maji kwa matumizi ya nyumbani. Hao wengine nadhani hawatalalamika sana ikiwa itasawazishwa kwa mtindo huo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie upande wa mifugo. Mwaka 2004 niliuliza swali nadhani pia nililizungumzia, matumizi mabaya ya dawa ambazo zime-*expiry*. Lakini nimjulishe tu Mheshimiwa Waziri kwamba, safari hii wamejitahidi wauza maduka, kuacha mtindo wa kuweka madawa yaliyo-*expiry*. Kwa hiyo, najua Mheshimiwa Waziri, umefanya kazi kubwa sana kufuatilia hilo, nakushukuru sana na Wananchi wanakupongeza kwa kufuatilia hilo kwa matumizi ya Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga.

Mhesimiwa Spika, pia na mimi nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kuuweka Mkoa wetu katika mpango wa kupata maji kutoka Ziwa Victoria. Wanawake wa Mkoa wa Shinyanga wanakutakia kila kheri kwa sababu kwa kweli kila unaloambiwa huwa

unalifuatilia. Nimesikia kwa wanawake labda wanaume wataniambia baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo mengine ameyesema kaka yangu, Mheshimiwa Leonard Derefa, sitaki niyarudie. Lakini niseme yale ambayo Wananchi na wanawake wa Mkoa wa Shinyanga, walioleta *fax* na Mheshimiwa Waziri nimempatia *fax* hiyo ili aweze kuona jinsi gani atakavyoweza kuwasaidia kwa sababu sisi ni Wabunge na wao wametokana na Ubunge ndiyo wakapata Uwaziri. Kwa hiyo, tunapopata kitu chochote ambacho kina malalamiko huwa tunawataarifu mapema. Nilimtaarifu hilo na *fax* nimempa ili aweze kujua namna gani atawasaidia na kuwatoa hofu.

Mheshimiwa Spika, nami pia niwaombe tu Wananchi wa Mkoa wetu wa Shinyanga kwamba, tusikatae kulipia gharama za maji. Lakini pia ombi lao nimeliwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Mkurugenzi wa Shinyanga najua yupo hapa, wataona jinsi watakavyotusaidia na kipindi hiki siyo kizuri kuweka migomo. Lakini haki inapotakiwa lazima ije kupitia Bunge hili, tukiwa wawakilishi wa Mkoa wa Shinyanga tunaomba Mheshimiwa Waziri ulifikirie.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kazi nzuri na mwongozo wako nikiwa katika Bunge hili Tukufu na pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, kwa ushirikiano wao na Maafisa wa Bunge, kwa jinsi walivyoweza kutusaidia katika masuala mbalimbali. Hali kadhalika walivyonihudumia nilipokuwa nimepata ajali mbaya ya gari mwaka 2002, kwa kweli nilipata huduma zote na nililipiwa gharama zote, hakuna madeni kwenye hospitali. Kwa misingi hiyo, nichukue nafasi hii kuwashukuru na pia nimshukuru Kiongozi wa Serikali Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi alivyotuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisisahau kabisa na hilo ni muhimu kwangu, kuwashukuru sana wapiga kura wangu wote wa Mkoa wa Shinyanga, akina mama, Viongozi wa Chama na Serikali, walionipa msaada kuweza kuwa Mbunge tangu mwaka 1995 mpaka 2005. Niwajulishe tu kwamba, mwaka huu kuna uchaguzi tena na mimi nitakuwa miongoni mwa wagombea kama walivyojitangaza baadhi yao kwenye Gazeti la Tanzania Daima.

Mimi nawakaribisha tu, haya ni mambo ya kisiasa, hayana ugomvi, hayana malumbano na safari hii kwa bahati nzuri tuna nafasi mbili za Ubunge katika Mkoa, basi tukifanya vizuri Wana-CCM kwa Mkoa wa Shinyanga, Wabunge Wanawake wawili watamsubiri Spika wetu, Mheshimiwa Pius Msekwa baada ya kuapa na wengine watatu tutakuja kuwasaidia kwenye kapu Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama wananisikia basi waone raha ya matarajio ya kuja Bungeni, pamoja na mimi Mbunge wao walionichagua huko nyuma na ninawatakia kila la kheri na afya njema, tuweze kuwa pamoja sina mabadiliko ya roho, roho yangu ni njema na ninawaombea Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote turudi. Mwenyezi Mungu, atupe nguvu ya kurudi hapa Bungeni. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo mfupi, nasema naunga mkono hoja ya kaka yangu, Mheshimiwa Edward Lowassa na shemeji yangu, Mheshimiwa Anthony Diallo, mia kwa mia na Mungu awape nguvu warudi tena. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza, kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili leo na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri wake na Watendaji wote, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa yeyote yule aliyepo ndani ya Bunge hili na atakayekuwa nje ya Bunge hili, atakayepata nafasi ya kupata kitabu hiki cha hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, basi atazame ukurasa kati ya 43 mpaka 51 na ukisoma yaliyoandikwa pale, utaridhika kabisa kwamba, hii ni moja ya Wizara ambayo kwa kweli inafanya kazi kisayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shughuli zake zinateremka kutoka katika Mikoa na katika Mikoa yote shughuli hizo zinaendelea katika Wilaya na zaidi ya asilimia 90 ya Wilaya zimeguswa. Lakini kutoka katika Wilaya, shughuli zinaendelea hadi katika maeneo mbalimbali ya Vijiji. Nasema hii ni kazi inafanyika kisayansi na kwa kweli kama tutaendelea hivi, matatizo ya maji yatapungua sana Kitaifa baada ya muda usiokuwa mfupi. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapongeza Wahisani ambao wameisaidia Wilaya ya Muheza wakiwemo wenzetu wa Ireland na *Irish Aid,* ambao wametusaidia sana katika miradi mingi ya maji. Lakini vilevile naupongeza sana Ubalozi wa Marekani, ambao umetusaidia hivi karibuni katika uchimbaji wa zaidi ya visima 10 virefu, viwili vikiwepo Kata ya Mkuzi, kimoja Magila, kingine Shule ya Sekondari ya Kerenge, viwili Ngomeni, Bagamoyo na kule Tingeni. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wananchi ambao wameshiriki katika kuchangia miradi mbalimbali ya maji katika maeneo mbalimbali ya vijiji ili kujiondolee kero hii kubwa ya maji.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, hasa kwa kuiweka Wilaya ya Muheza kuwa miongoni mwa Wilaya katika Mpango wa Benki ya Dunia wa Maji na Mazingira. Nampongeza sana na naamini kabisa Wilaya ya Muheza tutaitumia nafasi hiyo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ni vyema nikasema hapa kwamba, katika utekelezaji wa Programu hiyo ya Benki ya Dunia, Wilaya zitakuwa zinapishana katika utendaji hasa kutokana na utendaji wa watendaji tuliokuwa nao, yaani Wahandisi wa Maji. Pamoja na kwamba, Wilaya ya Muheza imeingizwa katika mpango huo wa Benki

ya Dunia tangu Julai, 2004, hivi karibuni tu vimepitishwa vijiji 10 katika Mpango huo na sasa ni Julai, 2005, maana yake karibu mwaka mzima sisi ndiyo tunaingiza vijiji 10, inawezekana tumeachwa nyuma na wenzetu.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo moja kati ya sababu ambazo nimekuwa nikijaribu kuzizungumzia kwamba, katika baadhi ya maeneo, Wizara itusaidie ili kuboresha ufanisi wa utendaji. Vinginevyo tutakuwa tumeingizwa katika Programu kubwa lakini tukaachwa nyuma na wenzetu. Hapa narudia tena na nilikwisha kulisema hili, ni vyma Wizara ikatusaidia vinginevyo fedha hizo katika mipango hiyo mikubwa ya Benki ya Dunia zitakuwepo, lakini baadhi ya Wilaya zitashindwa kuzitumia kutokana na ufanisi ambao unatokana na upungufu au mapungufu kwa watendaji. Inawezekana kabisa Wilaya ya Muheza ni kubwa na idadi ya Wahandisi tuliokuwa nao katika Idara hiyo ya Maji ni wachache, wanashindwa kumudu kasi ya maendeleo ya miradi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui Wizara itatusaidiaje hasa katika programu hii ya Benki ya Dunia. Lakini vilevile katika Programu nyingine ambayo namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwamba, ameiingiza katika Programu yake ya mwaka 2005/2006, nayo ni ukarabati wa Mradi wa Maji wa Ubebe-Kwemuhosi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningemwomba hapo Mheshimiwa Waziri atusaidie, tuna hamu sana ya utekelezaji wa mradi huo ambao safari hii umeingizwa katika mpango wake. Lakini inawezekana mpango huu ukachelewa kutekelezwa kutokana na hayo ambayo nimeyazungumza kuhusu utendaji katika watendaji. Kwa hiyo, kwa sababu sasa mpango huo utakuwa unasimamiwa na Wizara kwa kupitia Halmashauri yenyewe ya Wilaya ya Muheza, basi naomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie kuimarisha utendaji katika eneo hili ili kwa uhakika mradi huu uweze kutekelezwa. Mji wa Muheza una matatizo makubwa sana ya maji na kwetu sisi mpango huo wa Benki ya Dunia wa Maji na Mazingira, pamoja na mpango huu wa sasa wa mradi wa maji wa Ubebe-Kwemuhosi ni sehemu ya ukombozi mkubwa wa upatikanaji wa maji katika Mji wa Muheza.

Mheshimiwa Spika, lakini ndoto hii itakuwa kweli kama kweli miradi hii miwili itasimamiwa kikamilifu. Mradi wa maji wa Ubebe-Kwemuhosi utagusa zaidi ya Kata sita, utakuwepo katika Kata ya Magila, utasaidia kusambaza maji katika Mji wenyewe wa Muheza wenye Kata tatu za Masunguru, Majengo na Mbaramo. Vilevile utasambaza maji katika Kata ya Nkumba, Mbwebwela, Kwafungo na Tigeni. Ni mradi mzuri na wa uhakika na utawagusa watu wengi, lakini lazima tupate msaada katika kusimamia kuutekeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Muheza katika kutekeleza mradi uliokuwa wa siku nyingi wa maji katika Mji mdogo wa Lusanga, umechukua muda mrefu lakini hatimaye umekamilika. Wananchi wale wa Lusanga, ambao kwa muda wa miaka mingi wamekuwa wakipata matatizo makubwa sana ya upatikanaji wa maji, sasa wanapata maji. Hivi ninavyozungumza, wapo Wahisani ambao wamejitolea kusaidia kuongeza usambazaji wa maji katika Mji huo wa Lusanga, kutoka

Lusanga A sasa kwenda Lusanga B na Lusanga C na wametoa msaada wa vifaa vya mabomba na kusaidia usambazaji wa maji katika eneo hilo. Nawapongeza sana hao ambao wamejitolea kuwasaidia Wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Muheza unahitaji uangalifu mkubwa sana. Pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo niliyoitaja, upatikanaji wa maji katika miaka inayokuja ni vizuri tukaangalia mambo mawili makubwa yafuatayo:-

Kwanza, tuangalie uwezekano wa kuupatia Mji wa Muheza maji kutoka katika chanzo cha Mto Zigi. Sasa inahitaji utafiti na utafiti ni gharama na wote tunafahamu baadhi ya Halmashauri mapato yake ni madogo ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, pato lake halizidi zaidi ya shilingi milioni 200. Kwa hiyo, tulikuwa tunaiomba Wizara wakati inafanya jitihada za kutafiti maeneo ya uchimbaji wa visima virefu katika nchi, basi sisi katika Wilaya ya Muheza itusaidie katika hilo la kutafiti kwa kuweza kuupatia Mji wa Muheza maji kutoka katika Mto Zigi.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kwamba, katika chanzo cha maji tulichokuwa nacho cha kutoka katika Mlima wa Magoroto, tumekwenda tumefanya utafiti kuna uwezekano mkubwa wa kujenga bwawa la kuhifadhi maji katika maeneo yale hasa wakati wa mvua kubwa. Basi tungeomba pia Wizara itusaidie ili tuweze kuwa na vyanzo zaidi ya kimoja na hatimaye tuweze kuangalia ni chanzo kipi kitaweza kuupatia Mji wa Muheza maji ya uhakika kwa muda mrefu na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, hayo ni maombi mawili ambayo namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, atusaidie watu wa Muheza.

Mheshimiwa Spika, ningeomba pia Wizara hii watazame Mji wa Muheza, pamoja na maeneo mengine ambayo hivi karibuni zimeundwa Bodi za Maji na Muheza inaanza kupata hadhi ya kuwa Mji Mdogo na kuwa na Bodi ya Maji. Sasa katika baadhi ya maeneo kama hayo, Bodi za Maji zikishaanza kuundwa, kabla hazijawezeshwa na Mji wenyewe kuwezeshwa kiutendaji, huduma za fedha za maji zinazoletwa katika Halmashauri sasa zinaanza kuwekwa pembeni kwamba, haziwezi kutumika katika Mji kwa sababu sasa Mji una Bodi ya Maji. Sasa sina uhakika kama ushauri wa namna hii unapotolewa na Mhandisi wa Maji katika Baraza la Madiwani unakuwa ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, kama Mji haujajiandaa na hakuna maandalizi yaliyokwisha andaliwa, sidhani kama ni sahihi kuuondoa Mji huo katika mpango wa fedha zinazoletwa kwa ajili ya maji katika Halmashauri. Nadhani utaratibu ungelikuwa mpaka hapo Mji utakapokuwa umewezeshwa. Lakini kusema huwezi kutumia fedha hizo kuchimba kisima kirefu cha maji ndani ya Mji wa Muheza eti kwa sababu sasa kuna Bodi ya Maji, inayoshughulikia suala la maji katika Mji wa Muheza, sidhani kama ni sahihi. Nitaomba ushauri wa Mheshimiwa Waziri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni jema kwa Wilaya ya Muheza ni kwamba, tumefanya mawasiliano na wenzetu wa Jiji jipya la Tanga, Manispaa Kongwe ya Tanga, kuhusu uwezekano wa kukisaidia Chuo cha Kilimo cha Mlingano. Mradi ule

wa Maji wa Tanga ni wa Manispaa, lakini katika mazungumzo ya awali, ambapo nawashukuru sana wenzangu wa Chuo cha Utafiti wa Kilimo pale Mlingano, kwa kuyaanzisha na mimi nimekuwa nikiyaunga mkono, wamekubaliana kimsingi kwamba, litawezekana jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba tu Wizara nayo itusaidie kufanya mazungumzo hayo yawezekane ili Chuo cha Utafiti cha Kilimo cha Mlingano, kiweze kupata maji ya bomba kutoka katika Mradi wa Manispaa, ambayo vilevile yatasaidia sana vijiji viwili ambavyo vimekuwa vina matatizo sana, Kijiji cha Bagamoyo na Mkanyageni. Vijiji hivi vya Bagamoyo na Mkanyageni tumefanya kila jitihada ya kuvisaidia, tumechimba visima viwili pale Bagamoyo, kimoja kwa msaada wa Irish kikapata maji kwa muda baadaye maji yale yamekauka. Lakini kwa msaada wa Marekani pia tumechimba kisima kingine kirefu, kwa bahati mbaya maji yale hayakuwa yanafaa kabisa. Kwa hiyo, pamoja na kuwa na visima viwili pale, hali ya maji bado ni mbaya na kama mpango huu wa kusaidia Chuo hiki cha Utafiti cha Kilimo Mlingano utafanikiwa kutoka katika Manispaa ya Tanga, basi vijiji hivyo viwili ambavyo vipo jirani kabisa Kijiji cha Bagamoyo na Mkanyageni, navyo vitaweza kunufaika.

Mheshimiwa Spika, naomba basi nimalizie kwa kusema mambo yafuatayo kwamba; tunawapongeza sana kwa mradi mkubwa wa maji hasa ule wa Chalinze, umewagusa watu wengi na ni mradi mkubwa na mradi huo unaoendelea huko Shinyanga. Lakini vilevile tungetoa mapendekezo ili kulisaidia Jiji la Dar es Salaam, ambalo pia lina matatizo ya maji, tuangalie ule uwezekano wa kujenga bwawa kubwa kutoka katika Mto Rufiji. Mpango kama huo ukikamilika, kama utawezekana, pamoja na kwamba ni wa gharama, ndiyo utakaoweza kusaidia kuondoa tatizo kubwa la maji linalolikabili Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zake tatu za Temeke, Ilala na Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo muhimu niliyokuwa nimedhania ni vema niyazungumze na ninaomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana wapiga kura wote wa Jimbo la Muheza, kwa kazi nzuri wanayofanya na watarajiekwamba, Mradi huo wa Maji wa Ubebe-Kwemuhosi, utakamilishwa na wasiwe na wasiwasi na huyo bwana anayeitwa Bwana yangu, miradi hii sasa inakamilishwa na Chama cha Mapinduzi na watanufaika bila ya matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijachangia ningependa kuchukua nafasi hii, kukushukuru na upokee shukrani kutoka kwa wapiga kura wangu, wanakushukuru sana kwa kuja kufungua Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Longido. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kumshukuru sana, ndugu yangu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ipasavyo, kwa kweli ameitekeleza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kufanya jukumu moja kubwa sana la kuvunja Mkataba wa *City Water*. Ningependa kusema kwamba, Serikali iige mfano huo kwa Mikataba yoyote ambayo inanyanyasa na haiwasaidii Wananchi ivunjwe. Kwa hiyo, Wizara ya Nishati na Madini, warejee kuangalia Mikataba kama kuna ya aina hiyo, wasiogope kabisa kuivunja. *TANESCO* ningeomba hebu mrejee Mikataba ya aina hiyo, kwa sababu ukithubutu kufanya jambo ambalo linawanyanyasa Wananchi, huo ndiyo uongozi, Serikali iache uwoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa tu kusema kwamba, kwanza mimi namshukuru Mheshimiwa Rais sana, kwa kuigawa Wizara ya Kilimo na Mifugo. Sisi wafugaji tulinyanyasika sana wakati Wizara hizi mbili zilipounganishwa, kwa sababu Wizara ya Kilimo iliimeza kabisa Mifugo. Unaona tu mifugo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini utekelezaji hakuna. Ningeomba hata Serikali ijayo ya Awamu ya Nne, iangalie jambo hili kwa umakini sana.

Mheshimiwa Spika, sasa natoa wosia kwa Serikali ijayosijui Mawaziri watakuwa akinanani, lakini nategemea Mawaziri walioko hapa wengi watarudi. Sina wasiwasi kabisa kwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, nafahamu kabisa kwamba, atarudishwa. Kama hapa Bungeni anapewa sifa, kule Jimboni ndiyo zaidi, kuna uwezekano hata asipate mpinzani. Kwa hiyo, Bungeni nafahamu atarudi, lakini atapewa Wizara gani sijui. Natoa wosia kwa Waziri atakayekuja kwa upande wa mifugo, napenda kusema kwamba, hili suala la mifugo katika kipindi hiki cha Awamu ya Tatu ndiyo wamekuja sasa kupata sera ya mifugo na ndiyo mikakati ya utekelezaji wa mifugo inaanza. Kwa hiyo, labda kama ni kuiva itakuwa ni kwa kipindi cha Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba, kwanza niongelee suala la wafanyakazi. Katika Wizara hizi mbili, wafanyakazi wamekaa bila kujijua kwamba wanafanya nini, hawajui wako Kilimo, hawajui kama wapo Mifugo, wana-*hang* tu kama popo. Sasa tunataka basi watengenezewe sera nzuri na watengwe kabisa kama walivyotenga Kitaifa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Kilimo na Chakula Nimeshangaa mpaka juzi juzi bado fedha za Mifugo ziko Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa nini ziwepo kule na imeshatengwa. Kwa hiyo, tunataka wafanyakazi watengwe kabisa na watengwe Kitaifa mpaka kwenye Kata, Afisa Mifugo awe ni Afisa Mifugo siyo Afisa Mifugo na Kilimo tena, kwa nini awe na kilimo tena? Afisa wa Kilimo awe ni wa Kilimo. Kwa hiyo, ningeomba hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la madawa ya mifugo. Naomba madawa ya mifugo yasiwekewe kodi kabisa, pamoja na kutowekewa kodi, naomba yasambazwe mpaka vijijini kama inavyosambazwa mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbolea ikikosekana Kusini hili Bunge linawaka moto, Serikali inapata shida sana, lakini madawa ya mifugo yakikosekana hata awamu nzima ya miaka 10 hakuna mtu anayepiga kelele na Serikali inakaa kimya. Tunaomba basi kwa

vile Wananchi wapiga kura wa Tanzania ni wakulima na wafugaji, suala la madawa ya mifugo lizingatiwe yapelekwe mpaka vijijini. Majosho yote ambayo hayatumiki yakarabatiwe na maeneo ambayo hayana majosho yawekwe na uogeshaji wa mifugo uwe ni jambo la lazima, isiwe ni jambo la hiari. Kwa sababu baadhi wakiogesha na wengine wasipoogesha ni kwamba, hatuna tulilolifanya, ni afadhali wote tuogeshe kwa wakati mmoja na iwe ni lazima. Kwa hiyo, naomba Wizara hii ishughulikie sana suala la uogeshaji wa mifugo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la pembejeo. Nashangaa pembejeo ikihesabiwa kwa wakulima tu ndio wanapata pembejeo, wafugaji hawapati. Wizara hizi mbili tangu zilipochanganywa, sijawahi kumsikia mfugaji aliyepata mikopo kwa ajili ya pembejeo, yote inakwenda kilimo. Kama tunataka basi kuwasaidia Wananchi wetu, wakulima na wafugaji, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, iwe na fedha maalum kwa ajili ya pembejeo kwa wafugaji, hata kama ni kukopa nao wakope. Kama ni kukopa madawa nao wakope, kama ni kufaidika kwa ajili ya pembejeo nao wafaidike. Naomba suala hilo sijui kama kuna fedha ambazo naulizia kila wakati kama zimetengwa kwenye bajeti zikaenda Wizara inayohusika ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ningependa kuzungumzia machache kuhusu jimbo langu. Kwanza, namshukuru Waziri, pamoja na wataalamu na ndugu yangu Sai, Mkurugenzi wa Maji Vijijini. Kwa kweli ametusaidia sana na ni mtu ambaye ukienda kwake, kwa kweli atakusikiliza na atakusaidia. Kuna visima viwili virefu vilivyochimbwa kimoja Lesingeta na kingine Mwandara, ni maeneo yenye shida sana ya maji. Wizara imewasaidia imewachimbia visima, *pump test* imekwishafanyika lakini huo mradi umesimama. Naomba basi kwa vile kiangazi kimeanza, kila siku naulizwa kwamba, hivi visima mbona Serikali haiji kuvimalizia. Sasa naomba fedha ya hivyo visima viwili ili Wananchi waweze kupata maji.

Eneo lingine ni Mradi wa Tingatinga,Wananchi wanapata maji kutoka Mto Simba unaotoka kwa ndugu yangu, Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Mradi huo ni wa zamani sana, umewekwa wakati wa ukoloni, sasa mabomba yote yameoza. Wananchi wamenunua mabomba 350 yapo tu yamelala pale kijijini, lakini hayatoshi. Naomba Serikali iwasaidie kwa sababu Wananchi wameshaonesha nguvu kuwaongezea mabomba hayo ili waweze kukamilisha mradi huo kwa sababu kila mahali maji yanavuja, kwa hiyo, hawapati maji ya kutosha. Eneo lingine ni la Engikaret, watu wanapata maji kutoka Mlima Meru. Sasa kuna tatizo kati ya Arumeru na jimbo langu, kuna eneo ambalo hakuna watu. Siwezi kusema ni watu wa Arumeru, kwa sababu sina ushahidi, wamefukua mabomba 60 wakayaiba hapo. Kwa hiyo, maji hayafiki tena Engikaret. Naomba na eneo hilo wasaidiwe kununuliwa mabomba.

Kuna hili suala la MKUKUTA, kila Wizara inajaribu kuzungumzia hili suala. Ningeomba Wizara hii itueleze sisi wafugaji tutafaidikaje na hili suala la MKUKUTA. Naomba Wizara hii itenge fedha kwa ajili ya elimu ya wafugaji *(Capaticy Building),* ili wafugaji wasiwe wanafuga tu. Tunapenda tupate elimu waanzishe *SACCOS, t*unataka tupate elimu nao waanze kununua hisa katika *Unit Trust* au hisa yoyote, kwa sababu kila hisa inayotokea wafugaji wanakaa pembeni kana kwamba wao hawapo Tanzania, sio

kwamba hawataki, ni elimu. Naomba Wizara yako itenge fedha za kuelimisha hawa wafugaji ili wasiwe wanatembea na mifugo kila wakati, wawe na kazi nyingine mbadala ya mifugo. Ningeomba kwa kweli utafute namna, ukae na wataalamu wako, waangalie namna wafugaji watavyofaidika na hili suala tunaloliita MKUKUTA, liingie nalo kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri, kama alivyoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Nitaomba radhi kwa sauti yangu kukwamakwama, kwa sababu ya matatizo ya hapa na pale hivyo, nikisikika vibaya, nafikiri haitakuwa tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nitoe shukrani na pongezi kwa Waziri na Naibu wake, kwa kuisimamia vizuri Wizara hii. Pale mtu anapofanya vizuri, kwa kweli ni budi tumpongeze. Japo labda tumekuwa tunaeleweka vibaya, sisi kama Kambi ya Upinzani kwamba, wale wanaovulunda kwa kweli kwa mujibu wa taratibu zetu, hatuwezi kuwasamehe, lazima tutawakilisha umma na tutawasema ili waweze kujirekebisha na kufanya vizuri sawa na wengine wanaofanya vizuri. Kwa hiyo, Mawaziri hawa nawapongeza. Kama nilivyowahi kusema hapa, sisi Wapinzani hatuna roho mbaya kwamba, hata Serikali tunayotaka kuiunda ifikapo Novemba,2005, Mawaziri wanaoonesha kufanyafanya kazi vizuri, lazima tutawachukua katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Hatutegemei tutoe Ma-*TX* Mawaziri kutoka Afrika ya Kusini wala Uingereza. Kwa hiyo, *keep it up,* tutawaangalia angalia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi pia namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa sababu amekuwa mstari wa mbele kwa kweli katika kushughulika na miradi ambayo imezungumzwa hapa, mingine ya Bukoba kwa ajili ya mambo ya maji. Ipo ya *UN HABITAT* amekwenda kushiriki katika vikao mbalimbali na Bukoba amefika, nampongeza sana kwa kuwa mstari wa mbele. Ila naomba wakati mtakapokuwa mna-*wind up,* mnieleze ni mikakati gani imewekwa, ambayo itakwenda sambamba na miradi yote hii miwili. Mradi wa Wafaransa na huu wa *UN HABITAT,* kusudi kuondoa mwingiliano na huenda iwe katika kuondoa tatizo la mshika mbili kwa pupa, ukakosa yote kwamba, Wafaransa wamezungumzwa kwa muda mrefu sana, zimeletwa bajeti hapa miaka minne mfululizo, ambazo zimekuwa zinapitishwa mpaka hivi sasa, kwa hiyo, anazungumzwa Mfaransa lakini Wananchi wa Bukoba, hawajaona dalili ya mradi huo kuanza. Ningeomba wakati wa ku-*wind-up,* mjaribu kulifafanua kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi zote nilizozitoa hapa za Waheshimiwa Wabunge hawa, ningeomba niweke wazi suala moja ambalo nimetumwa na Wananchi wa Bukoba na Kagera kwa ujumla, kwa sababu mimi niko pale mjini, kwa hiyo, mtu yeyote anayetaka kwenda kwenye Wilaya za Vijijini lazima apite pale kwangu. Kwa hiyo, taarifa zote za mkoa mzima nazipata. Ni kuhusu tatizo la ranchi ya Kitengule. Chini ya utaratibu mpya ambao ulitangazwa na tukaupokea vizuri kwa mikono miwili, wa kubinafsisha ranchi. Kati ya watu waliohamasika kwa kiasi kikubwa walikuwa ni

Wananchi wa Mkoa Kagera. Wengi walijitokeza katika kununua *tender documents* ili waweze kuhusishwa katika programu hiyo ya ubinafsishaji kwamba, wauziwe maeneo ili waendeshe ufugaji wa kitaalamu. Pia wengi walikidhi matakwa yaliyohitajika ikiwa ni pamoja na kuandaa *project write up,* wakafanya *feasibility study* nzuri na wakaziwasilisha na naamini wahusika walikusanya fedha nyingi sana kutoka kwa Wananchi wa Kagera kufuatana na mradi huo.

Mheshimiwa Spika, sasa kitu nilichotumwa kuulizia na nitaomba Mheshimiwa Waziri, usingoje tukakutana kwenye mafungu, Wananchi wa Kagera, ambao kimsingi baada ya kutokana na sifa waliyopata ya kupewa Manispaa kwamba, luninga huko karibu kila nyumba wanasikiliza kwa makini suala hili kwamba, imetokea hivi karibuni kabla hawa watu walionunua *tender document,* waliofanya *feasibility study* kuitikia wito wa mradi huu wameshtuka kwamba, amekuja mwekezaji mwingine kabisa ambaye yeye sasa badala ya kufuga ng'ombe, ameuziwa ardhi kubwa na kuweka mradi wa kulima miwa kwa ajili ya kiwanda cha *Kagera Sugar.* Sasa Wananchi wanashindwa kuelewa nini kimetokea kwamba, ndio kuachwa kwenye mataa, ndio kuuziwa mbuzi kwenye gunia, ndio kutapeliwa na Serikali. Kwa sababu lile waliloambiwa wafanye, wamefanya lakini matokeo yake yamekuwa kinyume.

Wanaona ardhi inafyekwa kwa kasi, maeneo ambayo Serikali ilitaja hapa kwamba, yatakuwa ni maeneo ya mfano kwa upande wa Serikali, amepewa huyo bwana anafyeka, sasa wanaomba kupata maelezo ya kina mtueleze kama mmebadili matumizi ya ranchi hiyo. Mmebadili matumizi ya ranchi kwamba, badala ya ranchi tunakwenda kwenye mambo ya miwa sasa au waelezwe hatma ya maombi yao na gharama zao, walizoingia kufanya *feasibility study* na kadhalika. *Actually,* isingekuwa mimi Mbunge wao kuwatuliza, nafikiri sasa hivi wangekuwa Mahakamani, maana yake wamehisi kuna mchezo mchafu hapa unaendelea na huenda wakapoteza hata fedha zao.

Pia wanataka kujua ni *process* gani au *procedure* gani zimetumika mpaka huyo akapewa lile eneo la ranchi kulima miwa, alitumia *approach* gani? Kwa sababu wakati lilipotangazwa suala la kubinafsisha hii ranchil ziliwekwa taratibu za watu kuomba na watu wakaomba na bila shaka kwenye kuomba wengine wanapata, wengine wanakosa. Ukiachilia mbali kwamba, walioomba kwa sababu mambo ya ranchi hawajapewa na huyu amepewa, lakini wanauliza huyu bwana alipita mkondo gani? Wanatakiwa waelezwe humu humu Bungeni, alipita mkondo gani, kwa sababu haikutangazwa kwamba, labda ardhi imebadilishwa kwa matumizi ya kulima miwa, watu ambao wanataka kuwekeza kwenye miwa njooni mnunue hii ardhi na muwekeze. Ni *process* gani iliyotumika?

Hii naamini itaweza kusaidia kuondoa, kitu ninachokiita redio vifua, habari zisizokuwa rasmi. Maana yake wengi sasa hivi maneno yanayozungumzwa wanasema, mashamba hayo huyu bwana amepewa kwa kifua cha watu wakubwa, ndio wametumika pale na kwamba hata anavyolima vile vyote ni vya wakubwa. Ni mashamba ya wakubwa na *process* iliyotumika ni kubwa na ikatumika *shortcut* na ndiyo maana akapewa. Sasa nafikiri ili kuondoa doa hilo, maana yake wengine wanafikiri labda kwa sababu ule mkoa umetembelewa na wakubwa wengi mfululizo na wengi walitembelea

maeneo hayo, huenda kwamba waliokwenda kule kwa ajili ya kuona hicho kitu ambacho wame-*push* kwa misingi ya wao kunufaika. Tutaomba aliweke wazi hapa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba, suala la ranchi ya Kagera ni nyeti. Suala la ranchi ya Kitengule ni suala nyeti linawagusa Wananchi kwa sababu naamini, kwa kutii taratibu na sheria za nchi ndiyo maana ile ranchi imekuwepo. Wengi walikuwa hawaivamii na hata lilipokuja zoezi la kuwaondoa Wakimbizi wa Kinyarwanda waliokuwa wamehamia pale na mifugo yao, Wananchi walishiriki kikamilifu kwa kushirikiana na Serikali kuwaondoa ili Wananchi waendelee kuona fahari ya ardhi yao na matumizi ambayo yalikuwa yamekusudiwa ya kuwa na ranchi za Taifa. Sasa baada ya kuwaondoa Wanyarwanda, hawa Wakimbizi, sasa anakuja Mkimbizi mwingine, mhamiaji mwingine wa miwa, jambo ambalo hawako tayari kukubaliana nalo na nitaomba Serikali ilifafanue kwa uwazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunalizungumza hivi kwa sababu waathirika ni sisi kule Mkoa wa Kagera. Unapoingiza miradi mingine tofauti na ile iliyokusudiwa ya ranchi, unasababisha maafa mengine. Sasa hivi kwa bahati mbaya huyu mwekezaji tayari ameshahamisha ng'ombe wote wa eneo hilo ambalo lilikuwa la ranchi, amewahamisha amewahamishia Misenyi huko, pale ameanza kufyeka miti, ukifika pale hii hali inatisha na kwa ghafla Bukoba nyama imepanda kwa kiasi kikubwa. Sasa hivi kilo moja ya nyama inakwenda mpaka shilingi 1,400 au 1,500/= kutoka kwenye shilingi 800/= mpaka 900/= ilivyokuwa bei ya awali. Hii ni kwa sababu ng'ombe sasa hivi wameanza kuchukuliwa toka Mikoa ya Shinyanga na Mwanza, jambo ambalo halikuwepo. Sasa hili ni tatizo la kimsingi na sisi tunasema kwa kweli katika hali iliyo ya uwazi, Wananchi hawataielewa Serikali. Kama mnataka kunusuru kura zenu, nasema kama mnataka hizo kura zenu kidogo ambazo zinataka kupeleapelea, bora hili suala mlizingatie na mliangalie na mlishughulikie kwa haraka sana, mrudishe hii ranchi katika matumizi yale. Watu waliotangaziwa kununua hizo *blocks* zilizotangazwa wauziwe, zile *blocks* zilizotangazwa ni za Serikali kuonesha mashamba ya mfano, zirejeshwe kwenye matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, sisi Wananchi wa Kagera, pamoja na hicho kiwanda, tuna shida kweli ya sukari. Tunasema pamoja na hicho kiwanda kuwepo bahati nzuri kimeanza *production,* lakini kabla *production* ya hicho kiwanda kuanza, bei ya sukari ilikuwa shilingi 600/= au 700/= kwa kilo. Leo *production* imeanza na mauzo yameanza ya kiwanda hicho, bei ya sukari kwa kilo ni shilingi 1,000/=. Kwa hiyo, sisi tunasema huyu mwekezaji wa sukari, hajatusaidia chochote kumbe anataka kutumaliza na tusipate hata nyama. Sukari hatupati ya bei nafuu, nyama hatupati ya bei nafuu, imekuwa ni kuliwa sehemu zote mbili. Mmenipata hapo? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ombi la Wananchi wa Kagera, kwa sababu kwa kweli haya ni maafa ya Mkoa wa Kagera, kwa mwelekeo huu, nafikiri hatutafika popote. Tutaomba ufafanuzi kwa kweli nini kimetokea na hatua gani zinategemewa kuchukuliwa haraka kunusuru hali hii. Watu wajue fedha yao ipo au haipo, imeliwa vipi na huyu mtu aliyevamia ametoka wapi, kwa nguvu gani na kwa kifua cha akina nani? Hayo ndiyo wanataka kuyajua hapa hapa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa kumalizia niwashukuru Wananchi wa Bukoba Mjini, ambao wameendelea kunipa ushirikiano mkubwa. Pia niwashukuru Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa *CUF* Wilaya ya Bukoba, nilishukuru Baraza Kuu, kwa sababu limeshanitangaza kabisa kwamba, mimi ni mgombea pale kupitia tiketi ya *CUF,* kama nitafika salama hiyo tarehe 30 Oktoba, 2005. Sasa hicho kimbunga kinachokuja huko mbele, nasema kama walivyozungumza wenzangu hapa, wengine wamesema wakija watawadhalilisha watu kwenye majimbo, mimi namkaribisha mtu yeyote kwa sababu ndiyo demokrasia ya mfumo wa vyama vingi, ambao tuliukubali kwa mujibu wa Katiba yetu. Wananchi wa Bukoba ndio wenye uwezo wa kuweza kuamua nani awe Mbunge na zaidi watapima nini kimefanyika, nini wameshirikiana na mtu gani katika kufanya lile lililofanyika. Kwa njia hiyo, kwa sababu nimekuwa bega kwa bega na Wananchi wa Bukoba Mjini, naamini kuna kila sababu ya kumgalagaza yeyote atakayetokea pale Bukoba Mjini. Namkaribisha yeyote atakayetaka kupata mateso akaribie lile Jimbo la Bukoba Mjini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niingie katika mpango wa kuchangia hoja hii muhimu ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Hoja iliyoko mbele yetu ni kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ya mwaka wa fedha 2005/2006. Nimeshachangia kwa maandishi, nadhani umeona baadhi ya maswali na nimejua kabisa kwamba, maswali sio mikopo, na majibu sio malipo. Kwa hiyo, unaweza ukanijibu kimaandishi vile vile ili kusudi upate kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni moja ya Wizara ambazo zinapewa shukrani nyingi na hata Wapinzani waliunga mkono na Watanzania kwa ujumla, wanaona kama ni mashahidi kuona maendeleo kadhaa yanajitokeza na yamejitokeza kwenye kitabu hiki. Kwa kweli hiki ni kitabu kizuri kimeonesha mambo mengi na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi *hundred percent* katika Wizara hii. Hii inatokana na Waziri mwenyewe kujituma na Naibu Waziri wake na watendaji wake kuwa kundi moja.

Lakini kabla sijaweza kuzungumza lolote kwa Wizara hii, naomba nipongeze tu tendo la kuhamia Dodoma. Mmehamia Dodoma Wizara yenu, Wizara ya Tawala za Mikoa na Wizara ya Ushirika na Masoko. Nilizungumza mwaka 2004, nilipokuwa nikichangia Ofisi ya Waziri Mkuu, nikasema kumbe tendo la kuhamia Dodoma hamisha *Imamu,* usihamishe Masheikh. Kwa sababu Masheikh wako wengi, ukimhamisha *Imamu* akibaki kwenye msikiti kule atasema *allahu akbar,* yaani Mungu mkubwa, watakwenda kusali kule kule. Kwa hiyo, uongozi unaokuja naomba tafadhali sana Waziri Mkuu anakuwa Dodoma ndiyo *Imamu* wa Serikali yetu.

Nilizungumza vile vile kwa utani tu lakini kweli nimesema hata kinyonga mzee angeambiwa wakati matamko yale ya kuhamia Dodoma kipindi kile kinyonga mzee angeanza safari Dar es Salaam angekuja Dodoma na kurudi kufuata familia yake na kurudi Dar es Salaam na angefika na angekaa angetumia hata kilomita moja kwa saa 48, angetumia miaka mitatu tu yuko Dodoma kinyonga mzee na familia yake. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo ni kwamba, Wizara hii haikupata majaribu kwa sababu majaribu hujaribika ila imepata matokeo kwa sababu matokeo hutoweka. Kwa sababu majaribu mara nyingi yanapoharibika huleta vurugu baridi, kashfa za kina na maisha ya kutegana. Lakini matokeo yakitoweka huwa mara nyingi hutoweka kubaki kumbukumbu, Wananchi hufuatilia zaidi. Watu kama hao hutenda leo hawangoji kesho kwa sababu kesho ni ndoto, jana historia na leo ni vitendo. Wizara hii imetenda leo, kwa sababu kesho haiji na jana haisogeleki na leo haiondoki, kwa hiyo, tenda leo. Ahsante mnatenda leo na mmepata matokeo haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naingia sasa kwenye Muswada wenyewe, katika miradi ya maji ambayo imefanyika Jimboni Morogoro Kusini Mashariki. Natoa shukrani kwamba, mwaka 2003, niliamua kukuandikia barua ukatoa shilingi milioni 12 kwa ajili ya malambo matano na tayari malambo yale yamekamilika na tulikwambia uje kufungua lakini kipindi hiki kwanza nenda kapate kura za maoni za Wananchi wako wakurudishe baadaye tutafungua, baada ya kura za maoni utakuja kufungua. Tuna lambo la Ekenyo, Lugaga, Mkulazi, Chanyumbu, Molingwa na sehemu za Ngerengere, ambalo ndilo jibu ulilojibu juzi na kuna malambo mawili ambayo yanakusudiwa pale *DAFCO* Ngerengere tunayasubiri kwa hamu.

Vile vile napenda kuwapongeza wafugaji wa maeneo hayo, wamechangia kiasi kikubwa kweli cha fedha, kwa sasa hivi tunahamasisha wafugaji wengine maeneo ya jimbo hilo waweze kuchangia. Kwa sababu unapochangia wakati mwingine unaondoa vurugu kati ya wakulima na wafugaji, sasa hivi maji yamejaa na Wananchi wanatumia kwa raha mustarehe. Lakini mfugaji anachohitaji ni kupungua kwa bei ya madawa, madawa yaliyopitwa wakati wake yaondolewe katika maduka, kupunguza kodi ya aina ya madawa katika minada kuwe na huduma za kutosha, malambo ya kunyweshea yawe karibu, vile vile magonjwa ya mifugo kudhibitiwa na kuwekewa dhamana katika upande kufanya mifugo kama ni dhamana na maeneo yanapokaa ili waweze kukopa maeneo haya.

Kwa sababu Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Kilimo na Chakula wametengana basi kila mtu achukue eneo lake. Napendekeza kuwepo na mfuko wa pembejeo wa mifugo au ianzishwe Benki ya Wafugaji, sio lazima wajiingize kwenye *SACCOS*. Naomba Benki ya Wafugaji ianze kusudi wafugaji waweze kuwa wabia katika Benki hiyo.

Nazungumzia mifugo maana yake ni kuku, mbuzi, kondoo, sihodhi katika upande wa ng'ombe peke yake, wafugaji sio Wamasai peke yao. Kwa mfano, Ngerengere kuna wafugaji, kuna mtu anaitwa Maketemu, ambaye sio Mmasai, kuna Watanda, Salmin, Urembo, Mustapha, wote wanafuga vizuri sana na wana ng'ombe wengi karibu maelfu na

kuna ng'ombe katika ufugaji bora na wanachunga vile vile. Kwa upande wa wakulima na wafugaji, migogoro kwa kweli mwaka huu imepungua kwa sababu ya kuwakabidhi wenyewe. Ingekuwa inatumika Mahakama peke yake ingeleta matatizo. Lakini kwa mujibu wa wadau waliokutana kule Arusha, ambapo mimi nilikuwa mdau mmojawapo, tuliweka utaratibu mzuri, vitabu vile tulitoa *photocopy* na kuwapatia *VEOs* wa Vijiji ili waweze kuunda Kamati za Wafugaji na za wakulima, kuyamaliza mambo mengine kule kule kuliko kulundikana na kuleta ujirani mzuri tu katika masuala haya. Migogoro inaleta matatizo wakati mwingine kwa sababu unapokuwa na migogoro unaleta matatizo watu hawawezi kuendeleza maendeleo yao. Kwa hiyo, nimefurahi sana kwa hili.

Kwa upande wa Morogoro Vijijini, tunawapongeza *VHV, World Vision* na *World Bank* na Wananchi kwa ujumla. Halmashauri ya Wilaya walifanya miradi mikubwa mikubwa ambapo mradi kama wa Mkuyuni wa Maji umekamilika, Mradi kama wa Kilopa umekamilika na Miradi ya Kambara na Mkambarani bado inasuasua na Wananchi wa kule Kambara wasaidiwe, ambalo ni jimbo la Morogoro Kaskazini. Kambara pale pana matatizo kidogo ya mambo ya maji na mipaka ya wakulima na wafugaji. Hili litazamwe vile vile, tutasaidiana katika kumaliza hili. Wananchi wa Kisaki, Mbwade, Mvuha, Mikese, Tununguo, Kidugalo, maeneo ya Magindu kule Seregeti A hadi Lubumu, Ekenyu na Visaraka, wasaidiwe ili matatizo madogo madogo haya yakikua yataleta matatizo, yatakusumbua bure kama alivyosumbuliwa yule Maganga.

Mheshimiwa Spika, siku moja Maganga aliaga wanawe akaiita familia akasema nimepata *offer* kutoka Wizara fulani nakwenda Marekani. Akasema naomba wanangu mniagize. Wakaagiza vitu lakini mtoto mdogo anayeitwa Chrispin Maganga wa miaka mitatu, alimwambia baba mimi nataka baiskeli. Sasa Maganga alikwenda kukaa miaka mitatu Marekani, akajua huyu atasahau tu, akadharau. Wale wengine walioagiza vitu vikubwa vikubwa akawaletea. Baada ya miaka mitatu kurudi baiskeli amesahau. Alipofika pale nyumbani Chrispin akamwuliza baba umeleta baiskeli? Baba akamwambia samahani inakuja na ndege nyingine. Alijua atasahau tu.

Amemzonga yule baba mpaka ilibidi mtoto amdanganye sasa, akamwambia kama wewe hutoniambia kama baiskeli hukuninunulia, basi sikwambii aliyekuwa analala chumbani kwa mama. Ilibidi Maganga ainunue baiskeli akamwambia nimeipata imeshakuja tayari na ndege. Sasa akamwambia mwanangu baiskeli hii hapa, niambie kwa siri kabisa nani alikuwa analala chumbani kwa mama. Akasema nilikuwa nalala mimi. Alikuwa Chrispin kumbe alikuwa analala kwa mama yake kule alipoondoka. Sasa hizi kero ndogo ndogo hizi mnaweza mkapata gharama kubwa ya kununua baiskeli ghafla ghafla, zimalizeni mambo ya malambo haya malizeni ili yaishe msije mkanunua baiskeli za ghafla ghafla baadaye kabla Bunge halijaisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna mradi mwingine ambao ni mkubwa ulikuwa kule Mkulazi, mlijibu maswali hapa mara tatu. Kwa kweli Mheshimiwa Edward Lowassa, wageni wa Kitaifa walifika kule Mkulazi kuangalia masuala ya *JICA* na uliona barabara ile ambayo ilikuwa mbovu na sasa hivi inatengenezwa. Baada ya kupiga konde hapa inatengenezwa sasa hivi, greda lipo Matuli Km. 17.5, nimeambiwa kwa simu jana. Sasa ule mradi ulikuwa umeanzishwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri, Waholanzi mwaka

1989, *Before* Pawa, kabla mimi sijawa Mbunge, walikuwa wanaandika *BP,* yaani *Before Pawa. (Kicheko/ Makofi)*

Mwaka 1989 walikuwa wameleta karibu shilingi milioni tano za kusaidia Mradi wa Mkulazi na walinipokea nilipokuwa Mbunge, wakanikaribisha pale tukaunda chama kinachitwa MKUTIKO, kwa ajili ya kufuatilia hili.

Aliyekuwa Waziri wa Maji wakati ule kwa kweli tulisaidiana sana, na Afisa Mipango wa kule, baadaye Dayosisi ikakatika ikawa sasa Dayosisi ya Pwani na Dayosisi ya Morogoro, tukapata Askofu mpya pale, Baba Kitale, ambaye anauendeleza vizuri mradi ule.

Baadaye Wizara kwa wakati ule, ikanunua vifaa mbalimbali, ikapeleka trekta, tukapeleka matofali, tukapeleka vilevile na vifaa vingi tu vya kusaidia mradi ule na mabomba. Baadaye mabomba yale yakaja yakayeyuka ghafla. Nadhani huo ndiyo mgogoro uliotokea katika Kanisa la Kilutheri la Kiinjili kule Morogoro.

Bahati mbaya yule Katibu Mkuu aliyekuwepo wakati ule wa kanisa hili amefukuzwa sasa yupo Katibu Mkuu mwingine nadhani afuatilie kumbukumbu zile ili watume Tume kwenda kuangalia mahesabu ya mradi ule. Kwa sababu sasa hivi mradi wa maji umeshajijengea tayari malambo mawili kule. Kwa hiyo mradi ule sasa hivi watoe maelezo ili kuimarisha.

Nimesikiwa jana vijana wa kule wameunda Kamati ya kufuatilia Maji Kata ya Mkulazi, nashukuru nimewakaribisha wafike hata kesho waje ili kufuatilia, waanzie kwenye Kanisa la Kilutheri la Kiinjili, kuhoji fedha ambazo Waholanzi wamezileta kupitia Katibu Mkuu wao na kupitia Afisa Mipango wao, Ndugu Bogasi, ambaye alifanya kazi nzuri tu. Wafuatilie kule halafu na Serikali itachangia, yale kama ni maji ndugu tu, waanzie pale. Kama fedha zimeliwa Kanisa lifuatilie kwa kasi, kwa sababu dini sio mahali pa mchezo, dini, "D" ni duniani, ile "I" ni imani, "N" ni nia na ile "I" ya mwisho ni Ibada. Kwa hiyo, hakuna kitu cha mchezo mchezo. Wafuatilie kile kitu na mimi nitakwenda Mkulazi kesho kutwa kufuatilia barabara ile ili nipate jibu hilo. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ni kwamba, tumesema kwamba, wakati mwingine inatokana na ulafi na uroho, mlafi ni mtu mzuri, anakaribisha wenzake ila anawapunja, lakini waroho huficha hata mtu akiathirika yeye chakula hata kikiharibika. Ilifanyika operesheni moja pale Muhimbili, mtu mmoja alikuwa anafanyiwa operesheni ya macho ni *very sensitive*, lakini sasa hivi macho yanakuwa yanafanyika kwa kutumia *new test solution,* kwa utaratibu huo basi ilibidi walifanye haraka haraka, bahati mbaya Nesi kwa kutetemeka alitoboa lile jicho la mgonjwa, maji yakatoka, ilibidi Madaktari wamkalipie na hata kumkalipia haisaidii ilibidi ni lazima tusaidie hiki kitu. Bahati nzuri sana akapita paka mmoja mkubwa kwenye wodi, wakamkamata akapigwa sindano wakachukua jicho moja la paka likawekwa kwa yule mgonjwa, kuwekwa likafiti wakaambiwa Manesi mmeapa msiseme kwamba, hili ni jicho la paka tutashtakiwa, semeni kemikali. Wakaapa jicho likaunga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, siku ya majaribio, wakaziba jicho la paka wakamwambia taja waliokuwa mbele yako, akasema yule ni Spika na wale Makatibu, akamtaja Mheshimiwa Edward Lowassa, akataja na wengine na viongozi wa Upinzani. Wakaziba jicho la binadamu wakamwambia taja waliokuwepo, akasema naona mapanya tu, alikuwa haoni chochote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jicho la paka huoni hata kitu kimoja, unaona mawindo yako. Naomba viongozi ndani ya nchi hii, tuvae macho ya binadamu tuone tunaowaongoza, tusivae macho ya paka, tuvae macho ya binadamu ili tuone tunaowaongoza ili kuweka utaratibu mzuri wa kuwaongoza watu wetu. *(Makofi)*

Maji ni muhimu katika nchi hii, wamesema elimu ni ufunguo wa maisha, ingawa maisha sio kufuli, imesemwa kabisa maji nayo ni uhai wa nchi. *(Makofi/kicheko)*

Kwa hiyo, nimeshukuru sana kwamba, miradi katika Jimbo lile imekamilika

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asante. *(Makofi/ Kicheko)*

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ili na mimi niungane na wenzangu katika kuchangia hoja hii. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi nzuri kwa kweli anayoifanya, naona pongezi nyingi amezipata na bila kumsahau ndugu yetu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa kweli amesaidia sana katika ufuatiliaji hasa kwa upande wa wafugaji. Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii kwa kweli tunawapongeza sana na muendelee na kazi hiyo kwa kipindi kijacho na tunaamini tutaendelea kuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Mbarali, nimeona nichukue nafasi kwa kweli niishukuru Wizara hii, hasa Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya Wilayani Mbalali. Kwa sababu Wilaya ya Mbalali ni sehemu ambayo ni kame sana hasa kwa upande wa maji ya matumizi ya binadamu na hasa ukizingatia kwamba, kuna wafugaji wa aina zote wanaopatikana Tanzani hii na mifugo ni mingi zaidi ya 600,000. Lakini nasema upendeleo wa pekee, pamoja na shida na pesa zilivyokuwa ni shida kuzipata, lakini Wilaya ya Mbalali tumepata upendeleo. Nasema nimekuwa nikimsumbua pale ofisini na hapa ninapozungumza Wananchi wa Kata ya Madibila, wametuma salamu za pekee kwamba, zile pesa shilingi milioni 10 na Katibu Mkuu aliongezea shilingi milioni mbili, kuweza kukamilisha lile tatizo la maji, wamezipata wanakushuru sana. *(Makofi)*

Sasa vilevile niwapongeze Wananchi wa Mbarali, wameweza kuitikia wito kwa moyo mmoja kwa miaka mitano kwa kila kijiji kuweza kufungua mfuko wa maji na hii yote ni kutokana na tatizo la maji ambalo lilikuwa likiwazonga kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nashukrani zote, nimesoma katika kitabu, Mheshimiwa Waziri, anasema kuna mradi katika bajeti hii ya mwaka 2005/2006

kwamba, kutakuwa na mradi mkubwa wa upanuzi wa maji katika Wilaya ya Mbarali. Sasa nilitaka anifafanulie ni upanuzi wa aina gani na maeneo gani ambayo yatahusika hasa kwa eneo hili la Mbarali ili na Wananchi wa Mbarali waweze kusikia na nitakapoondoka hapa niweze kuwa na imani kuwa, sasa nikawaeleze Wananchi kwamba, mpango mkubwa unaokuja ni mzuri, tatizo la maji kwa matumizi ya binadamu litakuwa limeondoka kwa Wilaya yetu ya Mbarali.

Nasema hili kwa sababu amesema kwa mwaka huu mpaka sasa wamekamilisha kwa asilimia 53 kuondoa tatizo la maji vijijini. Mbarali kama ilivyo, anaifahamu ameshaitembelea Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kweli ni kame, tumechimba visima virefu 84 na pesa nyingine amekuwa akichangia yeye kutoka Wizarani kwake, lakini vinavyofanya kazi ni visima 14 tu mpaka sasa. Unachimba vinatoa maji kwa muda wa miezi miwili, mitatu, kinakauka, baadaye tena mnaanza kuchimba sehemu nyingine. Sasa hasara ya pesa zote na kila kisima kinagharimu zaidi ya shilingi milioni sita, sasa ukizidisha shilingi milioni sita mara 84, ni hela nyingi ambazo labda zingeweza kusaidia kutengeneza mradi mkubwa au mradi wa maji ya bomba kutoka kwenye Wilaya ambayo iko jirani. Sasa kama huo mradi ambao ameutoa Wilaya ya Mbarali, nikipata ufafanuzi mzuri na Wananchi wakasikia, naamini kabisa kero ya maji kwa Wilaya ya Mbarali itakuwa imeondoka na mimi naomba nimpongeze na kumshukuru kabisa kwa kuiangalia kwa jicho la pekee Wilaya yangu ya Mbarali na Jimbo langu la Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie upande wa mifugo. Mheshimiwa Waziri, anafahamu kwamba, Mbarali inawafugaji wakubwa kabisa wale wa Kisukuma, Wamasai na makabila mengine na hata wagogo. Sasa unaposema malambo, wanaangalia kwa mfano, wenzetu wa Kisukuma walihamia pale kwa kufuata sehemu ambayo ni ya chepechepe. Walikuja kufuata majani ya kulishia. Kweli ulinipa malambo kama manane nichimbe mwaka huu na Wasukuma wengine walikufuata mpaka hapa. Sasa unachimba malambo, wanasema sasa hayo malambo watakunywaje na malisho hayapo, sisi tulihamia huku kwa ajili ya kufuata sehemu ile ya Ihefu ambayo kuna majini ambayo tunaamini sisi ng'ombe wetu wakila wanazaliana sana. Sasa kumekuwa na ugomvi ambao upo kati ya Uongozi wa Wilaya, wa Mkoa na wafugaji, ni kitu ambacho hatuelewi kitaishaje na mifugo inazidi kuongezeka, mfugaji mmoja ana mifugo zaidi ya 1,000, 500 au 600, ukimwambia apunguze, haelewi maana ya kupunguza, yeye kazi yake anataka aone mifugo anaiona kwa mbali mita 100 ni mifugo yake tu.

Sasa malambo tunachimba na ukiwaambia ainisheni sehemu mnayofikiri tuchimbe malambo, wanasema hapana sisi tunaomba kabisa hii sehemu ya hifadhi ya wanyamapori basi tumegewe sehemu kidogo. Sasa tatizo kama ulivyowajibu kwamba, wewe ni Waziri wa Maji, vilevile ni Waziri wa Mifugo, nikiwaruhusu muingie pale Ihefu, ni tatizo maana yake vile vyanzo vya maji vitaharibiwa na maji hayatapatikana na pia umeme hautazailishwa. *(Makofi)*

Sasa nikisema mifugo isapate hifadhi vile vile nitakuwa nimekiuka kwamba, mifugo siiangalii inavyopaswa kama sera yako inavyosema, sasa sijui kwa hili tunafanyaje wote Mheshimiwa Waziri, kuhakikisha hili tatizo tunalitatua? Kama ni

kupunguza mifugo watapunguzaje na kama tutasema tuwatengee maeneo yao, maeneo wanayotengewa waweze kupata maji na malisho itakuwaje?

Kwa kweli Wilaya tumejitahidi kadri tunavyoweza na kwa sasa mapato mengi yalikuwa yanatokana na ushuru wa ng'ombe. Sasa tulipoufuta, hakuna mapato mengine Wilayani Mbarali zaidi ya mazao na mazao mengine ni mpunga, kitu kidogo sana. Ukisema Halmashauri itumie pesa zake kwa ajili ya kutenga maeneo na kuwatafutia maeneo imekuwa ni tatizo.

Kwa hiyo, nimekuwa nikikuomba mara nyingi na leo nakukumbusha kwamba, kwa kweli juhudi za pekee zichukuliwe kuhakikisha kwamba, tunasaidiana kwa maana Serikali Kuu iisaidie Halmasahuri, tunone tunafanyaje. Kwa sababu hawa wenzetu, tunaosema ni wawekezaji wa Wilaya ya Mbarali, lakini sehemu wanayoitaka ni lie ambayo Tanzania nzima tunaiangalia kwamba ni chanzo cha maji na ni sehemu muhimu sana kwa ajili ya uzalishaji wa umeme kwenye bwawa hili la Mtera na ukiwaruhusu tu, maji huku hayataenda. Tunawafanyaje hawa wafugaji au tunawatengea sehemu gani na kama tutaweza kuwasogeza labda kwenye sehemu nyingine labda Wilaya ambazo zinazunguka, ambazo tunafikiri watapata bwawa la maji na watapata malisho na kuwaelimisha?

Labda niungane na Mheshimiwa Lekule Laizer aliposema kwamba, tunazungumzia sasa hizi hisa za umoja, labda kweli elimu kwa pamoja, pesa itolewe kwamba, waelimishwe hawa wafugaji kwamba, badala ya kukaa na mifugo mingi sasa na wao wauze mifugo kwenye hizi hisa ambazo zinauzwa. Tungetumia hata mwezi mzima tukawasomesha kwamba, mkiuza ng'ombe wenu mkanunua hisa hizi ambazo zimetolewa, mwisho wa mwezi wa saba na wao wakawekeza faida watakayoipata kwenye ng'ombe, itakuwa ni ndogo zaidi kuliko kama wangewekeza kwenye hizi hisa angalau wakabaki na ile mifugo kidogo. *(Makofi)*

Sasa hii yote nafikiri tungeungana pamoja na Mheshimiwa hapa amesema ni mfugaji maarufu na mimi nimekuwa ni mfugaji sasa maarufu kwamba, tutoe elimu kwa kina, hawa wenzetu waweze kutuelewa hasa hawa wenzetu wa Kisukuma, nafikiri wanaona umaarufu wa kuwa ng'ombe ni mzuri zaidi kuliko kuwa na pesa, kwa sababu maisha hayabadiliki. Sasa tukitoa elimu, nafikiri wataitikia tu kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa ubinafsishaji wa hizi ranchi. Nasikia wenzangu wanasema lakini nasema, ubinafsishaji wa haya mashamba ya mifugo, yaani ranchi, kwa upande wa Wizara hii, umefanyika vizuri sana. Kwa kweli umekuwa ni wa ushirikishwaji, mimi nina ranchi kule ya Usangu ambayo tuliitangaza kwenye kila kijiji kwamba, kuna ranchi imegawanywa kwa hiyo, mfugaji yeyote au kama kuna chama chochote, wanaotaka wanaweza wakaomba. Vitabu vimeuzwa kwenye ofisi za Watendaji wa Kata, Halmashauri, kwa hiyo, kila mtu mwenye uwezo aliweza kununua na ile kazi imekamilika na namshukuru Meneja wa *NARCO* na watendaji wake. Kweli kazi ile imekamilika na mpaka sasa sijasikia malalamiko na nilipokuwa nachangia Wizara ya Kilimo hapa, nilisema kama Wizara ya Kilimo kwenye mashamba haya yote makubwa ya *NAFCO,* wengefanya kama

walivyofanya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, nafikiri malalamiko mengi yasingetokea. *(Makofi)*

Kwa sababu Wananchi wana uwezo wa kutumia ardhi yao hasa ukiwapa *option* kwamba, chukueni wakashindwa wenyewe, halafu sasa wakishindwa wenyewe inakuwa ni kitu kingine, lakini tukiwawezesha na tukawapa maeneo, maana yake ndiyo fursa yao ambayo inawafanya waondokane na umaskini. Sasa hilo, nalishukuru sana na nalipongeza.

Lakini nilikuwa nina swali moja kwamba, ile hati ya zile ranchi ni moja, labda tupate ufafanuzi baadaye, je, zile sehemu ndogondogo kila mmoja aliyepata kutakuwa na uwezekano wa kupata hati yake ili aweze kuitumia kwa ajili ya kukopa Benki kwa ajili ya kutafuta mitaji mbalimbali. Kwa sababu akishakabidhiwa inakuwa ni kwamba, unatumia ile hati tu ya ile ranchi kama ranchi. Sasa sijui utaratibu gani utatumika? Kwa hiyo, nitaomba nipate huo ufafanuzi ili watu waliopata zile sehemu waweze kuwa na jibu na kujua ni nini kitawanufaisha.

Kwa hiyo, sambamba na hiyo hiyo Ranchi ya Usangu, Mheshimiwa Waziri hajafika, lakini wataalamu wake wamefika, ile njia kwa kweli sio nzuri, inakuwa ni tatizo hata kwa wale wawekezaji wanaotaka kwenda kuangalia kwamba ni sehemu gani wamezipata. Sasa kama kutakuwa na bajeti yoyote, mkiweza kuangalia kwa njia yoyote, tuhikikisheni ili ile njia kwanza ilimwe iweze kupitika na pale ambapo wataalam watakao kwenda kuwaonesha wale waliopata zile sehemu iwe rahisi. Kwa hiyo, hilo niliomba nilisisitize kwamba, tuungane na Waziri wa Ujenzi, kwa maana ya *TANROAD* pale Mkoani, Waziri wa Fedha na Wizara yako, kuhakikisha kwamba, tunaboresha ile njia na tuweze kuwavutia wale ambao wamepata zile sehemu na waweze kufanya shughuli za mifugo kama ilivyoelekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni upande wa wataalam, tulikuwa tukizungumzia hapa mambo ya Afisa Kilimo na Afisa Mifugo. Hii Idara kwenye Halmashauri yetu inatusumbua sana, huyu Afisa Mkuu wa Idara wa Mifugo na Kilimo amekuwa na kazi kubwa, kwa sababu Wizara hizi zote ni kubwa. Kwa upande wa Mbarali, kilimo ni sekta kubwa sana na mifugo ni sehemu kubwa sana. Lakini amekuwa hata hana usafiri maana ukisema niiombe Wizara ya Kilimo, wamsaidie huyu mtu apate usafiri wa gari wanasema nendeni Mifugo. Kwa hiyo, kwa mfano, pale kwangu, Mkuu wa Idara ya Kilimo na Mifugo hana gari, ni mtu wa kuazima gari kwenye Idara nyingine, sasa hatujui ni Wizara gani ambayo itawajibika kuweza kumsaidia na kazi zinakuwa ni nyingi kwa sababu haieleweki kazi gani anazifanya, amesomea kitu gani na si rahisi mtu akawa anavitu vyote na akawa ana uwezo wa vitu vyote. Imekuwa ikituyumbisha sana na hata hawa Wahandisi ya Maji, pale kwangu nina Mhandisi wa Maji, kama ana Msaidizi ni mmoja na ilikuwa kichekesho wakati fulani, kwa sababu *Mister* ndiyo Mhandisi, Msaidizi mke wake. *(Kicheko)*

Sasa hiyo ni Idara imekamilika na ni Wilaya ambayo haina maji, sasa sielewi kama hili tatizo lilishawahi kufika huko au kama ni sisi ndiyo tunatakiwa tufanye hiyo kazi. Kwa kweli inachekesha huyu mtu utategemea aweze kufanya *planning* ya maji ya

Wilaya nzima, achore ramani, aweze kufanya mipangilio yote ya kuweza kupata maji katika Wilaya na ni mtu na mke wake ndani ya Idara moja, inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, hilo nilitaka kuonesha kwamba, hali ni ngumu na ndiyo maana tunapata matatizo na labda hata hizo bajeti zinazokuja haziwi zile za kimvuto sana na labda hata huu mradi ambao tumeupata ni kutokana na malalamiko ya Mheshimiwa Mbunge au na wataalam wako, ambao wamekuwa wakitembelea kule Mbarali kuona kwamba ni tatizo la maji

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niwashukuru sana na niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa kazi nzuri ambazo wamezifanya, bila kuwasahau watu wa *WWF*, wametusaidia sana, *DANIDA, UNICEF* na *FAO*. Kwa kweli wamesaidia sana katika kupunguza kero za maji za hapa na pale, kwa njia ya kutusaidia kuchimba visima na ninaomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi na kwanza moja kwa moja niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nikiwa mtoto niliwahi kupigana na mwenzangu, kuna gari ilipita nikasema gari yangu hiyo, yaani gari yangu ile, mwenzangu akasema sio yako yangu, basi ugomvi ulikuwa mkubwa pale ngumi zikaanguka, utoto huo. Yaani unazungumzia mambo ambayo hayawezekani kwa sababu ile gari ni ya mtu, sasa na hawa vijana wetu watoto tuwasamehe. Wanazungumza kuunda Serikali. Serikali itawezekana wapi kwa wao. Maneno ya kitoto hayo, sasa kwa kuwa ni watoto wa 1993, tuwaache wakikua wataacha. *(Makofi/kicheko)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Edward Lowassa, hili dume hili, Mheshimiwa Edward Lowassa ni mwanaume si mchezo, akisema jambo, linafanyika. Aliwahi kuniambia naleta *JICA* Mtwara, *JICA* wako sasa hivi Maulunga, Wajapani wale wanachimba maji sio mchezo. Kwa hiyo, ni dume hilo la mbegu siyo mchezo. Hongera sana kwa kazi yako nzuri, wanakutakia watu wa Mtwara mafanikio mema na watu wa Mtwara wanasema, Wamasai kama hamumrudishi Mheshimiwa Edward Lowassa Bungeni hapa, mwisho wenu darajani pale, hakuna kuleta mifugo Mtwara kutaka malisho. Mkimleta ruksa, kwa sababu ni mkombozi, atatupatia maji Mtwara Vijijini. *(Makofi)*

Wanasema watu wa Mtwara kwamba, wamesikia makubaliano yetu na Wizara kwamba, nikirudi mimi Mbunge wao nipeleke *District Master Plan* ya Maji Wizarani, ili tukae na Waziri, tuangalie chanzo cha maji cha Kitele, Chipwalapwata, Mbwamkunwa, Mchuchu, Mnyawi Makondeko, Mto Ruvuma, tunafanyaje ilie maji yaenee Mtwara Vijijini, wamesikia.

Lakini Mheshimiwa Edward Lowassa, watu wa Mtwara wanasema, pamoja na mpango huo, haina budi na wewe Wamasai wakurudishe. Mkae vile vile kwa sababu Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, kaeneza mbuzi Wilaya nzima na Wilayani wamepata pikipiki ya kuratibu Mpango wa Mbuzi, kuhakikisha wanazaliana, Mtwara Vijijini

tunaanza mifugo. Kwa nini Mtwara hawafugi, mambo hayo yako Mtwara tayari na nimeeneza baiskeli kila Kata, kwa sababu ya uratibu ngazi ya Kata. Sasa wanaomba, pamoja na mpango huu, mkirudi basi, mkae kitako mwone tunafanyaje kueneza ng'ombe. Tumeanza na mbuzi sasa wanataka na ng'ombe. Kwa hiyo, tukirudi tuangalie jinsi gani ya kumwaga ng'ombe Mtwara Vijijini ili waweze kupata njia mbadala ya kupata mapato, licha ya korosho, basi wapate kwenye mbuzi na baadaye wapate kwenye maziwa na ng'ombe. Lakini wanakutakia kila la heri.

Mheshimiwa Spika, niishukuru vile vile Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inayoongozwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Nilipata fursa ya kukaa na Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, wakati akiwa Waziri wa Afya, akanisaidia upatikanaji wa Madaktari Wasio na Mipaka, sasa hivi zahanati zote zimekarabatiwa.

Tukakaa na Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, akiwa Waziri wa Elimu, akanisaidia upatikanaji wa wafadhili wanaoitwa *Save the Children,* wamejenga madarasa mawili mawili kila shule. Wakaongeza na ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa hiyo, mambo kule siyo mabaya.

Nikakaa na Mheshimiwa Juma Nkhangaa, wakati akiwa Waziri wa Maji, akafanya mambo yake mabwawa yamechimbwa, watu wanakunywa maji. Nikakaa na Mheshimiwa Brigadia Jenerali Hassan Ngwilizi, tunafanyaje Vijiji kupata hati, vijiji vimepata hati na Mji Mdogo tumepata na Manispaa tumepata.

Nilikaa pia na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kuwapatia mikopo ya pembejeo mwaka 2004, watu wa Mtwara Vijijini, wanaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikiongozwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Spika, lakini shukrani za pekee zinamwendea Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kweli huyu ni Mkombozi wetu. Kwanza, ametustiri sisi wa Mtwara na Lindi, walikuwa wanatuzomea tukifika na meli haoo! haoo!, yaani tulikuwa tunaonekanaje sijui! Lakini sasa hivi Makabila yote wanapenda kuitwa Wamachinga. Wamachinga wa Dar es salaam pale siyo Wamakonde tu, kuna Wachaga, kuna Wakerewe, kuna Wazigua. Lakini ukimwita Mmachinga siku hizi anafurahi. Mheshimiwa Benjamin William Mkapa unayemsikia ameleta hadhi, lakini zamani ilikuwa ukimwita mtu Mmachinga anakutukana, mimi siyo Mmachinga! Lakini sasa hivi yeye mwenyewe anapenda aitwe Mmachinga. Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, angefanya vibaya mambo yangetuwia mabaya zaidi, lakini amefanya vizuri. Huyu kijana huyu, kumfanyaje sisi watu wa Mtwara huyu! Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, lazima uunde Kamati na Katibu wako awe *RAS* wa Lindi. Kamati nzito na kuweka mchango wa nguvu ili tumpokee kwa shangwe Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, akirudi nyumbani. Tuje tumfanyie mambo, tuweze kumjengea hata nyumba ya fahari moja kali sana kule kwao kama pongezi.

Juzi nilisimama Darajani nikaangalia, nikasema hivi Mtwara huku ikijengwa lami inapendeza vile vile. Kupendeza lami, Kibiti - Lindi lami safi na kila ukienda madaraja yanajengwa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa huyu. Mimi huyu namtabiria

kwamba, lazima aingie peponi huyu. Huyu ni mtu wa peponi moja kwa moja, *Inshallah!* Mwenyezi Mungu, mjalie aende peponi moja kwa moja. Kama peponi wanaingia Wakristo basi yeye Mkristo, kama peponi wanaingia Waislamu, umjalie atamke *Lailaha-ilallah-Muhammadan-Rasulullah,* yaani hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Wakati roho yake inachukuliwa na wewe Mwenyezi Mungu *(Allah-Subhanahu-wa-ta'ala),* huyu mkombozi si mtu wa mchezo huyu, tutashangaa sana tukimwona motoni. Ewe Mwenyezi Mungu, tunakuomba huyu tumkute yuko peponi. Mwenyezi Mungu, mpe maisha marefu, basi hapo utakapomchukua moja kwa moja peponi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kupata kura nyingi na kuwa Mgombea wa Chama cha Mapinduzi. Sisi wa Mtwara na Lindi, tunakusudia kumpa kura zote. Wamakonde wanasema, *kuntengeda imwana! Imwana* ni baba watoto, *kuntengeda* ni kumfanyia mambo ambayo hawezi kutoka kwenda nyumba nyingine. Wewe ukimwona mume anakwenda nyumba nyingine ni kwamba, wewe mke hukufanya vizuri, nipe maji, unampa moto, nipe moto unampa mawe, asiende nyumba nyingine? Nipe maji, unampa maji, anaenda msalani unambeba, yaani unamfanyia mambo ya kunoga, ataenda sehemu nyingine! Inaitwa *kutengeda!* Sasa sisi Wamakonde wa Mtwara na Lindi, tumepanga *kuntengeda imwana,* kwa kumpa kura zote, asiyetaka kumpa kura Mheshimiwa Jakaya Meisho Kikwete, tunamwomba tafadhali Mtwara na Lindi atupishe kidogo, aende sehemu nyingine akakae. *Imwana* huyu lazima *kuntengeda,* aanze kupata kura nyingi sana kule. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi niliwaomba Watanzania wampe bahshishi Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, angalau miaka mitatu, siyo kuvunja Katiba, hapana. Katiba iendelee vile vile ila zawadi miaka mitatu amalizie. Hapa walinielewa vibaya kwa sababu kulikuwa na midume ilikuwa inataka ile kitu ile. Lakini kumbe Watanzania walinielewa, wakasema tulia, siyo miaka mitatu, kumi, kwa sababu kijiti kile wametoa kwa baba mtu Mmachinga wa nguvu yule Mmakonde, Myao yule, wakakabidhi kwa watoto wetu, yaani nyumba ile ile maana hawa Wandengereko, Wakwele, Wazaramo, watoto wetu hawa. Kwa hiyo, wametoa kwa baba wakakabidhi kwa mtoto. Wametupa kazi vile vile ya miaka kumi, siyo mitatu, kama nilivyoomba. Kwa hiyo, wametupa kazi, itabidi sisi Wamakonde wa Mtwara na Lindi tuwakanye, tuwaelekeze, tuwaelimishe hawa Wandengereko, Wakwele, Wazaramo, wasituaibishe maanake kukonda kwa mbwa ni sifa mbaya ya mwenye mbwa. Sasa wakaifanya vibaya watoto hawa tutalaumiwa sisi baba zao. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa John P. Magufuli, awachukue Wandengereko wote, Wazaramo wote, awapeleke kwenye Daraja la Mkapa, waone madaraja yanavyojengwa, siyo wakipata wao waanze kutujengea madaraja kuweka weka mbao, hapana, Daraja lipo kama lile.

Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, uwapeleke Wandengereko kwenye Ofisi, waone zilivyokarabatiwa na zinavyong'ara. Siyo baada ya miezi sita tu kupangusa pangusa baibui! *(Makofi)*

Mheshimiwa Edward N. Lowassa, uwapeleke vile vile kule wanakochimba Wajapani, kulipa madeni ili kurudisha hadhi ya wafadhili siyo Wandengereko ninyi muanze kutolipa madeni, sisi baba zenu tulivyofanya si mmetuona. Lakini Mheshimiwa Waziri wa Elimu wewe uwapeleke kwenye mashule waone madarasa yanavyokuwa, siyo kuchukua miti na nyasi kuezeka ezeka, hakuna. Sisi baba zenu ona madarasa kwanza tulivyojenga. Lakini Mheshimiwa Basil P. Mramba, uwaoneshe takwimu Wandengereko hawa, tumetoka shilingi bilioni 27 mpaka shilingi bilioni 100 na kitu, namna hiyo. Siyo mtuletee hapa maneno ya Kindengereko, ukata, Tanzania hii ukata, halafu msitutie aibu sisi baba zenu.

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, uwaoneshe na uwaeleze Wandengereko Utawala Bora. Tulikuwa na barabara ya Kibiti Lindi, sasa inasema Mtwara, Kibiti, Dar es Salaam, Mwanza, hatuna ubaguzi sisi. Tunaeneza maendeleo sehemu zote. Siyo mkipata ninyi Wandengereko mjue kwenu tu, hapana, eneza nchi nzima, ndiyo Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya mambo mengi, lakini ninasikitika jambo moja tu, watu wa Mtwara Vijijini waliniuliza kumuenzi Mheshimiwa Marehemu Nyerere ni vibaya? Nikasema hapana kumuenzi si vibaya, wakaniambia tulia. Siku moja wakaja wapiga kura, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, tumeleta mzigo wa fedha. Mzigo wa fedha mmeupata wapi?

Kuna watu wanataka kugombea Ubunge Mtwara Vijijini, wametuletea fedha sasa tumekuletea wewe fedha hizi, zikusanye uzipeleke kwenye miradi ya maendeleo, maana Mheshimiwa Marehemu Julius Kambarage Nyerere, alisema wewe ukimwona mtu anachukua mbolea anapaka ukuta kama rangi, basi akizubaa ichukue, mwibie peleka shambani, hakuna matatizo kwa sababu yule alikuwa ana-*mis-allocate resources.* Sasa fedha wananunulia kura! Ni *mis-allocation of fund.*

Sasa Mtwara Vijijini wanakusanya zile fedha ambazo wamezi-*mis-allocate* wananipa mimi kupeleka kwenye miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, kuna fomu maalum, tumekusanya kama Sh. 270,000/= hivi tumepeleka kwenye shule za sekondari. Sasa *DC* anawatisha hawa watu wanaokusanya fedha na kupeleka kwenye miradi ya maendeleo. Jana alikuwa amewapanga foleni baadhi ya wapiga kura hawa kwenye Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata. Anawatisha kwamba, atawanyang'anya Kadi za CCM kupitia Ofisi ya Mtendaji wa Kata.

Wapiga kura wa Mtwara, wembe ni ule ule, leteni fedha hapa tupeleke kwenye miradi ya maendeleo, halafu muwapige chini vile vile kama mlivyowapiga Madiwani waliotoa fedha. Kwa nini *DC* anaingilia mambo ya Chama? Masuala ya Chama yanaishia kwenye Chama! Tuache tukusanye hizi fedha tupeleke kwenye miradi ya maendeleo. Tumepeleka Shule ya Sekondari ya Dihimba shilingi 100,000/= hizi hizi, tukapeleka Shule ya Nnima shilingi 50,000/=, tukapeleka Mahulunga shilingi 50,000/= na kuna fomu maalum mpiga kura akija na fedha anaandika nimeleta shilingi 10,000/= nilihongwa na fulani na-*surrender* kwa Mbunge, basi zikitimia shilingi laki moja tunapeleka kwenye miradi ya maendeleo, kinachomwudhi *DC* nini? Mheshimiwa Waziri Mkuu, mweleze *DC* wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala, hajachangia Maji wala Mifugo, lakini ni Mwaka wa Uchaguzi, ruksa. *(Kicheko)*

Kwa kuwa kuna Wabunge wawili walikwenda Mtera, sasa hiyo imetoa nafasi kwa wengine wawili waweze kuchangia ambao watachangia mchana, tulishakubaliana kwamba tunaweza kuchangia mpaka saa 11.30. Kwa hiyo, hawa wawili itakuwa ni Mheshimiwa George M. Lubeleje na Mheshimiwa Aridi Mwanache Uledi, wajiandae. Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.59 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Kama Wabunge wenzangu walivyoanza na mimi nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na wataalamu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inafanya kazi nzuri sana, mimi nakumbuka kabla ya kuundwa kwa Wizara hii kulikuwa na matatizo mengi sana, lakini baada ya kuundwa kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na nashukuru nilihudhuria warsha ya wafugaji iliyofanyika Arusha na ili kuweka mikakati jinsi gani ya kuboresha hali ya ufugaji katika nchi yetu. Kwa hiyo, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi nzuri unayofanya na hizi pongezi ambazo tunakupa ni za dhati kabisa. Kuna mabadiliko makubwa sana kuhusu sekta ya maji, pamoja na sekta ya mifugo.

La pili, nashukuru kwa kutupa heshima Wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa. Sherehe ya Huduma ya Mifugo kutimiza miaka 100 ilifanyika katika Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa. Kwa hiyo, hiyo ilikuwa ni heshima kubwa sana, ingeweza kufanyika mahali popote pale lakini tunakushukuru sana, Mheshimiwa Waziri, kwa kutupa heshima hii Wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelalamika muda mrefu kuhusu ukarabati wa Chuo cha Mifugo cha Mpwapwa, lakini sasa ninafurahi kusema kwamba, sasa hivi ukarabati umefanyika na kuna wanafunzi zaidi ya 170 wa kozi mbalimali za mifugo na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wameshatembelea Chuo hicho cha Mifugo, pamoja na Kituo cha Utafiti wa Mifugo, kwa hili nakushukuru sana. Ombi tu ni kwamba, bado kuna baadhi ya majengo ya utawala na baadhi ya nyumba za watumishi, kwa hiyo, ukarabati uendelee Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie Sekta ya Maji. Wilaya ya Mpwapwa ilikuwa na matatizo makubwa sana ya maji, wakati mimi naingia Bungeni mwaka 1990.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leonard Derefa, ukiendelea namna hiyo nitakutoa nje. Naomba uendelee Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati naingia Bungeni mwaka 1990, Wilaya ya Mpwapwa ilikuwa inapata huduma ya maji chini ya asilimia 50. Sasa nafurahi kusema, Wilaya ya Mpwapwa inapata huduma za maji zaidi ya asilimia 76 na hizi ni juhudi za Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wizara. Hivi sasa kuna miradi mikubwa sana ya maji, ambayo inafadhiliwa na *World Bank, British Water Aid,* pamoja na shirika letu la msaada la *World Vision.* Lakini na vilevile kwa sababu Sera ya Maji inasema lazima tuchangie mifuko ya maji, Wilaya ya Mpwapwa tumeshachangia zaidi ya shilingi milioni 17 kwa ajili ya kuchangia mifuko ya maji. Kwa hiyo na sisi tunatekeleza Sera ya Maji. Kuna vijiji ambavyo vilikuwa na matatizo makubwa sana ya maji, kwa mfano, Vijiji vya Sazima, Igoji Kusini, Chiseyu, Makutupa, Lupeta pamoja na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nafurahi kusema sasa hivi Wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. Kwa hiyo, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo ni muhimu sana katika nchi yetu, kwa sababu inachangia Pato la Taifa. Ukiangalia tuna mifugo zaidi ya milioni 18, lakini Pato la Taifa ambalo linachangiwa ni asilimia 18 tu, kwa hiyo ni kidogo sana. Nina hakika kwa sababu ya juhudi za Mheshimiwa Waziri, pamoja na watalamu wake wote, hivi sasa uboreshaji wa mifugo unaendelea katika nchi yetu, mifugo itachangia kiwango cha kutosha kabisa katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna matatizo mbalimbali ambayo yameikabili mifugo yetu hasa magonjwa ya kupe na magonjwa ya kupe yanaweza yakazuilika kabisa. Karibu asilimia 70 mpaka 80 ya ng'ombe wanakufa kwa sababu ya magonjwa ya kupe, tunaweza tukazuia kama tutakarabati majosho. Yapo majosho katika nchi yetu zaidi ya 2,000, lakini yanayofanya kazi ni kama 400 tu. Kwa hiyo, idadi kubwa ya majosho hayafanyi kazi. Ni kitu cha aibu kwa kweli kuona ng'ombe wanakufa kwa sababu hawajaongeshwa. Kwa hiyo, naomba Wizara yako Mheshimiwa Waziri, ijitahidi kukarabati majosho ikisaidiana na Halmashauri zetu za Wilaya. Hii itakuwa ni kinga kubwa ya kuzuia vifo vya mifugo ambao kwa kweli wanakufa kwa sababu ya haya magonjwa ya kupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kidogo kuhusu hii Sekta ya Maji, pamoja na kwamba, nilikwisha elezea, lakini bado tuna maeneo ambayo yana ukame na naishukuru Wizara, imeshaanza kuchimba mabwawa na malambo katika baadhi ya vijiji hapa nchini. Kwa hiyo, tuendelee kuchimba malambo na mabwawa ili tupate maji ambayo yatasaidia

sana Wananchi, pamoja na mifugo. Ukitaka kuboresha mifugo, lazima mifugo ipate huduma ya madawa na huduma ya maji.

Tunakushukuru kwa sababu baadhi ya Wilaya tumeshapata fedha kwa ajili ya kutuma malambo na mabwawa. Hivi sasa Belege na Mima wameshapata fedha kwa ajili ya kuchimba malambo kwa kukusaidiana na nguvu za Wananchi. Kwa sababu kama Serikali pekee, ichimbe mabwawa bila kushirikiana na nguvu za Wananchi, itakuwa ni vigumu. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Serikali iangalie maeneo yote ambayo kuna ukame, mabwawa na malambo yachimbwe, pamoja na visima virefu ili Wananchi waendelee kupata huduma ya maji safi na maji salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upandishwaji vyeo Watumishi, zoezi hili limekwenda vizuri naipongeza Serikali. Nilikuwa na matatizo makubwa sana katika Kituo cha Utafiti wa Mifugo, pamoja na Chuo cha Mifugo na Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo pale Mpwapwa, lakini ni wachache ambao hawajapandishwa vyeo. Lakini upandishwaji vyeo unakwenda pamoja na kurekebisha mishahara yao, haiwezekani unapanda daraja lakini unabaki kwenye mshahara ule ule. Kwa hiyo, naomba Wizara yako Mheshimiwa Waziri, ihakikishe kwamba, watumishi wanaopandishwa vyeo vilevile mishahara irekebishwe ili wapate kulingana na madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ya kwangu yalikuwa ni hayo, lakini kubwa zaidi ni kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wote kwamba, Wizara hii Wananchi wanaridhika kwamba, sasa inafanya kazi nzuri sana, kwa hiyo, endelezeni juhudi hizo na mimi nina hakika Wananchi wa Monduli, watakuchagua utarudi Bungeni na mimi kwa kuwa nimefanya mambo mazuri pale Mpwapwa, nashirikiana na Wananchi wangu vizuri na nitakuwa Bungeni mwaka huu baada ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kusema haya, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi, namtakie kila la heri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wote wa Wizara hii ili waweze kutekeleza majukumu yao, pamoja na kwamba, tuna tatizo la ufinyu wa bajeti lakini wanajitahidi sana kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja asante. *(Makofi)*

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Lakini kabla sijaanza mchango wangu, naomba nianze kwa kutoa pole kwa familia, ndugu na Wananchi wa Mkoa wa Rukwa, kufuatia kifo cha Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, kilichotokea hivi karibuni wakati wa mkutano huu wa Bunge. Namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwanza, kwa kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa na timu yake, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutuondolea kero hii ya maji nchini na mimi nina imani kabisa, kwa kasi hii tunayokwenda, Tanzania itaweza kujihakikishia upatikanaji wa maji safi maeneo yote ya mijini na vijijini. Kwa hiyo, nasema hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikianza mchango wangu, nizungumzie tu hali ya maji katika Jimbo langu la Nanyumbu. Katika maeneo yote Jimbo la Nanyumbu kuna mito mikubwa ya Lumesule, Lukwamba, Lukikwa na Mbangala, ambayo hupeleka maji yao katika Mto Ruvuma. Lakini vile vile kuna mito midogo mingi karibu kila sehemu ya Jimbo la Nanyumbu, ni kawaida kwa Wananchi wa Nanyumbu kuvuka mto mmoja au zaidi wanapokwenda mashambani. Mito hii hufurika maji wakati wa masika, hukauka wakati wa kiangazi, hivyo kusababisha uhaba mkubwa wa maji majira ya kiangazi. Sasa nimekuwa napiga kelele hapa kuwa, ikiwa mito hii maji yake yatahifadhiwa, nina hakika Jimbo la Nanyumbu kusingekuwa na upungufu wa maji.

Kwa hiyo, naiomba Serikali aidha isambaze teknolojia ya kukinga maji ya mito ili maeneo mengi yaweze kupata maji ambayo kwa kweli wanayakosa kwa kipindi kirefu cha kiangazi. Inawezekana ikahitajika teknolojia tu katika maeneo mengine na Wananchi wenyewe wakahamasika kuitumia teknolojia hiyo ili kukinga maji hayo ya mito. Lakini vile vile naamini kukinga maji ya mito na kuchimba visima, nadhani kuchimba visima ni gharama zaidi kuliko kukinga maji ya mto. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikafanya utafiti njia gani ni nafuu katika kuwaletea maji Wananchi kati ya kuchimba visima au kukinga maji haya ya mito. Nina hakika kabisa kuwa, hili la kukinga maji pengine lingesaidia na lingeonekana ni la nafuu kwa Serikali kuliko kukazania kuchimba visima hasa kwa Jimbo langu la Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie miradi michache ya maji iliyoko ndani ya Jimbo la Nanyumbu:-

(i) Mradi wa Maji wa Makong'ondela, huu ulianza miaka ya nyuma sasa inawezekana ni zaidi ya miaka 15, lakini hadi leo umekwama, hauendelei kujengwa hivyo, Wananchi hawajui hatima yake pamoja na ahadi nyingi za viongozi za kuendeleza mradi huu, lakini nasikitika hadi leo hakuna ambacho kinaendelea. Sasa Wananchi walishiriki sana katika uanzishaji wa Mradi wa Makong'ondela na kwa kweli walichangia kwa hali na mali hadi kufika hapo ulipo. Lakini sasa inaonekana mradi umetelekezwa kwa miaka kadhaa sasa hivi, hakuna kilichofanyika na kwa kweli hatujaelezwa kama Serikali inayo nia ya kuendelea na mradi huo. Kwa hiyo, ningeomba Serikali itueleze kama nia ipo na kama haipo basi Wananchi wa Makong'ondela waelezwe.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ambao umekwama ni ule wa maji wa Ndwika Mangaka, ulifadhiliwa na *TASAF,* lakini ulikwama kilomita chache kabla ya kufika Mangaka kutokana na kuishiwa mabomba, inasemekana kuwa wataalamu waliokadiria idadi ya mabomba basi hawakufanya vizuri ndio maana mabomba hayakufika Mangaka. Pamoja na kusubiri awamu ya pili ya *TASAF,* ningeomba Serikali

kuwa mradi huu ungemalizika kwa sababu Mji Mdogo wa Mangaka unakabiliwa na tatizo kubwa la maji hasa kipindi cha Julai hadi Novemba. Kwa hiyo, naomba Serikali kwa kuwaonea huruma Wananchi wa Mangaka, ichukue jukumu la kukamilisha Mradi wa Ndwika-Mangaka, ili tatizo lipungue kwenye mji ambao sasa unakaliwa na Wananchi wengi sana.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ni ya mabwawa ya Nangomba na Maneme, nayo yalifadhiliwa na *TASAF,* ujenzi umeshaanza lakini umekwama katikati baada ya kuishiwa fedha. Fedha zote za mradi ambazo zilitakiwa zimeshatolewa lakini kutokana na matumizi mabaya ya fedha hizo, mradi haukukamilika umeishia katikati na Wananchi wanahisi kuwa fedha hizi zimetumiwa vibaya na wasimamizi. Kwa hiyo, kwanza ningeiomba Serikali, ikiwa fedha zote zimetolewa na mradi haukukamilika, Serikali ifanye utafiti kujua kwa nini mradi haukukamilika, kama kuna ubadhirifu ambao utaonekana basi wale ambao wamehusika wachuliwe hatua za kinidhamu na kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi ya mabwawa ambayo vile vile ingefadhiliwa na *TASAF;* mabwawa ya Maratani na Namasogo, Mpwahiya na Mpombe. *Survey* zimeshafanyika na Wananchi walishiriki kikamilifu katika kufanya *survey* hizo na wataalamu ambao walikuja, lakini baada ya wataalamu hao kuondoka mpaka leo hakuna ambacho Wananchi wanaelezwa. Sasa ningeomba vile vile miradi hii maadamu ilikwishaleta matumaini kwa Wananchi wa maeneo hayo ikakamilishwa ili kuondoa adha hiyo ya maji ambayo inawakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa kisima pale Nandembo, ambao nao umekwama kutokana na kukosekana kwa *spares* au vipuri fulani fulani na mradi huu ni muhimu sana kwa Kata ya Lumesule. Kwa hiyo, ningeomba vile vile Serikali ikahakikishe Mradi wa Nandembo nao unakamilishwa ili kuondoa adha ya maji pale Nandembo.

Lakini vile vile jirani na Nandembo pale Michiga, kuna visima kama vitano hivi na kati ya hivyo ambacho kinafanya kazi ni kimoja tu nacho kiwango chake cha maji kwa kweli sio kikubwa. Ningeomba basi Serikali isaidie kufufua visima vyote hivyo ili vihudumie Mji Mdogo wa Michiga, ambao sasa una wakazi wengi kabisa ambao wanakabiliwa na tatizo sugu hili la maji. Niseme tu kuwa, maeneo mengi ya Jimbo la Nanyumbu yanakabiliwa na tatizo la uhaba wa maji. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iliangalie jimbo hili kwa nia ya kusaidia katika kutatua tatizo la maji. Naelewa kuwa kuna wafadhili ambao wamepelekwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, lakini ningeomba wafadhili hawa waelekeze macho Nanyumbu, kwa sababu matatizo yake ya maji ni makubwa zaidi kuliko sehemu nyingine za mikoa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia maji, sasa naomba kwa kifupi sana, nizungumzie Shamba la Mifugo na Nangaramo. Shamba hili liko ndani ya Jimbo la Nanyumbu na kuna matatizo machache ambayo kwa kweli yanawakabili wafanyakazi pale. Kwanza kabisa, ni uhaba wa maji kwa ajili ya binadamu na mifugo yenyewe. Wana bwawa dogo ambalo halitoshelezi kwa mahitaji yote, kwa hiyo, kwa sehemu kubwa ya mwaka mifugo na Wananchi wale wanakabiliwa sana na maji. Karibu na shamba hili

kuna mito miwili ambayo wakati wa masika maji inafurika lakini wakati wa kiangazi maji hukauka. Nadhani ingekuwa ni vizuri mito hii ikatumika aidha kwa kukinga maji yake ili yaweze kutumika kipindi kile ambacho maji hayapo.

Tatizo lingine kwenye shamba hili ni usafiri hasa watoto wakati wanakwenda shuleni, wanapita kwenye pori na vichaka ambavyo huwa maficho ya wanyama wakali kama simba na chui, hivyo kuhatarisha maisha yao. Kwa hiyo, ningeomba shamba liwe na usafiri wa uhakika angalau wa kupeleka mashuleni kwenye vijiji vya jirani ili wazazi wawe na imani watoto wao wanapokwenda shule na kurudi.

Tatizo lingine ni umeme, hawa ni wafanyakazi ambao wanakuwa kama kweli wametengwa sasa, wanakabiliwa sana na tatizo la umeme. Nilipotembelea pale waliniambia walikuwa wameshapewa kompyuta lakini walikuwa wanashindwa kuitumia kwa sababu hakuna umeme. Ningeomba kwa kweli angalau wapatiwe *generator* ambalo litawapatia umeme ili nao wajione kama wako mjini kuliko ilivyo sasa hivi ambapo wanajiona kama ni watu ambao wametengwa au wametelekezwa porini. Kwa hiyo, naomba Serikali ijaribu kuyatatua haya ambayo nimeyaeleza kwa ajili ya Shamba la Mifugo la Nangaramo ili wafanyakazi wale wajisikie kweli nao wako kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo mfupi, nitamke tu kuwa, naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa asilimia mia moja, lakini vile vile nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kuniruhusu nichangie hoja iliyo mbele yetu. Kwanza, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii finyu ili niweze kuchangia. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayoifanya, pamoja na Naibu wake. Niwapongeze wataalamu kwa kazi vile vile ambayo wanaifanya. Sisi Geita tulikuwa tunajisikia wanyonge sana muda mrefu sana tangu tumeingia hapa. Lakini sasa hivi tunaenda kifua mbele, kulingana na hotuba aliyoitoa na ahadi ambazo amekuwa akitupa na anatekeleza. Tulikuwa tunasikitika sana kuona maji yanatoka kwetu yanakwenda mbali kilomita 100, 200 mpaka 300 lakini tuliopo pale hatuoni kitu chochote. *(Makofi)*

Lakini sasa kwa ahadi aliyotamka leo kwamba, ameweka fedha kwenye Mradi wa Nyakagomba, ambao utasaidia karibu vijiji vya Chigunga, Nyakagomba, Kitigiri, Chakolongo mpaka Katoro, inanipa moyo kwa kweli. Nadhani ndugu zangu Wabunge, tumpe fedha bila maswali mengi huyu ndugu, roho yake ni nzuri na ana upendo mkubwa sana, kwa kweli tumejifunza wema ulio nao. *(Makofi)*

Nasema hivyo kwa sababu mwaka 2003, tulipewa fedha kuhusu mradi huo, ulianza mwaka 1976 ukawa umesinzia, mwaka 2001 Mheshimiwa Anthony Diallo, alikuja kuangalia akakuta hali ilivyo tukapewa fedha kidogo, wakaja wataalamu na watendaji wabaya wakaziramba zile fedha.

Nilikuwa naogopa kuzungumza Bungeni, niliacha kuchangia kabisa kwa sababu nilikuwa najua utaniambia hukufuatilia vyema. Sasa kwa wema ulionao, naona umetupa fedha nashukuru sana, lakini tunachoomba Mheshimiwa Waziri, tusaidie mradi huu uishe ni mkubwa kwa kweli unahitaji fedha nyingi na umekaa muda mrefu na ndani mabomba yale karibu yamekwisha haribika.

Tunaomba basi nguvu iwe kubwa zaidi uweze kukamilika na katika mradi huo, naomba vile vile ni vizuri kama ungeweza kufika kwenye Gereza la Butundwe na unakaenda vile vile hadi Katoro, kwa sababu Katoro ndio mji mkubwa sasa hivi, unafuatia Wilaya ya Geita, hauna maji kabisa na Gereza la Butundwe lile wafungwa ni wengi, ndio gereza kubwa nafikiri katika Kanda, gereza la kilimo katika Mkoa wa Mwanza, sasa hakuna maji, basi yakija yafike kule. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, kama ulivyo na roho nzuri na wema, hebu liangalie hilo katika mahesabu yako. *(Makofi)*

Lingine napenda kutoa shukrani kwa ahadi uliyotoa kwa Mji wa Geita, ni mji ambao ni wa zamani sana lakini cha kushangaza hauna maji. Ni mji ambao umezungukwa na dhahabu, ukisogea mbele kidogo kuna ng’ombe, kwenda kulia pamba ni nyingi, samaki wanavuliwa pembeni pale, maharage ni mengi, mahindi ni mengi na unahudumia katika nchi.

Sasa unakuta hakuna maji na Wananchi ni wengi, wameongezeka pale hakuna maji, lakini wewe umeahidi kutupa maji, tunakushukuru sana, roho yako iendelee na ninawaomba watu wa jimbo lako, wakupitishe roho hiyo nzuri nafikiri na kwako ni hivyo hivyo, kwa hiyo, wasikuletee matatizo huko. *(Makofi)*

Pamoja na ahadi hiyo, tunayo matatizo ya maji kwenye Jimbo la Msanda, Vijiji vya Nyalugusu, Rwamgasa, Mbukoli, Nyaseki. Kama ulivyosema mwaka 2003 kwamba, maji yaliyo katika maeneo hayo kuchimba visima ni tatizo kwa sababu maji mengi yana madini, kwa hiyo, yana madhara kwa binadamu. Kwa hiyo, watu wa kule wana shida sana ya maji, tunaomba msaada kama ikiwezekana maji yatakayokuja Geita, basi yasogee mpaka kwenye vijiji hivyo.

Lakini kwenye Kijiji cha Nyaseki, tunaomba lambo kwa ajili ya mifugo. Nyasegi na Vutovela ni vijiji viwili, sasa hivi kiangazi kimeingia vile vijiji wanaokaa pale ni ndugu lakini utashangaa itakapofika mwezi wa nane na wa tisa, hakuna kutembeleana ni mapanga, anayewahi pale anazuia wengine wasinyweshe kwa sababu ya kugombania.

Sasa tunaomba huo msaada hebu tuwekee lambo pale, najua una roho nzuri, ukimtuma Mheshimiwa Anthony Diallo, akatuletea bwawa moja pale kabla hujamaliza muda huu, najua utaenda vizuri. Jitahidi utuwekee pale kwa sababu hatujui mambo yanayokuja mbele, lakini kwa sababu Mheshimiwa Anthony Diallo, huwa anatembelea kule, anafahamu tabu tuliyonayo. Kwa hatua hii tuliyofikia, tusingependa Waziri aje aanze kufukuzwa na mishale, watu wanagombana, tunaomba mtuwekee bwawa la maji pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa Geita wamepata vyeo tunashukuru kwa hilo, lakini kuna mmoja alionyesha kitu cha ajabu, ana miaka karibu 20 hajapanda daraja. Basi naomba wajaribu kuangalia watu kama wale na wenyewe wapande wajisikie wanafanya kazi vizuri. Kwa sababu sielewi inatokeaje kwenye Wizara hii wanachelewa, lakini safari hii wamepanda.

Sasa kuwe na utaratibu mzuri kama wengine wanavyopanda baada ya miaka mitatu, mitano wanapanda. Nafikiri kuwe na utaratibu mzuri wa namna hiyo, wengine wamepanda sasa hivi nashukuru lakini kuna ambao bado nadhani havijafika lakini kama vimefika basi tunaomba waangaliwe.

Mheshimiwa Waziri, wengine sasa hivi tumefikia kwenye hatua za mwisho. Najua una hadhi, umejitahidi umekuja kututembelea, naomba kabla hatujafikia uchaguzi, nina imani kwa wananchi wako walivyo, kura za maoni huna matatizo baada ya kujaza fomu tu na baada ya kura za maoni nina imani utapita fika huko kwa sababu hiki cheo unachofika kule wakuone wanafurahia kuja kwako. Wewe unayetupa maji njoo uone huo mradi unavyofanana kusudi atakayekuja nina imani huwa kuna kukabidhiana, basi arithi vitu ambavyo utakuwa umemwambia hapa nimeacha hiki na hiki, karibu sana naomba ukubali kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, kwa heshima uliyonipa nichangie asubuhi, nilikuwa nimepata dharura, naomba nikushukuru sana. Lakini Wizara hii naipongeza, naomba tuwape fedha wakafanye kazi, wanafanya kazi nzuri sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE**: *Good morning, I have been reading your Excellent Budged Speech. This work will leave a long lasting (bright) legacy at the Ministry for years to come! Congratulations and best wishes for bigger things! There is however, one thing that needs your elaboration. Last year you included 38 Districts in your World Bank Funded Villages and Sanitation Project. We have selected Villages, opened Bank Accounts and are contributing money for the 5% requirement. But there is no Budgetary Money set aside for moving these projects ahead. What is the plan? Congratulations.*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mashine ya maji Engarenaibor, naomba kukumbushia *engine* ya maji ambayo Wizara hii imeagiza kwa ajili ya Kata hiyo. Walihitaji fedha kiasi cha Shilingi milioni 3.5. Hali huko ni mbaya kutokana na mvua kutonyesha. Bado naomba mtupatie ili fedha hizo zichangwe. Mwaka jana 2004 mifugo ya Kata hiyo ilihama kutokana na shida ya maji na hata mwaka huu 2005 kuna uwezekano wa kuhama.

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa msaada wake wa Sh.5,000,000/= kwa ajili ya kuchimba lambo. Hata hivyo nina masikitiko makubwa sana kwani fedha hiyo ni kidogo sana kwa shughuli iliyokusudiwa kwa sababu haikufanikisha. Hivyo, naomba Mheshimiwa Waziri aniongeze fedha ili kazi iliyokusudiwa imalizike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafurahi sana iwapo Mheshimiwa Waziri ataniletea *memo* ya maelezo yoyote.

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri na Naibu Waziri kwa jinsi wanavyosimamia Wizara hii kwa ufanisi mkubwa bila kuchoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Viongozi wa Wizara hii, bado kuna maeneo mengi ambayo hayana kabisa huduma ya maji safi na salama kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa vile walishafika Wilaya ya Bukombe na kujionea wao wenyewe matatizo ya maji yaliyoko Wilayani hapo. Aidha, nimjulishe Mheshimiwa Waziri Lowassa kuwa ule mradi wa Maji ya Bomba Msasa – Uyovu ambao yeye mwenyewe aliushuhudia mpaka leo haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa zilizopo, lakini bado kuna matatizo makubwa ya maji katika Mji wa Ushirombo ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe. Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira unaoendelea Mkoani Shinyanga kwa ufadhili wa Serikali ya Uholanzi katika Wilaya ya Bukombe bado unasuasua sana. Aidha, kuna hisia ya ubadhirifu wa fedha umefanyika kwenye mradi huu, kwani Mkandarasi anaonekana kulipwa fedha nyingi kuliko kazi aliyoifanya. Hivyo, naishauri Serikali ifuatilie mradi huo ili ione maajabu yaliyoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Wizara hii inaonekana kufanya kazi nzuri, nashauri iwe na mawasiliano ya karibu na Wawakilishi wao ko Mikoani na Wilayani ili wasiharibu kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Hotuba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ukarabati na upanuzi wa maji ya Mji wa Namtumbo mwaka 2004/2005 tuliahidiwa Shilingi milioni 30, hadi Juni zilipatikana Shilingi milioni 20 tu za kununulia vifaa. Je, mwaka huu tutapata fedha zaidi na kufikia Shilingi milioni 30 zilizopangwa huko nyuma mwaka 2004/2005?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Namtumbo wameongezeka watu na vifaa vya *reservoir* ya maji havitoshelezi Mji mpya wa Namtumbo. Je, tutasaidiwa msaada huo wakati wa 2005/2006?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu. Pia, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamana ya kuunganisha Sekta ya Maji na Mifugo haieleweki kabisa, kwani dhana ya maji inatakiwa kuwa inajitegemea kwa kuwa watumiaji wa maji ni kilimo, mifugo, binadamu, nishati, mazingira na viwanda. Kwa sasa maendeleo ya Sekta ya Maji chini ya mfumo wa sasa uliounganishwa na mifugo, ni dhahiri Wizara ya sasa inapendelea Sekta ya Mifugo. Natoa ushauri kuwa Sekta hii itenganishwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo, kutokomeza umaskini uliokithiri katika jamii ya wananchi wengi (asilimia 80% waliopo Vijijini) itategemea mageuzi katika kilimo kutoka kwenye kilimo cha kutegemea mvua na kuingia kikamilifu katika kilimo cha kumwagilia maji mashamba. Wizara kwa nini ina kigugumizi kikubwa kuhusu uvunaji maji ya mvua? Serikali sasa ione umuhimu mkubwa wa kuanzisha utaratibu wa kuvuna maji ya mvua kitaifa. Mvua inaponyesha popote Vijijini maji yavunwe na iwe raslimali muhimu ya Kijiji. Kitendo cha kuachia maji ya mvua kuvuruga na kutishia wananchi kama mafuriko na uzalishaji wa makorongo Vijijini ni uzembe unaoendelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Taasisi nyingi Kimataifa za Fedha zipo tayari kuisaidia Tanzania kuwezesha kujenga mabwawa madogo *(rural earth dams)* Vijijini hasa *ADB/ADF, EDF, IDA, BADEA* pamoja na nchi mbalimbali *(bilateral funding assistance).* Kwa nini Serikali isichukue nafasi hii ione umuhimu wa kuleta mageuzi makuu kwenye uchumi wetu na huduma za jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo aniunge mkono katika Mradi wa Kuvuna Maji ya Mlima Sekenke kwa matumizi ya kilimo kwenye Bonde la Wembere, Wilaya ya Iramba Mkoa wa Singida. Mradi huu utahusisha Kata za Urughu, Mtekente, Mtoa, Shelui, Ntwike, Tulya na Kidaru. Mradi huu *(write-up)* umekwishapelekwa Wizara ya Fedha kuombewa misaada kutoka *ADB/ADF, BADEA*, Italia na Belgium.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufufua mabwawa na kuchimba visima katika Wilaya mbalimbali, mradi huu ambao umefadhiliwa na Benki ya Dunia (IDA) haujawafikia wananchi wengi na hautekelezwi ipasavyo. Kwa Wilaya ya Iramba Jimbo la Iramba Magharibi, namsihi Mheshimiwa Waziri awasaidie wananchi kwa kufufua mabwawa yafuatayo: Kidaila, Kitusha, (Kata ya Kinampanda), Bwawa la Shelui, Bwawa la Tutu (Mji wa Kiomboi), Bwawa la Urughu (Kata ya Urughu), Bwawa la Mkulu (Kata ya Ulemo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya Maji Safi na Maji Taka katika Jiji la Dar es Salaam, huduma katika Jiji hili inaendelea kutawaliwa na rushwa. Huwezi kupata maunganisho ya maji safi Jijini pasipo kutoa chochote (rushwa). Leo ndiyo

unaona maunganisho yasiyo ya kitaalam na mabomba ya maji yamezagaa na kuvuja ovyo ovyo! Hivi Wizara inaelewa hivyo au imetoa baraka zake?

Pamoja na vitendo vya rushwa wananchi wananyimwa maji katika Kata nyingi za Dar es Salaam, lakini biashara ya kuuza maji inaendelea kushamiri na kwa bei inayoongezeka kila siku na biashara hii inaendana na a chochote kwa wakubwa (Meneja) wa huduma za maji. Vyombo vya Serikali vimulike tatizo hili la vitendo vya rushwa katika huduma ya maji Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Dar es Salaam wangependa kupata huduma ya kuunganishwa kwenye huduma ya maji taka. Mtaa wa *Regent Estate* sasa hivi umeingiliwa na mafuriko ya maji ya mvua na kwa hiyo, mashimo ya vyoo *(septic tanks – sewerage)* ya nyumba nyingi wamefurika hasa Mtaa wa Vikawe, nyumba karibu zote zina tatizo hili. Namwomba na kumsihi Mheshimiwa Waziri kuwa Mtaa wa Vikawe uunganishwe kwenye bomba la huduma ya maji taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kupongeza jitihada zinazofanywa na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na wataalam wake kwa kufanikisha azma ya kuwapatia Watanzania mahitaji yao muhimu ya maji safi, salama na ya kutosha kwa maendeleo na afya zao. Hili linadhihirishwa na kufikia kuondoa tatizo sugu lililokuwapo ndani ya Jiji la Dodoma kwa asilimia 100 na sasa kama tujuavyo zimeanza jitihada za kuyatumia maji ya Ziwa Victoria kwa Miji ya Kahama na Shinyanga jambo ambalo hapo nyuma lilikuwa ni ndoto tupu ukizingatia mikataba ya kikoloni iliyotunyima haki yetu na kuwapa wenzetu wa Sudan na Misri wafaidike, sisi tukibaki na umaskini wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Watendaji ndani ya Wizara ya Maji na Maendeleo na Mifugo. Baada ya kutanguliza hilo, sasa ningependa kwenda kwenye Jimbo langu la Morogoro Mjini kwa Ushauri.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Morogoro unatazamiwa kupanuka kwa kipenyo cha kilometa 30 kwa barabara za Morogoro/Dar es Salaam, Morogoro/Iringa na Morogoro/Dodoma. Hili limo kwenye uamuzi uliokwishafanywa na Vikao mbalimbali vinavyohusika ikiwamo *Full Council* ya Halmashauri ya Manispaa na *Regional Consultative Committee (RCC)* vilivyokaa mapema mwezi Aprili/Mei 2005. Kikao pekee kilichobaki kuidhinisha hilo ni cha Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa angalizo hilo ili Wizara na chombo chake kinachotoa huduma hiyo ndani ya Manispaa ya Morogoro (*MORUWASA*) waweze kuandaa kabiliano la ongezeko hilo la eneo la kupeleka huduma ya maji safi na salama litakaloendana na upimaji wa maeneo ya makazi yatakayojengwa siku za usoni. Upanuzi huo utachukua Vijiji vingi vikiwemo Mkambarani, Kizinga, Pangawe na Mikese kwa

barabara ya Morogoro/Dar es Salaam, Tangeni, Mzumbe, Sangasanga na Melela kwa upande wa barabara ya Iringa na Wami Dakawa kwa barabara ya Morogoro/Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hii, napenda kutoa ushauri kwamba vyanzo vipya vya maji vitazamwe kukidhi ongezeko hilo. Moja ni kuona uwezekano wa kujenga bwawa dogo kwenye Mto Mgolole (Vituli) kuvuna maji wakati wa mvua za masika na kuyahifadhi kwa matumizi ya wakati wa kiangazi. Chanzo cha pili ni Mto Wami ambao upembuzi yakinifu ulishafanywa miaka ya themanini mwishoni na tisini mwanzoni ambapo matanki ya kusafishia maji na hifadhi yalibainishwa kujengwa eneo la Mkundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo kingine ni Bwawa la Mindu ambalo lilibuniwa kujengwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilikamilika mwaka 1985 na kuzinduliwa na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Awamu ya pili ilihusu kuongeza kina cha maji kwa kuinua tuta lililopo kwa milimita 2.5 zaidi, lakini haikuwahi kutekelezwa hadi leo inapofikia miaka 20 sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ningependa kupata maelezo ya kina ili nijue ni nini kilichopelekea usanifu huu wa bwawa kutotekelezwa kama ilivyokusudiwa. Nafahamu sababu zinaweza kuwa ufinyu wa fedha, lakini siyo siri kwamba kadri unavyocheleweshwa gharama zinaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo hivi vitatu vikiangaliwa vizuri ndiyo ufumbuzi wa tatizo lililoko mbele yetu la uhaba wa maji baada ya upanuzi wa mipaka niliyoibainisha hapo juu.

Baada ya ushauri wangu huo, napenda kuunga mkono Hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa asilimia mia moja na kuwatakia utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumsifu na kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoweza kuianzisha Wizara hii na kuiongeza hadi kufikia hali hii ya juu kabisa. Sina wasiwasi kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo langu, ninayo matatizo makuu mawili kama ifuatavyo: -

Kwanza, ni Chuo cha Mifugo Madaba. Chuo hiki kina *site* nzuri na *infrastructure* zote - majumba ya kisasa, maji na umeme. Ardhi ni kubwa sana *(virgin land)*. Chuo hakina walimu wala wanafunzi. Naomba Mheshimiwa Waziri atume timu ndogo ya wataalam wakatazame na wapendekeze matumizi ya Chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Peramiho ni Mji mdogo, lakini mambo yake ni makubwa. Ni Kituo cha kwanza cha Wamisionari wa *Benedictine Fathers* Mkoani

Ruvuma. Ina Shule za Sekondari mbili, Hospitali kubwa, Chuo cha Ufundi, Chuo cha *Medical Sciences* na ina Vijiji vinane kuzunguka *mission* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wamisionari wametusaidia kutoa maji Kijiji cha Peramiho 'B', bado Peramiho 'A' na Vijiji kuzunguka *mission* hiyo. Wanaomba kupitia *DED* - Songea, Shilingi milioni 300 ili wachimbe visima virefu viwili na mabomba machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri anisaidie hayo mambo mawili.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Sekta ya Maji na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba nichangie maeneo yafuatayo: -

Kuhusu Sekta ya Maji, napenda kuipongeza/kuishukuru sana Serikali kwa kuwapatia wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa, huduma ya maji safi na salama. Miradi ya Maji ya Benki ya Dunia, *British Water Aid* imesaidia sana kupunguza tatizo la maji katika Wilaya ya Mpwapwa kufuatana na Sera ya Maji na Wilaya ya Mpwapwa. Kufuatana na Sera ya Maji, Wilaya ya Mpwapwa imechangia Mfuko wa Maji zaidi ya Sh.17,000,000/=. Wananchi wachangie Mifuko ya Maji.

Maeneo yote yenye ukame, Serikali ichimbe mabwawa/malambo na visima virefu ili maji hayo yasaidie huduma ya maji kwa binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Mipango: -

(i) Serikali iweke mkakati wa kupambana na magonjwa ya kupe *(Tick Borne Diseases)* kwa kuwa zaidi ya asilimia 70 –80 mifugo wanakufa kutokana na magonjwa ya kupe;

(ii) Mifugo ni Sekta muhimu sana kwa kuwa inachangia Pato la Taifa kwa asilimia 18. Kiwango hicho ni kidogo sana, mifugo iboreshwe ili iweze kuchangia zaidi Pato la Taifa kwa kuwa katika nchi yetu kuna zaidi ya ng'ombe 17,800,000;

(iii) Ukarabati wa Vituo vya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa, Chuo cha Mifugo Mpwapwa, Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo *(VICs)* uendelee na kupatiwa vitendea kazi vya kisasa;

(iv) Upandishwaji wa vyeo ni muhimu sana kwa watumishi na kurekebisha mishahara yao;

(v) Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Kanda ya Kati Mpwapwa kiwe Makao Makuu ya Utafiti wa Mifugo hapa nchini - kiwe Kituo cha Kitaifa;

(vi) Majosho 2024 ni 426 tu yanafanya kazi, ukarabati ufanyike kwa Halmashauri/Serikali; na

(vii) Bei ya dawa za kuogesha mifugo na dawa nyingine za mifugo ipunguzwe.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza kusema kwamba, naunga mkono Bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa - Mbunge na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Simanjiro ina tatizo kubwa la maji. Hata hivyo, natambua juhudi za Wizara kupambana na tatizo la maji katika Wilaya ya Simanjiro hasa kwa kuchimba mabwawa madogo. Naomba Serikali itekeleze Mradi wa Maji kutoka Pangani hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Orkesumet. Makao Makuu ya Wilaya ya Orkesumet kuna tatizo la maji na mradi huu umebuniwa toka mwaka 1981.

Tumeshuhudia miradi mikubwa ya maji ambayo ilifikiriwa haitawezekana, lakini Serikali ya Awamu ya Tatu na Wizara chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri miradi hiyo imewezekana kutekelezwa. Miradi hiyo ni Mradi wa Maji Chalinze na Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria hadi Shinyanga. Hongera Serikali ya Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iwaeleze wananchi wa Simanjiro ni lini huu mradi utaanza. Wananchi hao ni wa Vijiji vya Endonyo-Engijape, Orkesumet, Lormorijoi, Langai, Loonderkes, Kitwai ‘A’, Kitwai ‘B’, Namalulu, Naberera, Okutu, Lendanai na kadhalika. Nashukuru Wilaya ya Simanjiro kuwekwa kwenye Mradi wa Maji unaofadhiliwa na *World Bank.* Maandalizi ya utekelezaji yamekamilika**,** naona utekelezaji umechelewa. Je, ni lini mradi huu utatekelezwa?

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa hongera sana kwa Wizara kuhamia Dodoma. Wizara hii imehamia Dodoma na bado Waziri hajachubuka wala kupata mikosi. Awaambie wenzake kuwa Dodoma kuna makao mazuri sana, kungekuwa kubaya wengi wangerudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabonde nchini, miradi ndani ya mabonde yanayoorodheshwa kwenye jedwali Na.2, shughuli ndani ya mabonde hayo ni kinyume cha Mkataba wa Ardhiyoevu, Bioanuai na udhibiti wa shughuli ndani ya maeneo chepe chepe. Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchimbaji wa malambo, malambo ya Lugaga, Ekenywa, Milingwa na Mkulazi yamekamilika. Naomba malambo mawili au manne kama ifuatavyo: -

(i) Lambo la Kidugallo, la zamani limejaa matope.
(ii) Lambo Kinonko.
(iii) Lambo la *Newland* kufanyiwa ukarabati.
(iv) Lambo kwa wafugaji wa Magera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya dawa za mifugo ni ghali sana. Naomba Serikali isimamie bei ya dawa hizo. Pia, vyakula vya kuku na chanjo ni ghali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ule Mradi wa Maji ya Kisima Kirefu cha Ihembe la *DAFCO* (Serikali) na Kidugallo ambao unasimamiwa na *TASAF*, usimamiwe kwa karibu sana na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Maji wa KKKT Mkulazi mwaka 1989, Waholanzi walitoa fedha kulipatia Kanisa hili, walinunua vifaa vya maji vya mradi huo tangu mwaka 1992. Baadaye mradi ukafa ghafla, hakuna maelezo kwa wananchi hadi mimi niliamua kuomba *World Vision*, lambo limekamilika.

**MHE. DR. IBRAHIM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nawapongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri, Viongozi na Watumishi wa Wizara yote ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kibaha ni moja ya Wilaya ambazo zina matatizo ya maji. Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kutembelea Wilaya hiyo mwaka 2004 na kuzungumza na wananchi wa Kongowe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliahidi mwaka 2004 kwamba Wilaya ya Kibaha ingefaidika na Mradi Kabambe wa Kuboresha Sekta ya Maji kwa Jiji la Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo. Hata hivyo, sikusikia Kibaha ikitajwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Aidha, kuna maeneo ambayo yamekuwa sugu kwa ukosefu wa aji Kibaha. Haya ni pamoja na Soga, Msangani, Mwanalugali, Sofu na kadhalika. Naomba Wizara iweke Wilaya ya Kibaha katika mpango wa maboresho ya kupata maji, ukarabati na uchimbaji visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Mheshimiwa Naibu Waziri katika uchaguzi ujao.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika Wizara hii tokea mwaka 2000 hadi hii leo. Nawatakia mafanikio makubwa siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho cha mwaka 2000 – 2005, Jimbo langu limefaidika na mpango wa maji Vijijini. Vijiji vya Lwangu, Boimanda, Idunda, Mamongolo viliingizwa kwenye mpango wa mwaka 2004/2005 na kazi kubwa imefanyika kwa Kijiji cha Lwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliahidiwa kiasi cha Sh.58,000,000/= na hadi hivi sasa mradi wa Lwangu umepata fedha zote Sh.30,000,000/= na umekamilika. Sh.28,000,000/= hatujapata kwa ajili ya Vijiji vya Boimanda, Idunda na Mamongolo. Nina imani kuwa shughuli hii itakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Njombe Kusini tokea tupate uhuru halijapata mradi wowote wa maji ukiondoa hii niliyotaja hapo juu. Kwa hiyo, naomba Wizara iendelee kutusaidia kwani *survey* nyingi tumezifanya kwa msaada wa Wizara hii kutupa utaalam, lakini wananchi na mimi mwenyewe tumechanga fedha kwa makusudi hayo. Hivyo, naomba Wizara isituchoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na ninawatakia Waziri na Naibu wake uchaguzi mzuri.

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kuipongeza Wizara hii, hususan Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuendelea kufanya kazi vizuri katika kipindi kilichopita mwaka 2004/2005 na mpango mzuri wa kipindi kijacho cha mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imekuwa *vibrant,* nikiwa na maana kuwa angalau sasa chini ya Mheshimiwa Waziri Lowassa wanasonga mbele kwa ufanisi unaoonekana katika huduma za maji na mifugo. Hivi ndivyo tunapaswa kuendesha shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona jitihada dhahiri kama Mradi wa Maji Chalinze, Mradi wa Kuvuta Maji Ziwa Victoria na kadhalika. Tunakumbuka mvutano uliokuwepo wakati wa kutaka kuvuta maji ya Ziwa Victoria. Nchi zilizopo kando kando ya Mto Nile zilitaka juhudi za kuhudumia wananchi wetu zisifanikiwe. Waziri na Serikali zilisimama kidete kutetea hoja yake. Ninaipongeza sana Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro tunaishukuru sana Wizara na Serikali kwa namna zilivyoshughulikia suala la tatizo la maji hususan *West Kilimanjaro* kupitia Wafadhili wa nchi ya Ujerumani. Kwa niaba ya wananchi wa Kilimanjaro, tungependa kutoa shukrani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza kupitia Wizara hii tumeona kuhimizwa kwa nguvu umuhimu wa ufugaji bora hasa wa ng'ombe na wanyama wengine. Sasa hivi wafugaji wameanza kufahamu umuhimu wa kufuga kibiashara. Wafugaji wajue mifugo yao ni kitega uchumi kilicholala. Kelele nzuri za Waziri zinaanza kuzaa matunda, kwa mfano tumeanza kupata nyama nzuri na safi katika maduka makubwa *(Supermarkets)* zilizoko katika Miji mikubwa. Vile vile tumeanza *exports* za mifugo hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi mengine ya kuisifia Wizara hii. Ninaomba kumalizia kwa kuipongeza Wizara na Serikali kwa namna walivyoamua kuwatimua *City Water* baada ya kufanya kazi chini ya kiwango. Huu ni mfano mzuri wa namna ambavyo Serikali inatakiwa kusimamia mapinduzi ya mfumo wa uchumi wa soko. Mfumo wa soko huru si holela, unapaswa kusimamiwa kwa karibu sana na hivi ndivyo walivyofanya Wizara hii. Tuone mifano mingine kutoka Wizara nyingine kama Nishati na Madini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga hoja mkono na ninashukuru.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimpongeze Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ya kuboresha upatikanaji wa maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za maji taka, maoni yangu ni kwamba kuwepo na *flat rate* kwa huduma ya maji taka. Kumtoza mtu kiwango cha asilimia 30 ya maji safi kama ilivyo hapa Dodoma ni unyonyaji, kwani kama mtu ana bustani anatumia maji safi mengi na si kweli kwamba atatumia asilimia 30 ya hayo maji kama maji taka. Kwa hali hii, watu wataanza kurudi katika hali ya zamani ya kutumia *septic tanks.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya maji katika Chuo cha Maendeleo Kihinga – Kigoma na Kitagata Kasulu, Chuo hicho na Vijiji vya jirani vya Kihinga, Chankabwimba, Mungonya na Nkungwe havina huduma ya maji na watu hutembea kwa saa kadhaa kutafuta maji. Je, Serikali itakuwa tayari kuvipatia maji Vijiji hivi pamoja na Chuo hiki? Vile vile, Kata ya Kitagata Wilayani Kasulu nayo ina shida kubwa ya maji wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za mifugo, ningependa nielekezwe utaratibu wa kazi za Mabwana Mifugo. Nionavyo ni kwamba, wanafanya kazi kama Waganga wa Kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa Geita wamepata vyeo tunashukuru kwa hilo, lakini kuna mmoja alionyesha kitu cha ajabu, ana miaka karibu 20 hajapanda daraja. Basi naomba wajaribu kuangalia watu kama wale na wenyewe wapande wajisikie wanafanya kazi vizuri. Kwa sababu sielewi inatokeaje kwenye Wizara hii wanachelewa, lakini safari hii wamepanda.

Sasa kuwe na utaratibu mzuri kama wengine wanavyopanda baada ya miaka mitatu, mitano wanapanda. Nafikiri kuwe na utaratibu mzuri wa namna hiyo, wengine wamepanda sasa hivi nashukuru lakini kuna ambao bado nadhani havijafika lakini kama vimefika basi tunaomba waangaliwe.

Mheshimiwa Waziri, wengine sasa hivi tumefikia kwenye hatua za mwisho. Najua una hadhi, umejitahidi umekuja kututembelea, naomba kabla hatujafikia uchaguzi, nina imani kwa wananchi wako walivyo, kura za maoni huna matatizo baada ya kujaza fomu tu na baada ya kura za maoni nina imani utapita fika huko kwa sababu hiki cheo unachofika kule wakuone wanafurahia kuja kwako. Wewe unayetupa maji njoo uone huo mradi unavyofanana kusudi atakayekuja nina imani huwa kuna kukabidhiana, basi arithi vitu ambavyo utakuwa umemwambia hapa nimeacha hiki na hiki, karibu sana naomba ukubali kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, kwa heshima uliyonipa nichangie asubuhi, nilikuwa nimepata dharura, naomba nikushukuru sana. Lakini Wizara hii naipongeza, naomba tuwape fedha wakafanye kazi, wanafanya kazi nzuri sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE**: *Good morning, I have been reading your Excellent Budged Speech. This work will leave a long lasting (bright) legacy at the Ministry for years to come! Congratulations and best wishes for bigger things! There is however, one thing that needs your elaboration. Last year you included 38 Districts in your World Bank Funded Villages and Sanitation Project. We have selected Villages, opened Bank Accounts and are contributing money for the 5% requirement. But there is no Budgetary Money set aside for moving these projects ahead. What is the plan? Congratulations.*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mashine ya maji Engarenaibor, naomba kukumbushia *engine* ya maji ambayo Wizara hii imeagiza kwa ajili ya Kata hiyo. Walihitaji fedha kiasi cha Shilingi milioni 3.5. Hali huko ni mbaya kutokana na mvua kutonyesha. Bado naomba mtupatie ili fedha hizo zichangwe. Mwaka jana 2004 mifugo ya Kata hiyo ilihama kutokana na shida ya maji na hata mwaka huu 2005 kuna uwezekano wa kuhama.

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa msaada wake wa Sh.5,000,000/= kwa ajili ya kuchimba lambo. Hata hivyo nina masikitiko makubwa sana kwani fedha hiyo ni kidogo sana kwa shughuli iliyokusudiwa kwa sababu haikufanikisha. Hivyo, naomba Mheshimiwa Waziri aniongeze fedha ili kazi iliyokusudiwa imalizike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafurahi sana iwapo Mheshimiwa Waziri ataniletea *memo* ya maelezo yoyote.

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri na Naibu Waziri kwa jinsi wanavyosimamia Wizara hii kwa ufanisi mkubwa bila kuchoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Viongozi wa Wizara hii, bado kuna maeneo mengi ambayo hayana kabisa huduma ya maji safi na salama kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa vile walishafika Wilaya ya Bukombe na kujionea wao wenyewe matatizo ya maji yaliyoko Wilayani hapo. Aidha, nimjulishe Mheshimiwa Waziri Lowassa kuwa ule mradi wa Maji ya Bomba Msasa – Uyovu ambao yeye mwenyewe aliushuhudia mpaka leo haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa zilizopo, lakini bado kuna matatizo makubwa ya maji katika Mji wa Ushirombo ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe. Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira unaoendelea Mkoani Shinyanga kwa ufadhili wa Serikali ya Uholanzi katika Wilaya ya Bukombe bado unasuasua sana. Aidha, kuna hisia ya ubadhirifu wa fedha umefanyika kwenye mradi huu, kwani Mkandarasi anaonekana kulipwa fedha nyingi kuliko kazi aliyoifanya. Hivyo, naishauri Serikali ifuatilie mradi huo ili ione maajabu yaliyoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Wizara hii inaonekana kufanya kazi nzuri, nashauri iwe na mawasiliano ya karibu na Wawakilishi wao huko Mikoani na Wilayani ili wasiharibu kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Hotuba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ukarabati na upanuzi wa maji ya Mji wa Namtumbo mwaka 2004/2005 tuliahidiwa Shilingi milioni 30, hadi Juni zilipatikana Shilingi milioni 20 tu za kununulia vifaa. Je, mwaka huu tutapata fedha zaidi na kufikia Shilingi milioni 30 zilizopangwa huko nyuma mwaka 2004/2005?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Namtumbo wameongezeka watu na vifaa vya *reservoir* ya maji havitoshelezi Mji mpya wa Namtumbo. Je, tutasaidiwa msaada huo wakati wa 2005/2006?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu. Pia, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamana ya kuunganisha Sekta ya Maji na Mifugo haieleweki kabisa, kwani dhana ya maji inatakiwa kuwa inajitegemea kwa kuwa watumiaji wa maji ni kilimo, mifugo, binadamu, nishati, mazingira na viwanda. Kwa sasa maendeleo ya Sekta ya Maji chini ya mfumo wa sasa uliounganishwa na mifugo, ni dhahiri Wizara ya sasa inapendelea Sekta ya Mifugo. Natoa ushauri kuwa Sekta hii itenganishwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo, kutokomeza umaskini uliokithiri katika jamii ya wananchi wengi (asilimia 80% waliopo Vijijini) itategemea mageuzi katika kilimo kutoka kwenye kilimo cha kutegemea mvua na kuingia kikamilifu katika kilimo cha kumwagilia maji mashamba. Wizara kwa nini ina kigugumizi kikubwa kuhusu uvunaji maji ya mvua? Serikali sasa ione umuhimu mkubwa wa kuanzisha utaratibu wa kuvuna maji ya mvua kitaifa. Mvua inaponyesha popote Vijijini maji yavunwe na iwe raslimali muhimu ya Kijiji. Kitendo cha kuachia maji ya mvua kuvuruga na kutishia wananchi kama mafuriko na uzalishaji wa makorongo Vijijini ni uzembe unaoendelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Taasisi nyingi Kimataifa za Fedha zipo tayari kuisaidia Tanzania kuwezesha kujenga mabwawa madogo *(rural earth dams)* Vijijini hasa *ADB/ADF, EDF, IDA, BADEA* pamoja na nchi mbalimbali *(bilateral funding assistance).* Kwa nini Serikali isichukue nafasi hii ione umuhimu wa kuleta mageuzi makuu kwenye uchumi wetu na huduma za jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo aniunge mkono katika Mradi wa Kuvuna Maji ya Mlima Sekenke kwa matumizi ya kilimo kwenye Bonde la Wembere, Wilaya ya Iramba Mkoa wa Singida. Mradi huu utahusisha Kata za Urughu, Mtekente, Mtoa, Shelui, Ntwike, Tulya na Kidaru. Mradi huu *(write-up)* umekwishapelekwa Wizara ya Fedha kuombewa misaada kutoka *ADB/ADF, BADEA*, Italia na Belgium.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufufua mabwawa na kuchimba visima katika Wilaya mbalimbali, mradi huu ambao umefadhiliwa na Benki ya Dunia (IDA) haujawafikia wananchi wengi na hautekelezwi ipasavyo. Kwa Wilaya ya Iramba Jimbo la Iramba Magharibi, namsihi Mheshimiwa Waziri awasaidie wananchi kwa kufufua mabwawa yafuatayo: Kidaila, Kitusha, (Kata ya Kinampanda), Bwawa la Shelui, Bwawa la Tutu (Mji wa Kiomboi), Bwawa la Urughu (Kata ya Urughu), Bwawa la Mkulu (Kata ya Ulemo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya Maji Safi na Maji Taka katika Jiji la Dar es Salaam, huduma katika Jiji hili inaendelea kutawaliwa na rushwa. Huwezi kupata maunganisho ya maji safi Jijini pasipo kutoa chochote (rushwa). Leo ndiyo unaona maunganisho yasiyo ya kitaalam na mabomba ya maji yamezagaa na kuvuja ovyo ovyo! Hivi Wizara inaelewa hivyo au imetoa baraka zake?

Pamoja na vitendo vya rushwa wananchi wananyimwa maji katika Kata nyingi za Dar es Salaam, lakini biashara ya kuuza maji inaendelea kushamiri na kwa bei inayoongezeka kila siku na biashara hii inaendana na kutoa chochote kwa wakubwa (Meneja) wa huduma za maji. Vyombo vya Serikali vimulike tatizo hili la vitendo vya rushwa katika huduma ya maji Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Dar es Salaam wangependa kupata huduma ya kuunganishwa kwenye huduma ya maji taka. Mtaa wa *Regent Estate* sasa hivi umeingiliwa na mafuriko ya maji ya mvua na kwa hiyo, mashimo ya vyoo *(septic tanks – sewerage)* ya nyumba nyingi wamefurika hasa Mtaa wa Vikawe, nyumba karibu zote zina tatizo hili. Namwomba na kumsihi Mheshimiwa Waziri kuwa Mtaa wa Vikawe uunganishwe kwenye bomba la huduma ya maji taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kupongeza jitihada zinazofanywa na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na wataalam wake kwa kufanikisha azma ya kuwapatia Watanzania mahitaji yao muhimu ya maji safi, salama na ya kutosha kwa maendeleo na afya zao. Hili linadhihirishwa na kufikia kuondoa tatizo sugu lililokuwapo ndani ya Jiji la Dodoma kwa asilimia 100 na sasa kama tujuavyo zimeanza jitihada za kuyatumia maji ya Ziwa Victoria kwa Miji ya Kahama na Shinyanga jambo ambalo hapo nyuma lilikuwa ni ndoto tupu ukizingatia mikataba ya kikoloni iliyotunyima haki yetu na kuwapa wenzetu wa Sudan na Misri wafaidike, sisi tukibaki na umaskini wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Watendaji ndani ya Wizara ya Maji na Maendeleo na Mifugo. Baada ya kutanguliza hilo, sasa ningependa kwenda kwenye Jimbo langu la Morogoro Mjini kwa Ushauri.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Morogoro unatazamiwa kupanuka kwa kipenyo cha kilometa 30 kwa barabara za Morogoro/Dar es Salaam, Morogoro/Iringa na Morogoro/Dodoma. Hili limo kwenye uamuzi uliokwishafanywa na Vikao mbalimbali vinavyohusika ikiwamo *Full Council* ya Halmashauri ya Manispaa na *Regional Consultative Committee (RCC)* vilivyokaa mapema mwezi Aprili/Mei 2005. Kikao pekee kilichobaki kuidhinisha hilo ni cha Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa angalizo hilo ili Wizara na chombo chake kinachotoa huduma hiyo ndani ya Manispaa ya Morogoro (*MORUWASA*) waweze kuandaa kabiliano la ongezeko hilo la eneo la kupeleka huduma ya maji safi na salama litakaloendana na upimaji wa maeneo ya makazi yatakayojengwa siku za usoni. Upanuzi huo utachukua Vijiji vingi vikiwemo Mkambarani, Kizinga, Pangawe na Mikese kwa barabara ya Morogoro/Dar es Salaam, Tangeni, Mzumbe, Sangasanga na Melela kwa upande wa barabara ya Iringa na Wami Dakawa kwa barabara ya Morogoro/Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hii, napenda kutoa ushauri kwamba vyanzo vipya vya maji vitazamwe kukidhi ongezeko hilo. Moja ni kuona uwezekano wa kujenga bwawa dogo kwenye Mto Mgolole (Vituli) kuvuna maji wakati wa mvua za masika na kuyahifadhi kwa matumizi ya wakati wa kiangazi. Chanzo cha pili ni Mto Wami ambao upembuzi yakinifu ulishafanywa miaka ya themanini mwishoni na tisini mwanzoni ambapo matanki ya kusafishia maji na hifadhi yalibainishwa kujengwa eneo la Mkundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo kingine ni Bwawa la Mindu ambalo lilibuniwa kujengwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilikamilika mwaka 1985 na kuzinduliwa na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Awamu ya pili ilihusu kuongeza kina cha maji kwa kuinua tuta lililopo kwa milimita 2.5 zaidi, lakini haikuwahi kutekelezwa hadi leo inapofikia miaka 20 sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ningependa kupata maelezo ya kina ili nijue ni nini kilichopelekea usanifu huu wa bwawa kutotekelezwa kama ilivyokusudiwa. Nafahamu sababu zinaweza kuwa ufinyu wa fedha, lakini siyo siri kwamba kadri unavyocheleweshwa gharama zinaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo hivi vitatu vikiangaliwa vizuri ndiyo ufumbuzi wa tatizo lililoko mbele yetu la uhaba wa maji baada ya upanuzi wa mipaka niliyoibainisha hapo juu.

Baada ya ushauri wangu huo, napenda kuunga mkono Hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa asilimia mia moja na kuwatakia utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumsifu na kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoweza kuianzisha Wizara hii na kuiongeza hadi kufikia hali hii ya juu kabisa. Sina wasiwasi kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo langu, ninayo matatizo makuu mawili kama ifuatavyo: -

Kwanza, ni Chuo cha Mifugo Madaba. Chuo hiki kina *site* nzuri na *infrastructure* zote - majumba ya kisasa, maji na umeme. Ardhi ni kubwa sana *(virgin land)*. Chuo hakina walimu wala wanafunzi. Naomba Mheshimiwa Waziri atume timu ndogo ya wataalam wakatazame na wapendekeze matumizi ya Chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Peramiho ni Mji mdogo, lakini mambo yake ni makubwa. Ni Kituo cha kwanza cha Wamisionari wa *Benedictine Fathers* Mkoani Ruvuma. Ina Shule za Sekondari mbili, Hospitali kubwa, Chuo cha Ufundi, Chuo cha *Medical Sciences* na ina Vijiji vinane kuzunguka *mission* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wamisionari wametusaidia kutoa maji Kijiji cha Peramiho 'B', bado Peramiho 'A' na Vijiji kuzunguka *mission* hiyo. Wanaomba kupitia *DED* - Songea, Shilingi milioni 300 ili wachimbe visima virefu viwili na mabomba machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri anisaidie hayo mambo mawili.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Sekta ya Maji na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba nichangie maeneo yafuatayo: -

Kuhusu Sekta ya Maji, napenda kuipongeza/kuishukuru sana Serikali kwa kuwapatia wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa, huduma ya maji safi na salama. Miradi ya Maji ya Benki ya Dunia, *British Water Aid* imesaidia sana kupunguza tatizo la maji katika Wilaya ya Mpwapwa kufuatana na Sera ya Maji na Wilaya ya Mpwapwa. Kufuatana na Sera ya Maji, Wilaya ya Mpwapwa imechangia Mfuko wa Maji zaidi ya Sh.17,000,000/=. Wananchi wachangie Mifuko ya Maji.

Maeneo yote yenye ukame, Serikali ichimbe mabwawa/malambo na visima virefu ili maji hayo yasaidie huduma ya maji kwa binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Mipango: -

(i) Serikali iweke mkakati wa kupambana na magonjwa ya kupe *(Tick Borne Diseases)* kwa kuwa zaidi ya asilimia 70 –80 mifugo wanakufa kutokana na magonjwa ya kupe;

(ii) Mifugo ni Sekta muhimu sana kwa kuwa inachangia Pato la Taifa kwa asilimia 18. Kiwango hicho ni kidogo sana, mifugo iboreshwe ili iweze kuchangia zaidi Pato la Taifa kwa kuwa katika nchi yetu kuna zaidi ya ng'ombe 17,800,000;

(iii) Ukarabati wa Vituo vya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa, Chuo cha Mifugo Mpwapwa, Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo *(VICs)* uendelee na kupatiwa vitendea kazi vya kisasa;

(iv) Upandishwaji wa vyeo ni muhimu sana kwa watumishi na kurekebisha mishahara yao;

(v) Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Kanda ya Kati Mpwapwa kiwe Makao Makuu ya Utafiti wa Mifugo hapa nchini - kiwe Kituo cha Kitaifa;

(vi) Majosho 2024 ni 426 tu yanafanya kazi, ukarabati ufanyike kwa Halmashauri/Serikali; na

(vii) Bei ya dawa za kuogesha mifugo na dawa nyingine za mifugo ipunguzwe.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza kusema kwamba, naunga mkono Bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa - Mbunge na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Simanjiro ina tatizo kubwa la maji. Hata hivyo, natambua juhudi za Wizara kupambana na tatizo la maji katika Wilaya ya Simanjiro hasa kwa kuchimba mabwawa madogo. Naomba Serikali itekeleze Mradi wa Maji kutoka Pangani hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Orkesumet. Makao Makuu ya Wilaya ya Orkesumet kuna tatizo la maji na mradi huu umebuniwa toka mwaka 1981.

Tumeshuhudia miradi mikubwa ya maji ambayo ilifikiriwa haitawezekana, lakini Serikali ya Awamu ya Tatu na Wizara chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri miradi hiyo imewezekana kutekelezwa. Miradi hiyo ni Mradi wa Maji Chalinze na Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria hadi Shinyanga. Hongera Serikali ya Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iwaeleze wananchi wa Simanjiro ni lini huu mradi utaanza. Wananchi hao ni wa Vijiji vya Endonyo-Engijape, Orkesumet, Lormorijoi, Langai, Loonderkes, Kitwai ‘A’, Kitwai ‘B’, Namalulu, Naberera, Okutu, Lendanai na kadhalika. Nashukuru Wilaya ya Simanjiro kuwekwa kwenye Mradi wa Maji unaofadhiliwa na *World Bank.* Maandalizi ya utekelezaji yamekamilika, naona utekelezaji umechelewa. Je, ni lini mradi huu utatekelezwa?

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa hongera sana kwa Wizara kuhamia Dodoma. Wizara hii imehamia Dodoma na bado Waziri hajachubuka wala kupata mikosi. Awaambie wenzake kuwa Dodoma kuna makao mazuri sana, kungekuwa kubaya wengi wangerudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabonde nchini, miradi ndani ya mabonde yanayoorodheshwa kwenye jedwali Na.2, shughuli ndani ya mabonde hayo ni kinyume cha Mkataba wa Ardhiyoevu, Bioanuai na udhibiti wa shughuli ndani ya maeneo chepe chepe. Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchimbaji wa malambo, malambo ya Lugaga, Ekenywa, Milingwa na Mkulazi yamekamilika. Naomba malambo mawili au manne kama ifuatavyo: -

(i)Lambo la Kidugallo, la zamani limejaa matope.
(ii) Lambo Kinonko.
(iii) Lambo la *Newland* kufanyiwa ukarabati.
(iv) Lambo kwa wafugaji wa Magera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya dawa za mifugo ni ghali sana. Naomba Serikali isimamie bei ya dawa hizo. Pia, vyakula vya kuku na chanjo ni ghali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ule Mradi wa Maji ya Kisima Kirefu cha Ihembe la *DAFCO* (Serikali) na Kidugallo ambao unasimamiwa na *TASAF*, usimamiwe kwa karibu sana na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Maji wa KKKT Mkulazi mwaka 1989, Waholanzi walitoa fedha kulipatia Kanisa hili, walinunua vifaa vya maji vya mradi huo tangu mwaka 1992. Baadaye mradi ukafa ghafla, hakuna maelezo kwa wananchi hadi mimi niliamua kuomba *World Vision*, lambo limekamilika.

**MHE. DR. IBRAHIM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nawapongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri, Viongozi na Watumishi wa Wizara yote ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kibaha ni moja ya Wilaya ambazo zina matatizo ya maji. Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa kutembelea Wilaya hiyo mwaka 2004 na kuzungumza na wananchi wa Kongowe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliahidi mwaka 2004 kwamba Wilaya ya Kibaha ingefaidika na Mradi Kabambe wa Kuboresha Sekta ya Maji kwa Jiji la Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo. Hata hivyo, sikusikia Kibaha ikitajwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Aidha, kuna maeneo ambayo yamekuwa sugu kwa ukosefu wa maji Kibaha. Haya ni pamoja na Soga, Msangani, Mwanalugali, Sofu na kadhalika. Naomba Wizara iweke Wilaya ya Kibaha katika mpango wa maboresho ya kupata maji, ukarabati na uchimbaji visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Mheshimiwa Naibu Waziri katika uchaguzi ujao.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika Wizara hii tokea mwaka 2000 hadi hii leo. Nawatakia mafanikio makubwa siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho cha mwaka 2000 – 2005, Jimbo langu limefaidika na mpango wa maji Vijijini. Vijiji vya Lwangu, Boimanda, Idunda, Mamongolo viliingizwa kwenye mpango wa mwaka 2004/2005 na kazi kubwa imefanyika kwa Kijiji cha Lwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliahidiwa kiasi cha Sh.58,000,000/= na hadi hivi sasa mradi wa Lwangu umepata fedha zote Sh.30,000,000/= na umekamilika. Sh.28,000,000/= hatujapata kwa ajili ya Vijiji vya Boimanda, Idunda na Mamongolo. Nina imani kuwa shughuli hii itakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Njombe Kusini tokea tupate uhuru halijapata mradi wowote wa maji ukiondoa hii niliyotaja hapo juu. Kwa hiyo, naomba Wizara iendelee kutusaidia kwani *survey* nyingi tumezifanya kwa msaada wa Wizara hii kutupa utaalam, lakini wananchi na mimi mwenyewe tumechanga fedha kwa makusudi hayo. Hivyo, naomba Wizara isituchoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na ninawatakia Waziri na Naibu wake uchaguzi mzuri.

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kuipongeza Wizara hii, hususan Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuendelea kufanya kazi vizuri katika kipindi kilichopita mwaka 2004/2005 na mpango mzuri wa kipindi kijacho cha mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imekuwa *vibrant,* nikiwa na maana kuwa angalau sasa chini ya Mheshimiwa Waziri Lowassa wanasonga mbele kwa ufanisi unaoonekana katika huduma za maji na mifugo. Hivi ndivyo tunapaswa kuendesha shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona jitihada dhahiri kama Mradi wa Maji Chalinze, Mradi wa Kuvuta Maji Ziwa Victoria na kadhalika. Tunakumbuka mvutano uliokuwepo wakati wa kutaka kuvuta maji ya Ziwa Victoria. Nchi zilizopo kando kando ya Mto Nile zilitaka juhudi za kuhudumia wananchi wetu zisifanikiwe. Waziri na Serikali zilisimama kidete kutetea hoja yake. Ninaipongeza sana Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro tunaishukuru sana Wizara na Serikali kwa namna zilivyoshughulikia suala la tatizo la maji hususan *West Kilimanjaro* kupitia Wafadhili wa nchi ya Ujerumani. Kwa niaba ya wananchi wa Kilimanjaro, tungependa kutoa shukrani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza kupitia Wizara hii tumeona kuhimizwa kwa nguvu umuhimu wa ufugaji bora hasa wa ng'ombe na wanyama wengine. Sasa hivi wafugaji wameanza kufahamu umuhimu wa kufuga kibiashara. Wafugaji wajue mifugo yao ni kitega uchumi kilicholala. Kelele nzuri za Waziri zinaanza kuzaa matunda, kwa mfano tumeanza kupata nyama nzuri na safi katika maduka

makubwa *(Supermarkets)* zilizoko katika Miji mikubwa. Vile vile tumeanza *exports* za mifugo hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi mengine ya kuisifia Wizara hii. Ninaomba kumalizia kwa kuipongeza Wizara na Serikali kwa namna walivyoamua kuwatimua *City Water* baada ya kufanya kazi chini ya kiwango. Huu ni mfano mzuri wa namna ambavyo Serikali inatakiwa kusimamia mapinduzi ya mfumo wa uchumi wa soko. Mfumo wa soko huru si holela, unapaswa kusimamiwa kwa karibu sana na hivi ndivyo walivyofanya Wizara hii. Tuone mifano mingine kutoka Wizara nyingine kama Nishati na Madini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga hoja mkono na ninashukuru.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimpongeze Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ya kuboresha upatikanaji wa maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za maji taka, maoni yangu ni kwamba kuwepo na *flat rate* kwa huduma ya maji taka. Kumtoza mtu kiwango cha asilimia 30 ya maji safi kama ilivyo hapa Dodoma ni unyonyaji, kwani kama mtu ana bustani anatumia maji safi mengi na si kweli kwamba atatumia asilimia 30 ya hayo maji kama maji taka. Kwa hali hii, watu wataanza kurudi katika hali ya zamani ya kutumia *septic tanks.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya maji katika Chuo cha Maendeleo Kihinga – Kigoma na Kitagata Kasulu, Chuo hicho na Vijiji vya jirani vya Kihinga, Chankabwimba, Mungonya na Nkungwe havina huduma ya maji na watu hutembea kwa saa kadhaa kutafuta maji. Je, Serikali itakuwa tayari kuvipatia maji Vijiji hivi pamoja na Chuo hiki? Vile vile, Kata ya Kitagata Wilayani Kasulu nayo ina shida kubwa ya maji wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za mifugo, ningependa nielekezwe utaratibu wa kazi za Mabwana Mifugo. Nionavyo ni kwamba, wanafanya kazi kama waganga wa kujitegemea. Mfugaji analipia kila kitu kuanzia usafiri, dawa na huduma za Mganga. Mbaya zaidi kiwango hiki hakieleweki, kwani ni mapatano kati ya mfugaji na mganga. Hivi waganga hawa wanalipwa na Serikali? Kwa nini kusiwepo na ratiba za waganga kuwazungukia wafugaji na kutoa ushauri bila kuwategemea wafugaji kuwaita na kulipia usafiri hio?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri huo, naunga mkono hoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga tena mkono hoja hii ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Pamoja na mchango niliochangia kwa kuongea, kuna mambo ambayo muda haukutosha kuyaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mashamba ya West Kilimanjaro ikifika wakati wa kugawa mashamba hayo, wananchi wafugaji ambao wako kwenye maeneo hayo wapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ranchi ambayo wakati wa Marehemu Mheshimiwa Sokoine alianzisha ufugaji wa ng'ombe za Vijiji nane. Walichanga ng'ombe zikawekwa kwenye ranchi hiyo na kutumika kwa muda wa miaka 10. Naomba ranchi hiyo warudishiwe wananchi waanzishe SACCOS na kufugia huko. Tuko tayari kuanzisha SACCOS kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye majumuisho Mheshimiwa Waziri anipatie jibu la shamba hilo. Ahsante.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa - Mbunge na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa hotuba yake nzuri sana ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Hotuba ile ilikuwa makini na imeweka mwelekeo madhubuti hasa katika kipindi cha mwaka 2005/2006. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba nichukue fursa hii kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuhusu ahadi yake aliyoitoa hapa Bungeni nilipouliza swali linalohusu Mradi wa Maji ambao unahudumia pia Shule ya Sekondari ya Siha ambayo mtoto wake alipigwa risasi (Adili Abuu Uronu) kufuatia mgogoro wa maji kati ya Shule na eneo la Kijiji jirani ambacho baadhi ya wanakijiji wamekuwa wanalumbana nao mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri - Mheshimiwa Edward Lowassa, atusaidie kuwasiliana na Mkurugenzi wa *KfW* aliyepo Dar es Salaam, Dr. Hartman ili atusaidie kuharakisha *Levishi Water Supply Project* ambao upembuzi yakinifu umekwishafanyika na kukamilika na pia ambao *KfW* imekubali kuufadhili.

Ni matumaini yangu kuwa baada ya Mkuu wa Mkoa kuwasiliana na Dr. Hartman na pia *Mr*. Braasch kufanya hivyo baada ya Kikao cha tarehe 24 Machi, 2005 na endapo Mheshimiwa Waziri naye atatusaidia kusukuma suala hilo, naamini watatusaidia katika uharakishaji wa utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara hii kwa ujumla hasa kwa Waziri, Naibu Waziri kwa kazi kubwa waliyoifanya katika Wizara hii wakishirikiana na Wafanyakazi wa Wizara hii akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara na Wafanyakazi wote kwa ujumla. Ushirikiano wao ndio uliwafikisha hapa kuonyesha mafanikio makubwa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza au kuiuliza Wizara katika Bajeti ya mwaka 2004/2005 ilisema kuwa World Bank wana utaratibu wa kusambaza maji katika Mji wa Nzega na Vitongoji vyake. Je, Mradi huu upo au mmeishia wapi? Nilitaka kujua na kuweza kuwafahamisha wananchi wangu wa Nzega ambao walikuwa na shauku kubwa ya kutaka kujua ni lini Mji wao utapata huduma ya maji ya uhakika yasiyokuwa na mgao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kutoa maamuzi ya kutoa maji ya Ziwa Victoria kuyapeleka Shinyanga na Kahama. Lakini tatizo litatatulika katika baadhi ya maeneo na ukimaliza moja huwa na mengine mawili huzaliwa hivyo naomba Mji wangu wa Nzega upewe maji ya Ziwa Victoria ili kuweza kuondoka kero ya maji Mjini Nzega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga Mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna mradi mkubwa wa kusambaza maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na hatimaye Tabora na kadhalika. Kadhalika kumekuwa na maendeleo makubwa ya shughuli za Viwanda kando kando mwa ziwa hilo. Aidha, miradi ya madini nayo inaongezeka kwa kasi.

Ni dhahiri kwamba kukua kwa shughuli za maendeleo kando kando mwa Ziwa kunapelekea pia uchafuzi wa mazingira ya sehemu hizo. Utafiti kwa sasa unaonyesha kwamba uchafuzi wa maji katika Ziwa Victoria, bado haujafikia kiwango cha kutosha. Lakini kwa kadri siku zinavyokwenda ni wazi kwamba uchafuzi utaongezeka kama hatua madhubuti hazitakuchukuliwa kuidhibiti hali hiyo.

Naishauri Serikali iwe inafanya uchunguzi wa mara kwa mara kuona viwango vya uchafuzi wa maji na kuchukua hatua zinazofaa. Aidha, wenye viwanda na shughuli za migodi kando kando mwa ziwa walazimishwe kuchukua tahadhari ya hali ya juu kuona kwamba maji ya ziwa hayachafuliwi.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nitumie fursa hii, ili kwa niaba yangu binafsi na Wapigakura wangu wa Jimbo la Kwimba, nitoe salamu za rambirambi kwa familia na Wapigakura wa Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliofariki katika kipindi cha karibuni cha Bunge hili. Kwanza ni Mheshimiwa Abdulkari Towagale Kiwanga - Mbunge wa Kilombero; pili, Mheshimiwa Ahamed Diria - Mbunge wa Rahaleo; Tatu, Mheshimiwa Frank Michael Mussati - Mbunge wa Kasulu Mashariki; Nne, Mheshimiwa Theodos James Kasapira - Mbunge wa Ulanga Mashariki; na Nne, Mheshimiwa Margareth Bwana.

Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu hawa wote mahali pema Peponi. Amina. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya katika Wizara hii katika miaka hii mitano. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yangu binafsi na Wapigakura wa Jimbo la Kwimba, napenda vile vile niitumie fursa hii kuishukuru Wizara hii kwa jinsi inavyoangalia Wilaya ya Kwimba, hasa kwa suala la upatikanaji wa Maji. Wilaya ya Kwimba, ni moja ya Wilaya kame hapa nchini na ndiyo Wilaya pekee Mkoani Mwanza isiyogusana na ziwa. Maeneo makame zaidi Wilayani Kwimba ni katika Tarafa ya Mwanashimba.

Kati ya miaka ya 1972 - 1978 kulikuwa na mpango wa kupeleka maji Mwanashimba kutokea Rurela. Mradi huo haukufanikiwa. Kati ya miaka 1994 - 1995 kulikuwa na mradi wa Hesawa. Visima virefu 35-40 ilikuwa vichimbwe katika Tarafa ya Mwanashimba. Mradi huu nao haukufanikiwa sana kwa vile hadi sasa ni visima vinne tu ndivyo vinavyofanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wizara hii kwa fedha ambazo Wizara hii imekuwa ikileta Wilayani kwa ajili ya malambo. Yanasaidia sana. Malambo kwa Wilaya yetu ndiyo mkombozi wa watu wa Kwimba na mifugo yao. Tunashukuru sana kwa misaada na huruma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa kuweka iwe mojawapo ya Wilaya 60 za kwanza katika mradi wa maji wa msaada/mkopo toka Benki ya Dunia. Tunashukuru sana.

Napenda nitoe shukrani zangu za pekee kwa Mheshimiwa Anthony Diallo, aliyekubali kunipatia takribani masaa matatu nikaweza kukaa Ofisini kwake tukijadili faida na uwezekano wa Mwanashimba kuingizwa katika mradi wa kupeleka maji toka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga. Ombi ambalo hatimaye lilichuliwa na kukubaliwa na watalaamu wa Wizara hii. Nawashukuru sana wataalam wa Wizara hii kwa kukubali wazo na ombi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba sasa ni Wizara kufanya mawasiliano ya karibu zaidi na uongozi wa Wilaya ya Kwimba ili mapema Wilaya ijue nafasi na majukumu yake katika mradi huu. Mpaka sasa mradi (njia ya mabomba hadi Mhalo Kata ya Bupanwa haijajulikana wazi kwa wakazi wa eneo hilo. Aidha, Wilaya nayo haijawa na ufahamu wa kutosha wa mradi huu. Mawasiliano kati ya Wizara na Halmashauri ya Wilaya ni muhimu ili watu wakaonufaika na mradi huo nao wakaarifiwa wajue wajibu na matarajio yao.

Ombi la pili, ni Wizara hii kwa kushirikiana na TAMISEMI watupatie mtaalam anayestahili kwa ngazi ya Wilaya, ili maendeleo ya maji Wilayani, yaweze kwenda haraka.

Ombi la tatu, ni kwa Wizara hii, kadri uwezo utakavyokuwa unaruhusu tuongezewe fedha ya kuchimba na kusafisha malambo ili kuinusuru Kwimba.

Ombi nne na la mwisho ni kuangalia uwezekano wa mradi huu wa kupeleka maji Shinyanga ufike hadi Ngudu, Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Edward Lowassa - Mbunge na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa hotuba nzuri sana ambayo ina maelezo ya wazi na kina, pia takwimu muhimu. Naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia moja.

Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Anthony Diallo - Mbunge na Naibu Waziri, Bwana Vincent Mrisho - Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kumsaidia Waziri kwa ufanisi wa hali ya juu.

Pia, nampongeza Waziri kwa kutoa ushauri makini kwa Rais na Serikali kwa jumla na kufanikiwa kuvunja mkataba na City Water. Hongera sana na naunga mkono hatua zilizochukuliwa. Naishukuru Wizara kwa kutekeleza ahadi ya kukarabati mradi wa maji wa Mgwashi. Kazi inaendelea vizuri. Katika hotuba ya Bajeti ukurasa wa 43 kifungu Na.78 kutakuwa na ukarabati wa miradi ya maji – Lushoto. Je, ni miradi gani wa Jimbo la Bumbuli itashughulikiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MWANAMKUU M. KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri apokee shukrani zangu za dhati kabisa kwa msaada wake alionipa. Pia, nawashukuru sana vijana wake, walimsaidia sana kijana wangu mpaka akaweza kupata ng'ombe wazuri tu na hivi sasa tunao nyumbani Zanzibar na wana afya nzuri.

Pia, kijana wangu alipata nafasi ya kwenda kupata Semina juu ya ufugaji bora ambayo wanamalizia leo. Kwa hiyo, nashukuru sana Mungu atujalie kheri sote. Ahsante.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Awali ya yote, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika maandalizi ya Bajeti hii iliyoandaliwa kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwombea Mheshimiwa Waziri Edward Lowassa na Naibu Waziri wake, warudi tena Bungeni ili wakamilishe miradi mbalimbali waliyoianza kuitekeleza na ile ambayo wanakusudia kuitekeleza. Naridhika na utendaji wa Wizara hii mpya ambayo Mheshimiwa Waziri ni mwasisi kwa kuzingatia utendaji wake mzuri. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kwa kutaka kuwa na kumbukumbu sahihi. Kiambatanisho namba tatu ukurasa wa 89 namba 15 Mkoa wa Ruvuma, sensa ya mwaka 2002 inaonyesha kuwa Mkoa wa Ruvuma, ulikuwa na wakazi

zaidi ya 1,017,000 na siyo 943,037 kama ilivyoonyesha kwenye taarifa hii kwa misingi hii asilimia ya wanaopata huduma ya maji ni ndogo kuliko asilimia 56.67 iliyoonyeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanavijiji wa Mbinga Mashariki, wanao utamaduni wa kujenga mifereji ya maji hadi majumbani kwa kutumia nguvu ya msukumo *(force of gravity)* suala la ufundi siyo tatizo, lakini tatizo ni upatikanaji wa vifaa *(plastic pipes).* Sasa ningependa kukumbushia tena kuwa ili Mheshimiwa Waziri apate picha kamili, namwomba atembelee Mbinga, ili aone ninachosema. Naamini na ninamwombea Mheshimiwa Waziri, arudi tena Bungeni na aendelee kuiongoza Wizara aliyoiasisi.

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na takwimu zilizopo inakadiriwa kuwa mchango wa Sekta ya Mifugo katika Pato la Taifa ni asilimia 6.1. Makadirio haya mara nyingi huzingatia uzalishaji wa maziwa, nyama, mayai na ngozi.

Mchango wa Sekta hii katika kuwapatia wananchi ajira, nguvukazi na mbolea ya samadi bado haujazingatiwa ipasavyo. Ni vyema sasa Wizara ikafanya tathmini ya kina juu ya mchango wa sekta hii kwa kuingiza mchango unaotokana na upatikanaji wa ajira, nguvukazi na mbolea ya samadi. Kutokana na hayo, ni dhahiri kwamba Pato la Taifa litokanalo na Sekta ya Mifugo litakuwa kubwa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za mifugo zilizopo nchini nazo pia zinaonekana ni ndogo kulingana na hali halisi ilivyo. Kwa mara ya mwisho sensa ya mifugo *(total counts)* ilifanyika mwaka 1984. Takwimu hizi ziliboreshwa mwaka 2002 kutokana na *livestock sampling* iliyofanyika sambamba na sensa ya mazao ya kilimo. Hesabu zilizopatikana zinafanyiwa extrapolation kupata idadi kamili.

Takwimu zilizopatikana kwanza zimekuwa na walakini kutokana na sababu zifuatazo:-

· *Sampling* iliyofanyika haikuwahusika wataalam wa mifugo;

· *Sampling* ilifanywa wakati wa mavuno na kwa wakati huo mifugo hususan ng’ombe, mbuzi na kondoo huchungwa mbali sana na maeneo ya kilimo na kwa hiyo, haingekuwa sahihi kufanya sampling ya mifugo wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali, ifanye juhudi za makusudi kufanya sensa (total count) mapema iwezekanavyo ili idadi kamili ya mifugo nchini ijulikane. Kwa kufanya hivyo, kutatuwezesha kupanga mipango madhubuti na makini ya kuiendeleza Sekta hii.

**MHE. ERENEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono shughuli za Wizara hii kwa asilimia mia moja. Pia, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kufuatilia ahadi walizoahidi kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa katika kipindi cha Bajeti cha mwaka jana 2004, Mheshimiwa Waziri alitamka wazi kuwa Geita itapata maji kabla ya kumalizika mwaka 2005. Ahadi hii iliwafurahisha sana wananchi wa Geita na Vitongoji vyake, Wizara iliamua kutoa kiasi cha Sh.5,000,000/= kwa ajili ya upembuzi yakinifu na kazi hiyo imeshafanyika kwa hilo naipongeza Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo ni muda aliomweka Waziri wa mwaka 2005. Je, kweli Mji wa Geita utapata maji? Kama kweli utapata maji hayo kutoka Ziwa Victoria, itatumia miujiza gani kuyafikisha Mjini? Kwa kuwa inaonyesha hakuna dalili za kufika kwa maji na katika Bajeti hii sioni kiasi chochote kilichotengwa kwa ajili ya kuupatia Mji wa Geita maji.

Je, ahadi ya Waziri ilikuwa ya kuwatuliza wananchi wa Geita au alikuwa na lengo gani? Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, awaeleze wananchi wa Geita lini atapeleka maji ya ziwa Mjini Geita.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kuandaa Bajeti makini na yenye utendaji wa hali ya juu. Hakika Mheshimiwa Waziri Lowassa amekuwa ni mfano wa kuigwa katika uchapakazi wake mkubwa. Aidha, sambamba na hotuba hii, wananchi wa Jimbo la Busega, wamempatia pongezi kubwa kwa jitihada za Wizara yake katika kuwasaidia kupata miradi ya maji ya Nassa, Kalemera na Malambo ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo la Busega lina matatizo makubwa sana ya maji, namwomba Mheshimiwa Waziri, katika Bajeti hii asaidie sana kupatikana kwa fedha Sh.20,000,000/= kwa ajili ya mradi wa maji wa Nyashimo. Mradi huu ulishawekewa miundombinu ya bomba lakini pampu ya maji imezeeka sana na haifanyi kazi. Hivyo fedha hizi zijenge Pump House na kununua pampu mpya ya umeme ili kuwezesha kusukuma maji. Umeme tayari upo mpaka eneo la Pump House.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, bado namwomba Mheshimiwa Waziri, asaidie pia kutenga fedha kwa ajili ya malambo ya Nyaluhande, Mkula na Nyangili kwani hali ya maji bado ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuwapongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa uchapaji kazi mahiri na makini uliowezesha Wizara hii kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na timu yao nzima kwa kazi kubwa wanayoifanya kuipatia nchi yetu maji safi na salama. Pamoja na pongezi hizo, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *City Water*, ningependa Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho ya hotuba yake atoe ufafanuzi wa kina kuhusu Mkataba uliokuwepo/ulioko kati ya Serikali na City Water. Je, ni nini hasa athari ya kesi iliyofunguliwa London na *City Water* kwa Serikali na kwa nchi yetu kwa ujumla? Kuna taarifa kuwa Serikali kwa kuvunja Mkataba haikufuata vipengele vilivyowekwa katika Mkataba huo ambapo Serikali yetu iliuweka saini.

Kwa kuwa Wilaya ya Karatu, yenye Vijiji 45 kwa hivi sasa ina miradi ya maji katika Vijiji 35 kwa msaada wa wafadhili mbalimbali na kwa kuwa kila mara tumekuwa tukifanya jitihada za kupata uongozi wa Wizara kuja kufungua miradi hiyo, lakini jitihada hizo hukwamishwa na Viongozi wa Serikali Wilayani, jambo ambalo hata mwaka huu Naibu Waziri alipotaka kuzindua akaambiwa kuwa ataalikwa na DED na hadi leo hakuna mwaliko na akiambiwa aalike hachukui hatua:-

Je, Wizara kupitia Bunge hili iko tayari kuwapongeza wafadhili wetu wakuu yaani *MISEREOR* ya Ujerumani, *ISF* ya Spain, Caritas Australia, *CRS* ya Marekani, Ubalozi wa Uholanzi kwani pamoja na itikadi ya siasa waliosaidia ni Watanzania na misaada yao imesaidia sana kupunguza mzigo kwa Serikali yetu?

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na pia nampongeza Waziri Edward Lowassa, kwa kazi nzuri hasa baada yeye kuingia Wizara hii. Wizara imebadilika kwa uongozi wake akisaidiana na Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, alinipatia visima viwili Galula, Mbuyuni viwili na Mbangala kimoja. Tayari vimechimbwa, lakini bado kuwekwa pampu. Namwomba Waziri asaidie juu ya jambo hilo kwani ni kero kubwa sana hata Wapinzani wanalisemea sana. Nilipokwenda Wizarani walinieleza tayari wametenga Shilingi milioni 20 kumalizia ile kazi na nilitegemea sasa ingekuwa tayari wameshafunga hizo pampu. Sijui kinachoendelea. Naomba Waziri atoe amri visima vile vimalizike wakati huu huu wa sasa kama pesa ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa katika Kata ya Mkwajuni Makao Makuu ya Jimbo, lakini visima vya maji vilivyopo pale Kijiji cha Mwambeni, ambao nao hawana maji. Naomba Wizara isadie juu ya jambo hili. Vijiji vya Wanzani na Ifuko vilikuwa na maji lakini mpaka sasa maji hayatoki, mradi mzima una matatizo. Kimsingi, naomba wananchi wachange ili mradi ule urudie hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo Vijiji kama Patsmela, Mwembeni, Mbala, Iseche, Namkukwe, Kininga, Mheza, vina matatizo makubwa ya maji. Naomba angalau kisima kimoja kimoja katika kila Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri, anifahamishe kuhusu mradi wa EU ambao ulikuwa usaidie kujenga mradi wa maji wa Vijiji vya Kininga na Kampalala ambao unatoa maji toka mlima wa Kwimba. Mradi huu kama umefutwa utakuwa

umepoteza matumaini ya kupata maji Vijiji vya Kata ya Kapalala, Vijiji vya Udinde, Kapalala, Kininga na Lukwa. Hivi sasa mambo ni magumu sana kwa wanavijiji hawa.

Namwomba Waziri asaidie kupata maelezo Wilayani, nini kimekwamisha mradi huu. Wananchi wanalalamikia sana ukiwa wa mradi huu. Bado tumepata matatizo makubwa sana juu ya magomvi ya wakulima na wafugaji. Tatizo la msingi ni uhaba wa malambo licha ya wafugaji kuhamasishwa. Fedha tunazopata hazitoshi kupata malambo ambayo yangeweza kukidhi hali ya wingi wa mifugo huko Wilaya ya Chunya. Tunaiomba Wizara iongezee budget juu ya Jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi niliyopewa ya kuchangia hoja ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ambayo naiunga mkono asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Lowassa kwa hotuba yake ya kina na maelezo mazuri sana. Pia, nawapongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Diallo, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Dawasa na Viongozi wapya wa *DAWASCO* ambao sasa wamechukua nafasi ya *City Water* kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar es Salaam unakabiliwa sana na matatizo ya kukatikakatika kwa (upatikanaji wa) maji ya bomba. Hii imeathiri sana afya za wananchi. Kwa takribani miaka mitatu sasa nimeiomba Wizara *(City Water) DAWASA* kutatua tatizo la ukosefu wa upatikanaji wa maji safi na salama kwenye maeneo au Kata zifuatazo:-

Kata ya Mwananyamala eneo zima la kila upande wa Barabara ya Kawawa Mkwajuni, Mafere, Moscow pazi, Komakoma, Kinondoni Mjini na Kinondoni Shamba pamoja na eneo la Kumbukumbu, Kata ya Ndugumbi eneo lote la Barabara ya Kagera, Kagera Mikoroshoni, Kata ya Tandale, Tandale Sokoni kwa Tumbo, Kata ya Kijitonyama, Kata ya Mzimuni na Kata ya Magomeni-Suna A,B,C.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kata ya Makumbusho nimeiomba Wizara *(DAWASA)* na iliyokuwa *City Water* zaidi ya mara sita ku-extend bomba la maji linalotoka Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, kwenda mpaka eneo la Shule ya Mwanyanamala Kisiwani kuwa liendelee (*extend*) mpaka Mwananyamala Kisiwani proper kwenye watu na pia liongezwe hadi Mchangani karibu na Msikiti ili iwe rahisi na nafuu kwa wananchi kuvuta hayo maji hadi majumbani mwao.

Naomba tena Serikali, *DAWASA* na sasa *DAWASCO* wanisaidie kulimaliza hilo tatizo pamoja na kuboresha upatikanaji wa maji kwenda Kata nilizozitaja hapo juu, yaani Mwananyamala, Tandale, Ndugumbi, Hananasifu Kinondoni, Kijitonyama, Mzimuni na Magomeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natambua sana juhudi za Wizara, DAWASA na Inshallah *DAWASCO* za kuhakikisha kwa upatikanaji wa maji safi na salama unaboreshwa Jijini Dar es Salaam na hasa Jimbo la Kinondoni. Naafiki mia kwa mia ombi la Wizara la kupewa hizo fedha kwa ajili ya kutimiza malengo yake ya mwaka huu wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani sana kwa Wizara ya Maendeleo ya Maji na Mifugo, hususan kwa kutenga fedha kwa ajili ya kufufua mradi wa maji ya Chankorongo–Nyakagomba. Naomba mradi huo upanuliwe uweze kufikia Vijiji vya Katoro na Kasema ikipitia Gereza la Kilimo la Butundure. Naomba pia kisima cha Katoro/Buseresere ambacho Mheshimiwa Waziri aliahidi kwa wananchi bado haijakamilika. Naomba kikamilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Nyakagomba ulianza mwaka 1976 mpaka leo haujakamilika. Naomba ukamilishwe. Ni vyema ningefahamishwa mwaka huu mradi huo umetengewa pesa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Napongeza kwa dhati kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii katika kuendeleza Sekta ya Maji na Mifugo. Hongera.

Napenda kuwasilisha matatizo yafuatayo ili yafanyiwe kazi. Kwanza, tatizo la Maji katika Mji wa Manyoni. Nashukuru Wilaya ya Manyoni kuingizwa katika mpango wa Maji kupitia mkopo wa Benki ya Dunia. Hivi sasa Vijiji 10 vya awamu ya kwanza maandalizi ya kuchimba visima yameanza. Lakini Mji wa Manyoni una tatizo kubwa sana la maji. Msukumo wa Wizara unahitajika ili kusaidia kupatikana maji Mjini Manyoni.

Kukamilisha Bwawa/Lambo la Mwanzi (Manyoni Mjini) katika kutafuta vyanzo vya maji kwa Mjini Manyoni, naomba fedha toka Mfuko wa TZM/Japan Ford Counter Fund na tulipewa Shilingi milioni 56, kuanzisha Bwawa la Mwanzi. Mradi huo bado haujakamilika.

Naleta ombi kwa niaba ya Halmashauri Wizarani la Shilingi milioni tatu ili kukamilisha mradi huu, lakini bado majibu hayajaja kule katika Halmashauri. Tunaomba Wizara isaidie kukamilisha bwawa hilo ili kupunguza kero ya Mji wa Manyoni Mjini. Naridhia kutoa shukurani kwa kazi nzuri na msaada wa ujenzi wa mabomba mnaotupatia. Vile vile, katika hotuba yenu, Wilaya ya Manyoni ni moja ya maeneo mliyoyataja katika upanuzi wa huduma za maji mwaka 2005/2006. Kwa niaba ya wananchi wa Manyoni tunatoa shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Naunga mkono hoja. Pongezi kwa utendaji mzuri wa Wizara kwa kipindi chote cha miaka 10 na taarifa ya Wizara inajieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu ni miongoni mwa maeneo yenye ukame wa mara kwa mara hususan Tarafa ya Ismani. Tarafa ya Ismani haina mito wala mabwawa, lakini eneo hilo lina wafugaji wa makabila mengi sana wakiwamo Wamasai. Naomba Wizara ifikirie kunipa angalau Shilingi milioni 30 ili tuchimbe bwawa litakalokuwa Kijiji cha Igula. Bwawa hili litatumika kwa mifugo ya Vijiji vya Ngano, Nyang'oro, Kihorogola, Mangawe na Ismani. Kijiji hicho kipo katikati, hivyo bwawa hilo moja litakuwa la msaada sana kwa Vijiji sita.

Aidha, uwezo ukiwepo, naomba kisima cha maji kimoja Kijiji cha Kimsude na Kijiji kingine cha Izazi. Naunga mkono hoja.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi kuchangia hoja hii. Naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu na Wizara yake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyoshughulikia matatizo ya maji katika Jimbo langu. Sasa hivi matatizo ya maji katika Vijiji vya Jimbo langu ni dogo sana na hasa pale ambapo wataalam walishindwa kupata chanzo cha maji, hivyo walishindwa kuchimba visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mradi wa kuleta maji Mjini toka bwawa la Itamuka, naomba kasi iongezeke kwani tangu mradi uanze kushughulikiwa ni muda. Je, ni matatizo gani ambayo bado yanazuia au kuchelewesha mradi huu? Ni fedha toka kwa Wafadhili au ni taratibu za manunuzi ndio bado zinachelewesha kazi kuanza.? Wananchi wanaopitiwa na bomba walishataarifiwa na walishahama na wengine msimu huu hawakuweza kulima mashamba yao kwa kuhofu baadaye kuharibiwa mashamba yao, lakini bado hawaoni kazi ikianza, wanatusumbua sana. Naomba kazi hiyo ianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya mwaka jana 2004/2005 nilimjulisha Mheshimiwa Waziri katika uchangiaji kuwa vipo Vijiji vitatu ambavyo kwa nguvu zao walichimba mabwawa madogo. Lakini kwa vifaa duni na fedha kidogo, mabwawa hayo hayaweki maji ya kutosha. Nilimwomba Waziri, Wizara yake itusaidie kutupa msaada wa kuunga mkono nguvu za wananchi hao. Je, Waziri anakumbuka hilo? Vijiji hivyo ni Manga - Kata ya Mtipa, Mungumaji - Kitongoji cha Kititimo katika Kata ya Mungumaji na Mtamaa - Kata ya Mtamaa. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kama anaweza kusaidia Vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado suala la majosho ya kuogeshea mifugo ni tatizo sana. Usimamizi unaotakiwa kufanywa na Vijiji ni hafifu kwa sababu zifuatazo:- Kwanza, uhaba wa wataalamu wa mifugo, ughali wa dawa za kuogesha na kutokuwa na maji sehemu nyingine karibu na majosho hayo. Hivyo, bado tatizo la magonjwa ya

mifugo yatokanayo na kupe yanaendelea kusumbua na hivyo kuharibu zao la mifugo. Je, Serikali inachukua taratibu gani za kurekebisha matatizo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja ya Waziri asilimia mia moja.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha manung'uniko yangu kwa Wizara hii hasa kuhusu maji Wilayani kwangu na Jimbo langu la Mbozi Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu ndilo pekee lenye uzalishaji mkubwa wa zao la kahawa ambalo huchangia kwa kiwango kikubwa uchumi wa Taifa letu. Usafi wa kahawa bora hutegemea usafishaji wake kwa maji safi. Nimeomba mara nyingi Kata ya Iyula, Msia, Igamba, Isansa, Itaka na Nambinzo, kwa muda wote huo, nimeahidiwa kuchimbiwa visima ambavyo vimeshindwa kukidhi haja na lengo lililotarajiwa. Visima vingi hukauka maji wakati wa kiangazi na ndio wakati wa kusafisha kahawa.

Kumekuwa na kuhangaika sana na miradi ya maji ya mtiririko yalionyesha kutatua tatizo hili katika Kata ya Iyula kwa msaada wa dhehebu la KKKT Kanda ya Konde. Wananchi walihamasishwa na kuchangia gharama za upembuzi wote na kuukamilisha. KKKT waliahidi kuchangia Shilingi milioni 800 kiasi ambacho ni nusu ya gharama. Wizara iliombwa kuchangia sehemu iliyosalia Shilingi milioni 800. Wizara ilikubali na Waziri aliahidi World Bank itachangia kiasi hicho.

Cha kushangaza, hakuna kinachosemwa katika bajeti hii. Wananchi wamehamasishwa kuanzisha Mfuko wa Maji kwa kila Kijiji (Iyula, Iwowa, Idiwili, Welui, Ruanda, Myovizi na Nsenjele). Hali hii haieleweki na wananchi wa Vijiji hivyo. Naomba maelezo, maana Waziri analijua suala hili kwa kuwa ni la muda mrefu.

Pili, kama ni suala la visima, basi viandaliwe visima virefu vitakavyowezesha maji kuwepo hata wakati wa kiangazi.

Tatu, sehemu zinazofanyika minada ziangaliwe kama Kamsamba, Msangano na Iyula ili majosho yawepo na mifugo ipate kuhudumiwa. Aidha, utaalam wa vifaa kwa mifugo ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa maana kwamba nitapata maelezo ya kueleweka.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye nguvu na mwenye hekima, ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini na yeye ndiye aliye juu, mkuu, mwenye uwezo wa kuweka Serikali za wanadamu na Mabunge ya Mataifa, kwa kutupa uhai na afya njema tukaweza kukutana hii leo ndani ya jengo hili kutekeleza wajibu wetu.

Kadhalika nikupongeze wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43 (5) (b) (c) toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuungana na wenzangu na kwa niaba ya wananchi Jimbo langu la Utaani, nitoe rambirambi zetu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliotangulia mbele ya Haki. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hawa Peponi. Amina.

Aidha, napenda kuwashukuru wale wote ambao waliungana nami na kunifariji kutokana na msiba wa kufiwa na Mjomba wangu, Sheikh Salim Bin Ali Bin Salim na ndugu yangu Asha Binti Abbas Jecha, waliofariki hivi karibuni. Nasema ahsanteni sana. Mwenyezi Mungu awape Marehemu hawa makazi mema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwapongeza wale wote ambao wameteuliwa na Vyama vya Upinzani kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wagombea wenza. Kadhalika nimpongeze Mheshimiwa Maalim Seif Shariff Hamad, Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi CUF kwa kuteuliwa kuwa Mgombea wa nafasi ya urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Nawatakia wagombea wote wanaoteuliwa na Vyama vyao waendeshe Kampeni zao katika muda muafaka, kushindana kwa nguvu za hoja kwa namna ya kiustaarabu, kiungwana bila kutumia hila wala ghilba na kwa kuzingatia kudumisha amani, utulivu na upendo uliopo miongoni mwa Watanzania ili hatimaye tuendeshe uchaguzi ulio huru na wa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni muhimu mno kwa maisha ya viumbe. Mfumo wa maisha wa viumbe haukamiliki pasi na kuwepo maji. Mwenyezi Mungu amekuwa anawaruzuku waja wake neema hii ili kuendeleza mfumo wao wa maisha.

Ushahidi wa maneno haya ni pale Mwenyezi Mungu alipotuambia katika Quaran Sura ya 16 aya 10 na ninanukuu: “Yeye ndiye anayekuteremshieni maji kutoka mawinguni, kwa hayo, mnapata kinywaji na kwa hayo inaota mimea ambayo humo mnalisha wanyama.” Mwisho wa kunukuu.

Aidha, kitabu cha Nabii Yeremia 6:24 kinatuambia na ninanukuu: “Wala hawasemi moyoni mwao, basi na tumche Bwana Mungu wetu, aletaye mvua; mvua ya mwaka na mvua ya vuli, kwa wakati wake na kutuwekea juma za mavuno zilizoamriwa.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni kiungo muhimu sana kinachochangia kwa kiasi kikubwa kuondoa umaskini kutokana na kutoa nishani ya umeme, kuwa na usalama wa chakula, maendeleo ya viwanda, madini, kustawisha mazingira na kwa maana hiyo kuendeleza uhai wa viumbe. Kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba wakati wote maji safi na salama yanapatikana kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikubali na nikiri kwamba Serikali imekuwa inajitahidi sana kuondoa matatizo ya upatikanaji wa maji safi na salama. Mradi wa Maji wa Chalinze, ule wa Ziwa Victoria na mengineyo ni miongoni mwa ushahidi wa hayo.

Lakini pia tukiri kwamba huduma za kuwapatia maji safi wananchi waishio Vijijini haijapiga hatua kubwa sana. Tegemeo lao la upatikanaji wa maji kwa watu wengi wa Vijijini ni maji ya madimbwi, visima vifupi, mito, mabwawa na malambo. Vyanzo hivi vya maji mara nyingi havikidhi mahitaji yao ya kila siku hasa nyakati za kiangazi. Aidha, nyakati za mvua vyanzo hivi huchafuka kwa taka na matope na hivyo kuhatarisha afya za watumiaji.

Pamoja na ukweli kwamba Tanzania ni nchi ambayo imejaaliwa na rasilimali ya maji kwa wingi mno na yanayopatikana kirahisi kutoka katika vyanzo vyake, takriban zaidi ya asilimia sita ya eneo la nchi yetu ni maji, lakini bado mwanamke wa Kitanzania kwa wastani hupoteza masaa manne akitafuta maji. Mahitaji ya maji huongezeka sambamba na ongezeko la watu, shughuli za uzalishaji viwandani, kilimo na kadhalika. Hivyo basi, usimamizi madhubuti wa rasilimali hii ni muhimu sana kuondoa umaskini, kuboresha afya za jamii, kuhakikisha usalama wa chakula, maendeleo ya kiuchumi na uendelevu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Wizara, kasi ya usambazaji wa maji hasa Vijijini ni mdogo kiasi kwamba imekuwa ni kero kwa wananchi wengi. Inakadiriwa kuwa ni asilimia 46 ya wananchi waishio Vijijini hawapati huduma ya maji safi na salama. Uchimbaji wa visima vifupi bado haujawa suluhisho la kudumu la tatizo la maji. Ni dhahiri kuwa, hakuna mwekezaji atakayewekeza kiwanda Vijijini ikiwa tatizo la maji halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Kukosekana kwa viwanda Vijiji kunaathiri sana kukua kwa uchumi na upatikanaji wa ajira na hatimaye ni kuongezeka kwa umaskini. Huduma ya maji safi na salama Mijini, nayo imekumbwa na matatizo kadhaa, pamoja na kwamba inakisiwa kuwa asilimia 73 ya wakaazi wa Mijini wanapata huduma hiyo.

Kwa ujumla tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama linatokana na sababu kuu nne. Kasi ya ongezeko la watu, uharibifu wa vyanzo vya maji, uchafuzi wa mazingira na uchakavu wa miundombinu ya kusambazia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za kufanyia ukarabati miradi ya maji Vijijini zimekuwa ni kwa awamu kutokana na ufinyu wa bajeti kutosheleza mahitaji makubwa ya kazi hiyo. Mingi ya miradi hiyo imechakaa kwa kuwa imejengwa zamani, pia kukosa matengenezo ya mara kwa mara na kutowashirikisha kikamilifu wananchi wanyewe katika ujendeshaji wa miradi hiyo.

Aidha, matatizo mengine ni pamoja na kukosekana kwa mikakati madhubuti na uratibu juu ya mpango wa kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua kwa matumizi ya binadamu.

Pamoja na kubinafsisha baadhi ya Mamlaka za Maji, mpango huu bado mpaka sasa haujafanikiwa kuondoa kero ya upatikanaji wa maji. Maji hayawafikii walengwa wengi kama inavyotarajiwa na hata hao wanaoyapata, huwa ni kwa baadhi ya wakati na wakati mwingine sio safi. Wananchi bado wanalazimika kuingia gharama kuchemsha maji hayo au kutia dawa ya kuulia vijidudu.

Maji ya visima yanayotumiwa na wananchi wengi sio safi na salama, kwani visima vingi ni vifupi na vimechimbwa kwenye maeneo yenye misongamano mikubwa ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwepo kwa miundombinu chakavu ya maji taka au kutokuwepo kabisa miundombinu hiyo, maji mengi ya visima huchanganyika na vinyesi hasa wakati wa mvua. Kutokana na hali hii, kipindupindu ni ugonjwa wa kudumu hapa nchini.

Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kupanua wigo wa uwekezaji katika ujenzi na upanuzi wa miundombinu ya maji safi na maji taka Mijini.

Lakini ni vyema ikatoa kipaumbele kwa Mashirika na Makampuni ya Kitanzania, kuepuka Wawekezaji wakorofi kutoka nje ya nchi ambao hatimaye wanaweza kuingiza mkenge kama ilivyofanya Kampuni ya *City Water.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hatua iliyochukuwa kukatisha Mkataba na Kampuni ya *City Water* kutokana na utendaji mbovu wa majukumu yake ya kuwapatia maji safi wananchi wa Dar es Salaam na baadhi ya sehemu za Mkoa wa Pwani. Ni vyema tukalichukulia kuwa hili ni funzo kwetu na sasa tuwe makini zaidi katika kutafuta wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Kambi ya Upinzani tutakapopata ridhaa ya wananchi kuongoza nchi hii, katika hatua za kuondoa kero ya upatikanaji wa maji safi na salama na uondoaji wa maji taka katika Miji yetu, tunatarajia kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kazi ya usambazaji wa maji tutaweka chini ya Mashirika ya Umma ambayo yanaweza kuingia ubia na Makampuni yenye uzoefu wa kujenga miundombinu ya maji na kusimamia usambazaji.

Pili, Mashirika hayo yataundwa kila kanda ili kupata wawekezaji wa uhakika na wenye uwezo.

Tatu, Mashirika haya yataingia Mikataba na Serikali itayowawajibisha kusambaza maji Mijini na Vijiji katika uwiano ulio sawa. Aidha, Mikataba hii itakuwa wazi na kwamba Serikali haitavumilia ukiukwaji wa namna yoyote ya masharti ya Mikataba itayowekwa.

Nne, Makampuni yanayoshughulika na uchimbaji wa visima na yale yanayotengeneza maji ya chupa yatakuwa na haki ya kuendelea na kazi zao bila

kuathiriwa na Mikataba baina ya Serikali na Makampuni juu ya usambazaji wa maji ya bomba.

Tano, Mabonde ya asili yenye uwezo wa kutumika kama mabwawa ya kuhifadhia maji yatatayarishwa ili mito ielekezwe kwenye mabonde hayo au mabwawa badala ya maji mengi kupotea baharini.

Sita, tutahakikisha maji kutoka katika maziwa yanatumika ipasavyo kwa kuyaelekeza nchi kavu kwa njia ya mifereji na kusambazwa katika mabonde na mabwawa ya maeneo kame. Kadhalika, maji ya mvua ambayo hugeuka kuwa mafuriko na kuleta maafa yanaweza yakabadilishwa mwelekeo kwa kujenga mikondo na mifereji itakayoelekea kwenye mabonde au mabwawa.

Saba, Serikali itafanya kazi ya kusambaza maji, lakini wananchi watapewa jukumu la kuyamiliki na kuyatunza katika utaratibu wanaojipanga wenyewe. Miradi mikubwa ya maji Vijijini itakabidhiwa kwa wananchi wenyewe ili waweze kuisimamia, kuiendesha kwa kutumia vyombo vitavyotambulika kisheria na vitakavyoundwa na wananchi kwa ridhaa yao wenyewe.

Aidha, wananchi watatunga sheria ndogo za utumiaji na utunzaji wa maji yao na vyanzo vyake, wataalamu watahusika pale tu panapohitajika ufundi na ushauri.

Kwa kuzingatia umuhimu wa maji kwa maisha ya binadamu na vyote vinavyomzunguka, tutaipa kipaumbele na kuiongeza Bajeti ya Sekta ya Maji iwe si chini ya asilimia 10 ya bajeti yote ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina wajibu mkubwa wa kuwaandaa vijana wetu kuwapa taaluma ya maji ili kuwawezesha kuchukua nafasi za ajira kwenye Mashirika na Makampuni yanayozalisha na kusambaza maji.

Aidha, Serikali inashauriwa kukiimarisha zaidi Chuo cha Maji cha Rwegarulila na kuanza kuchukua hatua za kukipandisha hadhi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sambamba na hatua hiyo, taaluma iwe imetolewa Shuleni juu ya uvunaji, utumiaji na utunzaji wa maji. Wanafunzi wataweza kujifunza mapema na kupata mwamko wa kuona umuhimu wa kutunza mazingira na vyanzo vya maji, hatua itayopelekea kuimarika upatikanaji wa maji ya kutosha nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Maendeleo ya Mifugo, kwa mujibu wa takwimu zilizopo imechangia asilimia 6.1 ya Pato la Taifa. Aidha, kiasi cha asilimia 40 ya kaya za wakulima ni wafugaji na kwa hiyo, ni chanzo cha upatikanaji wa ajira nchini. Ni dhahiri kwamba Sekta hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa.

Tanzania ina jumla ya ng'ombe 17.7, mbuzi milioni 12.5, kondoo milioni 3.5, ng'ombe 880,000 na kuku milioni 47. Huu ni utajiri mkubwa wa nchi, kwani licha ya kuchangia

pato la Taifa, huwapatia wananchi ajira, mbolea na chakula bora na hivyo kuboresha afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kushangaza pamoja na wingi wa mifugo tuliyonayo, mwamko wa ulaji wa mazao ya mifugo ni mdogo mno na hasa ukizingatia viwango vinavyopendekezwa kimataifa. Kwani kwa wastani Mtanzania kwa mwaka hula kilo 12 za nyama, mayai 54 na maziwa lita 39.

Viwango vinavyopendekezwa kwa mwaka na *FAO* kwa afya ya mwanadamu ni kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300. Tunaweza kuona ni kiasi gani sisi Watanzania tulivyo nyuma katika matumizi ya rasilimali zetu za mifugo. Hii ni kasoro kubwa na hakuna budi tubadili mifumo yetu ya chakula kwa manufaa ya afya zetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa Sekta ya Mifugo kwa mwaka katika nchi zilizo chini ya Jangwa la Sahara ni wastani wa asilimia 2.2. Hiki ni kiwango kidogo sana ukilinganisha na mahitaji yanayotokana na ongezeko la watu la asilimia 2.8 kwa mwaka. Nchi hizi zina wajibu wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo ili kukidhi mahitaji ya mwanadamu.

Hapa nchini petu hatua kadhaa zinachukuliwa ili kuleta maendeleo ya mifugo. Mkazo zaidi umewekwa kuongeza uzalishaji, utafiti, kudhibiti maradhi ya mifugo na kukuza soko la mazao ya mifugo. Mafanikio yanaonekana na hii ni kutokana na juhudi na ushirikiano baina ya Wataalam na Watendaji.

Programu mbalimbali zimeandaliwa kwa lengo la kuinua kipato cha mfugaji na kujiondolea umaskini. Miongoni mwa hatua zinazochukuliwa ni pamoja na:-

- Kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa kuboresha ng’ombe wa asili;
- Kuongeza ubora wa malisho;
- Kuzalisha mitamba bora wa maziwa na kuwapatia wafugaji;
- Kuendeleza vyanzo vya maji, kujenga mabwawa na kuchimba malambo kwa ajili ya upatikanaji maji;
- Kukuza taaluma ya mifugo kwa Watendaji na Wafugaji;
- Kudhibiti maradhi ya mifugo;
- Upatikanaji wa vifaranga bora wa mayai na nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kwamba vifaranga milioni 29.9 vimezalishwa mwaka huu unaomalizika na uzalishaji wa mayai umeongezeka kufikia milioini 1,800, ukilinganisha na milioni 910 mwaka 2003/2004.

Maziwa yameongezeka kutoka lita bilioni 1.18 mwaka 2003/2004 hadi kufikia lita bilioni 1.38 mwaka 2004/2005. Uzalishaji wa nyama nao umeongezeka kutoka tani 348,000 mwaka 2003/2004 kufikia tani 378,509 mwaka 2004/2005.

Maendeleo haya ni ya kupongezwa. Ni vyema basi nikachukua nafasi hii kuwapongeza Viongozi na Watendaji wote wa Wizara hii kwa juhudi kubwa wanayoichukuwa katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maendeleo yaliyopatikana, wafugaji bado wanakabiliwa na matatizo kadhaa ambayo kwa namna moja au nyingine yanawakwaza katika kuleta maendeleo ya ufugaji hapa nchini. Miongoni mwa matatizo hayo ni pamoja na:-

- Madawa ya mifugo, yamekuwa hayapatikani kwa wakati hasa Vijijini na mara nyingi yanakuwa ghali sana, matokeo yake ni kuenea kwa magonjwa mbalimbali na hasa ya milipuko;

- Hakuna utaratibu ulioandaliwa ama unaeleweka wa kuwapatia mikopo wafugaji. Aidha, wafugaji wengi hawana uwezo wa kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha kutokana na masharti magumu yanayowekwa. Kadhalika kwa bahati mbaya Sekta hii haivutii wawekezaji binafsi kutokana na gharama kubwa za uwekezaji;

- Upatikanaji maji ni tatizo hasa katika sehemu kame za nchi. Aidha, mabwawa na malambo ni machache na mengi ni ya kina kifupi;

- Kilio cha wafugaji cha kutaka paundwe Bodi ya kuendeleza ufugaji nchini bado hakijasikilizwa; na

- Tafiti nyingi zinazofanywa hazilengi katika kutatua matatizo halisi ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya upinzani inaamini kabisa kuwa chanzo cha haya yote ni kutokana na:-

- Serikali kutosimamia kwa makini sheria ndogo zilizowekwa ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa nchini;

- Uhaba wa viwanda vya kusindika mazao yatokanayo na mifugo, masoko ya uhakika na kukosekana miundombinu ya kuwezesha kuuza bidhaa za mifugo humu nchini na soko la kimataifa; na

- Lakini kubwa zaidi ni ufinyu wa bajeti. Fedha zinazotengwa kwa matumizi ya Wizara hii hazitoshelezi kulingana na umuhimu wa maendeleo ya Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu itakapoingia madarakani Novemba mwaka huu 2005, inakusudia kufanya yafuatayo:-

- Bajeti kwa ajili ya miradi na shughuli za maendeleo ya Sekta ya Mifugo itaongezwa kukidhi mahitaji yake;

- Vivutio mbalimbali vitawekwa ili kuvutia wawekezaji kuwekeza katika Sekta hii;

- Maeneo maalum ya ufugaji yatatengwa ili kupunguza tatizo la wafugaji kuhamahama kunakosababisha uharibifu wa mazingira, migogoro kati ya wafugaji na wakulima na kuenea kwa magonjwa ya mifugo;

- Tutaanzisha Bodi ya Mifugo nchini itakayopewa jukumu la kuendeleza mifugo ikiwa ni pamoja na kuanzisha Taasisi za Fedha zitakazowawezesha wafugaji kupata mikopo yenye masharti nafuu;

- Sheria zilizotungwa zitasimamiwa ipasavyo na kwa umakini katika utekelezaji wake ili pamoja na mambo mengine, kudhibiti kuenea kwa maradhi ya mifugo;

- Viwango vya elimu kwa Watendaji vitaendelezwa ili kuongeza tija kwa kuboresha uelewa na uwezo wao; na

- Huduma za ughani, upatikanaji wa madawa na pembejeo nyingine utaimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nidhukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Edward Baraka Ngoyay Lowassa - Mbunge na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Anthony Mwandu Diallo - Mbunge na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza wajibu wao na kusukuma mbele maendeleo ya Taifa hili. Naamini bila mshikamano ulio madhubuti, maendeleo haya yasingeweza kupatikana. Ninawaomba wazidishe juhudi na ari ya kazi ili kuongeza ufanisi na tija katika kazi zao.

Mheshimiwe Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru kwa namna ya pekee, wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo na Ardhi na hasa Mheshimiwa Aliachim Simpasa - Mwenyekiti na Mheshimiwa Alhaj Shawej Bin Abdallah - Makamu Mwenyekiti, kwa kunipa ushirikiano wa hali ya juu katika muda wote. Walikuwa wananithamini kama mwenzao, kadhalika wamekuwa wanathamini sana mchango wangu ninaotoa katika Kamati.

Nawatakia kila la kheri wateuliwe tena na Vyama vyao kugombea nafasi ya Ubunge katika Uchaguzi Mkuu ujao. Kadhalika niwashukuru ndugu Nenelwa Mwihambi na Hancha Abdallah Makatibu wa Kamati hii kwa kazi yao nzuri waliyokuwa wanaifanya ya kuratibu shughuli za Kamati.

Ama pia nawashukuru Wabunge wenzangu wote kwa maelewano na mashirikiano mazuri tuliyokuwanayo kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru viongozi wote wa Kamati ya Upinzani, wanakambi pamoja na Watendaji wote katika Ofisi yetu kwa jinsi ambavyo tumekuwa tunashiriiana. Kusema kweli wameifanya kazi yangu kama Mbunge na kama Msemaji Mkuu wa Wizara hii kuwa nyepesi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa takriban Wabunge wote tuliomo humu tumeingia kupitia Vyama vya siasa, ni vyema basi nikachukua fursa hii adhimu kuwashukuru kwa dhati kabisa Viongozi na wanachama wa Chama changu, Chama cha Wananchi (*CUF*), kwa kuniteuwa kuwa Mgombea wa nafasi hii ya Ubunge katika Uchaguzi uliopita. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Utaani kwa kunichagua kwa kura nyingi sana kuniwezesha kuwa Mbunge wao na kuwatumikia katika kipindi chote cha Ubunge wangu. Nasema ahsanteni sana kwa uamuzi wenu na kwa ushirikiano mkubwa mliyonipa.

Ni vyema sasa nikachukuwa nafasi hii adhimu kuwashukuru mke wangu, watoto wangu pamoja na familia yangu yote kwa kunivumilia na kuniunga mkono wakati wote hasa ninapokuwa mbali nao nikitekeleza wajibu wangu. Mwenyezi Mungu atawalipa thawabu nyingi juu ya subira yao.

Mwisho kabisa, lakini sio kwa umuhimu, napenda nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mnaifanya kuliongoza Bunge hili Tukufu. Kadhalika, nimshukuru Katibu wa Bunge na Watendaji wote kwa kuweza kubeba majukumu yao vizuri na kuweza kutulea vizuri sisi Wabunge kwa kipindi chote ambacho tumekuwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa dhati kabisa kwa kufanikisha mradi wa maji mkubwa wa kisasa na wa aina yake, mradi wa Chalinze kwa lengo la kusambaza maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kwa yafuatayo:-

Moja, kueneza huduma kwa Vijiji vingi kuliko ilivyokusudiwa kwani maji yanayozalishwa kwa siku mita za ujazo 800 ni mengi zaidi kuliko watumiaji.

Pili, naishauri Serikali kuhakikisha kuwa Mawakala wanakusanya fedha kwenye Vituo vyote, kulingana na uhalisi wa utumiaji wa mita na waweze kuziwasilisha fedha zote kunakohusika ili kukabiliana na ubadhirifu na ujanja ambao unaweza ukaikosesha Serikali mapato na atakayepatikana na ubadhirifu hatua za kisheria zichukuwe mkondo wake.

Tatu, kuhusu mawasiliano kwenye maeneo ya mradi, kwa kuwa mradi unaendeshwa kwa kutumia *remote control sensor* kwenye matanki, hazifanyi kazi kutokana na matatizo ya kiufundi.

Hivyo, ninaishauri Serikali kulipatia ufumbuzi tatizo hilo ili matatizo yasiendelee na kupelekea kutokea kwa tatizo lingine, yaani bora kinga kuliko tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kuupatia mradi huu magari mapya japo manne, kwani magari yaliyopo hivi sasa matano ni chakavu na yanaharibika mara kwa mara na kupelekea gharama ya uendeshaji kuwa juu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yanaendelea kupungua maeneo kadhaa nchini, hii imetokana na watu wengi kuharibu vyanzo vya maji kwa kukata miti na hata kuchoma moto kwenye vyanzo hivyo ambavyo, Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata wanashuhudia uharibifu huo na hakuna hatua zozote wanazozichukua, angalau kutoa taarifa kwenye maeneo husika. Hivyo, ninaishauri Serikali kuwachukulia hatua za kisheria Watendaji wa Vijiji na Kata ambao watavumilia kutoa taarifa za uovu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kuwalinda wafanyakazi wa Wizara hii, na hasa Wataalam na gonjwa hatari la UKIMWI, ninaishauri Serikali kutenga fungu maalum la fedha kuwagharamia wataalam hao kuwachukua wanandoa wao pindi wakipangwa kazi nje ya Vituo vyao vya kazi katika Wilaya, Mkoa au hata nje ya nchi, ambapo imebainika wataalam wengi huambukizwa virusi vya UKIMWI wakiwa safarini wanapopangiwa kazi na kushindwa kuvumilia kutokana na kukaa huko kwa wiki kadhaa bila ya wanandoa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kutenga fedha za posho maalum kwa wafanyakazi wa Wizara hii ambayo itawahamasisha wafanyakazi katika azma ya Serikali ya MKUKUTA kwani mifugo inaendelea kuimarika siku hadi siku, hivyo methali ya mcheza kwao hutunzwa, itekelezwe kwa vitendo kwa wafanyakazi wote wa Wizara hii. Naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia, naomba nimpongeze Mheshimiwa waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote wa Wizara kwa hotuba nzuri iliyochambua kwa kina mambo yote yaliyofanyika mwaka 2004/2005 na mipango inayoeleweka na itakayofanyika katika kipindi cha mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Mbinga Mashariki na mimi mwenyewe binafsi naunga mkono yale yote yaliyowakilishwa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo mimi ninaomba mara nyingi kwa Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya wananchi wangu lakini bado hadi hii leo sijasikilizwa. Nina imani katika bajeti hii maombi yangu yatazingatiwa.

Maombi ya maji Kata ya Kingwikiti, Mtipwili, Chiwanola, Ngumbo na Mbaha na maombi ya maji katika Vijiji vya Kijiji cha Litumbakuhamba, Lundu na maombi ya maji Mji wa Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi haya ni ya siku nyingi sana nimeyafikisha kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuongea na kuandika lakini sijasaidiwa hadi hii leo. Nina matumaini sana katika mwaka huu wa fedha nitasaidiwa. Hivyo, nakushukuru mapema. Ahsante sana.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninatumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Wataalam na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba yake hii nzuri ya kimaendeleo na iliyojaa ufanisi mkubwa kwa Taifa letu hili la Tanzania na kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hotuba hii asilimia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndio muhimili mkuu kwa maisha ya watu, mifugo na hata misitu. Kwa hiyo, ni lazima Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuipatia uwezo wa kifedha ili iweze kutoa huduma nzuri na za uhakika ya maji na kuleta maendeleo makubwa ya mifugo hapa nchini petu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kazi mzuri zinazofanywa na Wizara hii ninaiomba pia kujenga uwezo wa wataalam walio katika Wizara hii ili kuleta maendeleo zaidi kwa Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama maendeleo makubwa zaidi yanaweza kufikiwa hasa katika Sekta ya Mifugo, pia kutachangia maendeleo makubwa ya wananchi na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, ninaiomba tena Wizara hii kuwaelimisha na kuwahamasisha wafugaji nchini hasa kwa wale wenye mifugo mingi sana kuuza baadhi ya mifugo yao ili waweze kujenga nyumba nzuri na za kisasa kwa ajili ya maisha yao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya vitu vinavyompa mtu heshima na utu ni kuweza kumiliki nyumba nzuri ya kuishi ambayo inamwezesha mtu kuwa katika hali nzuri ya afya na maendeleo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tunataka kulichangia ni kuomba Serikali kupitia Wizara hii kupeleka huduma za maji, zile Shule zote ambazo zimejengwa kwa mpango wa MMEM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ubora wa ujenzi wa Shule hizi katika maeneo mbalimbali hapa nchini, kwa kweli zinastahili kupelekewa huduma za maji ambayo yataweza kutumiwa na wanafunzi hao pamoja na wataalam na wananchi ambao wanaishi karibu na maeneo hayo ya Shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ninaiomba Wizara hii ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kufanya utafiti wa kina utakaowezesha yale maji mengi yanayopatikana katika maporomoko mbalimbali hapa nchini yaweze kutumika vizuri kwa matumizi ya watu, mifugo na kwa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri vyanzo na maporomoko haya kuwekewa miundombinu iliyo mizuri na ya kisasa ili kuyatumia maji kwa mafanikio makubwa kwa ajili ya maendeleo ya watu na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo na maporomoko haya ni lazima yasimamiwe vizuri ili yasije yakaathirika kwa kukauka au kuchafuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naitumia fursa hii kupongeza sana Wizara kwa hatua iliyoichukua juu ya Kampuni ya *City Water*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hiyo ambayo ilisababisha kuwepo kwa hofu kubwa miongoni mwetu sisi wengine juu ya hatua hiyo nzito na ya kijasiri na kufanya hofu kuwa ingeleta matatizo katika uamuzi huu ambao tuliona kuwa tungeliingiza Serikali yetu katika mgogoro mkubwa na Kampuni hiyo kitu ambacho kingesababisha kupoteza fedha nyingi zaidi kama Kampuni ingalikuwenda Mahakamani na kushinda kesi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hiyo haikujitokeza na kwa kweli uamuzi huu wa Wizara umeungwa mkono na karibu wananchi wote wa nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipoisoma taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo katika mwaka 2004/2005, ukurasa wa saba, umeeleza juu ya Sekta ya Mifugo. Nikinukuu sehemu hiyo inaeleza kuwa:-

"Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya majosho bado sio nzuri." Naiomba Serikali yetu kuiwezesha Wizara hii kwa kuipatia fedha na vifaa ili Wizara hii iweze kuweka hali nzuri katika majosho yetu yote hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mifugo yetu itakosa majosho, inaweza kuathirika kwa maradhi na hatimaye kufa, jambo ambalo linaweza kurudisha nyuma matumaini na maendeleo ya mifugo yao na hatimaye kuwaingiza katika umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa kama hali ya majosho hayo sio nzuri, Wizara na Serikali yetu itaimarisha majosho haya ili kuleta maendeleo kwa wafugaji wetu nchini na maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hotuba hii asilimia kwa mia. Ahsante.

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo - Mheshimiwa Edward Lowassa kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa mambo mengi. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru na kuipongeza Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa kutuletea mradi wa RWSSP Wilayani Kilosa. Vijiji vya Deshata, Nguyami; Meshagi na Mkalama katika Jimbo langu la Gairo vimepatiwa maji safi na salama kwa kutumia mbinu shirikishi. Kwa niaba ya wananchi wa wanaoishi katika Vijiji hivyo, natoa shukrani za dhati kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna kero kubwa ya maji katika Mji mdogo wa Gairo. Mji mdogo wa Gairo ni miongoni mwa Miji midogo tisa iliyoingizwa katika mradi wa kupatiwa maji kwa utaratibu ule ule shirikishi wa wananchi kuchangia asilimia tano ya gharama za mradi. Tangu mwaka 2002/2003 wananchi walikwishatimiza wajibu wao, lakini mpaka sasa wanangojea, hawaoni dalili ya utekelezaji.

Mradi huu sasa umeingia katika malumbano ya kisiasa. Wapinzani wanaibeza Serikali ya Chama Tawala kwamba imeshindwa kutimiza ahadi yake na wana-CCM nao wametumbukia katika kutoa lawama kwa Serikali na wakati huo huo kumhusisha Mbunge wa Jimbo la Gairo kwamba tumeshindwa kuiondoa kero kubwa ya maji katika Mji mdogo wa Gairo.

Mbaya zaidi wananchi wanahoji imekuwaje Afisa katika Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo anayefanya kazi kwenye Makao ya Wizara Dar es Salaam amechimbiwa kisima kwenye eneo la nyumba yake hapo Gairo na Wakala wa Serikali wa Uchimbaji Visima Ubungo na yeye kufaidika kuwa na maji wakati wananchi wa Mji mdogo Gairo wanaililia Serikali kuwapatia maji bila mafanikio yoyote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamwomba Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo anisaidie, atoe kauli rasmi ya kuelezea hatua iliyofikiwa na Serikali kuiondoa kero ya maji katika Mji mdogo wa Gairo. Wananchi wameanza kukosa imani kwa Serikali na Mbunge wao na hali hii ni ya hatari katika mwaka huu wa Uchaguzi Mkuu. Kauli hiyo itarudisha imani ya wananchi kwa Mbunge wao Dr. Aaron D. Chiduo na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mifugo, mwaka 2003 nilitoa taarifa ya ugonjwa wa mifugo hususan ng’ombe waliokuwa wamepata kizunguzungu na kuzagaa kuelekea upande mmoja na kuchanganyikiwa na kupagawa akili na kupooza na kuanguka. Bahati nzuri wataalam kutoka Kituo cha Uchunguzi wa Maradhi ya wanyama Arusha – *Integrated Tick and Tickboard Desease Control Project Veterinary Investigation Centre* walifanya uchunguzi wao katika Vijiji vya Ndeogomi, Madege, Leshata na Ngayaki katika Jimbo langu la Gairo, Kata ya Chakwale na kugundua kuwa

mifugo hao walikuwa wamepata ugonjwa wa Ormilo *(Borine Cerebral Theikuiosis)* na walitoa maagizo ya tiba iliyofanikiwa. Tunashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi zinazofanywa sasa katika maeneo hayo ni kuchimba majosho ya kuwaogesha mifugo kuua kupe na hivyo kuudhibiti ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kurudia kuiomba Wizara kulihimiza Shirika la misaada la Ufaransa *AfD* ambalo ndilo lilipewa jukumu la kutupatia maji katika Mji mdogo wa Gairo lichukue hatua za haraka lianze kutekeleza mradi huo.

Baada ya maelezo hayo, nahitimisha mchango wangu kwa kuwapongeza Mheshimiwa Edward Lowassa - Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Mheshimiwa Anthony Diallo, Naibu Waziri, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakifanyia kuiongoza Wizara na nawatakia kila la kheri na mafanikio ya ushindi katika Uchaguzi Mkuu ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MIZENGO K.P. PINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mpanda Mashariki kati ya Majimbo matatu yaliyoko Wilayani Mpanda yenye tatizo kubwa la maji. Tarafa ya Meja ya Mpimbwe ina wakazi 76,000. Wengi wao asilimia 75 ni wahamiaji – Wasukuma. Wana mifugo mingi inakadiriwa kufikia 200,000 na wakulima wakubwa na mazao ya mahindi, mpunga, mtama na kadhalika. Tatizo lao kubwa ni ukosefu wa maji safi na salama na malambo ya maji.

Nilikwishawasilisha maombi maalum kwa kuwasilisha andiko *(write-up)* kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na akanijibu na kunipa matumaini makubwa ya kunitafutia ufadhili. Ombi hili limefikia wapi?

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na maendeleo ya mifugo kwamba ni muhimu sana, Wizara hii itambue umuhimu wa majosho ya mifugo kama ni moja ya njia muhimu ya afya ya mifugo mingi kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika hata pia mifugo kama mbwa kwa ajili ya ulinzi wanahitaji majosho. Kwenye maeneo ya Vijijini kwenye Wilaya ya Nyamagana kama vile Bulongwa, Mbolani, Butimba na kadhalika wanafuga ng'ombe wa kienyeji lakini hawana majosho.

Hali kadhalika wafugaji wa kisasa wangefurahia kupata majosho kwenye maeneo yao ingewarahisishia sana ufugaji wao na kuosha mifugo yao badala ya kunyunyizia au kupulizia dawa mifugo yao. Kwa kukutana kwenye josho pia kunachangia nafasi ya kuona mifugo ya wenzao na pia kubadilishana mawazo na uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mwanza Jijini, watu wengi sasa wanafuga mbwa kwa ajili ya ulinzi na pia kuna wanyama waliozoea kuishi nao. Kwa kuwa sasa mbwa Jijini Mwanza wanazidi kuongezeka, suala la josho kwa mbwa ni muhimu sana. Mbwa

tunawafahamu na tabia yao pia tunaifahamu. Kumwosha mbwa na siyo kwenye bwawa la kudumbukia *(dip)* ni vigumu na watu wengi wanashindwa kwa hiyo wanyama hawa wanabakia na viroboto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwaka 2001 tulikuwa na josho la mbwa *(dip)* Mwanza ambalo kwa kweli lilikuwa linafanya kazi nzuri ya kuosha *(dip)* wanyama hao.

Pia, sambamba na joisho *(dip)* hilo, Wizara ilikuwa ikiendesha clinic ya wanyama kwenye eneo hilo hilo. Lakini huduma zote hizi sasa sizioni Jijini Mwanza. Nahisi wakazi wa Mwanza sasa hawana uhakika wa wapi wapate huduma hiyo kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jiji la Mwanza wanashangaa pamoja na mimi mwenyewe, kwa nini huduma muhimu kama hii haiendeshwi na Wizara?

Nina hali ya masikitiko makubwa kwa suala la majosho kwa mifugo yote pamoja na josho (dip) hili la mbwa na clinic ya wanyama vilianzishwa na Serikali ya Wakoloni na kuendelezwa hapa nchini. Kwa nini Wizara hii ambayo tunaiendesha sisi Wazalendo ivuruge huduma hii muhimu? Naomba kupata maelezo na wote wananchi wa Jiji la Mwanza waelewe kwamba hili limekwendaje.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza hotuba hii jinsi ambavyo imetayarishwa vizuri. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Lowassa na Naibu wake Mheshimiwa Diallo pamoja na Wataalam wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia suala la maji katika Wilaya mpya ya Kilolo. Kilolo ni Wilaya mpya, hivyo ninajua kuna mpango mzuri wa usambaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa nafasi hii, nitoe taarifa nzuri toka Kilolo kwamba wenzetu wa Kanisa la Anglican Church wameamua kutusaidia kuleta maji zaidi ya Vijiji vinne mojawapo ikiwa ni Kilolo (Mji). Hivyo, kwa kupitia Bunge hili Tukufu, ningemwomba Mheshimiwa Waziri atoe shukrani kwa kazi hiyo nzuri ambayo tayari imeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa shukrani nyingi kwa wenzetu wa Lutheran Church ambao wamechangia uchimbaji wa visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa pongezi kubwa kwa Wizara hii ambayo mwaka jana 2004 tulitengewa fedha kidogo kwa ajili ya Mji mdogo wa Ilula. Mji huu unakua kwa kasi kubwa, hivyo, hata kila kiasi tunachopata hakitoshi kabisa. Kwa hiyo, ningependa nijue kama mwaka huu tumetengetewa tena. Hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvunaji wa maji ni la muhimu sana, kwani maji yanaendelea kupungua duniani. Hivyo, kama mkakati hautafanywa, hali itakuwa mbaya. Uchimbaji wa malambo utiliwe mkazo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana wafugaji ambao wapo karibu na barabara, sehemu nyingi hakuna alama la vivuko za mifugo, ningeomba Wizara hii iwasiliane na Wizara ya Ujenzi, alama hizo ziwekwe kuondoa usumbufu na ajali. Pia, bei za madawa ya mifugo pia zipewe ruzuku ili bei zipungue kidogo.

Jambo la mwisho, ningeomba ufanyike mkakati mzuri na Wizara zote zinazohusika kwa kushirikiana na Wizara hii kuhusu tatizo la plastics. Mifugo mingi inakufa tena vibaya. Naomba Mheshimiwa Lowasa na Naibu Mheshimiwa Diallo, mrudi tena Bungeni.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri sana na kwa mafanikio makubwa na ya kihistoria yaliyopatikana tangu kuundwa kwa Wizara. Mchango wangu uko katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Bihalamulo ni miongoni mwa Wilaya zilizomo katika mradi wa World Bank, lakini katika utekelezaji wa mradi sikuona ni lini utekelezaji huo utaanza, kwani Wilaya kwa upande wake ilishatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu Mradi wa Maji, Biharamulo Mjini. Napenda kupongeza kwa barua niliyoandikiwa na Wizara ambayo inaeleza utekelezaji wake ukiwemo mradi wa *UN – HABITAT*. Napendekeza wakati Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho atoe maelezo ya kina, kwa ajili ya uelewa wa wananchi na uwekaji wa kumbukumbu sahihi kwenye Hansard.

Matatizo ya maji katika Kata za Nyabusozi na Nyamugogo, amini usiamini wananchi wa Kata hizi hulazimika kuhama wakati wa kiangazi ili kwenda kutafuta maji, hivyo, unatakiwa utafutwe ufumbuzi wa kudumu. Naomba Wizara isaidie pale ambapo uwezakano upo ili kuwanusuru wananchi hawa na adha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa maji wa Ziwa Victoria, kwa kuwa katika Wilaya (Jimbo la Biharamulo-Magharibi) hakuna chanzo cha kuaminika cha maji, nashauri Mradi huu ufanyiwe utafiti wa kina ili utakapotekelezwa upunguze tatizo la maji katika Jimbo la Biharamulo Magharibi kwa asilimia 70. Nawasilisha.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu. Kabla sijafanya hivyo naomba na mimi nijumuike na Wabunge wenzangu kwa kutoa pole na rambirambi kwa wenzetu waliotutoka. Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajitahidi kujibu baadhi ya hoja, lakini ambazo sitaweza kuzijibu Mheshimiwa Waziri atakuja kutolea ufafanuzi. Kwanza kabisa nitajaribu kutoa jibu ambalo Mheshimiwa Leonard Derefa ameliomba litoke kwetu na jibu hilo ni la kuhusu bei za maji. Napenda niungane naye kwa maelezo yote aliyoyatoa kusema

kwamba bei za maji iliyopo nina hakika kwamba sasa hivi kwa Mamlaka ya Maji ya Mji wa Shinyanga ni sahihi kulingana na gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Nyama, Mheshimiwa Waziri atalijibu kwa ufasaha zaidi. Hoja nyingine ilitoka kwa Mheshimiwa Esha Stima, Mbunge wa Viti Maalum alizungumzia kuhusu gharama za maji kwa Mji wa Shinyanga.

Nilivyoelewa ni kama aliunga mkono ila akawa na hoja kwamba kwenye flat rate gharama ni juu sana. Lakini tukilinganisha hii gharama imepandishwa lini, nina hakika Mheshimiwa Esha Stima kwa vile ni mkaaji wa Shinyanga atakubaliana nami kwamba gharama hizi ni chini sana ukilinganisha hata na Miji iliyo jirani, Ukichukulia Mwanza maji yako juu, Nzega maji yako juu zaidi na sehemu zote zinazozunguka Shinyanga.

Sasa Shinyanga kulinganisha na kwamba maji yao wanayapata kutoka kwenye mabwawa kwa sasa hivi na maji kutoka chini ya ardhi ni gharama sana kuyapampu kuja juu, kama ni kutoka kwenye bwawa ni gharama sana kuyasafisha, kwa hiyo, ninaomba wananchi wa Shinyanga walielewe hilo na ni vizuri tukashirikiana ili huduma izidi kuboreshwa. Tunapenda tumshukuru Mheshimiwa Esha Stima kwa kutoa shukrani kwamba uuzwaji wa madawa yaliyoharibika, umepungua na hilo nalo ameshaliona.

Mheshimiwa Herbert Mntangi, tunamshukuru kwa kusema Wizara inaendeshwa kisayansi. Shukrani kwa wafadhili na tunapenda pia tuungane naye kuwashukuru sana wafadhili ambao wanafadhili miradi mbali mbali kwenye Wilaya yake ya Muheza na nina hakika amekuwa akifuatilia kwa bidii sana nadhani ndio sababu mambo yananyooka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la Watendaji Wilayani kwamba taaluma ni ndogo, hilo ni la kihistoria. Kama unavyofahamu, huko nyuma na imeshatokea mara nyingi, nakumbuka Mheshimiwa Waziri alikwenda Wilaya moja huko Kaskazini akakuta mtu anaitwa *Engineer* lakini hana cheti chochote.

Sasa haya matatizo yako kwenye Wilaya nyingi na hii inatokana na matatizo ya ajira. Huko nyuma mnafahamu zilisimamishwa, sasa hivi Halmashauri nyingi hazina uwezo lakini sasa hivi ndio zimepata uwezo wa kuajiri wataalam. Nina hakika tatizo hili litapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa maji Ubembe Kwemuhosi nina hakika jitihada tunazozifanya zitatufikisha pazuri tu na chini ya huu mradi wa Benki ya Dunia utakapoanza rasmi baada ya matatizo haya kutatuliwa, maeneo hayo yote yataingizwa kwenye mradi na kufadhiliwa. Mji wa Muheza kwa vile mradi huu umeanza kabla ya kubadilika kwa status ya Mji, nina hakika ni maamuzi ya Wilaya yenyewe kusema kwamba ni vizuri kuendelea.

Tumeona sehemu nyingi taratibu za namna hiyo zimehusisha pia maeneo ambayo yalikuwa Miji kwa sababu mwanzoni mradi unapobuniwa ule Mji ulikuwa na status ni

kama inajumuisha Wilaya. Kwa hiyo, hilo ni maamuzi ya Wilaya yenyewe. Nina hakika mtalitatua, sisi tuko tayari kupokea.

Mamlaka ya Tanga kwa kweli haiwezi kupeleka maji nje ya eneo la Jiji la Tanga kwa sababu sasa hivi ukisema wapeleke maji mpaka Mlingano inakuwa mbali sana na inaweza kuwa gharama. Tutajaribu kuangalia uwezekano mwingine, labda kuchimba kisima au source nyingine ya maji kwenye eneo hilo. Lakini kwa sasa hivi ni vigumu sana kupeleka maji eneo la Mlingano.

Mheshimiwa Herbert Mntangi tunakubali na wazo lako la kutazama vyanzo vingine kwa Jiji la Dar es Salaam na study sasa hivi chini ya program ya kuboresha utoaji maji Jiji la Dar es Salaam inaendelea. Jitihada zinaendelea kutafuta source ya pili au source nyingine zaidi ya hiyo tuliyonayo. Kwa hiyo, tumeangalia maeneo mengi maji chini ya ardhi, maana kuna maji mengi sana sehemu kama Chalinze chini ya ardhi wataalam wameshangaa kukuta maji ambayo ni mengi, wanasema ni kama cubic kilomita 148 ambayo ni maji mengi sana. Sasa tunaangalia ipi njia ambayo itakuwa rahisi kidogo kwa ajili ya kusaidia Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Lekule Laizer alizungumzia kwamba Wizara ya Mifugo ibakie na maji, nadhani hilo ni la kisera na inamuhusu sana Bwana mkubwa huyu atakayekuja. Wafanyakazi watengewe kule Wilayani, pia ni la kisera ambalo linahusisha Wizara ya TAMISEMI, nadhani wamesikia kilio hicho na kila mara Mheshimiwa amekuwa ukisimama hapa, hoja yake ilikuwa ni hiyo ya kutenganisha huko Wilayani kuwe na Ofisi za Kilimo tofauti na Ofisi ya Mifugo. Fedha kwa ajili ya pembejeo tumejitahidi sana kwenye Bajeti iliyopita na ninakumbuka alilisemea na tumejaribu kuangalia huku na huku, tatizo linakuja ni fedha. Ingekuwa rahisi kutoa fedha kutoka Mfuko wa Serikali kusaidia uagizaji wa pembejeo hizi ingekuwa kazi rahisi. Lakini tunaangalia mbinu mbali mbali pamoja na kuangalia uwezekano wa kupata msaada.

Mheshimiwa Lekule Laizer, madawa ya mifugo sasa hivi hayana kodi ila kinachotokea ni kwamba unajua kunapokuwa na mahitaji mengi, kawaida yanavuta bei. Sasa vitu kama hivyo vinatokea sio kwa madawa ya mifugo tu kwamba mtu anapata kitu kwa bei ya Sh.20/= tu. Juzi nilikuwa kwa Mheshimiwa Lucas Selelii, mtu ananunua maji kutoka kwenye Mamlaka inayotoa maji Mjini Nzega Sh. 20/= debe, anaondoka na baiskeli haizidi hata kilomita moja anauza Sh.80/=, sasa bei mara nne. Sasa na watu wala hawashtuki lakini kama hiyo hiyo bei ingetolewa au ingetozwa na Serikali au chombo cha Serikali ingekuwa kilio.

Mheshimiwa Menyekiti, lakini ndio hivyo demand ikiwa kubwa mara kwa mara supply inakuwa ndogo na bei zinakuwa ni kubwa. Kwa hiyo, utakuta madawa wananunua bei rahisi wanauza kwa bei ghali sana.

Kulikuwa na suala kwamba majosho yakarabatiwe, nakubali ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tumekuwa tukituma fedha nyingi sana, tumetuma mwaka huu wa fedha ulioishia juzi, tumetuma fedha kwa mwaka jana zaidi ya Shilingi bilioni moja kwenye Halmashauri za Wilaya. Lakini sasa ndio hivyo kuna maeneo mengine unakuta

msimamizi sio mzuri, unakuta kwamba hatupati kazi au hatupati matunda ya fedha hizo zimekwenda kufanya kitu gani. Lakini tunafuatilia kama Wizara kuona kwamba fedha tunazozituma zinatumika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo kwa wafugaji, Mheshimiwa Lekule Laizer unaelewa utaratibu sasa hivi, Mheshimiwa Rais juzi alikuwa anazungumza kwamba Mabenki yetu yajaribu kuangalia sasa mambo ya ukopeshaji kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na maeneo mengine ya kiuchumi. Sasa hivi walikuwa wanajali sana mambo ya biashara. Nina hakika kwamba Mabenki yetu hilo wamesikia na nina hakika kwamba katika mikopo hatutapata matatizo katika siku zijazo, tunaweza kupata mikopo kutoka kwenye Mabenki.

Mheshimiwa Willfred Lwakatare nitakupa jibu kwa ajili ya *UN-HABITAT*. Sasa hivi wamepata *consultant* ambaye anaangalia maeneo ambayo yanaweza kusaidiwa haraka sana na mradi huu wa *UN-HABITAT. AFD* na *UN-HABITAT* miradi yote inashabihiana, tunaelewa hilo kwa sababu wote kwenye report zao wametambua mradi wa mwenzao, tuseme *UN-HABITAT* wanatambua kwamba *AFD* wamefanya *study* kwa hiyo hapatakuwepo na tatizo la ku-*duplicate*.

Mheshimiwa Semindu Pawa, tunakubali shukrani na tunashukuru sana kwa jitihada zako unazozionyesha kusaidia Jimbo lako na Wilaya ya Morogoro Vijijini. *(Makofi)*

Waziri Mkuu hilo umelizungumza ni la kuhusu Dodoma. Nadhani hilo siwezi kulitolea jibu ni la kisera. La kwenda kufungua mradi ambao visima vimechimbwa, nina hakika tukipata nafasi tutaweza kuja kufanya kazi hiyo na hasa malambo ambayo umeyataja ya Vijiji vya watani zangu, majina magumu sana siwezi kuyarudia.

Kwa upande wa madawa, kodi zipunguzwe, tunasema hakuna kodi. Magonjwa ya mifugo kudhibitiwa, tunafanya hiyo kazi kwa bidii. Kuhusu kupunguza migogoro, imepungua sana na tunakushukuru sana wewe umehusika kwa kiwango kikubwa hasa maeneo ya Morogoro. Pongezi World Vision na wengine hawa wanatusadia, nina hakika kwamba wamesikia. Mheshimiwa Estherina Kilasi wa Mbarali, upanuzi wa maji Mbarali upo mradi wa Madibila, ndio tumetoa milioni 43 ili kuukamilisha.

Pia, tutanunua bomba na vifaa vingine, nadhani unaufahamu na ulikuwa unaufuatilia sana. Nilidhani utakuwa umeshaona kwenye kitabu mapema na umejitahidi sana, nina hakika wananchi wako wanahitaji kukupongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Kuhusu wahamiaji, tunaelewa, sasa hivi tunawaondoa watu na Serikali imekuwa kupitia Serikali za Mikoa, Wilaya, tumejaribu sana kuwaambia watekeleze kuondoa watu maeneo ya vyanzo vya maji. Tatizo letu nadhani ukiliangalia sana ni la maono, yaani watu wanavyoangalia, tunapowaambia kama Serikali kwamba tushirikiane katika hili naona kwamba inaleta dhana tofauti.

Utakuta watu hawatii nina hakika kwamba Sheria sasa hivi kwa kiwango kikubwa tataanza kuzitekeleza kama inavyotakiwa. Kwa sababu watu wanasahau kwamba Serikali

ni chombo cha nguvu, lakini tumekuwa tukitumia kwa sababu ya lugha tuliyozoea tunawaeleza wananchi tushirikishwe tufanye hivi, lakini unakuta wanavunja Sheria halafu baada ya muda waanza kulalamika.

Haya matatizo tunayoyapata ya maji, vyanzo vyake ni kwamba tuliharibu vyanzo vya maji. Malambo mengi sana yaliyochimbwa kati ya mwaka 1962 mpaka mwaka 1966 yote yamejaa tope siyo kwa sababu ya matumizi ya kawaida. Utakuta wamelima majaruba ya mipunga ya upande wa pili watu wamehamia karibu na hayo malambo sasa utakuta kwamba ni kilio kinachoanzishwa na sisi wenyewe. Kwa hiyo, nina hakika kwamba tutajaribu sasa hivi kutekeleza Sheria ili tuweze kutokana na matatizo ambayo yanaweza kutufika.

Kuhusu uuzaji wa ranchi nakushukuru Mheshimiwa Estherina Kilasi, tumefanya vizuri, ilikuwa kwa uwazi kabisa na tunakushukuru sana kwa kulitambua hilo. Mheshimiwa Abdillahi Namkulala mradi wa mbuzi nina hakika unazungumzia kwamba umekwenda vizuri na tunashukuru kwa hilo kusikia kutoka kwa Mheshimiwa Abdillahi Namkulala. Nina hakika wanyama wengine au mifugo wengine watafuata jinsi uzoefu unavyozidi kujengeka kwa wananchi.

Mheshimiwa George Lubeleje nadhani alikuwa anapongeza sana, tunashirikiana naye sana na tunamshukuru sana, amekuwa na sisi muda wote. Nina hakika nguvu za Serikali za kifedha zinavyozidi kuja nina hakika mambo yote yatafuata.

Mheshimiwa Aridi Uledi amezungumzia kuhusu hifadhi ya maji, matatizo ya kisima Michiga na maeneo mengine ambayo ameyataja Nangaramo. Nina hakika shamba la Nangaramo bahati mbaya sana mimi wakati mwingine naweza kusema kwamba wale wafanyakazi na jumuiya iliyopo hapo hawapendi kujituma. Lile lambo nilishaliona, wangeweza wakalisafisha hata kwa kutumia majembe ya mkono. Kama unakumbuka, Mheshimiwa Aridi Uledi malambo yote yaliyotengenezwa baada ya Uhuru yalichimbwa kwa mkono na bado mengine yapo mpaka leo.

Sasa hilo lambo lipo lilichimbwa na trekta sawa, lakini lime-silt upande wa juu wangeweza kutengeneza kwa kushirikiana na wanakijiji ambao wamekuwa wakisaidiwa maji. Nina hakika kwamba lambo hilo leo lingekuwa linaweza kuwavusha wakati wa kiangazi. Kwa hiyo, naomba sana kwa jitihada zako na nina hakika ana bidii sana kusaidiana nao, aende uwaeleze kwamba kama fedha hatupati tusife moyo tujaribu kufanya hata kwa majembe ya mkono. Maana ni kazi ndogo sana ya kuweza kulitunza hilo lambo.

Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba nadhani ulikuwa unatupongeza sana na safari hii umeona fedha zimetengwa kwa ajili ya kufanya usanifu kwa Mji wa Geita wenyewe na mradi huu wa Nyakagombo uliokuwa unauzungumzia, kuufikisha Katoro itakuwa kuna umbali kidogo. Tutaomba utuachie nafasi tuweze kuangalia uwezekano huo.

Kuna michango ambayo imetolewa kwa maandishi, nitaomba niende haraka haraka, kuna Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, mfumo kama unavyoelewa

Mheshimiwa Peter Kabisa maji katika kipindi cha miaka mitatu yamekuwa taabu sana kwa sababu ya uchakavu wa mitambo na mabomba mengi sana yameoza. Lakini sasa hivi chini ya ukarabati unaoendelea, nina hakika matatizo ya maji Dar es Salaam yatapungua.

Mheshimiwa Paul Ntwina, pampu ya visima vilivyochimbwa, tumetenga Shilingi milioni 10 kwa ajili ya kununua pampu maeneo hayo na nina hakika kwamba baada ya kutupitishia Bajeti hapa tutaweza kupata vifaa hivyo viende kufungwa. Mheshimiwa Mizengo Pinda na yeye alichangia maji Tarafa ya Mbimbwe, nina hakika kwa vile tumeshapata project right up ya mradi huo, tunajaribu kuangalia wapi tunaweza kupata fedha.

Mheshimiwa Steven Kazi, majosho ya Buhongwa, Mkolani na Butimba, Mwanza katika miaka miwili tumepeleka majosho karibu saba na mawili yako kwenye eneo la Jiji. Sasa swali lingine umeuliza kuhusu josho la mbwa ambalo limebomolewa. Kwanza lilikuwa katikati sana ya Jiji na lilikuwa ni hatari hata wakaaji walio karibu na josho moja lilikuwa kwenye road reserve, kwa hiyo, limeondolewa ili kupisha ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mbunge wa Singida Mjini, maji kutoka lambo la Itamka nadhani mradi unaufahamu umefanya kazi kwa bidii sana na unaelewa fika kwamba mkopo tumeshapata kutoka ABADEA na shughuli inaendelea ni kuomba Mungu tu Inshallah urudi uweze kuendelea na kazi. *(Makofi)*

Majosho ya madawa kama nilivyoeleza tumekuwa tukipeleka kwenye Wilaya zetu kwa kipindi kirefu chote hiki cha Bajeti iliyopita.

Mheshimia Omar Mjaka Ali, alizungumzia juu ya Shule zilizojengwa chini ya Mradi wa MMEM, zipelekewe maji. Tunafanya hivyo kwenye maeneo yanayowezekana na fedha zinatumwa kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi umeuliza maji katika baadhi ya Kata, sasa tumezungumza na kurugenzi yetu ya maji, Vijiji ijaribu kuona kwamba maeneo ambayo umeyaainisha yanaingizwa kwenye Mradi wa Maji unaofadhiliwa na World Bank, pamoja na baadhi ya miradi inayozunguka Mji wa Wilaya ya Mbinga.

Kwa hiyo, hilo tunalishughulikia vizuri sana kwa sababu umekuwa ukitoa kilio hicho kwa kipindi kirefu na Maofisa wetu wote karibu wanafahamu tatizo hilo. Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, nadhani alikuwa anazungumza juu ya shughuli ambazo Wizara imezifanya, sensa ya mifugo ni muhimu, kwa bahati mbaya sana sensa hii ingeweza kufanyika wakati wanahesabu watu kwa sababu watu walikuwa wanahesabiwa pamoja na vitu vyao kama wanaulizwa una vioo vingapi?

Nadhani ilikuwa makosa kwamba tulisahau tu tungeweza kuingiza mifugo kwa binadamu wangeweza kusema nina ng’ombe 50 ingekuwa kazi rahisi. Lakini sasa hivi tunatafuta fedha kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki alizungumzia kuhusu Mbinga. Nadhani nimeshatoa majibu na tunakushukuru unafuatilia kila siku.

Mheshimiwa Semindu Pawa ulileta kwa maandishi pia mchango wako. Maeneo chepechepe kama nilivyoeleza Sheria zetu za vyanzo vya maji hazifuatwi kama inavyotakiwa, nakubaliana na wewe kabisa kwamba tunafika mahali tunavunja hata makubaliano yetu ya kimataifa. Vyanzo vya Maji utakuta vingi maeneo chepechepe yamegeuka kuwa maeneo ya kulimwa mpunga. Kwa hiyo, utakuta kwamba wana-broke maji yasiingie kwenye stream za mito zinazotunza baionuwai ambayo inahitajika katika uhai wa mwanadamu. Kuhusu malambo nadhani nimeshakujibu Mheshimiwa Semindu Pawa.

Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, alizungumzia flat rate, napenda kusema kwamba mambo ya flat rate kwa sababu tumeyarithi, kwa kweli ni vigumu sana kukadiria kwamba mtu ametumia maji kiasi gani au amepata maji kwa muda wa siku ngapi? Maana dhana halisi ya flat rate ilikuwa ni kwamba nakubaliana na wewe tumia maji unavyotaka utalipa kiasi fulani mwisho wa mwezi.

Sasa siku ambazo hutapata maji sitakuwa nafanya hivyo kwa makusudi. Nadhani ndio ilikuwa dhana hiyo tunapowawekea mita kwa sasa hivi watu wanalipa kuliangana na mita, sasa nina hakika kwamba jinsi ambavyo mita zinanunuliwa, zinafungwa, tatizo hili la *flat rate* litapungua.

Wengi wanasema flat rate bei iko juu, lakini ukweli ni kwamba Miji mingi sana maji tunayapata kwa shida, mfano Kigoma Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Kigoma imezungukwa na milima, kupampu maji kutoka huko Lake Tanganyika na unajua Lake Tanganyika iko kwenye Rift Valley iko chini. Kupampu maji kuyafikisha kwenye maeneo ya milima tunatumia umeme mwingi sana na unafahamu mfano kama Kigoma nadhani mteja kuliko wote wa *TANESCO* ni Mamlaka ya Maji. Karibu nusu ya umeme unatumika kwa Mamlaka ya Maji, kwa hiyo, gharama ni kubwa sana na ni vizuri tukalielewa hilo.

Mheshimiwa George Lubeleje, nadhani nimeshajibu maswali uliyoyauliza, Mheshimiwa Prof. Mbawala ulikuwa unaomba Shilingi milioni 30 kwa ajili ya kumalizia kazi ambayo imeanzwa. Juzi juzi tu tulitoa Shilingi milioni 20 mwezi wa sita na nina hakika kwamba hilo unalitambua na tunakushukuru sana kwa jitihada unazozifanya. Tukipata nafasi ya kupata fedha tena zaidi nina hakika hatutasahau wananchi wa Namtumbo.

Mheshimiwa Robert Mashala, matatizo ya maji Ushirombo kisima kimeshachimbwa chini ya mradi wa Netherlands, ambao unafadhiliwa na Netherlands kwa ajili ya maji kwa Mkoa wa Shinyanga. Sasa hivi wanaitisha tender kwa ajili ya kuyasambaza maji hayo ambayo kisima kimechimbwa chini ya mradi huo. Nina hakika matatizo ya maji yataendelea kupungua jinsi siku zinavyokwenda.

Mheshimiwa Anne Makinda, tunapokea shukrani zako na unaomba msaada uendelee tumejitahidi sana na umekuwa ukifuatilia, nina hakika kwamba tutafika tu kwa sababu

wananchi wako ni wepesi sana kuchangia na wanakubali kushirikiana na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Kibaha tunajua matatizo ya maji Kongowe, Msangani, Mwanarugali na Sofu na tunajitahidi uzalishaji wa maji utakapozidi kwenye sehemu hii ya Upper Ruvu kwenye chanzo chetu cha maji na ukarabati huu ukaendelea ambao utaweka bomba ambalo litakuwa mahsusi kwa ajili ya maeneo ya Kibaha na Kongowe na sehemu hizo ulizozitaja, matatizo yatapungua. Tunajitahidi sana, iko chini ya mradi, fedha zake zipo na nina hakika subira itatufikisha hapo tunapohitaji kufika.

Mheshimiwa Salome Mbatia maji Kilimanjaro nadhani ndio wakati najibu swali asubuhi ulisikia kwa kweli Mkoa wa Kilimanjaro chini ya Kili Water wafadhili wako wengi KFW inshallah Mungu awape nini zaidi? Miradi ya maji ni mingi inakwenda kule.

Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Chalinze Water Project umesema kunakuwa na technical problems. Huu mradi ni mkubwa sana na unahitaji utaalam ambao unatakiwa ujengeke kwa kuzingatia experience. Sasa ninafahamu sana kuna sehemu za remote control nakumbuka siku ile tulikuwa wote zimeharibika lakini kama unavyoelewa mradi ule bado uko chini ya guarantee. Kwa hiyo, wataalam wa Kichina nadhani mliwaona bado wanashughulikia, watakapofikia hatua ya kutukabidhi ule mradi nina hakika tutakuwa tumejenga uzoefu wa kutosha na tutakuwa na vipuli vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uliuliza swali ankra feki bado zinatoka kila siku? Tunasisitiza kwamba Mamlaka zetu wawe waangalifu hatupendi bills ambazo zinawekwa kwa makadirio na maeneo mengi sana tumefanya hivyo ukizingatia mfano Mwanza, Arusha, Tanga hata Dodoma sasa hivi matatizo madogo madogo hayo yamepungua sana. Lakini tunawasisitizia sana kila siku wafanyakazi wetu kwamba mambo ya service ndio yanayozalisha fedha ambazo zinajenga uchumi wa dunia hivi leo. Sasa ni vizuri kutoa service ambayo ni nzuri ili wateja wawe willing kulipa bila kusumbuliwa, lakini mtu anakuwa ni mgumu sana kulipa kama service inakuwa mbovu.

Masuala mengine Mheshimiwa Waziri nadhani atajaribu kutoa majibu ambayo ni ya msingi. Kichaa cha mbwa bado ni tatizo tumekubaliana kushirikiana na Wizara ya Afya ili tutatue hili tatizo, ni tatizo kubwa kwenye baadhi ya maeneo. Malisho ya mifugo tunaangalia uwezekano sasa hivi wa kutatua tatizo hilo. Nadhani mlipokwenda Mpwapwa mmeona kuna kitengo kabisa kinashughulikia hilo. Madawa ya mifugo upatikanaji na bei hilo tunajaribu kusaidiana na sekta binafsi na tunajaribu sasa hivi kuangalia uwezekano wa kudhibiti watu ambao wanaleta madawa feki.

Mheshimiwa William Shellukindo City Water Services tunashukuru na nadhani kwa kutuunga mkono kama ilivyotuunga mkono Kamati ya Mheshimiwa, nina hakika tutapata nguvu, angalau walisema kwamba tuwe waangalifu kwenye shughuli za kibiashara ya Mikataba, huwezi ukamzuia mtu kushtaki. Kila mtu anajua ana haki na kila mtu anadhani kwamba anastahili haki fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtu anakwenda Mahakamani lakini tutajitetea kwenye hili tumefanya maamuzi ambayo yamezingatia utaalam wote na tumekuwa tukishirikiana na Ofisi zote husika za sheria na kadhalika.

Mheshimiwa Edson Halinga maji ya gravity Kata ya Iyura Wizarani tunalo hilo umelileta siku nyingi na tuna hakika ni katika kufuatilia tu, tutajitahidi kadri tunavyoweza kupata fedha ili mradi huu uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Bujiku Sakila, Tarafa ya Mwamashimba iko kwenye huu mradi wa kupeleka maji Shinyanga na kwa kweli atakayeanza kupata maji yanayotoka Lake Victoria kwenda Shinyanga ni Mwamashimba, ndiyo watakaoanza kunywa maji haya miezi michache ijayo. Kwa hiyo, licha ya kwamba rafiki yangu afya yako ilikuwa siyo nzuri lakini umefuatilia sana hili na nina hakika wananchi wako watalisikia. (Makofi)

Mheshimiwa Leonard Shango, rafiki yangu huyu alikuwa African Development Bank anafuatilia kila siku maswali yake Bungeni ni umwagiliaji, kilimo cha umwagiliaji na amechangia vizuri sana wakati wa Wizara ya Kilimo nina hakika kwamba ni katika kuongeza nguvu Serikali isikie ina kitu ambacho Serikali pia inazingatia ili kupunguza matatizo ya uhaba wa chakula na kadhalika.

Kufufua mabwawa, tunafanya hivyo lakini mabwawa mengine ufufuaji wake hasa unahitaji nguvu pia za wanamaeneo wenyewe. Mfano mzuri nitakueleza. Malya tulikuta bwawa lile lilikuwa lime limejaa tope, kumbe walikuwa wameziba mfereji unaoingiza maji ndani ya bwawa. Tulipozuia kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga sasa hivi lile bwawa lina maji mengi sana huwezi kuamini. Kwa hiyo, malambo mengi sana au mabwawa mengi sana yanaweza yakarudi katika hali zake za kawaida kwa kuzingatia tu masharti ambayo yaliwekwa.

Kwa bahati mbaya sana waliokuwa mabwana malambo, zamani tulikuwa na Bwana Malambo District Council zilikuwa zinaweka watu ambao wanaangalia yale mabwawa na malambo, waliwaondoa sasa walipowaondoa watu wakavamia maeneo. Nina hakika kwamba jitihada kama hizi tukizifanya tutafika mahali pazuri ili tuweze kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, tumemaliza mradi hivi karibuni wa kutoa maji kwenye bwala wa Kilimi, kwa hiyo, kwenye bajeti hii tumeweka fedha tena Shilingi milioni 30 kwa ajili ya kuchimba visima sehemu ambako bomba linapita kwa sababu bomba kipenyo chake siyo kikubwa sana cha kuanza kugawa maji njiani lakini tunatoa fedha kwa ajili ya kuchimba visima kukidhi mahitaji ambayo wanakijiji sehemu ambako bomba linapita.

Maji ya Lake Victoria tunakuhakikishia kwamba nguvu za Serikali zinavyozidi kupatikana maji yatafika Nzega kwa sababu design ya bomba kwenda Shinyanga inazingatia maji yanayoweza kufika Nzega. Inshallah tukipata fedha, nina hakika mambo yatakuwa safi. Mheshimiwa William Lukuvi nadhani Mheshimiwa Waziri atajibu.

Mheshimiwa Venance Mwamoto umezungumza vitu vya msingi sana. Uvunaji wa maji ya mvua tumesisitiza sana mwaka huu wa fedha 2005/2006, tumekuwa tukisema hilo, alama kuwekwa barabarani sehemu ambako mifugo imepita, nadhani Wizara ya Ujenzi wamesikia na Wizara ya TAMISEMI. Plastics bado ni matatizo na ninapenda kukuhakikishia Mheshimiwa Venance Mwamoto kwamba utaratibu uko mbioni, tutazuia plastics laini zisitumike kuweka maji, taratibu zinamalizika na ninahakika kwamba hii balaa ya plastic itapungua sana.

Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kuhusu Shule ya Siha nadhani Mheshimiwa Waziri atajibu. Mheshimiwa Anatory Choya, mchangiaji wa mwisho, World Bank project inahusisha Mji wa Biharamulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na mimi naunga hoja mkono mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WIZARA YA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunikaribisha tena jioni hii nihitimishe hoja tuliyoianza asubuhi. Niruhusu kabla ya kuhitimisha na kujibu hoja, niwatambue Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi na wale ambao wamechangia kwa kusema. Waliochangia kwa maandishi ni:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu Frederick T. Sumaye, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Aaron Chiduo, Mheshimiwa Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Esha Stima na Mheshimiwa George M. Lubeleje. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Issa Salim, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mwanamkuu Kombo, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Omar Mwenda, Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Pius Mbawala na Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya na Mheshimiwa Dr. Mary Nagu. *(Makofi)*

Waliochangia kwa kusema ni Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa

Lekule Laizer, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba na Mheshimiwa Anthony Diallo Naibu Waziri wangu, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Anthony Diallo, amejitahidi sana kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na kwa kweli nampongeza na kumshukuru sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuweza kujibu hoja zote na hata mimi sikusudii kufanya hivyo isipokuwa napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kabla hawajaondoka hapa tarehe 29 Julai, 2005 tutawaletea majibu yao mengi kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijakwenda kwenye hoja nyingine nianze kwa kusema hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amenikumbusha kwamba Wilaya ya Hanang haikuonekana sana kwenye miradi, ningependa kusema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mbunge wa Hanang amefanya kazi kubwa sana kufuatilia miradi ya Jimbo lake la Hanang. Hanang walipata mradi mkubwa wa fedha kutoka Japan lakini bahati mbaya wakagundua kwamba maji chini ya ardhi kule Hanang yana madini ambayo hayafai kwa matumizi ya binadamu, ndiyo maana maji Hanang yamechelewa sana. Lakini ningependa kumhakikisha yeye na sasa kumhakikisha Mheshimiwa Dr. Mary Nagu kwamba Hanang iko katika Mpango wa Benki ya Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa maelezo yako uliyoyatoa na yale ya Kamati. Namshukuru pia Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Msemaji wa Upinzani kwa kutuunga mkono katika mambo mengi sana. Naomba nirudie jambo moja ambalo amelisema Naibu Waziri na ambalo mmelisema asubuhi la *City Water*. Tunashukuru sana kwa kuungwa mkono na wananchi na ninyi Waheshimiwa Wabunge kuhusu hatua zetu dhidi ya *City Water*. Ninapenda kuwahakikishia kwamba tulishauriana kwa karibu sana na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na uamuzi huo ulikuwa ni uamuzi wa Baraza la Mawaziri na siyo mtu mmoja. *(Makofi)*

Uamuzi ule umezingatia maslahi ya nchi yetu, hatutaki mtu yeyote afikiri sisi ni The Banana Republic hivi, anaweza akaja akatudanganya danganya, tulitaka ijulikane na Watanzania wafahamu hivyo kwamba tumefuata taratibu zote hatukutaka tudanganywe na hatutakubali tudanganywe. Hata wakienda arbitration tumesimama katika miguu na miamba mizuri sana na tuna hakika ya kushinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nirudie alilolisema Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo waliyoyaomba Wabunge wakiwemo Mheshimiwa Lucas Selelii juu ya maji ya Ziwa Victoria. Lakini ningependa kutumia nafasi hii ingawa nitasema huko mbele lakini niseme wazi kwamba aliyesukuma jambo hili na kulisimamia kikamilifu sana ni Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa. Uamuzi wake ndiyo umetuwezesha kutekeleza jambo hili. Fedha zinazotakiwa nilisema asubuhi ni zaidi ya Shilingi bilioni

176, katika bajeti mnayogawana sungura uende Kilimo, Elimu na hata sehemu nyingine kwa kweli bila nguvu za Rais mwenyewe na uamuzi wake tusingefika hapa.

Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana kwamba ametuwezesha kutekeleza jambo la kihistoria katika nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini jambo ambalo vilevile litasaidia Watanzania walio wengi kama alivyosema, bomba limetengenezwa kwa namna ambayo hatimaye tukiwa na pesa maji yatakuja Nzega, Igunga, Singida na hata mkitaka yatafika Dodoma. Kwa hiyo, ni mradi ambao ni wa manufaa kwa Watanzania na tuombe Mungu kwamba mambo yameanza vizuri yanakwenda vizuri. Niseme kwamba wataalamu wa Wizara yetu wanafanya kazi nzuri sana katika kuusimamia mradi huu. Ningependa kuwashukuru na kuwasifu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu na mimi nisemee kidogo kuhusu mifugo. Namshukuru Mheshimiwa Salome Mbatia alipoandika katika maelezo yake alipochangia kwa maandishi alisema angalau siku hizi tunaona nyama zetu kwenye Super Markets kubwa pale Dar es salaam. Mimi nakubaliana naye, wale mnaokula nyama hapa Dodoma angalieni hata ubora wa nyama Dodoma umebadilika sasa. Maana ni wa viwango sasa vya Kimataifa. Baada ya kuleta machinjio pale, aina ya ngombe anayetaka aletwe kwenye machinjio ni ngombe mkubwa na mzuri, ukimleta mdogomdogo hafai kwenye machinjio. Maana yake hiyo tumebadilisha biashara yetu ya mifugo kuwa sasa ya kisasa. *(Makofi)*

Nilitembelea pale Mtibwa, wanafanya Feed looting ng'ombe wengi sana lakini Kampuni ya nchi jirani kwa kuona ng'ombe wale walivyo wazuri wamewa book wote, wote wameshauzwa wanapeleka kwenye mahoteli ya Kenya. Sasa tumemwomba yule Mwekezaji pale sasa awasaidie wafugaji wadogo wadogo na wenyewe wafuge kwa namna hiyo ili wamuuzie yeye halafu tupate soko. Kwa hiyo, nasema sekta inakwenda mbele na nina hakika Mwenyezi Mungu ataendelea kutubariki iweze kwenda mbele zaidi ya hapa tulipo, ndiyo maana nalisema hili ili kuunganisha na hoja ya Mheshimiwa Leonard Derefa.

Kwanza Mheshimiwa Leonard Derefa napenda kukiri mbele ya Bunge hili na wananchi wa Shinyanga wanisikie kwamba Mbunge mmoja aliyefuatilia kwa karibu sana matatizo ya maji Shinyanga ni Mheshimiwa Leonard Derefa. Amefuatilia wakati wa matatizo ya maji pale Shinyanga wakati wa kiangazi, amefuatilia wakati bwawa lilipokauka kabisa tukaanza kuchimba visima ndiyo maana tulipomaliza kazi ile tulimteua yeye mwenyewe awe Mwenyekiti wa Bodi ile kwa kazi nzuri aliyoifanya. *(Makofi)*

Leo wananchi wa Shinyanga, maji yanakuja ya Lake Victoria yanakaribia kama alivyosema Naibu Waziri karibuni sana yatafika Shinyanga. Tutafuta tatizo la maji Shinyanga, itakuwa ni historia, lakini ni jitihada za Wabunge wenu. Kwa maji ya Ziwa Victoria lazima nikiri Wabunge wote wa Mwanza na Shinyanga wamesimama kidete kulifuatilia jambo hili. Naomba wananchi mtakapokuwa mnawahukumu Wabunge hawa

mkumbuke walioleta maji ya Ziwa Victoria ni pamoja na Wabunge wa Shinyanga na Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja ya Mheshimiwa Wilfred Lwakatare aliyoitoa asubuhi. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Wilfred Lwakatare kwa kuwa muwazi. Pamoja na aliyoyasema lakini ningependa kumpa maelezo yafuatayo:- Hii ni Serikali ya uwazi na ukweli na ni Serikali ambayo haina kificho, lakini Serikali ni ambayo Sera zake ziko wazi na zinajulikana. Ulikuwa ni uamuzi wa Serikali kwamba tuwashirikishe wananchi wazalendo katika kufuga kibiashara.

Kwa hiyo, tukasema katika zile ranch unaacha hekta 20,000 zinabaki chini ya *NARCO* unagawa ndogo ndogo hekta mpaka 4,000 kwa Watanzania wenye nia ya kufuga kibiashara na hizi hekta 20,000 hekta 20,000 nisikilize kwa makini, maelezo ya Baraza la Mawaziri tutaziandaa mpaka hapo tutakapopata a Strategic Investor Mtanzania.

Kwa hiyo, tukimpata leo tunampa. Kwa hiyo tukimpata leo tunampa, tukimpata keshokutwa tutangoja. Nia yetu ni kuhakikisha kwamba ardhi ile haiendi kwa wageni. Mimi leo ningeshtuka sana kama Mheshimiwa Wilfred Lwakatare angeniambia kwamba ardhi ile mbona umemuuzia mgeni. Napenda kuwahakikishia Watanzania hatukumuuzia mgeni, tumempa Mtanzania aliyejitokeza mwenye nia ya kuwekeza na ambaye ana record ya kuwekeza vizuri sana hapa Tanzania.

Nitaeleza. Ranch iligawanywa kwenye ranch ndogo ndogo 13 zenye jumla ya hekta 21,000 zikabaki za mfano hekta 22,000. Hizi 13 Mheshimiwa Wilfred Lwakatare wale walioomba bado hawajapewa kwa sababu tuna utaratibu wa kupata consultant anayeangalia ile business plan je inakubalika? Je, huyu mtu kweli anataka kufunga au ni utapeli?

Kwa hiyo kuna consultant lakini napenda kukuhakikishia kwamba kabla ya mwisho wa mwezi wa Nane wale walioomba watu 55 watapewa 13, lakini tunaomba wasubiri mpaka utaratibu ukamilike. Iko kwa consultant, nawahakikishia watu wala hawana haja ya kulalamika, mambo yanakwenda vizuri na mimi nina hakika watu wa Bukoba wale ni wazoefu wa biashara, bwana haya mawazo sijui wameyatoa wapi! Wale ni wazoefu sana wa biashara na wanajua kuna utaratibu wa kufuata. Kwa hiyo, waambie tunafuata utaratibu.

La pili, lile eneo lilibaki la strategic investor, tukampata huyu Mtanzania ambaye ndiyo aliyefufua kiwanda cha Kagera kilichokuwa kimekufa. Leo kiwanda kile kinazalisha sukari nyingi sana. Kiwanda kile leo kimeajiri wafanyakazi wengi sana na Mtanzania huyu amepata mkopo wa kuanzisha kiwanda kingine pale pale kwenye eneo la Kitengule na kuzalisha tani 350,000 za sukari kwa mwaka. Lakini siyo hiyo tu, anaanzisha utaratibu wa *out growers* kwamba siyo yeye anayelima miwa, watalima wenye mashamba jirani.

La pili, kiwanda kitaajiri wafanyakazi watakapoanza 3500 mpaka 8500. Sera ya Chama Cha Mapinduzi ni kutafuta ajira kwa vijana na Watanzania wengine. Hapa tumetekeleza

sera bila kuyumba na tunaamini kwamba akitoa ajira hii itasaidia sana Watanzania wengi wa Bukoba ambao hawana ajira na hasa vijana. *(Makofi)*

La tatu, anaendelea kufanya kazi ya msingi tuliyokubaliana atakuwa anafuga pale lakini utaratibu wake ni wa feed looting. Kwa hiyo, hahitaji eneo kubwa sana, ndiye anayefanya Mtibwa, ndiyo yeye ninayesema ng'ombe wake wote wamekuwa booked pale, kwa mwaka atakuwa anatoa ng'ombe wasiopungua 20,000 kwa utaratibu wa feed looting na kwa sababu ana molasses kutoka kwenye kiwanda cha sukari, molasses hii ndiyo vilevile itakayokuwa inawafaa wale wafugaji wengine wadogo wadogo ambao watakuwa wamezunguka ranch ya Kitengule.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, jambo limekwenda ndani ya utaratibu wa Serikali. Umeuliza process, kazi ya Serikali ndiyo inayosimamia nani mwekezaji aende wapi na imekwenda kwa utaratibu unaokubalika wa uwazi, hakuna tatizo hata kidogo. Tumempata mwekezaji Mtanzania mwenye nia njema na sisi tunamkumbatia kwa nguvu zetu kwa ajili ya ajira na sukari kwa ajili ya Tanzania. *(Makofi)*

Lakini kama nilivyosema, wakikosa hao Kitengule tunazo ranch nyingine za *Kikulula Complex* na Misenyi. Misenyi bado haijatangazwa, tutapata pale jumla ya ranch nyingine 39. Watu wako wanaotaka waombe na kama waki-qualify, sisi hatuna matatizo, watapata lakini napenda kutoa mashaka yote, radio kifuani, sijui radio kitu gani, hakuna chochote Mzee, mambo yako ndani ya utaratibu na tutatue tatizo la ajira katika Mkoa wa Kagera pamoja na Wilaya ya Bukoba Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuiga wenzangu walichofanya kwa kutoa shukrani mbalimbali. Kwanza niwashukuru wananchi wa Jimbo la Monduli ambao wamenileta hapa miaka hii 10, niwashukuru na kuwaomba kwamba ninakuja tena waendelee kuniangalia kwa jicho la huruma. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini pili, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge tumefanya kazi pamoja, tumesukuma maendeleo ya nchi yetu kwa pamoja, tumehuzunika pamoja na tumefurahi kwa pamoja. Nawashukuru na kuwapongezeni. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu tumefahamiana na Waziri Mkuu miaka mingi sana na alipokuwa Waziri Mkuu amenisaidia sana katika kazi yangu. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa kazi yake nzuri kutusaidia katika Wizara yetu pamoja na yule Marehemu aliyetangulia ambaye alikuwa katika Sekta ya Mifugo. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kweli na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo imekuwa ni kitu kimoja. Namshukuru sana Makamu wa Rais alivyotusaidia kwa kazi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme nimefanya kazi katika Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa furaha kubwa sana kwa sababu ninayo timu ya wasomi wengi sana waliokaa pale nje na walioko upande ule.

Mafanikio yaliyopatikana katika Wizara hii si yangu ni hao wataalam wa Wizara yangu ambao nilikuwa nawaongoza. Napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana kwa msaada ambao wamenipa mimi na kumpa mwenzangu Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Diallo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshukuru kipekee Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, amenipa nafasi kushiriki katika timu iliyofunga magoli nadhani timu yetu ya Mawaziri chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu tumefunga magoli mengi. Ninamshukuru kwa kunipa nafasi ya kutumikia nchi yangu kwa miaka yote hii. Namtakia kila kheri anapostaafu na nina hakika nchi yetu itaendelea kumtumia katika nyanja nyingi na hasa hii ya Kimataifa ambayo ametujengea heshima kubwa duniani.

Namshukuru Naibu Waziri wangu, tumeshirikiana vizuri, tumesaidiana vizuri na amenipa uzoefu mkubwa wa *Private Sector.* Namshukuru sana kwa kazi nzuri na ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namalizia kwa kumshukuru mke wangu Regina na watoto wangu kwa kunipa support. Nadhani mke wangu Regina yupo hapo na watoto wangu wako kule, naomba wasimame. Wamekuja kuniona nikimalizia n'ngwe hii, nawashukuru sana kwa sababu kama walivyosema wenzangu walionitangulia "Behind every successful man there is woman." *(Makofi)*

*(Hapa familia ya Mheshimiwa Edward Lowassa ilisimama kuonekana kwa Waheshimiwa Wabunge)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa kwa heshima na taadhima nawaomba Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono, mtupatie fedha hizo zikafanye kazi kwa faida ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 49 - Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo**

Kif. 1001 – *Administration and General* … … Shs.2,211,159,400/=

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Programme 10, Sub-vote 1001, 250100 kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi mzuri kuhusiana na hoja niliyoiwasilisha. Nilipenda kupata majibu na amejitahidi sana

kuelezea process jinsi ilivyofanyika na akapewa huyo mtu anayeitwa strategic investor. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kupata maelezo ya ziada na kuhoji maamuzi ya Serikali kwamba wanakuwa wameangalia nini au wame-vision kwenye kitu gani iwapo ardhi kwa kipindi cha miaka kadhaa inakuwa imelengwa kwa matumizi ya jambo fulani then ije tu hatua za haraka haraka au za consider labda upande mmoja wa jambo kwa misingi ya kwamba ni strategic investment? Hasa unapoamua kubadilisha matumizi ya eneo lilotengwa kama ranchi ya ng'ombe au mifugo na kuamua kuweka suala la kulima miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hili kwa sababu huko mbele tunakokwenda yeyote anaweza kuwa kwenye mamlaka na anaweza akaamua kutumia kipindi anachokuwa kwenye mamlaka kuamua matumizi fulani kwa sababu ya kuangalia jambo fulani kwa wakati huo aliopo pale madarakani na badala ya kuangalia jambo ambalo lilikuwa limekusudiwa kama long term plan.

Hivyo tunatambua suala hili la ranchi lilikuwepo kwa miaka mingi na kama nilivyosema, hapo mwanzoni wananchi wa Mkoa wa Kagera wamekuwa wanayalinda hayo maeneo kwa sababu ya matumizi ya kuwa ranchi kwa matumizi ya kufuga mifugo na ni kwa manufaa ambayo vilevile wanakuwa wameyalenga ikiwa ni pamoja na kupata nyama za kutumia, maziwa na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala ambalo limezungumzwa hapa ni kwamba Serikali imeangalia sana suala la ajira kama alivyosema Mheshimiwa Waziri za wakata miwa ambao nasikitika kwamba kwa wakati fulani hata Mkuu wa Mkoa na wakati mwingine Viongozi mbalimbali wa Serikali waliwahi kulalamika kwamba wananchi wa Bukoba hawajitokezi katika ajira za kukata miwa. Sasa mimi nataka kumhakikishia Mheshimiwa Waziri kwamba hata hizo ajira bado ni questionable kwa faida ya wananchi wa Bukoba Mjini na Mkoa wa Kagera za kukata miwa kwa takwimu hizo alizonisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala linabaki pale pale kwamba wananchi wa Mkoa wa Kagera wangependa zaidi kwamba maeneo hayo ambayo wameyaangalia kama mboni yao ya jicho yaendelee kuwa ranchi ya kuweza kufugia mifugo badala ya kuweka miwa. Hii tunaisisitiza kwa msingi mmoja tu kwamba, hata hiyo sukari nimeeleza hapa asubuhi kwamba huyo strategic investor baada ya kuja yeye, sukari kilo moja ni Sh.1,000/= badala ya bei ya zamani ambapo sukari ilikuwa inatoka kwenye sources nyingine ambapo ilikuwa inauzwa kwa Sh. 600/= au Sh. 700/= kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuja kwake huyo strategic investor imeonakena kwamba badala ya kupata, tumepatikana na huenda tukaendelea kupatikana na hii ni kwa sababu huyo strategic investor pamoja na Serikali imemsaidia kumpa eneo la kulima miwa. Lakini yeye mtizamo wake anaangalia soko la nje. Sukari nyingi inakwenda nje na matokeo yake pale Kagera hatuwezi kupata hata hiyo sukari ambayo inazungumzwa. Kwa hiyo, matokeo yake badala ya kuondoa umaskini katika Mkoa wa Kagera

mnatuongezea umaskini kwa maamuzi hayo mnayokuwa mnayaangalia zaidi, matakwa ya strategic investor.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Kagera wenyewe wanaona kwamba kama Serikali imeangalia suala la kunufaika kutokana na strategic investor, basi huyo strategic investor wa sukari aweke kibano cha kuhakikisha anapunguza bei ya sukari kwa misingi kwamba source ya sukari hivi sasa iko karibu na wananchi wa Kagera. Sawa na ambavyo mwananchi wa Dar es Salaam anavyonufaika na kiwanda cha Cement kuwa karibu pale Dar es Salaam kwa kununua mfuko wa Cement kwa Sh.9,000/= wakati mwananchi wa Bukoba ananunua mfuko wa Cement kwa Sh.15,000/=. Kwa hiyo, tunaomba hilo liangaliwe zaidi. Mheshimiwa Waziri hana haja ya kujibu. Nafikiri amenielewa na Serikali na bwana mkubwa yupo hapa pamoja na kwamba anaondoka. Mmenielewa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Unataka kujibu Mheshimiwa Waziri maana yeye mwenyewe amesema kwamba haina haja ya kujibu. Basi naomba mtulie.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuweke rekodi sawasawa. Narudia maelezo yangu. Hakuna kilichobadilika. Eneo la mifugo litaendelea kuwa ni la mifugo lakini intensively tunazungumza juu ya hekta 21,000. Kwa hiyo, unazigawa unaweka kiwanda cha sukari halafu unaweka ng'ombe kwa *feed looting system.*

Mimi namshangaa sana Mheshimiwa Wilfred Lwakatare akithubutu kusema katika hadhara hii kwamba hakuna Watanzania wanaotaka kufanya ukataji miwa. Anakataa kwamba hakuna Watanzania wa Bukoba wanaotaka kuanzisha mashamba ya kukata miwa wawe out growers wa miwa! Mimi nina uhakika hasemi kwa niaba ya wananchi wa Bukoba katika hili. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Anajisemea mwenyewe!

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuihakikishia Kamati yako kwamba mambo yamefanyika katika utaratibu mzuri. Tumeitazama visionary vizuri sana kuwaangalia Watanzania wanufaike kiuchumi na kwa ajili ya ajira yao. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … … … … Shs. 808,141,600/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … … Shs. 1,252,127,000/=
Kif. 1004 - *Livestock Research and Training Institutes*…... .... ... ...Shs. 2,710,007,500/=
Kif. 2001 - *Water Resource Assessment and Exploration*..... ... . Shs. 2,595,859,400/=
Kif. 2002 – *Central Stores* … … … … … Shs. 535,076,900/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi*

*bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 - *Water Laboratory* … … … … … … Shs. 956,323,400/=

**MWENYEKITI:** Naona kuna Mheshimiwa Bernadina Ndaboine.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 3001 - Matumizi ya Majisafi na Majitaka Mijini. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu swali langu, alijibu matumizi ya majisafi wakati mimi nilikuwa nimeulizia huduma ya matumizi ya majitaka. Ni kwamba kwa sasa huduma ya matumizi ya majitaka Mijini….

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mbunge, naona hicho kifungu bado hatujakifikia. Ngoja tumalizie hicho kifungu, halafu utauliza. Bado hatujakifikia hicho kifungu unachokizungumzia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Urban Water Supply and Sewerage* … Shs. 2,136,622,100/=

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Bernadine Ndaboine.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali langu ni kwamba mimi niliulizia huduma ya majitaka Mijini, kwa sasa wana-charge asilimia 30 ya matumizi ya majisafi. Lakini ni kwamba majitaka huwezi kuyawekea mita.

Kwa hiyo, unakuta mtu ambaye anaishi peke yake katika nyumba kama ana bustani anamwagilia majisafi akichajiwa asilimia 30 ya majisafi ni kwamba atachajiwa zaidi kuliko hata nyumba wanayoishi watu 10 lakini hawana bustani. Kwa hiyo, ningeomba iwe flat rate kwa huduma ya majitaka.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani anisamehe mama sikusikia, nilijibu majisafi. Mheshimiwa Bernadine Ndaboine hii tunafuata formula ambayo ni established kwamba maji yanayoingia ndani ya nyumba tuseme ukiingiza lita 10 utayanywa, utayatumia chooni kawaida asilimia 73 yanatakiwa yatoke. Lakini kwa sasa hivi Mamlaka zinakomea kuchaji asilimia 30 lakini ni kwa rate ambayo iko chini siyo sawa na ya maji ambayo yangekuwa safi. Sasa kama mtu anatumia maji kwa ajili ya bustani, maji ambayo yako treated pia huwa haruhusiwi na mara kwa mara tunawazuia wasitumie maji ambayo ni treated kwa ajili ya bustani au kwa matumizi ambayo siyo ya binadamu. Kwa hiyo, hiyo rate ni standard na dunia nzima wanachaji hivyo, siyo Tanzania tu. Ni kwamba maji unayoyapata percent yake inabidi iondolewe na kusafirishwa kwa ajili ya kusafishwa au kwa ajili ya matumizi mengine.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 - *Rural Water Supply* … … ... ... … Shs. 4,080,113,200/=
Kif. 5001 - *Water Resources Institute* … ... ... ...Shs. 814,865,000/=
Kif. 6001 - *Drilling* … … … … … … ... ... Shs. 161,058,000/=
Kif. 7001 - *Veterinary Services* … … … ... Shs. 2,690,121,800/=
Kif. 8001 - *Animal Production* … … … ... Shs. 3,918,796,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … … ... ... ... Shs. 3,459,000/=
Kif. 1004 - *Livestock Research and Training Institutes*... ... ... ... ... Shs. 635,100,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Water Resource Assessment and Exploration* ... ... ... ... Shs.316,000,000/=

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi umeniona. Wakati nikichangia kwa maandishi, niliongolea kwa uchungu sana kuhusu suala…

**MWENYEKITI:** Ututajie na kifungu kabisa ili Mheshimiwa Waziri aweze kujibu.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 2001, kifungu kidogo 4981 - River Basin Management. Wakati nikichangia kwa maandishi nilizungumzia suala la kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo na mifugo na katika mchango wangu huo wa maandishi nilielezea hasa kuwa Serikali itoe tamko wazi kuwa mvua inapoanguka Kijijini maji yale ni rasilimali ya Kijiji kile, yavunwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili suala, kuna kigugumizi kikubwa kwa sababu halitamkwi wala Serikali haitaki kutamka. Dunia hii inakwenda kwa kuvuna maji na haiendi kwa kutegemea mvua aidha kwa mifugo au kwa kilimo. Sasa nataka kujua kuwa katika kifungu hiki wanaongelea mabonde makubwa ya mito River basin Management; Je, Mikoa ya ukame ambayo ina mabonde madogo madogo na milima midogo midogo kuna makorongo maji hayo hayavunwi na Wizara haitaki kutamka kabisa itaendelea kuvuna maji kule kule au ku-manage maji kule kwenye mito mikubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu pia kwa maandishi niliongelea mradi ambao nimeuandika mimi mwenyewe na nimeupeleka Wizara ya Fedha wa kuvuna maji katika milima ya Sekenke ambayo itajumuisha Kata saba. Bonde lile la Wembere litakuwa kijani kama maji yatavunwa na yakitoka milimani yapitie mashambani badala ya kwenda moja kwa moja kwenye mbuga na kwenye ziwa na

kugeuka kuwa chumvi. Sasa hii nchi itaendeleaje kama tutaendelea kudharau suala la kuvuna maji? Mimi nataka maelezo kamili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Leonard Shango kwa sababu amekuwa consistency sana kwa suala la kuvuna maji. Kila tulipoleta bajeti yetu maoni yake kwa maandishi na alipozungumza alizungumzia suala la kuvuna maji. Nakubaliana naye, tunaheshimu kabisa maoni yake na kama ameona bajeti yetu imekuwa inaongezeka mwaka baada ya mwaka katika eneo la kuvuna maji, kwa kweli katika Mikoa ya ukame hatuna njia isipokuwa kuvuna maji ya mvua. Nilikuwa naeleza hapa juu ya Hanang kwamba maji yao chini ya ardhi yana matatizo. Hawana milima yenye maji mengi ukiacha Mlima Hanang, solution yao tu ni kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Leonard Shango kwamba tunalizingatia na tunaliombea fedha. Najua yeye ni mtaalamu alikuwa *ADB*. Matumaini yangu ni kwamba Waraka wake alioupeleka Wizara ya Fedha utakubalika ili Bonde la Wembere libadilike liwe zuri sana. Nashukuru sana. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

| | | |
|---|---|---|
| Kif. 2003 - | *Water Laboratory* … … … … … | Shs. 90,000,000/= |
| Kif. 3001 - | *Urban Water Supply and Sewerage* ... | Shs.86,730,600,000/= |
| Kif. 4001 - | *Rural Water Supply* … … … … | Shs.28,739,200,000/= |
| Kif. 5001 - | *Water Resource Institute* … … … | Shs. 435,900,000/= |
| Kif. 6001 - | *Drilling* … … … … … … | Shs. 678,000,000/= |
| Kif. 7001 - | *Veterinary Services* … … … … | Shs. 1,285,200,000/= |
| Kif. 8001 - | *Animal Production* … … … …. | Shs. 848,000,000/= |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2005/2006 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makisio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoja hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka 2005/2006 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha Bunge, kuna jambo moja nataka nilitolee maelezo kidogo. Nilimweleza Mheshimiwa Leonard Derefa kwamba kama akiendelea na mchezo pale nitamtoa nje. Sasa nimepata viji-note vingi. Lakini kwanza nataka niseme kwamba Mheshimiwa Leonard Derefa leo ana furaha sana. Lakini nimekuja kugundua furaha yake ni nini baada ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kuanza kufagilia habari yake jinsi alivyojitahidi kwa masuala ya maji kule kwake. Kwa hiyo na mimi nampongeza sana alikuwa na furaha iliyopita kiasi. Kwa hiyo, alianza kidogo kupiga kelele pale nikajaribu kumvumilia vumilia, lakini nikaona Waheshimiwa Wabunge wengi wanaanza kumtazama. Halafu nikamvumilia kidogo nikaona Mheshimiwa Anne Makinda anaanza kumnyamazisha lakini akawa hasikii. Baadaye, nikaona Mheshimiwa George Lubeleje anayechangia naye akaanza kushindwa kuchangia akaanza naye kumwangalia nikaona inakuwa vurugu. Lakini ni rafiki wa kila mtu Mheshimiwa Leonard Derefa na kila siku ana furaha hivyo hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, sidhani kama hii ni issue ambayo kweli Mwandishi wa Habari angeweza kuona ni habari tu ya kuweza kuandika. Sidhani kama ni habari ya kuandika. Habari inayoweza kuandikwa kuhusu yeye ni hii ambayo Mheshimiwa Edward Lowassa amesema juu yake. Namtakia kila kheri. Lakini hili lingine nadhani halina sababu. Basi Mheshimiwa Leonard Derefa tunaendelea na utani wetu wa kila siku. Kila siku unaniita ndilanha na mimi ninasema ling'ombe lihanya wanajua Wasukuma.

Sasa baada ya maelezo hayo, naahirisha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.58. jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu tarehe 18 Julai, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*